# ULEKSIKALISHAJI, UKRIOLISHAJI NA MIKAKATI YA KIWINGI-LUGHA KATIKA DISKOSI ZA SHENG'

**NA**

**HARRIET KHATENJE IBALA**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU KATIKA KISWAHILI, KATIKA IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA, KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI JAMII**

**CHUO KIKUU CHA MOI**

**NOVEMBA, 2018**

# IKIRARI

## IKIRARI YA MTAHINIWA

Tasnifu hii imetokana na uchunguzi wangu asilia na haijawasilishwa katika chuo chochote kwa ajili ya kutahiniwa.

____________________ ____________________________

Harriet Khatenje Ibala — Tarehe
SASS/D.PHIL/KIS/03/09

## IKIRARI YA WASIMAMIZI

Tasnifu hii imewasilishwa ili kutahiniwa kwa ushauri na idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Moi

____________________________ ____________________________

Prof. Nathan O. Ogechi — Tarehe
Idara ya Kiswahili na Lugha
Nyingine za Kiafrika,
Chuo Kikuu cha Moi.

____________________________ ____________________________

Dkt. Robert Oduori — Tarehe
Idara ya Kiswahili na Lugha
Nyingine za Kiafrika,
Chuo Kikuu cha Moi.

## TABARUKU

Kwa mwenyezi Mungu, muumba wa vyote, na wazazi wangu wapendwa marehemu Bw. Paul Ibala na Bi. Alidah Kasiti Ibala kwa kujitolea kwenu, na jitihada zenu za dhati. Mling’ang’ana pasipo kukosa matumaini, mkanilea na kunielimisha. Na kwa mawaidha yenu, katika hali zote za maisha yangu. Rabuka awazidishie neema, rehema na wema.

## SHUKRANI

Ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kufika hapa nilipo wakati huu; kwa kunipa uhai, siha njema na hekima za usomi.

Ningependa vilevile kukishukuru Chuo Kikuu cha Moi na hasa Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika kwa kunipa fursa ya kuzamia katika taaluma hii ya Isimu Jamii na lugha ya Kiswahili. Shukrani za pekee ziwaendee wasimamizi wangu, Prof. Nathan Oyori Ogechi na Dkt. Rorbert Oduori, ambao walinielekeza vyema kama wasimamizi wangu, na kwa muda wao mwingi walionipa nilipokuwa nikishughulikia kazi hii. Kwa kweli, kazi hii haingekamilika bila msukumo na kujitolea kwao.

Shukrani za dhati ziwaendee walimu wangu wote, na wahadhiri wa Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi, kama vile Prof. Nathan Ogechi, Prof. Mwamzandi, Prof. Kahiga, Dkt. Robert Oduori, Dkt. Allan Opijah, Dkt. Mosol Kandagor, Dkt. Magdalene Wafula, Dkt. Samwel Obuchi, Dkt. Toboso, Dkt. Mbwarali, Mwl. Collins Mumbo, Mwl. Davies Mukuria, Mwl. John Munyua, Mwl. Vincent Magugu, Mwl. Tecla Muge na Mwl. Naomi J. Cherono. Asanteni sana kwa ushauri wenu wa mara kwa mara. Mwenyezi Mungu na awazidishie neema.

Siwezi kuwasahau wazamifu wenzangu, Eucabeth Ung’au - Mong’are, Wasike Misiko na Charles Wasike. Kila tulipohimizana mzigo ulionekana mwepesi na safari hii kuwa fupi. Asanteni sana.

Aidha wazazi na aila yangu kwa jumla, juhudi zenu za kunilea, kunisomesha na kunipa ushauri katika kila kiwango cha elimu na maisha yangu hakuwezi kusahaulika kamwe. Mmekuwa wa msaada mkubwa kwangu. Nazidi kuwaombea Mola awazidishie neema na Baraka ili mzidi kuwafaa wengine maishani.

# IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza uleksikalishaji, ukriolishaji na mikakati ya kiwingi-lugha ambayo hutumika katika ubadilishaji msimbo baina ya Sheng' na Kiswahili. Madhumuni ya utafiti yalikuwa kuhakiki mbinu za uleksikalishaji zinazotumiwa katika Sheng' kwa kuzingatia vigezo vya Pegitosca, kufafanua sifa zinazopinga upijini na ukriolishaji wa Sheng', kupambanua mikakati ya kiwingi-lugha inayojitokeza katika diskosi zenye Sheng' na kuchanganua tungo zenye Sheng' kwa kuzingatia nadharia ya 4M. Utafiti wenyewe ulichunguza mbinu za uleksikalishaji na mikakati ya kiwingi-lugha inayotumiwa katika diskosi zenye Sheng' ili kudhihirisha iwapo msimbo wa Sheng' ni msimu, lahaja ya Kiswahili, lugha, sajili, Pijini au Krioli. Nadharia mbili zilitumiwa katika utafiti huu: Kwanza, nadharia ya Pegitosca ya Kiingi ilitumiwa katika uhakiki wa mbinu za uleksikalishaji zinazotumiwa katika Sheng' na pili, nadharia ya 4M ya Myers-Scotton ilitumiwa ili kupambanua mikakati ya kiwingi-lugha na kuchanganua tungo zenye Sheng'. Data ya utafiti huu ilikusanywa kutoka kwa Shule tatu za upili zilizoteuliwa kimakusudi. Familia mbili za mitaani na makundi mawili ya vijana wanaoishi mitaani kutoka mitaa miwili katika kaunti ya Kisumu walihojiwa. Ili kuwafikia watafitiwa mahususi mitaani mbinu ya usampulishaji wa bonge-luji ilitumiwa. Kiranja mmoja katika kila shule iliyoteuliwa alitumiwa kupata sampuli ya wanafunzi 120 ambao walipewa karatasi na kuombwa waandike barua kwa marafiki zao wakitumia lugha waipendayo. Vilevile diskosi baina ya wanafunzi hawa zilirekodiwa. Katika sampuli ya familia za mitaani, mtafiti aliwahoji na akarekodi diskosi za vijana na wazazi waliokuwa wakiishi katika mitaa miwili iliyoteuliwa. Matokeo ya utafiti huu yamethibitisha kwamba Sheng' ni msimu na si lahaja, Pijini, Krioli wala lugha. Mbinu za kipekee za uleksikalishaji zinazotumiwa katika Sheng', ambazo hazikuwa zimebainishwa katika tafiti za awali kama ufinyaji wa maana na uhamishaji wa maana ziligunduliwa katika uchunguzi huu. Matokeo hayo yameonyesha kwamba mofimu nyingi amilifu zinazotumiwa katika mtagusano baina ya msimbo wa Sheng' na Kiswahili huwa za Kiswahili. Kuhusiana na mofimu nne (4M) zinazoshiriki katika ujenzi wa miundo ya UM yenye Sheng', iligunduliwa kwamba Sheng' hutumia mofimu amilifu za Kiswahili kwa vile haina mofimu zake amilifu. Hata hivyo, Sheng' ina mofimu chache amilifu ndiposa tasnifu hii ikahitimisha kwamba msimbo wa Sheng' ungeimarika kiasi cha kuwa na mofimu amilifu nyingi, huenda ingeweza kutumiwa mara nyingi pia kama lugha solo. Tasnifu hii inapendekeza haja ya kustawisha nadharia ya 4M ili iweze kufafanua pia miundo ya lugha mojamoja, na nadharia ya Pegitosca ili itofautishe nguzo za kuchambua msamiati na istilahi.

# ABSTRACT

This research sought to study lexicalization, creolization and multilingual strategies which are applied in Sheng' and Kiswahili code switching. It was based on four objectives: first, anchored on Pegitosca criteria, it sought to analyze the various lexicalization techniques which are used for building Sheng' words; second, to elaborate the multilingual strategies which are utilized in code switching (hereafter CS) involving Sheng'; third, to explain the various features which are relevant in discussing and concluding on whether Sheng' is a Swahili dialect, a language, a pidgin or a creole; and lastly, it sought to analyze CS structures which are generated from a juxtaposition of constituents from Kiswahili and Sheng'. The study was guided by two theories: Kiingi's Pegitosca theory was used in the study of lexicalization techniques. Carol Myers-Scotton's 4M model was relevant in the study of multilingual strategies, pidginization/creolization aspects and in the analysis of CS structures. Data was collected from three secondary schools (one girls' school, one boys' school and one mixed school) which were purposively selected and from two suburban contexts. Snow balling technique was used so as to arrive at specific respondents in suburban contexts. A prefect in each of the selected schools was used to sample 120 students who were provided with writing materials and asked to write letters to their friends in languages which they liked. The students in the selected schools and the youths plus street families in the selected suburban contexts were also interviewed and their conversations were recorded for analysis. The findings of this study have shown that Sheng' is not a Pidgin, Creole, Register or Swahili dialect but a season or a kind of Slang. Unique lexicalization techniques have been unearthed such as reduction and semantic transfer in this study. In relation to the four kinds of morphemes (4M) described by Myers-Scotton, the findings have demonstrated that the functional morphemes which are used in the kind of language contact which was studied are basically from Kiswahili. Sheng' is devoid of its own functional morphemes. In that vein, this study concludes that if Sheng' could have developed its own functional morphemes, then it would be possible to have it as a matrix language. This study recommends that there is a need to advance the 4M model such that it can be used in the description of monolingual structures and that Pegitosca criteria should differentiate the principles to be targeted in the analysis of vocabulary from those for use in the analysis of terminologies.

# YALIYOMO

IKIRARI ..... ii
TABARUKU ..... iii
SHUKRANI ..... iv
IKISIRI ..... v
ABSTRACT ..... vi
YALIYOMO ..... vii
ORODHA YA MAJEDWALI ..... xi
ORODHA YA VIELELEZO ..... xii
ORODHA YA VIFUPISHO ..... xiii
ISTILAHI ZILIZOTUMIWA KATIKA TASNIFU ..... xiv
**SURA YA KWANZA ..... 1**
**MISINGI YA UTAFITI ..... 1**
1.0 Usuli wa Suala la Utafiti ..... 1
1.1 Suala la Utafiti ..... 3
1.2 Malengo ya Utafiti ..... 3
1.3 Nadharia Tete za Utafiti ..... 4
1.4 Umuhimu wa Utafiti ..... 4
1.5 Upeo wa Utafiti ..... 7
1.6 Mbinu za Utafiti ..... 8
1.6.1 Muundo wa Utafiti ..... 8
1.6.2 Uteuzi wa Sampuli ..... 10
1.6.3 Mbinu za Kukusanya Data ..... 11
1.6.4 Vifaa vya Utafiti ..... 13
1.6.5 Mbinu za Kuchanganua Data ..... 14
1.6.6 Maadili ya Utafiti ..... 15
1.7 Matatizo Yaliyomkabili Mtafiti ..... 15
1.8 Hitimisho ..... 16
**SURA YA PILI ..... 17**
**MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA ..... 17**
2.0 Utangulizi ..... 17
2.1 Mapitio ya Maandishi Yanayohusu Sheng' ..... 17
2.1.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Chimbuko la Sheng' ..... 17
2.1.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Uamilifu wa Sheng' ..... 21

2.1.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Muundo wa Sheng' ....... 24
2.1.4 Yaliyoandikwa Kuhusu Athari za Sheng'....... 27
2.1.5 Yaliyoandikwa kuhusu Tipolojia ya Sheng'....... 34
2.1.6 Yaliyoandikwa Kutokana na Tafiti za Sheng' ....... 38
2.2 Msingi wa Kinadharia....... 44
2.2.1 Nguzo za Nadharia ya 4M Zinazohusu Miundo ....... 44
2.2.2 Nguzo za Nadharia ya 4M Zinazohusu Upijini/Ukriolishaji ....... 51
2.2.3 Nadharia ya Pegitosca....... 51
2.2.3.1 Nguzo za Nadharia ya Pegitosca....... 52
2.3 Hitimisho....... 55
**SURA YA TATU ....... 56**
**ULEKSIKALISHAJI, UPIJINI NA UKRIOLISHAJI WA SHENG' ....... 56**
3.0 Utangulizi....... 56
3.1 Mbinu za Uleksikalishaji katika Sheng' ....... 56
3.1.1 Mnyambuliko....... 56
3.1.2 Uradidi ....... 64
3.1.2.1 Uradidi wa Silabi ....... 64
3.1.2.2 Uradidi wa Neno zima ....... 65
3.1.3 Udondoshaji ....... 67
3.1.4 Uhamishaji wa Maana....... 69
3.1.5 Ufinyaji wa Maana....... 72
3.1.6 Uundaji Kinasibu ....... 73
3.1.7 Ufupishaji-tohozi ....... 75
3.1.7.1 Ufupishaji-tohozi wa Nomino za pekee....... 76
3.1.7.2 Ufupishaji-tohozi wa Nomino za kawaida....... 79
3.1.8 Uundaji Kiakronimia ....... 81
3.1.9 Urefushaji wa Umbo....... 83
3.1.10 Uundaji wa Kiantonimia....... 84
3.1.11 Uundaji wa Kionomatopia....... 86
3.1.12 Usarufishaji....... 87
3.1.13 Ukopaji....... 89
3.1.14 Mwambatano....... 94
3.1.15 Upanuzi wa Kisemantiki....... 95
3.1.16 Ujenzi Ghairi....... 96

3.2 Upijini na Ukriolishaji wa Sheng' ......................................................................98
3.2.1 Sifa Zinazoashiria kuwa Sheng' Haijawahi kuwa Pijini................................98
3.2.1.1 Sheng' Haikuibuka katika Muktadha wa Dharura..................................99
3.2.1.2 Fonolojia na Mofolojia za Sheng' Hazikutokana na Usahilishaji wa Zile za Lugha Changizi ..........................................................................100
3.2.1.3 Sheng' Haijakuwa Ikitegemea Viziada-lugha ili Kujaliza Ukosefu wa Msamiati ..........................................................................101
3.2.1.4 Maeneo ya Matumizi ya Sheng' Yanakiuka Yale ya Pijini ..................102
3.2.1.5 Sheng' Imekuwa na Miundo Mituamo Kinyume na Ilivyo kwa Pijini..102
3.2.1.6 Sheng' Haikuibuliwa kwa Vikundi Viwili vya Kijamii kama Lingua Franka ..........................................................................102
3.2.2 Sifa Zinazopinga Ukriolishaji wa Sheng' ..................................................103
3.2.2.1 Hali Zinazoathiri Usarufishaji wa Sheng'............................................103
3.2.2.2 Hali za Kijamii Zinazoathiri Ukriolishaji wa Sheng' ............................106
3.3 Tofauti baina ya Msimu, Pijini na Krioli ..........................................................109
3.4 Hitimisho..........................................................................................................112
**SURA YA NNE ..................................................................................................114**
**MIKAKATI YA KIWINGI-LUGHA KATIKA SHENG' NA UCHANGANUZI WA TUNGO ZAKE KWA VIGEZO VYA 4M ...................................................114**
4.0 Utangulizi.........................................................................................................114
4.1 Mikakati ya Kiwingi-Lugha katika Diskosi Zenye Sheng' ................................114
4.1.1 Uchanganyaji Msimbo.................................................................................115
4.1.2 Wingishaji-Maradufu...................................................................................120
4.1.3 Ushabihiano ...............................................................................................122
4.1.4 Ujozi-Msimbo ............................................................................................125
4.1.5 Utatu-Msimbo .............................................................................................127
4.2 Uchanganuzi wa Tungo Zenye Sheng' kwa Vigezo Vya 4M.............................131
4.2.1 Mchango wa LS na LC kwa Miundo Yenye UM .......................................131
4.2.1.1 Mseto wa Viambajengo vya LS na LC ................................................132
4.2.1.2 Vizingwa vya Lugha Solo katika Miundo yenye UM ..........................133
4.2.1.3 Vizingwa vya LC katika Miundo yenye UM........................................134
4.3 Mkuku wa Kimofosintaksia Unaozingatiwa.......................................................135
4.3.1 Kanuni ya Mfuatano wa Mofimu................................................................135
4.3.2 Kanuni ya Mofimu Amilifu ........................................................................139

4.4 Hitimisho....................................................................................................140
**SURA YA TANO ....................................................................................................141**
**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ....................................................................141**
5.0 Utangulizi....................................................................................................141
5.1 Matokeo ya Utafiti ....................................................................................................141
5.1.1 Matokeo kulingana na lengo la kwanza la utafiti ........................................141
5.1.2 Matokeo Kulingana na Lengo la Pili la Utafiti ............................................148
5.1.3 Matokeo Kulingana na Lengo la Tatu la Utafiti ..........................................151
5.1.4 Matokeo Kulingana na Lengo la Nne la Utafiti............................................153
5.2 Mahitimisho ....................................................................................................155
5.3 Mapendekezo ....................................................................................................169
MAREJELEO ....................................................................................................175
VIAMBATISHO....................................................................................................184
Kiambatisho I: Mwongozo wa Usaili ....................................................................184
Kiambatisho II: Idhini ya Utafiti Kutoka NACOSTI ............................................185
Kiambatisho III: Kibali Cha Utafiti ......................................................................186

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1.1: Hatua za Utafiti ........................................................................... 9
Jedwali 2.1: Sifa ya Upatanisho ...................................................................... 36
Jedwali 2.2: Vigezo vya Pegitosca ................................................................... 52
Jedwali 3.1: Mnyambuliko wa Vitenzi vya Sheng’ ..................................................... 62
Jedwali 3.2: Udondoshaji kama Mbinu ya Uleksikalishaji .......................................... 69
Jedwali 3.3: Muhtasari wa Sifa Zinazopinga Upijini wa Sheng’ ................................ 99
Jedwali 3.4: Tofauti Kati ya Msimu, Pijini na Krioli ................................................ 110

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo 2.1: Uanishaji wa Mofimu ............................................................... 50
Kielelezo 4.1: Uchanganyaji-Msimbo baina ya Msimu na Lugha ............................ 116
Kielelezo 4.2: Wingishaji-Maradufu kwenye Nomino za Sheng' ............................. 122
Kielelezo 4.3: Ujozi-Msimbo baina ya Msimu na Lugha ......................................... 125
Kielelezo 4.4: Mkakati wa Kiwingi-lugha akilini mwa Mwanaujozi-msimbo .......... 126
Kielelezo 4.5: Utatu-Msimbo baina ya Msimu Mmoja na Lugha mbili .................... 127

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| **K.C.P.E** | - | Kenya Certificate of Primary Education |
| **K.C.S.E** | - | Kenya Certificate of Secondary Education |
| **KN** | - | Kirai nomino |
| **KT** | - | Kirai kitenzi |
| **KV** | - | Kirai vumishi |
| **LC** | - | Lugha changizi |
| **LS** | - | Lugha solo |
| **SACMEQ** | - | African Consortium for Monitoring Educational Quality |
| **TUKI** | - | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| **UKIMWI** | - | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| **UM** | - | Ubadilishaji msimbo |
| **4M** | - | Modeli ya Mofimu Nne [mwendelezo wa nadharia ya lugha solo] |
| **PEGITOSCA** | - | Kifupisho cha **P**recision (Udhahiri), **E**conomy (Ikitisadi), **G**enerativity (Uzalishaji), **I**nternationality (Umataifa), **T**ransparency (Uangavu), anti-**O**bscenity (Utusani), **S**ystemicity (Utaratibu maalum), **C**onsistency (Utaratibu ulio sawa), **A**ppropriateness (Ukubalifu na ufaafu) |

## ISTILAHI ZILIZOTUMIWA KATIKA TASNIFU

| | | |
|---|---|---|
| Istilahi | - | Terminology |
| Launi isiyotarajiwa | - | Marked variety |
| Launi-takaro | - | Substrate varieties |
| Lugha chasili | - | Source language |
| Lugha mahuluti | - | Hybrid language |
| Lugha pokezi | - | Recepient language |
| Lugha solo | - | Matrix languagesss |
| Lugha-tuhinga | - | Superstrate language |
| Lugha-takaro | - | Substrate language |
| Mofimu za kileksika za lugha-tuhinga | - | Superstrate-content morphemes |
| Msamiati | - | Vocabulary |
| Msimbo pokezi | - | Recepient code |
| Ubadilishaji msimbo | - | Inter & intra-sentential switching |
| Uchachawizaji | - | Interference |
| Uchanganyaji msimbo | - | Intra-sentential switching |
| Uhusika wa kisarufi | - | Case marking |
| Ujenzi ghairi | - | Metathesis |
| Ukopaji kwa muda | - | Nonce borrowing |
| Uleksikalishaji | - | Lexicalization |
| Uradidi wa Silabi au neno | - | Reduplication |
| Usampulishaji wa bonge-luji | - | Snow balling technique |
| Usilabifishaji-Upya | - | Resyllabification |
| Uundaji Kinasibu | - | Coinages |

| | | |
|---|---|---|
| Usarufishaji | - | Grammaticalization |
| Ushabihiano | - | Convergence |
| Wanaunusu-lugha | - | Semilinguals |
| Wingishaji-Maradufu | - | Double pluralization |

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.0 Usuli wa Suala la Utafiti

Sheng' ni msimbo unaofanana na Kiswahili ambao, ingawa unahusishwa zaidi na vijana, unatumiwa hata na wazee kama chombo cha mawasiliano katika miktadha mingi hivi sasa. Kabla ya utafiti huu, Sheng' imechunguzwa kwa kuzingatia malengo tofauti tofauti na kwa kuongozwa na nadharia mbalimbali. Baadhi ya matokeo ya tafiti hizo yanakinzana na kwa hivyo kusababisha utata katika ufafanuzi wa sifa zake za kiisimu.

Tafiti nyingi kama zile za Kioni (2002), Waihenya (1996), Amisi (1997), Nyagaka (1995), Kimei (1997) na Mohochi (2000) zilijikita katika uchunguzi wa athari za Sheng' kwa matumizi ya Kiswahili na Kiingereza. Tafiti hizo zilijibana kwenye upeo huo pasipo kuchunguza mikakati ya kiwingi-lugha inayohusika katika sentensi zenye Sheng'. Mbinu za uleksikalishaji[1] na mikakati ya kiwingi-lugha inayoshiriki katika ujenzi wa sentensi hazikuchunguzwa kwa lengo la kudhihirisha iwapo Sheng' ni msimu, ni Pijini[2] au ni Krioli[3]. Baadhi ya watafiti, kwa misingi hiyo, waliweza kudokeza kuwa Sheng' ni Krioli bila kudhihirisha ithibati za ukriolishaji wake.

---

[1] Uleksikalishaji ni mchakato wa kiisimu unaohusu uundaji, urekebishaji na ukopaji wa msamiati na istilahi.

[2] Pijini ni launi ya lugha inayoibuliwa katika muktadha wa mtagusano wa lugha ambapo wahusika hawana lingua franka.

[3] Krioli ni Pijini ambayo imeimarika kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki na baadhi ya watoto wameanza kujifunza kama lugha ya kwanza na kwa hivyo ina wazawa-lugha wake.

Isitoshe, tafiti za awali kama za Mohochi (2002), Mbaabu na Nzuga (2003) na Ogechi (2002) hazikuchunguza ushiriki wa mofimu za aina mbalimbali na mpangilio wao kama vijenzi vya miundo yenye Sheng'. Mikakati mbalimbali ya kiwingi-lugha inayohusika katika uzalishaji wa miundo yenye Sheng' ambayo ingeweza kudhihirisha au kupinga upijini wa Sheng' haikubainishwa na watafiti hawa. Mikakati hiyo imechunguzwa na kufafanuliwa katika utafiti huu mintarafu ya nadharia ya 4M.

Maelezo ya wataalamu yanaonyesha kuwepo kwa mitazamo mitatu inayopingana kuhusu Sheng'. Mtazamo wa kwanza ni ule wa waandishi kama Bosire (2013) wanaorejelea Sheng' kama mfumo-lugha kwa maana ya lugha inayofaa kuhesabiwa pamoja na lugha 43 zinazozungumzwa nchini Kenya.

Mtazamo wa pili umetokana na wataalamu kama vile Mazrui (1995) na Githiora (2002) wanaoonyesha kuwa Sheng' ni msimbo unaotokana na UM unaofanyika baina ya Kiswahili na Kiingereza. Watafiti wengine wanaounga mkono mtazamo huu wamedai kuwa Sheng' ni msimbo ulioibuka kutokana na mtagusano uliotokea baina ya lugha mbili au zaidi zikiwemo zile za kiasili (Mbaabu na Nzuga, 2003; Ogechi, 2002).

Mtazamo wa tatu nao ni ule unaodai kwamba Sheng' iliibuka kutokana na Pijini na ikageuka kuwa Krioli. Mtazamo huo unatatanisha mno na umepingwa na wataalamu kama vile Osinde (1986). Madai ya Maingi (2014) yanazidisha utata huo unaohusiana na dhana hii pale anapoeleza kuwa Sheng' ina sifa zinazoweza kuionyesha kama lugha, kama Krioli na kama msimu. Kuwepo kwa mitazamo hii inayopingana kuhusu Sheng' kulichochea kufanywa kwa utafiti huu. Hii ni kwa maana uchunguzi wa kina wa sifa za uleksikalishaji, usarufishaji na hata mikakati ya kiwingi-lugha inayofuatwa ungeweka wazi ikiwa Sheng' ni sajili, msimbo, UM, lahaja ya Kiswahili, lugha, msimu au Krioli (Kingei, 1987; Maingi, 2014).

## 1.1 Suala la Utafiti

Upambanuzi wa mikakati ya kiwingi-lugha na uleksikalishaji katika diskosi za Sheng' ni muhimu kwa wanaisimu jamii wanaotaka kujua sifa zake za kiisimu zinazoiwezesha Sheng' kufanikisha mawasiliano. Uchunguzi huu wa mikakati hiyo ulihitajika kufanywa ili kulijibu swali ambalo halikuwa limejibiwa kuhusu iwapo Sheng' ni sajili, lahaja ya Kiswahili, msimbo au Krioli ambayo imeibuka kama lugha bainifu. Sifa za Sheng' jinsi ilivyo kwa sasa hazikuwa zimechunguzwa kabla ya utafiti huu ili ijulikane iwapo ina sifa za misimu kama msimu wa Kiingereza (Slang) au ni Krioli vile inavyodaiwa. Mathalani, mbinu za uleksikalishaji zinazotumika ili kuendeleza Sheng' hazijakuwa zimehakikiwa kwa mujibu wa nadharia ya Pegitosca ili kubainisha iwapo inaendelea kuashiria upanuzi wa msamiati unaoambatana na ukuaji wa msimu au Krioli. Ili kulijaza pengo hilo la kiuchunguzi, utafiti huu ulifanywa kwa kuongozwa na malengo yafuatayo.

## 1.2 Malengo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza mbinu za uleksikalishaji na mikakati ya kiwingi-lugha inayotumiwa na wazungumzaji wa Sheng' kwa kujikita katika madhumuni mahususi yafuatayo:

i. Kubainisha na kufafanua mbinu za uleksikalishaji zinazotumiwa katika Sheng' kwa kuzingatia vigezo vya Pegitosca.
ii. Kufafanua sifa zinazopinga upijini na ukriolishaji wa Sheng.'
iii. Kupambanua mikakati ya kiwingi-lugha inayojitokeza katika miundo yenye Sheng'.
iv. Kuchanganua tungo zenye Sheng' kwa kuzingatia nadharia ya 4M.

### 1.3 Nadharia Tete za Utafiti

Hatua zilizofuatwa katika utafiti huu kuanzia ukusanyaji wa data, uchanganuzi na mahitimisho ziliongozwa na nadharia tete zifuatazo:

i. Mbinu za uleksikalishaji zinazotumiwa kupanua msamiati wa Sheng' haziafiki vigezo vya Pegitosca.

ii. Sifa za kileksika na za kimuundo za Sheng' zinapinga upijini au ukriolishaji wake.

iii. Mikakati kadhaa ya kiwingi-lugha huhusika ili kufanikisha uwasilishaji wa maana katika diskosi zenye Sheng'.

iv. Mkuku unaofuatwa na mofimu katika ujenzi wa miundo yenye Sheng' na mofimu zinazoshiriki si bainifu.

### 1.4 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti wa misimbo kama Sheng' inayotokana na mtagusano wa lugha ni muhimu katika taaluma ya Isimu Nadharia. Matokeo ya utafiti wa aina hii yanaweka wazi elementi zinazohusu michakato ya uleksikalishaji katika misimbo ambayo haijakuwa na mifumo thabiti ya kisarufi kama Sheng'. Matokeo ya utafiti huu yataweza kuwafaidi wanaisimu nadharia wanaolenga kuibua au kuendeleza nadharia zinazohusu umoja-lugha au wingi-lugha. Matokeo yenyewe yanafaa kwa ukadiriaji wa ufaafu wa nadharia zilizotumika hasa kuhusiana na masuala ya wingi-lugha, msimu, Pijini na Krioli. Ufaafu wa vigezo vilivyofanikisha uchunguzi huu umeweza kudhihirika. Matokeo hayo, kwa hivyo, yanaweza kutumiwa ili kustawisha nadharia kama vile Pegitosca na 4M ili ziweze kudhihirisha utoshelevu wa kiuchunguzi na kiufafanuzi.

Watafiti wenye ari ya kujifahamisha na masuala yanayohusu uchakataji wa miundo, wataweza kufaidika kutokana na ufafanuzi unaofanywa katika tasnifu hii. Wao

wataweza kurejelea sehemu zinazoonyesha ni katika kiwango kipi cha uzalishaji wa diskosi unaofanyika akilini ambapo mofu mbalimbali huzanzuliwa.

Uchanganuzi, ufafanuzi na mahitimisho ya utafiti huu ni muhimu kwa wanaisimu jamii wanaoshughulikia mitagusano ya lugha katika miktadha ya wingi-lugha kwa sababu ya aina ya mtagusano-lugha uliochunguzwa. Utafiti wa aina hii unawafaa kwa ubainishaji wa mtagusano-lugha unaofanyika baina ya msimu na lugha. Hii ni kwa sababu, kama inavyojitokeza katika utafiti huu, namna ambavyo UM baina ya Sheng' na lugha unafanyika hutofautiana na ule unaofanyika baina ya lugha mbili. Hii ni kwa sababu, kama inavyodhihirika katika uchanganuzi wa data, Sheng' haina mkuku wake wa kisarufi ila inategemea ule wa Kiswahili.

Kutokana na upekee wa kushughulikia upijini na ukriolishaji wa Sheng', matokeo ya utafiti huu yanafaa tanzu za Isimu kama vile Isimu Nadharia na Isimu Fafanuzi. Kwanza, matokeo yanaweza kutumiwa na wanaisimu fafanuzi ili kutatua suala kuhusu iwapo Sheng' iliibuka kama Pijini au ni msimu. Matokeo hayo ni muhimu katika kuikosoa nadharia tete inayochukulia kwamba Sheng' ilikuwa pijini, ikawa Krioli na kwa sasa ni lugha ambayo inapaswa kuhesabiwa na lugha zinazopatikana nchini Kenya.

Matokeo ya utafiti huu ni muhimu kwa taaluma ya Leksikografia. Hii ni kwa sababu umechunguza mbinu zinazotumika katika uundaji wa msamiati. Vile inavyodhihirika katika uchanganuzi wa data, wazungumzaji wa Sheng' waliochunguzwa walidhihirisha mbinu za kipekee zinazotumiwa kupanua msamiati wa lugha. Hapana budi kwamba kugunduliwa kwa mbinu hizo kutaweza kuchochea uchunguzi zaidi wa lugha na hata misimu ili kubainisha namna ambavyo mbinu hizo na hata nyinginezo zinaweza kutumiwa ili kukuza msamiati na istilahi. Hii inamaanisha kuwa mahitimisho ya utafiti

huu yanafaa vilevile kwa utathmini na uimarishaji wa mbinu na nadharia za kileksikografia.


Inatarajiwa pia kwamba watafiti na wadau wengine wanaotaka kujua zaidi kuhusu Sheng’ wataweza kuifikia tasnifu hii. Hii ni kwa vile Sheng’ inatumiwa zaidi katika mawasiliano miongoni mwa makundi nyeti kama vijana, majangili, utingo, wafanyibiashara na hata walanguzi wa dawa za kulevya. Aidha, msimbo wa Sheng’ hutumiwa hivi sasa na wanasiasa, wahubiri, katika matangazo ya kibiashara, katika mitandao ya kijamii na hata katika vyombo vya habari. Hii inamaanisha kwamba uchunguzi wa msimbo huu hauwezi kuepukika kama wenzo mojawapo unaoathiri maendeleo ya kijamii kwa njia moja au nyingine. Hivyo basi, uchanganuzi na ufafanuzi wa Sheng’ unaofanywa katika tasnifu hii unaweza kuwaauni wazungumzaji, walimu, wanafunzi, wazazi na hata serikali. Wao wataweza kujua maana za baadhi ya maneno kwa pamoja na masuala mengine yanayohusu Sheng.

Matokeo ya utafiti huu, kwa mujibu wa lengo lake la tatu, yatachangia pakubwa kusawiri taswira inayomfaa mwalimu wa lugha ajue kuhusu mtagusano wa kimuundo unaotokea baina ya Kiswahili na Sheng’. Matokeo haya ni muhimu kwa walimu wa Kiswahili kwa maana wataweza kugundua pale ambapo wanafunzi wamechopeka maneno ya Sheng’ kwenye mkuku wa Kiswahili. Wataweza vilevile kutofautisha kati ya ubunifu wa mwanafunzi katika Kiswahili na matumizi ya maneno ya Sheng.’ Hii ni kwa sababu mwalimu asiyeelewa uhalisia huo anaweza kukosea kwa kuvichukulia vizingwa vya Sheng’ vinavyojitokeza katika maandishi ya wanafunzi kama njia ngeni za ubunifu. Mchango huo ni muhimu kwa vile matumizi ya msimbo wa Sheng’ hayawezi kukomeshwa kabisa na mtagusano wake na Kiswahili utakuwa ukiendelea hata siku zijazo.

## 1.5 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kaunti moja (kaunti ya Kisumu) kati ya kaunti arobaini na saba zinazopatikana nchini Kenya. Mtafiti alijiwekea upeo wa kuchunguza shule tatu za upili pekee na mitaa miwili pekee katika kaunti hiyo. Wanafunzi mia moja ishirini [arobaini kutoka kila shule iliyoteuliwa] walishirikishwa katika uandishi wa barua. Kutokana na sampuli hiyo, barua sitini pekee zilichanganuliwa. Makundi mawili ya vijana wa mitaani na familia mbili zilizoishi mitaani zilichunguzwa katika mitaa miwili iliyochunguzwa katika utafiti huu.

Kaunti ya Kisumu ina eneo la kilomita 2085.9 mraba na ina takriban wakaazi elfu 968,909 kwa kutegemea uhasibu wa idadi ya watu uliofanywa mwaka wa 2010 (Republic of Kenya, 2010). Kaunti ya Kisumu inapakana na kaunti ya Vihiga kwa upande wa Kaskazini, kaunti ya Nandi katika upande wa Kaskazini Mashariki, kaunti ya Kericho katika upande wa Mashariki, kaunti ya Homabay upande wa Kusini Magharibi na hatimaye kaunti ya Siaya katika upande wa Magharibi vile inavyoonyeshwa katika ramani ifuatayo.




**Ramani ya Eneo la Utafiti: Kaunti ya Kisumu**

**Asili:** Google maps

Mtafiti alijikita katika kaunti hii ya Kisumu kama eneo la utafiti kwa sababu utafiti wa aina hii, mintarafu ya mapitio ya maandishi yaliyofanywa na mtafiti, haujawahi kufanywa pale ila umekuwa ukifanywa katika kaunti zingine kama vile Nairobi, Nakuru, Kisii na Eldoret. Mtafiti aliteua eneo hili la utafiti kwa vile alikuwa analielewa vyema na yeye mwenyewe ni mkaazi wa eneo hilo na alifundisha katika shule za upili za kaunti hiyo kwa miaka mingi. Kwa hivyo, mtafiti alikuwa akifahamu na kulielewa eneo husika vyema. Jambo hili lilimwezesha kufika mitaa na shule alizoteua kwa urahisi na kukusanya data jinsi ilivyohitajika.

## 1.6 Mbinu za Utafiti

### 1.6.1 Muundo wa Utafiti

Muundo wa utafiti huu ulikuwa wenye awamu mbili kuu za utafiti mwigo na utafiti mkuu. Utafiti mwigo ambao ulilenga kuthibitisha ufaafu wa vifaa na uwezekano wa

kutafitika kwa suala ulifanywa majuma mawili kabla kuzamia utafiti wenyewe. Utafiti huo mwigo ulitekelezwa katika mtaa mmoja na shule moja katika kaunti ya Kisumu, haya yakiwa baadhi ya maeneo yaliyokuwa yameteuliwa na mtafiti katika sampuli yake. Kutokana na utafiti huo, mtafiti aliweza kuiandaa ratiba ya ukusanyaji data kwa kuzingatia hali halisi miongoni mwa watafitiwa. Ni katika utafiti mwigo huo ambapo mtafiti alionelea kuwa ilifaa ashirikishe usaili kama mbinu ya kukusanya data ambayo ingefaa kwa lengo linalohusu upijinishaji.

Awamu ya pili ya utafiti huu ilihusu utafiti halisi uliofanywa baada ya utafiti mwigo. Utafiti huo mkuu ulifuata hatua kumi kwa ujumla katika miktadha ya shule na mitaa. Mathalani, kwenye miktadha miwili ya shule, wanafunzi kwanza walipewa karatasi ili waandike barua, pili, mazungumzo yao yalirekodiwa na katika hatua ya tatu wakahojiwa. Katika mitaa miwili iliyochunguzwa, kila mtaa ulikuwa na hatua mbili. Hii ni kwa vile mtafiti alikuwa, kwanza akirekodi mazungumzo ya vijana katika mitaa miwili kisha akawahoji vijana hao halafu akarekodi mazungumzo ya wazazi wa familia zinazoishi mitaani kutoka mitaa hiyo miwili iliyoteuliwa na akawahoji wazazi wa familia hizo vile inavyoonyeshwa katika Jedwali 1.1 lifuatalo.

**Jedwali 1.1: Hatua za Utafiti**

| **Maeneo** | **Hatua** | **Shughuli** |
|---|---|---|
| Shule mbili za upili | Hatua 1 | Wanafunzi kuandika barua |
| | Hatua 2 | Kurekodiwa kwa mazungumzo ya wanafunzi |
| | Hatua 3 | Kuhojiwa kwa wanafunzi |
| Mitaa miwili | Hatua 4 | Kurekodi mazungumzo ya vijana kisha kuwahoji |
| | Hatua 5 | Kurekodi mazungumzo ya wazazi wa familia za mitaani kisha kuwahoji |

### 1.6.2 Uteuzi wa Sampuli

Kaunti moja ya Kisumu iliteuliwa miongoni mwa kaunti arobaini na saba, kama sampuli ya utafiti. Mtafiti aliweza kufanya uteuzi wa sampuli ya kimakusudi wa shule tatu katika kaunti hiyo kwa kuzingatia mawazo ya Wamahiu na Karugu (2002) na Gall (1996). Wao wanadahili kuwa kiuhakiki, matumizi ya sampuli ya kimakusudi huzalisha matokeo bora na yenye kutegemewa hata kama idadi iliyoteuliwa ni ndogo. Mtafiti aliweza kuteua shule moja ya wavulana, moja ya wasichanana, moja ya mseto kwa ajili ya kuhakikisha kuwa kuna uwakilishaji unaotosha hata ingawa elementi ya jinsia haikuwa ikichunguzwa katika utafiti huu.

Mtafiti aliweza kuteua kidato cha tatu pekee katika kila shule iliyochunguzwa kama sampuli wakilishi. Alifanya uteuzi huo kwa kuandika vijikaratasi vinne na kuandika 'kidato cha kwanza', 'kidato cha pili', 'kidato cha tatu' na 'kidato cha nne' kisha akavikunjakunja na kumpa mtafitiwa mmoja akiteue kimoja. Mtafitiwa huyo alikiokota kijikaratasi chenye 'kidato cha tatu' ndiposa mtafiti akajikita katika darasa hilo kama sampuli yake ya utafiti. Mtafiti alitumia mbinu hii ya usampulishaji ili kuimarisha uyakinifu katika utafiti wake.

Baada ya kuteua kidato cha tatu kama darasa la kuchunguzwa, mtafiti aliwapa wanafunzi arobaini kutoka kila shule zoezi la kuandika barua kwa rafiki yake kwa lugha aipendayo. Aliweza kumpa kiranja wa kidato cha tatu karatasi arobaini pekee kwa kila shule iliyochunguzwa ambaye naye alikuwa akiwateua kinasibu wanafunzi ambao wangeandika barua hiyo. Kutokana na barua mia moja ishirini zilizokusanywa kutoka shule tatu zilizochunguzwa, mtafiti aliweza kuteua kimakusudi sampuli ya barua ishirini ishirini zilizokuwa zimeandikwa kwa kutumia msimbo wa Sheng' kwa ajili ya uchanganuzi katika utafiti huu. Sampuli ya barua sitini zilizokuwa zimeandikwa kwa

msimbo wa Sheng' ziliteuliwa kimakusudi kulingana na madhumuni ya utafiti huu. Gall (1996) amepambanua kwamba lengo kuu la sampuli ya kimakusudi huwa kuwalenga wale watafitiwa pekee ambao huenda wana habari za kutosha zinazohusu madhumuni ya utafiti. Usampulishaji wa aina hii vilevile uliufaa utafiti huu, kwa vile, kama anavyoonyeshwa na Enon (1998), matumizi yake huimarisha ufaafu wa matokeo. Hii inamaanisha kwamba barua zilizokuwa zimeandikwa na watafitiwa kwa Kiswahili au Kiingereza pekee hazikushirikishwa kama data ya kuchanganuliwa.

Ili kufanya uchunguzi wa Sheng' mitaani, mtafiti alitumia mbinu ya usampulishaji wa bonge-luji ili kuwafikia watafitiwa mahususi. Alifanya hivi kwa kumtambua mtafitiwa mmoja ambaye angemsaidia kuwatambua watafitiwa wengine ambao nao wangemsaidia mtafiti kuwatambua wengine (Leedy, 2000; Battarcherjee, 2012). Mbinu hii ilimsaidia mtafiti awatambue watafitiwa, mahali na wakati ambapo angewachunguza katika mitaa miwili aliyoichunguza.

Kando na kutumia mbinu ya usampulishaji wa bonge-luji kuwateua watafitiwa wake, mtafiti aliteua kimakusudi mitaa miwili jijini Kisumu. Mtafiti alitumia usampulishaji huo wa kimakusudi ili kuteua sampuli wakilishi ya mitaa miwili: Mtaa mmoja [Kondele] unaopatikana karibu katikati ya jiji unaokaliwa na watu kutoka jamii mbalimbali na mtaa mwingine [Nyalenda] unaopatikana mbali kutoka katikati ya jiji na ambao umepakana na makazi ya tabaka la matajiri yanayojulikana kama Milimani. Mtafiti aliweza kuiteua mitaa hiyo kwa sababu ingeweza kumzalishia data inayowakilisha Sheng' inayozungumzwa katika mazingira tofauti tofauti.

### 1.6.3 Mbinu za Kukusanya Data

Mbinu zilizotumiwa katika ukusanyaji wa data katika utafiti huu ni pamoja na kurekodi mazungumzo kwa kutumia kinasa sauti, uandishi wa barua na mahojiano. Ili kuondoa

upungufu ambao ungetokana na mbinu zilizotajwa hapo juu, mtafiti aliweza kutumia mbinu za utazamaji, kusikiliza na kunakili kwenye shajara. Ushirikishwaji huo ulifanywa kwa lengo la kupata data ambayo ingetosheleza malengo ya utafiti huu, jinsi anavyopendekeza Battercharjee, (2012). Namna ambavyo mbinu hizi zilitumiwa imefafanuliwa katika ibara zifuatazo.

Mtafiti alirekodi mazungumzo ya wanafunzi kati ka mazingira yasiyokuwa rasmi ndani na nje ya madarasa. Aliweza pia kunasa mazungumzo ya watumiaji wa Sheng' katika mitaa miwili. Mbinu hizi zilitumiwa kwa sababu mtafiti alitaka kujua uhalisia unaohusu msamiati, miundo na ukriolishaji wa Sheng'. Mintarafu ya Battercharjee (keshatajwa), kurekodi mazungumzo kunamwezesha mtafiti kunakili mambo muhimu katika mazungumzo jinsi yanavyotokea. Mbinu hii ya kurekodi mazungumzo katika mazingira halisi ilifaa zaidi kwa sababu, kama anavyodai Leedy (2000) uchunguzi unaofanywa katika miktadha halisi ni muhimu kwa tafiti za kiisimu zinazofanywa kwa kina. Miktadha halisi huweza kujenga taswira sahihi inayolengwa katika Isimu Fafanuzi. Mbinu hii humwezesha mtafiti kurekodi data halisi inayoweza kutegemewa.

Wanafunzi arobaini wa kidato cha tatu katika kila shule iliyoshirikishwa katika utafiti walipewa zoezi la kuandika barua kwa marafiki wakitumia lugha waipendayo [Idadi maalum ya barua zilizoteuliwa na kuchanganuliwa imebainishwa katika sehemu ya uteuzi wa sampuli kwenye tasnifu hii]. Kwa vile Sheng' ni lugha ya utambulisho baina ya vijana (Osinde 1986, Abdulaziz na Osinde, 1997 na Githinji, 2006) mtafiti aliamua kuwapa zoezi la kuandikia rafiki zao barua. Ili kufanya hivi, mtafiti alikisia kwamba wangetumia Sheng' kama msimbo unaotarajiwa miongoni mwa vijana (Myers-Scotton, 1993a), kinyume na lugha ambayo wangetumia kumwandikia mzazi au mwalimu.

Mtafiti aliwahoji baadhi ya wanafunzi katika shule zilizoteuliwa katika utafiti huu. Aliweza kuwasaili wale ambao hawakuwa wenyeji wa Kisumu kuhusu usawa na tofauti zinazojitokeza baina ya msamiati wa Sheng' unaozungumzwa na wenzao shuleni na Sheng' wanayoitumia kwingineko. Mtafiti vilevile aliweza kuwauliza kuhusu mwelekeo wa msamiati wa Sheng' ili kutambua iwapo maneno yanayotumiwa katika msimbo huu yamekuwa thabiti au yanaendelea kubadilikabadilika. Maswali hayo yalilengwa ili kutupa picha halisi kuhusu upijini au ukriolishaji wa Sheng'.

Vijana waliokuwa wakitumia Sheng' mitaani pamoja na familia zilizokuwa zikiishi mitaani zilihojiwa. Kusailiwa kwao kulilengwa kubaini masuala yanayohusu upataji au ujifunzaji wa Sheng', iwapo wana lugha za kwanza zisizokuwa Sheng' na iwapo walikuwa na lugha iliyokuwa ikiwaunganisha kama lingua franka kabla ya kujifunza Sheng'. Wao vilevile waliweza kuulizwa iwapo wanawapokeza watoto wao wanaozaliwa mitaani msimbo wa Sheng' au lugha zao za kwanza. Wazazi hawa walihojiwa vilevile kuhusu iwapo watoto wa familia zingine za mitaani walikuwa wakijifunza Sheng' kutoka kwa wazazi wao au kutoka kwa watu au watoto wengine mitaani. Baadhi ya maswali yaliyokuwa yakimwongoza mtafiti katika kuwasaili watafitiwa yameshirikishwa katika tasnifu hii kama kiambatisho.

### 1.6.4 Vifaa vya Utafiti

Katika kukusanya data ya utafiti huu, nilitumia vifaa anuwai. Kifaa cha kwanza ni kinasa sauti, aina ya Sanyo (TRC-650). Kinasa sauti hicho kilikuwa na uwezo wa kunasa mazungumzo kwa umbali wa karibu mita hamsini. Hivyo basi, ingeweza kunasa mazungumzo ya watafitiwa hata kikiwa kimefichwa ndani ya mfuko.

Vifaa vingine vya kukusanya data ni kalamu na shajara. Shajara ilitumiwa kurekodi tabia za wahusika na mambo mengine ambayo huenda hayangerekodiwa na kinasa sauti

kama vile watoto wadogo wa familia za mitaani walikuwa wakiongea Dholuo au Kiswahili wakati mtafiti alipokuwa akiwasaili wazazi wao. Vilevile mtafiti alitumia karatasi zilizokuwa na vipimo vya A4 ambazo aliwapa wanafunzi ili kuandikia barua kwa marafiki zao kwa kutumia lugha waipendayo.

Kando na vifaa vilivyotajwa hapo juu, mtafiti alitumia mwongozo wa usaili ambao ulikuwa na maswali yaliyolengwa kuulizwa [Tazama Kiambatisho]. Maswali hayo yalikuwa ya aina tatu. Hii ni kwa kuwa kuna yale ambayo wanafunzi wangeulizwa, yale ambayo yangejibiwa na wazazi wa familia zinazoishi mitaani na mwisho yale ambayo mtafiti angewauliza vijana wanaoishi mitaani.

### 1.6.5 Mbinu za Kuchanganua Data

Utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo. Hatua ya kwanza baada ya kurekodi mazungumzo ya watafitiwa katika utafiti huu ilikuwa kufanya unukuzi. Hili lilifanywa kwa kuyasikiliza mazungumzo yaliyorekodiwa na kuyanukuu kwa kuandika neno kwa neno. Baada ya unukuzi, mtafiti alitenganisha data iliyofaa kwa ufafanuzi wa malengo ya utafiti kuhusu Sheng'.

Kwa sababu utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo, tafsiri, mifano na ufafanuzi ni baadhi ya mbinu zilizotumiwa katika uchanganuzi wa data, kama wanavyopendekeza Mugenda na Mugenda, (1999). Data iliainishwa na kuchanganuliwa kwa kuongozwa na nadharia mbili: Kwanza, mbinu zilizotumiwa katika uleksikalishaji wa Sheng' zilibainishwa, zikaainishwa na hatimaye zikachanganuliwa kwa mujibu wa nadharia ya Pegitosca katika sura ya tatu. Pili, kwa kuongozwa na nadharia ya 4M, mifano, ufafanuzi na majedwali yalitumiwa katika sura ya nne ili kufanya uchanganuzi wa data kwa azma ya kupambanua sifa zinazopinga upijini na ukriolishaji wa Sheng' na kubainisha mikakati ya kiwingi-lugha inayohusika katika ujenzi wa miundo yenye Sheng'.

Mifano yote yenye Sheng' iliyozalishwa na watafitiwa na ikashirikishwa katika uchanganuzi imetafsiriwa hadi Kiswahili na tafsiri yake kuandikwa kwa herufi za 'Agency FB'. Maneno ya Kiswahili yameandikwa kwa herufi za kawaida; yale ya Sheng' yameandikwa kwa herufi za mlazo (italiki) katika sentensi zenye UM. Hata hivyo, uchanganuzi na ufafanuzi wote wa data ulifanywa kwa Kiswahili katika tasnifu hii.

### 1.6.6 Maadili ya Utafiti

Mtafiti aliomba kibali cha kufanya utafiti (tazama kiambatisho 2). Vilevile, mtafiti alifuata hatua kadhaa zilizolengwa kuhakikisha kuwa maadili ya utafiti yamezingatiwa katika utafiti huu. Kwanza, mtafiti aliomba idhini kutoka kwa wakuu wa shule na watafitiwa waliombwa idhini wakati wowote kabla ya kuchunguzwa shuleni na mitaani (Mugenda na Mugenda, 1999). Pili, kama inavyojitokeza katika kazi za watafiti kama vile Bentahila na Davies (1983) na Ogechi (2002), watafitiwa walikuwa wakiarifiwa kwamba data iliyokusanywa ilikuwa ikilengwa kufanyiwa uchambuzi wa kiisimu tu. Isitoshe, mtafiti aliwahakikishia watafitiwa wake kwamba majina yao yote hayangetajwa katika tasnifu na ndivyo alivyofanya. Utafiti huu haukujihusisha na masuala yoyote ambayo yangeathiri mazingira, usalama au afya za watafitiwa.

## 1.7 Matatizo Yaliyomkabili Mtafiti

Hapo awali mtafiti alikumbwa na tatizo la kutosikika kwa baadhi ya mazungumzo yaliyonaswa. Hali hii ilitokana na hali ambamo sauti hizi zilinaswa. Wakati mwingi mazungumzo yalinaswa nje ya darasa, katika mazingira ambayo hayakuwa rasmi, kama vile wakati wa michezo na mashindano ya shule za upili ya drama na uimbaji. Wakati mwingine vilevile, watafitiwa hawakuwa wamekaribiana wakati wa kunasa mazungumzo haya, hivyo basi kuwa mbali na kinasa sauti. Aidha, kunao watafitiwa

ambao walikuwa wanaongea kwa sauti za chini mno. Hali hii ilisababisha unukuzi wa mazungumzo yao kuwa wa kutatiza.

Ili kujiepusha na matatizo haya, mtafiti aliweza kutumia vyombo vya kupaza sauti vilivyopatikana katika idara ya huduma za usikilizaji na utazamaji ya maktaba ya Margaret Thatcher, katika Chuo Kikuu cha Moi. Baadhi ya mazungumzo yaliyonaswa hayangeweza kusikika kamwe. Kwa hivyo, ilimbidi mtafiti kurudia zoezi zima la kunasa mazungumzo ya wanafunzi. Shughuli hii ilimgharimu mtafiti hela na muda zaidi, kwa kurudia kazi hii mara kwa mara.

### 1.8 Hitimisho

Sura hii imeangazia masuala ya kimsingi ya utafiti huu, yakiwemo usuli, suala, malengo, nadharia tete, umuhimu na eneo la utafiti wa sasa. Aidha sura hii imeangazia mbinu mahususi za kukusanya na kuchanganua data zilizotumiwa katika utafiti wa sasa. Uteuzi wa sampuli, upeo, vifaa vya utafiti, maadili ya utafiti kwa pamoja na matatizo yaliyomkumba mtafiti ni vipengee vingine vilivyoelezewa katika sura hii.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

## 2.0 Utangulizi

Sehemu ya kwanza ya sura hii inahakiki baadhi ya maandishi yaliyokwisha kuandikwa kuhusu mada ya utafiti yaliyofikiwa na mtafiti kabla ya na wakati wa utafiti huu. Sehemu ya pili ya sura hii inafafanua misingi ya nadharia mbili zilizomwongoza mtafiti katika ukusanyaji, unukuzi, uainishaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

## 2.1 Mapitio ya Maandishi Yanayohusu Sheng'

Mapitio ya maandishi yanayohusu Sheng' yameonyesha kuwa kuna waandishi ambao wamejikita zaidi katika kuangaza chimbuko lake huku wengine wakijihusisha na uamilifu wake. Wataalamu wachache wamechunguza Sheng' kwa mkabala wa kimuundo. Mchango wa kazi zilizoandikwa na wataalamu wengine kwa kazi hii unaangaziwa katika sehemu zifuatazo za sura hii.

### 2.1.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Chimbuko la Sheng'

Watafiti wengi wa kiisimu (Osinde, 1986; Kembo-Sure, 1992; Mbaabu, 1996; Ogechi, 2002 & 2005; Mbaabu na Nzuga, 2003; Githinji, 2006) wanasema kuwa neno Sheng' lilitokana na vianzi viwili 'Sh' na 'eng' vilivyotokana na maneno mawili 'Swahili' na 'English' vilivyoambatanishwa ili kuunda umbo moja. Wanaeleza kuwa Sheng' imetokana na uchanganyaji wa zaidi ya lugha hizi mbili kwani msamiati wake hutokana na lugha nyingi zinazozungumzwa nchini Kenya. Mbaabu anasema kuwa Sheng' iliibuka kutokana na lugha zingine nyingi, na kwamba msamiati na sarufi yake sio sahili. Kwa kiwango kikubwa Sheng' inatumia sarufi ya Kiswahili. Hali hii imepingwa

na wataalamu wengi kama vile Waihenya (1996), ambaye anasisitiza kuwa Sheng' hubadilikabadilika kila mara na haina muundo wake wa kisarufi. Kwa mtazamo wa Waihenya, watumiaji wa Sheng' huvunja sheria zote za kisarufi na anahitimisha kuwa msimbo wenyewe ni chombo sahili tu cha mawasiliano.

Momanyi (2009) anadai kuwa neno 'Sheng' ni utohozi wa maneno mawili, **S**wa**h**ili na **Eng**lish, ingawa baadhi ya msamiati unaoundwa hauchukui maneno ya Kiswahili na Kiingereza pekee. Momanyi anasema kuwa maneno mengi ya lugha za kikabila katika janibu zetu yameingizwa kwenye hazina ya msamiati wa 'Sheng' na kuifanya iwe na utata mwingi katika kupambanua mofolojia na sintaksia yake. Momanyi anakiita kilugha kwani anasema hakina utaratibu mahsusi unaofuatwa katika uundaji wa maneno, ndiposa kimesheheni utata mwingi.

Naye Ogechi (2005) anasema kuwa 'Sheng' ni lugha ya mseto iliyoibuka katika mazingira changamano ya wingi-lugha jijini Nairobi. Aghalabu inazungumzwa na vijana na hata watu wenye umri wa makamu na imezagaa katika maongezi ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika miktadha ambayo si rasmi. Kimsingi, sarufi yake ni ya Kiswahili lakini kupitia ubadilishaji msimbo, inachuma kifonolojia, kimofolojia na kisintaksia kutoka lugha zingine za Kenya zinazozungumzwa katika jiji la Nairobi kama vile Dholuo, Kikikuyu, Maasai, Luhya, na lugha za pwani kama vile Kigiriama na Kitaita. Ogechi anaongezea kuwa msimbo huu unasikika kama Kiswahili unapozungumzwa.

Mtafiti mwingine ambaye amechangia mjadala unaohusu chimbuko la Sheng' ni Githinji (2006). Kutokana na kazi yake tuliweza kugundua kuwa lengo la kukidhi haja za kimawasiliano baina ya vijana walioishi katika mitaa ya mabanda hasa kwenye vyumba vidogo vidogo zilichochea uchipukaji wa Sheng'. Githinji anaeleza kuwa

watoto na wazazi walitangamana na kuishi pamoja katika mazingira haya finyu. Hali hii ilikuwa ngumu na ilitinga uhuru wao wa kimawasiliano yaliyohitaji faragha. Ilibidi watafute msimbo wa kuzungumzia masuala yaliyowahusu kuambatana na tamaduni za kijamii (Mbaabu na Nzuga 2003). Maoni ya Githinji yanaoana na yale ya Kembo-sure (1992) anayefafanua kuwa Sheng' ilianzia katika mitaa ya mabanda kule Nairobi, ambako vijana walijitokeza na lugha ya siri dhidi ya wazazi wao. Hali hii ilichochea kuzuka kwa Sheng'.

Githinji (keshatajwa) anabainisha kwamba sababu nyingine ilikuwa ya kisaikolojia ambapo vijana walitumia Sheng' kujitambulisha kama kundi maalum lenye mitazamo tofauti na makundi mengine. Falsafa yao ya maisha ilidhihirika kupitia muziki wa kizazi kipya, mavazi mbalimbali pamoja na matumizi ya Sheng'. Sheng' iliweza kuleta umoja baina yao kama vijana na kuvunja mipaka ya kikabila kwa kuwaleta pamoja kama kundi maalum. Kundi hili lilipitia changamoto za kiuchumi kwa kukosa kazi ya maana, utajiri na madaraka katika serikali na jamii kwa jumla. Hali hii ilielezwa bayana zaidi kupitia matumizi ya Sheng' waliyoiona kama lugha yao wenyewe. Sifa hii inayohusishwa na uamilifu wa kujinasibisha vikundi kama vya vijana inaashiria upekee wa Sheng' katika utafiti huu kama msimu.

Osinde (1986) na Abdulaziz na Osinde (1997) wameeleza kuwa Sheng' ilichipuka kama lugha ya kujitambulisha ya vijana katika mashariki mwa Nairobi katika miaka ya 1970. Hapana budi kwamba Nairobi ni eneo muhimu linalohusishwa na chimbuko la Sheng' katika miaka hiyo ya sabini kwa vile watu wengi walikuwa wakitafuta kazi katika jiji kwani hakukuwa na magatuzi. Hata hivyo, kwa mtazamo wa utafiti huu, Osinde na mwenzake hawajabainisha ni kwa jinsi gani launi za Sheng' zinazozungumzwa katika maeneo mengine ya taifa zilifika kule iwapo asili yake ni Nairobi.

Spyropoulos (1987) naye anaeleza kuwa Sheng' ilitumiwa mnamo 1950 lakini ikaenea sana mnamo miaka ya sabini (karne ya ishirini). Anadokeza kuwa kile kilicho wazi ni kuwa sarufi ya Sheng' ni kama ya Kiswahili. Anabainisha kwamba msamiati wake hubadilikabadilika na neno moja la Sheng' huweza kuwa na visawe vingi (Ngesa, 2002, Ogechi, 2002). Dai hilo la Spyropoulos linalohusu 1950 halilingani na dai la Mazrui (1995) na Mazrui na Mphande (1990) wanaosema kuwa Sheng' ilikuweko kule Nairobi katika miaka ya 1930 na ilitumiwa baina ya wezi wa mfukoni. Madai ya Spyropoulos kwamba sarufi ya Sheng' hufanana na sarufi ya Kiswahili yalichochea haja ya kufanywa kwa uchunguzi huu ili kubainisha kulingana na lengo la pili la utafiti iwapo Sheng' ni 'lugha' (Krioli) yenye mfumo wake wa kisarufi unaofanana tu na wa Kiswahili au 'si lugha'.

Kwa maelezo ya Momanyi (2000), vijana ndio wanaohusika katika ujenzi na uendelezaji wa Sheng' hapa nchini Kenya. Wao huona fahari kubwa wanapozungumza Sheng'. Wengi wao hawawezi kujieleza katika lugha zao za kiasili, Kiswahili sanifu wala Kiingereza bila kupenyeza maneno ya Sheng'. Maoni haya ya Momanyi yanaungwa mkono na Mbaabu na Nzuga (2003) wanaoashiria kuwa, miongoni mwa vijana, Sheng' ni lugha ya kujitambulisha. Hata hivyo, tasnifu hii inasisitiza kwamba ufafanuzi wa wazungumzaji wa Sheng' uliofanywa na Momanyi unaowaashiria kama watu wasioweza kumudu au kujieleza kwa lugha zingine unapaswa kuthibitishwa kwa kutumia data halisi. Hii ni kwa sababu unawaweka wazungumzaji katika kategoria ya wanaunusu-lugha ambao hawana umilisi wa lugha zote wanazozijua ilihali baadhi ya wazungumzaji wa Sheng' wana umilisi wa Kiswahili na/au Kiingereza na lugha za kiasili.

Wakichangia mjadala unaohusu chimbuko la Sheng', Abdulaziz na Osinde (1997) wanaeleza kwamba hapo awali msimbo wa Sheng' ulikuwa ukitumiwa na vijana jijini Nairobi lakini kwa sasa unatumiwa kote nchini katika mazingira mbalimbali yenye mtagusano wa lugha na utamaduni. Kwa mtazamo wao, Sheng' ni dhihirisho la uchangamano wa lugha uliomo majijini kama vile Nairobi, Kisumu na Mombasa na katika miji mingine mikubwa kama vile Eldoret na Nakuru. Katika maeneo hayo Kiswahili, Kiingereza na lugha za kiasili hutumiwa kwa njia changamani na isiyo thabiti. Mazao ya hali kama hii ni ubadilishaji msimbo, uchanganyaji msimbo usiokuwa na utaratibu maalum na uhamishaji lugha.

Addulaziz na Osinde (keshatajwa) wanaongezea kuwa vijana humu nchini Kenya hutoka katika jamii mbalimbali na hubuni msimbo wa Sheng' ili uwawezeshe kuwasiliana wenyewe kwa wenyewe katika jamii ndogondogo wanazounda. Hili linamaanisha kuwa msimbo wa Sheng' unaozungumzwa na jumuiya fulani ya vijana hutegemea eneo la kijiografia na jamii wanamotoka. Kwa mfano, iwapo eneo fulani lina wazungumzaji wengi wa Kikikuyu au Dholuo, basi aina ya Sheng' inayozungumzwa itakuwa na asilimia kubwa ya maneno ya Kikikuyu au Dholuo. Ingawa hatukulenga katika utafiti huu kuchunguza takwimu zinazohusu kiwango ambacho lugha zingine hushiriki, imebainika pakubwa kwamba mkuku wa kimofosintaksia unaotumiwa katika Sheng' unahusiana na ule wa Kiswahili ila tu mofu zinachopekwa kutoka lugha mbalimbali.

### 2.1.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Uamilifu wa Sheng'

Wataalamu wengi waliochunguza Sheng' wamebainisha matumizi tofauti tofauti ya msimbo wenyewe. Wao wamehitimisha kuwa Sheng' ni msimbo unaotumiwa na vijana kwa uamilifu wa kuficha siri katika mawasiliano miongoni kwa sababu nyinginezo.

Wao ni pamoja na Abdulaziz na Osinde (1997), Mbaabu na Nzuga (2003), Mazrui (1995), Kingei (2001), Kiessling na Mous (2001) na Ogechi (2002, 2005, 2008) Kupitia uchunguzi wao wa Sheng' wamebainisha matumizi kadha wa kadha ya msimbo wenyewe. Maandishi yao yanayohakikiwa katika aya zifuatazo za sura hii yalifaa kwa utafiti huu kwa kubainisha baadhi ya sifa zilizofaa kwa uchanganuzi wa sifa za Sheng' katika tasnifu hii ili kujibu swali linalohitaji kuthibitisha au kupinga upijini wake.

Mintarafu ya Momanyi (2009), wazungumzaji wa sasa wa Sheng' ni vijana ambao wana uwezo wa kuzungumza Kiswahili vyema lakini ambao hukaidi kanuni za lugha hii na kubuni msimbo wao kwa ajili ya kujitambulisha na wenzao. Kwa mtazamo wake, waliopitia mfumo wa elimu wa nane, nne, nne (8:4:4) ambao uliweka Kiswahili kuwa somo la lazima ndio wanaotumia Sheng' kwa kiwango kikubwa zaidi. Kuhusu uamilifu wa Sheng, Momanyi anadahili kuwa ni muhimu kukumbuka kuwa, mara nyingi, misimbo kama Sheng' isiyokubalika katika miktadha rasmi hutumiwa kutambulisha makundi fulani ya kijamii. Hii ni kwa sababu mmoja wao anapoweza kuzungumza msimbo huu vizuri hupata hadhi miongoni mwa wanachama wa kikundi chake. Hali hii hufungia watu wasio wa kikundi hiki nje na kuwapa wanachama utambulisho wa kipekee. Msimbo huu hutumiwa na wanafunzi wa shule za msingi na za sekondari katika mawasiliano yao yasiyo rasmi. Msimbo wa Sheng' sasa unatawala diskosi miongoni mwa wachuuzi wa bidhaa, madereva na utingo wa magari ya usafiri, watoto wa mitaani na hata wafanyi biashara wadogo katika soko zetu. Kulingana na lengo la pili la utafiti huu, ugunduzi wa Momanyi kuhusu muktadha ambamo Sheng' hutumiwa ulikuwa muhimu kuhusiana na sifa zinazopinga ukriolishaji wake. Hii ni kwa vile Pijini ambayo inaimarika kuwa Krioli haitarajiwi kutumika katika miktadha finyu tu kwa uamilifu maalum pekee ila huendelea kustawishwa kiuamilifu ili itekeleze dhima

nyingi katika mawanda mapana kadiri inapotumika. Uchunguzi huu ulithibitisha pia kuwepo kwa ufinyu huo wa kiuamilifu.

Sifa moja ya Sheng' ipo kwenye idadi ya maneno yanayotumiwa kurejelea kitu kimoja. Mfano mzuri ni ule wa maneno yanayotumiwa kurejelea 'Msichana'. Mbaabu na Nzuga (2003) wanadahili kuwa kuna maneno zaidi ya thelathini yanayorejelea msichana katika launi hiyo ya lugha. Wnataja vilevile zaidi ya maneno ishirini yanayorejelea polisi, zaidi ya kumi ya kurejelea kahaba na zaidi ya ishirini kurejelea bangi. Maneno haya ni mengi hivyo kwa sababu ni njia moja ya kuweka siri, kwani jina moja linapojulikana na watu nje ya watumiaji wa neno hilo, neno jipya hutungwa, ingawa lile la awali halitupiliwi mbali mara hiyo hiyo. Mbaabu na Nzuga wanasema kuwa maneno ambayo hupatikana katika kikundi hiki ni kama ya mvinyo, mihadarati, uhusiano wa kimapenzi baina ya vijana na ngono. Maneno haya hutumiwa, mara nyingi, kuonya wenzao kuhusu hatari inayoweza kutokea wakati huo, kwa hivyo haja ya kuwa na maneno ishirini kurejelea polisi.

Akizungumzia sifa za Sheng' zinazofungamana na uamilifu wake, Ogechi (2002) anaonyesha kuwa punde tu neno la Sheng' linapojulikana kwa watu wengine na kutumiwa nao, linapoteza umuhimu wake na lingine huundwa mara moja. Neno jipya huweza kuundwa kwa kulifupisha neno asili au kwa kuzigeuza sauti zake. Mathalani, maneno kama vile *banana, malaika, manyanga, manyake, kirenge, chikii na chikoo* yanamyorejelea 'msichana' ni mifano ya Sheng' inayochukua mwelekeo huo. Neno '*manyake'* limeundwa kwa kulifupisha na kuzigeuza sauti za neno '*manyanga'*. Huenda neno '*manyanga'* lilikuwa limejulikana kwa watu wengi ndiposa wazungumzaji wa Sheng' wakalibuni lingine *'manyake'* ili kuwasilisha maana ile ile lakini kwa kutumia umbo tofauti. Uchunguzi wetu uligundua kuwa sifa hii inaidhihirisha Sheng' kama

msimu huku ikipinga ukriolishaji wake. Ugunduzi wa tasnifu hii ni kwamba sifa hii ya kubadilishabadilisha msamiati si kibainishi cha Pijini, Krioli wala lugha.

### 2.1.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Muundo wa Sheng'

Kazi ya Ogechi (2002) inadhihirisha kuwa sintaksia ya Sheng' ni kama ile ya Kiswahili, ambayo ni lugha ya kibantu. Inaonyesha pia kwamba asili ya msamiati ni lugha zinazozungumzwa nchini Kenya. Aghalabu maneno mengi ya Sheng' ni yale yaliyokopwa kutoka lugha za kiasili kuliko lugha za kigeni kama vile Kiingereza.

Kulingana na Mbaabu (2002), utamaduni wa jamii, elimu ya jamii aina ya kazi au ajira inayofanywa na wazungumzaji wa Sheng' ni baadhi ya mambo yanayoathiri aina ya Sheng' inayozungumzwa. Kwa mujibu wa mwanaisimu huyu, kuna maneno ambayo hayatasikika katika kikundi kimoja cha wazungumzaji wa Sheng' lakini yanatumika katika kikundi kingine. Anaeleza kwamba kuna maneno ambayo matumizi yao yamejikita katika miktadha ya vijana shuleni kama vile majina ya shule. Kazi ya Mbaabu inaonyesha kuwa maneno yanayotumiwa na vijana au wanafunzi mara nyingi ni yale yanayohusiana moja kwa moja na maisha yao shuleni au nyumbani. Kwa mfano:

Chapati na sasa *chapo*
Chips na sasa *chibaz*
Mbaabu (2002:175)

Mbaabu (keshatajwa) anaendelea kudai kuwa katika vyuo vikuu msamiati wa Sheng' huwa umenogezwa kielimu. Hata hivyo, anabainisha kuwa wakati mwingine msamiati wa shule za Sekondari hubebwa na kuendelea kutumiwa katika vyuo vikuu. Mbaabu anaonyesha vilevile kuwa kuna seti ya maneno ya Sheng' inayohusiana na uchumi. Seti hiyo ya maneno hutumiwa sana miongoni mwa vijana ambao wanashiriki katika shughuli za kibiashara.

Anataja mifano kama:

| | | | |
|---|---|---|---|
| a) | Pesa | - | Chapaa, mango, nyandu |
| b) | Shilingi tano | - | Kobole, ngovo |
| c) | Shilingi kumi | - | Ashu |
| | | | Mbaabu (2002:175) |

Kutokana na maoni haya ya Mbaabu (keshatajwa), tunaona kuwa aina za Sheng' kwa kutegemea aina ya wazungumzaji. Inajitokeza kuwa Sheng' inayozungumzwa na watoto ni tofauti na ile inayotumiwa na vijana wanaofanya kazi. Vilevile kazi hiyo imebainisha kuwa Sheng' inayotumiwa mjini ni tofauti na ile inayotumiwa mashinani. Hii ilimaanisha kuwa aina ya Sheng' inayozungumzwa hutegemea mazingira na aina ya wazungumzaji. Ugunduzi huo wa Mbaabu ulituongoza katika uteuzi wa sampuli ya shule na mitaa ya utafiti ndiposa tuweze kupata data kutoka kwa miktadha yenye uwakilishaji ufaao.

Aghalabu maneno ya Sheng' hufuata mofosintaksia ya Kiswahili pale yanapotumiwa ili kuunda sentensi. Hata hivyo, kwa maelezo ya Mbaabu na Nzuga (2003:123), Sheng' haifuati sheria za kimofolojia za Kiswahili kila mara. Wataalamu hawa wametoa mifano ya maneno mawili ya Sheng' *'mbao'* na '*mabao'*. Wanaonyesha kuwa kwamba '*mabao'* si wingi wa '*mbao*'. Wanabainisha kuwa neno '*mbao'* katika Sheng' lina maana ya 'shilingi ishirini' ilhali '*mabao'* lina maana ya 'njaa'. Mfano mwingine walioutoa ni '*sanya'*. Neno hilo lina maana ya 'kuiba' katika Sheng'. Sheria za kimofolojia za Kiswahili zinaruhusu kunyambuliwa kwa umbo hilo kuwa *'sanywa'* kwa maana ya 'kuibwa'. Kwa upande mwingine, katika Sheng', neno '*sanywa'* lina maana tofauti kabisa ambayo ni 'kulewa chopi'. Katika maneno mengi ya Sheng', mnyambuliko wake hauleti maana kwa namna sawa na inavyofanyika katika Kiswahili ila inaweza kubadilikabadilika. Hata hivyo, utafiti wetu ulionyesha kuwa dhana ya

'njaa' haikuwa ikirejelewa kama '*mabao'* na watafitiwa wetu ila kama '*maubao'*. Huenda umbo la Sheng' '*mabao'* lililoripotiwa na Mbaabu na mwenzake ama lilikuwa limetamkwa vibaya katika utafiti wao au lilikuwa linatumika tu katika eneo walilofanyia utafiti.

Baadhi ya maneno ya Sheng' yanatofautiana sana na ya Kiswahili hasa katika matumizi ya viambishi awali. Mbaabu na Nzuga (2003:124) wanatoa mfano wa '*buda'*, neno la Sheng' lililo na maana ya 'baba' na neno '*kabuda'* ambalo lingetarajiwa kumaanisha 'baba mdogo' lakini kisemantiki kipashio 'ka-' katika Sheng' hakibebi dhana ya udunishaji tofauti na ilivyo katika lugha za kibantu. Umbo hili '*kabuda'* katika Sheng' ni neno la kawaida lililo na maana ya mwanamume yeyote ambaye ni wa umri unaokaribiana na wa babake mzungumzaji. Tofauti na ilivyo katika Kiswahili, kuna nomino za pekee zinazotaja watu katika Sheng' ambazo hazina hali ya umoja. Kwa mfano, neno '*ndito'* lililo na maana ya 'wasichana' halina hali ya umoja inayomrejelea 'msichana'. Mbaabu na mwenzake kwa fahiwa hii walikuwa wakilinganisha miundo ya maneno Sheng' na Kiswahili walakini utafiti huu ulilenga kuchunguza mbinu za uleksikalishaji zinazowezesha kuzalishwa kwa maneno yenyewe.

Hata hivyo, Mbaabu na Nzuga (keshatajwa) wanaashiria kuwa kuna hali ambazo zinadhihirisha uhusiano uliopo baina ya Sheng' na Kiswahili. Wanatoa mfano wa neno la Sheng' '*gondi*' kuiba. Kuiba ni '*kugondi'*. Hapa kiambishi awali *ku-* kimetumiwa vile kinavyotumiwa katika Kiswahili. Kupitia mnyambuliko wa neno hilo, mwizi atakuwa '*mgondi'* na wingi wake utakuwa '*wagondi'*. Vilevile, wanatoa mfano mwingine, ambao ni wa neno la Sheng' '*soo'* linalorejelea 'mia moja' na lingine '*kobole'* linalomaanisha 'tano'. Wazungumzaji wa Sheng' huunganisha maneno haya mawili ili kuibuka na '*soo kobole'* kwa maana ya 'mia tano'.

### 2.1.4 Yaliyoandikwa Kuhusu Athari za Sheng'

Maandishi mengi yameandikwa kuhusu athari za Sheng' kwa ujifunzaji au ufundishaji wa lugha rasmi. Githinji (2013) anaeleza kwamba matumizi ya Sheng' miongoni mwa wanafunzi yameshutumiwa kila mwaka na viongozi wa elimu kama mojawapo ya sababu kuu zinazoleta matokeo yasiyoridhisha katika mitihani ya Lugha hasa Kiswahili katika KCSE na KCPE.

Kioni (2002) anaeleza kwamba walimu wengi wanalalamika kuhusu kuongezeka kwa matumizi ya msamiati wa Sheng' na kukiukwa kwa kaida za sarufi katika insha za wanafunzi. Anaashiria kuwa Sheng' inaathiri vibaya matokeo ya wanafunzi katika mitihani ya masomo ya lugha. Kioni anasisitiza kuwa ipo haja ya kushugulikia suala la Sheng' kwa dharura kwani imeathiri pakubwa ujifunzaji na ujifundishaji wa masomo ya lugha.

Mara nyingi Kiswahili inapotumiwa katika mawasiliano mijini na hata mashambani, msamiati wa Sheng' hupenyezwa. Kioni (keshatajwa) anabainisha kwamba vijana hupendelea sana kutumia msamiati wa Sheng' badala ya maneno ya Kiswahili pale wanapowasiliana wenyewe kwa wenyewe. Wao huuzoea msamiati huo na hatimaye wanajipata wameutumia darasani na hata katika mazungumzo yao ya kawaida. Kioni anaongezea kuwa hali hii ni hatari mno, kwa maana msamiati wa Sheng' hupenyezwa hata katika mitihani ya kitaifa. Kioni anasisitiza kwamba vijana wengi hufanya makosa mengi ya kisarufi na hatimaye wakafanya vibaya katika ujifunzaji wa lugha kwa vile wanasahau kuwa Sheng' hupaswa kutumiwa tu katika mawasiliano yao pekee na kuitumia katika miktadha rasmi.

Kioni, ambaye ameshatajwa, akiwa mwalimu wa somo la Kiswahili aliyestaafu anachangia kwamba Sheng' ina athari kubwa kwa masomo ya lugha, hasa Kiswahili. Anasema kuwa wanafunzi wake walikuwa na makosa mengi ya kisarufi katika mazungumzo na maandishi yao ya Kiswahili. Kioni anatoa mifano ya makosa kama vile *tunaendaga* badala ya huenda, *chezanga* badala ya hucheza na *gishagi* badala ya mashambani. Kioni anaendelea kusema kuwa ni vigumu sana kuthibitishia mwanafunzi kuwa neno walilotumia la Sheng' si sawa kisarufi, kwani hawaelewi kuwa Sheng' si Kiswahili sanifu. Anasema kuwa hata baada ya mwanafunzi kuelewa, utapata ametumia maneno haya katika maandishi yake ya Kiswahili. Kwa upande mwingine, Kioni anaeleza kuwa tatizo hili linaweza kutatuliwa. Yeye anapendekeza kule kusisitizwa kwa mafundisho ya lugha sanifu shuleni ili wanafunzi waweze kujua tofauti kati ya Sheng' na Kiswahili.

Momanyi (2009) ana maoni sawia na haya. Yaye anadahili kuwa Sheng' huathiri vibaya ujifunzaji rasmi wa lugha darasani. Momanyi anasema kuwa hali hii hutokea kwa sababu wanafunzi hushindwa kutofautisha baina ya Kiswahili sanifu na lugha yao ya mawasiliano. Anaendelea kusema kuwa walimu wengi wamegundua kuwa wanafunzi wengi wana uwezo wa kujieleza vyema katika Sheng' kuliko Kiswahili sanifu. Mbali na haya, Momanyi anasema kuwa unyanyapaa unaoandamana na Sheng' umefanya watu wengi wasitake kuhusishwa na Sheng', kwani mara nyingi Sheng' huhusishwa na utingo wa gari za usafiri, walanguzi wa mihadarati, wanamuziki wa fokafoka na vijana walioacha shule. Anasema kuwa katika ulingo wa elimu Sheng' ni msimu wa kijambazi ; msimbo wa siri unaohusishwa na wakora na usioeleweka kwa urahisi. Watu wazima wengi hawaelewi Sheng' na baadhi ya wazazi wa watoto wanaoenda shuleni wangependelea msimbo huu upigwe marufuku kwa sababu unaleta mgongano kati ya vijana na wazazi au watu wazima, na pia unaleta kiwewe katika familia na darasani.

Hata hivyo, Momanyi anadahili kuwa itakuwa vigumu kuondoa Sheng' miongoni mwetu kwani, kama njia nyingine yoyote ya mawasiliano, ina wazungumzaji wake ambao huipa uhai na kuiendeleza.

Akifafanua kuhusu matumizi ya Sheng' katika vyombo vya habari, Momanyi (keshatajwa) anayaunga mkono madai ya Mlacha (1995) na Kimei (1973) kwamba vyombo vya habari vina nafasi kubwa ya kuwafikia mamilioni ya watu kwa wakati mmoja na hivyo kuiendeleza lugha. Wataalamu hawa wana haki ya kudai kuwa vyombo vya habari vina uwezo mkubwa sana wa kuendeleza au kuharibu lugha, Kimei anaonya kuwa ni muhimu daima tahadhari ichukuliwe katika matumizi ya Kiswahili kwenye vyombo vya habari. Tahadhari hii ni pamoja na kutotumia Sheng' katika upeperushaji wa habari na matangazo ya idhaa kwa taifa.

Mohochi (2000) naye anadahili kuwa kinachochangia Sheng' kuendelea ni stesheni zetu za televisheni na redio ambazo zimetoa nafasi kubwa kwa msimbo wa Sheng', ambapo vipindi mahsusi hutumia msimbo huu. Anaendelea kusema kuwa vipindi kama hivi vina athari za milele za kiisimu kwa watoto wanaoenda shule na vijana. Hii ni kwa vile baadhi yao hupenda kujitambulisha na wahusika fulani katika vipindi hivyo wanaotumia msimbo huo. Mohochi anaeleza makosa yanayojitokeza katika vyombo vya habari hasa pale Kiswahili inapotumiwa. Miongoni mwa makosa anayotaja ni matumizi ya Sheng' ambayo husikika katika vipindi kadha wa kadha. Mohochi anasema kuwa utamsikia mtu akisema, katika muktadha rasmi kwamba *"Yule mzee alipigwa ngeta".* Analalama kuwa Sheng' inapoingizwa katika matumizi rasmi ya lugha yanakuwa makosa makubwa. Ugunduzi wa Mohochi unaashiria hasara za vyombo vya habari kwa ustawi wa Kiswahili. Utafiti wetu ulihusiana na kazi ya Momanyi, Mlacha, Kimei na Mohochi katika uchunguzi wao wa vijana huku

ukitofautiana nao kwa misingi ya kutojihusisha na sampuli ya watoto wala athari za vyombo vya habari zinazohusiana na matumizi ya Sheng'.

Waihenya (1996) anapinga matumizi ya Sheng' akisema kuwa hiki ni kilugha kisichokuwa na mfumo kamili wa kisarufi, utaratibu wa Kiisimu na msamiati wake hubadilikabadilika kila uchao. Waihenya analalama kuwa Sheng' ni kilugha ambacho hutumiwa tu kwa mawasiliano rahisi na iliyo huria. Kwa mtazamo wake, wanaotumia kilugha hiki huvunja sheria zote za miundo ya kiisimu pamoja na za usarufi. Anasema kuwa yeyote anayetafuta njia ya kuwasiliana kwa urahisi huchanganya na kuzichachawiza Kiingereza, Kiswahili na lugha za kiasili. Waihenya anaeleza kuwa tatizo lingine la Sheng' ni kwamba kilugha chenyewe hutumiwa na kikundi fulani cha watu ili kujitambulisha. Anadokeza kwamba vijana wengi hutupilia mbali ile haja ya kujifunza Kiswahili sanifu pindi wanapojiingiza katika kikundi kinachozungumza Sheng'. Anaashiria tena kwamba kwa vile Sheng' hubalikabadilika kila mara, mwelekeo wake ni ule wa kuzidisha msamiati wake kila dakika. Waihenya anaona haya kuwa matatizo makubwa sana katika ujifunzaji na ufundishaji wa lugha. Ufafanuzi wa Waihenya uliashiria kwamba uundaji wa msamiati hufanywa katika Sheng' lakini mbinu zinazotumika katika uundwaji huo hazijafafanuliwa. Kwa sababu hiyo, mbinu hizo zimechunguzwa, zikachanganuliwa na kufafanuliwa katika tasnifu hii ili kujibu lengo la kwanza la utafiti huu.

Mtaalamu mwingine anayetoa tetezi kuhusu Sheng' ni King'ei (2000). Anaeleza kuwa Sheng' ambayo ni mkusanyiko wa Kiingereza, Kiswahili na lugha za kiasili unapendelewa sana na vijana ambapo wengi wao huwa ni wanafunzi wa shule za Sekondari. Kazi ya King'ei inaonyesha kuwa lugha isiyokuwa sahihi ni kizingiti kikubwa kwa ufundishaji wa masomo ya Sayansi na mengineyo. Inaonyesha tena kuwa

mwanafunzi asiyeweza kujieleza vyema akitumia lugha sahihi huanguka mitihani ya kitaifa. Utafiti huu unatofautiana na kazi ya King'ei inayopinga mno matumizi ya Sheng' baina ya wanafunzi. Hii ni kwa vile utafiti huu hautoi hitimisho linalounga mkono au linapinga matumizi ya Sheng' ila ulilenga kufafanua Sheng' jinsi ilivyo tu vile inavyohitajika kwa tafiti za kiisimu. Utafiti huu kwa sababu hiyo haukulenga kuchunguza ubaya au uzuri wa Sheng' ila umechangia kuweka wazi sifa za Sheng' kama Msimu kwa maana ni wa Kiisimu fafanuzi.

Amisi (keshatajwa) anasisitiza kuwa Sheng' huathiri mno ujifunzaji wa Kiswahili, hivyo husababisha matokeo mabaya ya wanafunzi katika Kiswahili. Amisi anasema kuwa kuenea kwa maneno ya Sheng' kumekuwa kizingiti kikubwa katika juhudi za mwalimu za kufundisha lugha. Anasema kuwa Sheng' imekuwa adui mkubwa wa watumiaji wa lugha. Anaashiria vilevile kwamba Sheng' imefanya ufundishaji wa Kiswahili na Kiingereza kuwa kazi ngumu sana. Ingawa ubainishaji wa Amisi kuhusu namna Sheng' inavyojitokeza kama kizingiti kwa elimu ni muhimu, hakubainisha iwapo Sheng' ni lahaja ya Kiswahili au launi iliyotokana na Pijini. Amisi anadahili kuwa upataji wa lugha yoyote ile hutegemea namna yule anayejifunza anafanya mazoezi ya kuitumia. Hali hii inaendelea kubadilika kwani wanafunzi wengi wamezama katika ujifunzaji wa Sheng' badala ya Kiswahili na Kiingereza. Mazoezi wanayofanya mengi ni ya Sheng', hivyo basi hali hii imeathiri ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili. Mipaka ya utafiti huu, tofauti na kazi ya Amisi, haikufikia athari za msimbo wa Sheng' kwa lugha ila ulijikita katika uleksikalishaji wake na mikakati ya kiwingi-lugha inayohusika katika matumizi yake.

Sheng' imekuwa tatizo kubwa kwa wanafunzi wa shule za upili. Amisi anadai kuwa mwanafunzi hawezi kupata stadi zote za lugha ya Kiswahili bila muundo-msingi bora

wa lugha yenyewe. Anasema kuwa ni muhimu wanafunzi wajitahidi katika kusikiliza kuzungumza, kusoma na kuandika kwa wingi lugha wanayofunzwa shuleni, ili wapate sheria, sarufi, mazungumzo na kuandika vyema lugha yenyewe. Hivi wanafunzi wataweza kujiepusha na zile athari mbaya zinazotokana na Sheng' na lugha ya mama.

Nyagaka (1995) anapuuza Sheng' na kusema kuwa Sheng' sio lugha kamili, bali ni kilugha tu cha kujitambulisha na kikundi fulani cha watu katika jamii. Nyagaka anasikitika kuwa mbali na Sheng' kupenyezwa katika mazungumzo ya kila siku, imeenea vilevile katika maandishi, na hii ni aibu kubwa. Nyagaka anasema kuwa sifa za Sheng' yaani lafudhi, toni, ishara na hata jinsi ilivyoundwa zinachukiza. Nyagaka analalama kuwa mzungumzaji wa Sheng' hawezi kuzungumza Kiswahili wala Kiingereza vizuri. Wakati mwingi hali hii hutokea kwa ajili za wazungumzaji wa Sheng' kutaka kujitambulisha na kikundi cha wazungumzaji wengine wa Sheng'. Msikitiko wa mtafiti kama Nyagaka kuhusiana na matumizi ya Sheng' huweza kuondoa uyakinifu katika uchunguzi na ufafanuzi wa miundo na maumbo ya Sheng'. Ili kudumisha uyakinifu, utafiti huu kwa upande wake haukufanywa kwa lengo la kupinga au kuunga mkono matumizi ya Sheng'.

Naye Kimei (1997) anawaunga mkono wataalamu wengine walioteta kuhusu Sheng' akisema kuwa Sheng' ni tisho kubwa kwa lugha za Kiingereza na Kiswahili. Kimei anadahili kuwa Kenya ilidhihirisha matumizi ya Kiswahili na Kiingereza kama lugha faafu za mawasiliano katika shughuli rasmi kama elimu. Hata hivyo, katika shule za upili lugha hizi zinashindana na Sheng'. Kwa sababu hii, matumizi ya Kiswahili na Kiingereza yamedhoofishwa na Sheng'! Akilinganisha hali ya lugha nchini na jinsi wanafunzi walivyozamia Sheng', Kimei (1997:12) amemnukuu Socrates aliyesema;

> Filosofia inasema kuwa walimu hutenda kazi yao kama wakunga; wao husaidia wanafunzi wao kuyapanga mawazo yao na kuyaeleza kwa njia yenye mantiki. (Tafsiri Yetu).

Naye Obbo (2006) analalamika kuwa Sheng' inaenea upesi sana na kutumiwa Afrika mashariki kote, hata katika mtandao. Kwa mujibu wa Obbo, matumizi ya Sheng' kwenye mtandao utaeneza Sheng' hata zaidi, huku idadi ya watu wanaoitumia ikipanda na hata kuwa ya juu kuliko watumiaji wa Kiswahili sanifu. Obbo anasema kuwa matumizi ya Sheng' yanashusha hadhi ya wenyeji wa Afrika Mashariki kwani ni kilugha kinachoathiri vibaya utamaduni wa watu wa Afrika Mashariki.

Alipokuwa akitangaza rasmi matokeo ya mtihani wa kitaifa wa darasa la nane mwaka wa 2011 (KCPE), Waziri wa Elimu wakati huo, Profesa Sam Ongeri alitoa tetesi kuwa watahiniwa hawakufuzu vyema ilivyotarajiwa katika masomo ya Kiswahili na Kiingereza. Waziri alilalamika kuwa kutofanya vyema katika masomo haya ya lugha kulisababishwa na athari zinazotokana na matumizi ya kilugha cha Sheng'. Alisema kuwa watahiniwa kutoka shule za mashambani walipata alama za juu kuliko wenzao wa shule za mjini, ambako matumizi ya Sheng' yametanda. Waziri Ongeri aliwalaumu watu wanaotajika katika jamii wakiwemo wanasiasa ambao hutumia Sheng' ili kuwavutia vijana. Waziri hakulalamikia tu matokeo ya mtihani wa K.C.P.E bali alilaumu Sheng' kwa nafasi mbaya ambayo taifa la Kenya lilipewa katika mashindano ya ubora wa elimu katika bara la Afrika, ya *African Consortium for Monitoring Educational Quality* (SACMEQ). Kenya ilichukua nafasi ya tano katika mashindano ya kujua kusoma na kuandika ilhali katika isibati, ilichukua nafasi ya pili. Kwa mujibu wa Ongeri, nafasi ya nyuma katika kujua kusoma na kuandika inasababishwa na matumizi ya Sheng' baina ya watu wanaotajika katika jamii, ambao wanafunzi huishia kuiga mienendo yao. Ongeri anaonya kuwa tabia kama hii hurudisha kiwango cha elimu

chini na akawataka viongozi na washikadau katika kushughulikia suala hili (Orengo na Opiyo, 2011).

### 2.1.5 Yaliyoandikwa kuhusu Tipolojia ya Sheng'

Sehemu hii inaangazia maandishi yanayojaribu kufafanua Sheng' kitipolojia. Maandishi yenyewe yanapingana na yanashirikisha yale yanayoainisha msimbo wa Sheng' katika kategoria ya ubadilishaji msimbo, ya lugha, ya lahaja, ya lugha mahuluti, ya Pijini na hata Krioli.

**Kwanza**, kuna baadhi ya watafiti ambao wameainisha, wakachunguza na wakafafanua **Sheng' kama Ubadilishaji Msimbo.** Wao wanadai kuwa Sheng' ni launi inayotokana na ubadilishaji msimbo baina ya Kiswahili na Kiingereza. Mtazamo huu unadokeza kuwa viambajengo vinavyojenga miundo ya Sheng' hutoka Kiswahili na Kiingereza. Kwa mfano, Mazrui (1995), ambaye anaainisha Sheng' kama aina moja ya ubadilishaji msimbo anaashiria kwamba Sheng' hutumia miundo ya kimofosintaksia ya Kiswahili. Uhakiki wa mtafiti ulionyesha kuwa mifano iliyotumiwa na Mazrui (1995:176) ili kuiainisha Sheng' katika tipolojia ya ubadilishaji msimbo ambayo ni *ali-relax*, *ali-come* na *ime-elapse* yalikuwa na dosari. Sababu iliyomfanya Mazrui achukulie kuwa mifano hiyo inaonyesha Sheng' kama ubadilishaji msimbo wala sio ubadilishaji msimbo baina ya Kiswahili na Kiingereza si wazi. Hii ni kwa vile, uchunguzi wetu wa maandishi na usemi wa watafitiwa wetu ulionyesha kuwa maumbo ya Sheng' yanawakilishwa kama *'alikam', alinishoo',* na *'alirilaks'* wala sio 'alicome', 'alinishow' na 'alirelax' kama ilivyowakilishwa na Mazrui. Kwa kutegemea uchanganuzi wa data uliofanywa katika utafiti huu, tasnifu hii inadadisi kwamba miundo ya Sheng' ingewasilishwa kama 'alicome', 'alinishow' na 'alirelax', basi ingethibitisha kwamba Sheng' ni ubadilishaji msimbo hali ambayo inapingwa na

matokeo ya utafiti huu. Kwa mtazamo wa tasnifu hii, madai kuwa Sheng' ni ubadilishaji msimbo yana dosari inayohusiana na ubainishaji wa ni lini mgotanisho baina ya lugha kama Kiswahili, Kiingereza na hata lugha za kiasili utaweza kurejelewa kama Sheng' na ni lini utaweza kurejelewa kama ubadilishaji msimbo mtupu.

Msomi mwingine anayeunga mkono tipolojia inayodai kwamba Sheng' ni aina ya ubadilishaji msimbo ni Bosire (2006). Anafafanua kwamba Sheng' huundwa kwa kuweka pamoja vipengele mbalimbali kutoka lugha anuwai. Kwa misingi hiyo, anadai kuwa Sheng' ni mfano tu wa ubadilishaji msimbo. Ndiposa Bosire aweze kudai hivyo, alichukulia kwamba wazungumzaji wa msimbo huu ni wazungumzaji wa lugha zote zinazohusika, walakini, baadhi ya maneno ya Sheng' yametoka kwa lugha za kiasili ambazo baadhi ya wazungumzaji wa Sheng' hata hawazijui. Madai haya yalichangia kujenga suala la utafiti huu na malengo yetu. Mtazamo huo wa akina Bosire na Mazrui kwamba Sheng' ni aina moja tu ya msimbo unaochanganya lugha inatofautiana na mtazamo unaodai kuwa Sheng' ni lahaja.

**Pili**, kuna mtazamo unaochukuliwa kwamba **Sheng' ni lahaja ya Kiswahili au hata lahaja ya vijana** (Githiora, 2002). Tofauti na lahaja nyingine za kimaeneo, Sheng' haina mipaka ya kijiografia. Wazungumzaji wa Sheng' wametawanyika katika miji mingi nchini Kenya. Ndiposa Sheng' ichukuliwe kama lahaja pia, upatanisho wa kisarufi unaozingatiwa katika Kiswahili unapaswa kufuatwa katika msimbo wenyewe. Haya yanadhihirika katika jedwali 2.1 lifuatalo ambapo viambishi vinavyotumiwa katika sentensi za Kiswahili vinadhihirisha upatanisho wa kisarufi lakini vile vinavyotumika katika sentensi za Sheng' havidhihirishi upatanisho. Kwa mfano, nomino 'mbwa' katika Kiswahili huchukua viambishi tofauti katika Sheng', kama inavyoonyeshwa katika jedwali 2.1 lifuatalo;

**Jedwali 2.1: Sifa ya Upatanisho**

| | **Kiswahili** | **Sheng'** |
|---|---|---|
| 1 | Mbwa alibweka | Mbwa *ilibweka* |
| 2 | Mbwa walibweka | Mbwa *zilibweka* |
| 3 | Kiatu changu ni kizuri | Kiatu *yangu* ni *mzuri* |
| 4 | Vyatu vyangu ni vizuri | Vyatu *zangu* ni *nzuri* |

Kwa kuzingatia sifa hizi za upatanisho [zilizotumiwa ili kudai kuwa Sheng' ni lahaja ya Kiswahili] zinazoonekana katika Jedwali 2.1, tasnifu hii imehitimisha kuwa Sheng' si lahaja ya Kiswahili kwa sababu lahaja za Kiswahili hudhihirisha sifa sawa za upatanisho kinyume na inavyofanywa katika Sheng'. Aidha, lahaja zote za Kiswahili huzingatia upatanishi sawa hasa katika ngeli 1 na 2 (A-WA). Isitoshe, kila lahaja ina lugha mame ambayo ina wazawa lugha wenye msingi mmoja na wazungumzaji wa lahaja kama ilivyo kwa Kiamu na Kimvita, jambo ambalo haliyumkiniki katika muktadha wa Sheng'. Hivyo basi, inajitokeza kuwa Sheng' si lahaja ila launi ya kijamii tu.

**Tatu**, wapo watafiti ambao wameibainisha **Sheng' kama Msimbo.** Wataalamu hao ambao ni pamoja na Osinde (1986), Spyropoulos (1987) na Abdulaziz na Osinde (1997) wanadahili kuwa Sheng' ni msimbo wa vijana. Ubainishaji wa iwapo Sheng' ni msimbo wa kijamii au wa kimaeneo huhusishwa na mtazamo huu. Kwa mtazamo wa tasnifu hii, kule kuirejelea Sheng' kama 'msimbo' tu hakutoshelezi kubainisha sifa zake za kiisimu. Hii ni kwa vile istilahi hii 'msimbo' ina utata kwa vile inaweza kutumiwa kurejelea 'miondoko ya mwili', 'sura za nyuso', 'maneno', 'lahaja', 'lugha', 'Pijini', 'picha',

'rangi' na mengine mengi. Hivyo, ilifaa uchunguzi huu wa kina ufanywe ili kubainisha hasa 'msimbo wa Sheng' ni msimbo wa aina gani.

**Nne**, kuna mwainisho wa kitipolojia unaodai kuwa **Sheng' ni aina ya msimu**. Kwa mfano, Mazrui (1995) anadahili kuwa Sheng' ni aina ya msimu unaobadilikabadilika na ambao muundo wa vipengele vyake vya kisarufi sio wa kawaida. Kwa fahiwa hiyo, Mazrui hakudai tu kwamba Sheng' ni msimu ila aliapinga pia dai kwamba Sheng' ni mojawapo ya lahaja za lugha yoyote ile. Matokeo ya utafiti huu yanayopinga ukriolishaji wa Sheng' mintarafu ya lengo la pili (1.2.2) yamethibitisha maelezo ya Mazrui kama inavyojitokeza kwenye uchanganuzi wa data. Kwa mujibu wa Mazrui, miundo ya Sheng' hujengwa kupitia usanisi wa vipengele anuai kutoka lugha mbalimbali ambavyo huunda kilugha kilicho na utamaduni-jamii wake. Hili ni tukio linalotokana na mtagusano na mchanganyiko wa lugha mbalimbali. Ingawa hatukulenga kuchunguza masuala ya kijamii na yale ya utamaduni, uchunguzi wetu ulionyesha kuwa kaida za kijamii na utamaduni unaofungamana na matumizi ya Sheng' haufananifanani na ule wa lugha zilizochangia vijenzi vilivyotumika kuunda miundo ya Sheng' – hii ni sifa muhimu (ambayo ilikuwa nje ya upeo wa utafiti huu) inayofaa kwa kubainisha kuwa 'msimu (wa Sheng')' si Krioli, lugha wala lahaja.

**Tano**, Sheng' imeweza kuanishwa kitipolojia **kama lugha-mahuluti**. Aina hii ya uanishaji wa kitipolojia inaashiria kwamba lugha moja (kama Kiswahili) hutoa mkuku wa kimofosintaksia inayotumiwa na Sheng' kisha msamiati unachangiwa na lugha zingine. Kwa mfano, Abdulaziz na Osinde (1997) wameirejelea Sheng' kama 'lugha-mahuluti'. Wataalamu hawa wametoa mifano maalumu inayoonyesha kuwa Sheng' hutumia mkuku wa kimofosintaksia wa Kiswahili ili kuunda sentensi za Sheng' huku ikichota msamiati kutoka lugha anuwai, kama vile Kiingereza na lugha nyingine za

kiasili. Baadhi ya msamiati wa Sheng' huundwa kinasibu, huku mwingine ukiundwa kwa kuhamisha maana vile kauli 'kupiga pasi' inapewa maana ya 'kuiba' katika Sheng'.

Madai ya Childs (1997) yanaunga mkono uanishaji wa Sheng' kama lugha mahuluti. Anaashiria kuwa Sheng' ni lugha mahuluti kwa namna sawa na lugha nyingine za Kiafrika kama vile Lingala na Indoubilkule zinayozungumzwa katika Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo na Sango inayozungumzwa kule Afrika ya Kati. Childs anaeleza kwamba launi hizo zinaweza kufananishwa na Sheng' kwa vile ziliibuka katika maeneo ya miji barani Afrika. Kwa mtazamo wa utafiti huu, Childs alitumia kigezo kimoja kinachohusu chimbuko la Sheng' ili kuamua kwamba Sheng' ni lugha mahuluti ndiposa akaamua kuiweka katika kategoria ya lugha mahuluti pasipo kuchunguza vipengele vyake vingine ili kufikia hitimisho kamilifu na yakinifu zaidi.

Kashoki (1972) anabainisha kuwa wazungumzaji wa Bemba ya mijini hupenda kutumia mseto wa launi za lugha. Wao huona fahari sana wanapotumia maneno mapya ya kigeni mahali pa yale ya kawaida, au kutumia maneno mapya yaliyopanuliwa kimaana. Launi wanazozitumia mijini zinaonyesha hali inayoaminika kijamiii kuwa ya ustaarabu. Kutokanana na ufafanuzi wake, Kashoki anaidhihirisha Sheng' kama lugha mahuluti ambayo ni zao la mchanganyiko wa lugha na utamaduni. Ubainishaji huo wa Sheng' kama lugha mahuluti ulijenga msingi uliochochea utafiti huu kwa vile ulikuwa ukitofautiana na fafanuzi za wataalamu wengine.

### 2.1.6 Yaliyoandikwa Kutokana na Tafiti za Sheng'

Waatalamu wengi wa lugha wamefanya utafiti kuhusu msimbo wa Sheng` kama vile Osinde (1986), Omulando (2001), Kembo-Sure (1992) na Mazrui (1995). Wengi wao

wamedai kuwa Sheng’ ni msimbo unaotumiwa miongoni mwa vijana ili kuficha siri zao huku wakiwabagua wazazi wao. Kembo-Sure (1992), kwa mfano, anadai kuwa msimbo huu ulitumiwa sana katika mitaa ya mabanda na kwamba umasikini katika mabanda uliwalazimu vijana kutafuta njia ambayo wangetumia ili kuwasiliana bila wazazi kuelewa walichozungumzia. Kwa sababu hiyo, walibuni maneno ya kutumia na punde tu yalipojulikana kwa wazazi wao, waliyabadilisha na kuyabuni mengine. Ingawa motisha zilizochochea kuchipuka kwa Sheng’ hazikuchunguzwa kama lengo kuu la utafiti huu, baadhi ya watafitiwa wetu pia waliashiria kwamba wanautumia msimbo huo kwa ajili ya kuwabagua wazazi, walimu na hata vijana wengine katika mawasiliano. Uthibitishwaji huo hatimaye umechangia mahitimisho yaliyofanywa katika tasnifu hii kwamba Sheng’ haina sifa za Pijini wala Krioli kwa kuwa Pijini na hatimaye Krioli hupaswa kuwaunganisha wadau kuliko kuwabagua wengine katika muktadha wa mawasiliano.

Mwanaisimu mwingine ambaye amefanya utafiti wa Sheng’ ni Githinji (2006). Mtafiti huyu amechunguza Sheng’ kama zao la mahusiano ya kijamii linalodhihirishwa na matumizi mbalimbali ya leksia tofauti. Utafiti wa Githinji ulikuwa ukihusiana na utafiti huu licha ya kwamba ulikuwa na malengo tofauti. Hii ni kwa kuwa aliweza kuchunguza matumizi ya maneno ya Sheng’ yanayotofautiana kwa kutegemea mazingira ya matumizi. Jambo hili huzua sinonimu nyingi katika Sheng’. Utafiti wetu uligundua pia kuwa utohozi huhusika katika uzalishaji wa sinonimu katika Sheng’ na ukabaini kuwa utohozi mwingi unaoambatana na matumizi ya mbinu zingine za uleksikalishaji ukitumiwa kuunda msamiati unaorejelea dhana moja huondoa elementi ya iktisadi katika Sheng’.

Utafiti wa Omulando (2001) kuhusu Sheng' ulilenga hoja za kielimu ambapo alizichanganua kaida zinazoutawala mwingiliano wa lugha katika muktadha wa elimu. Kupitia uchunguzi wa matokeo duni ya Kiswahili na Kiingereza katika mitihani ya kitaifa, Omulando waliweza kufasiri athari za Sheng' katika matumizi ya lugha za Kiswahili na Kiingereza na matokeo duni ya mitihani ya kitaifa. Matokeo ya utafiti wa Omulando yalionyesha uhusiano wa matumizi ya Sheng' na matokeo duni ya mitihani ya lugha kwenye shule za upili.

Kuna tafiti nyingine ambazo zimelenga mtazamo wa kiisimu (Echessa, 1990, Fink, 2002, Ogechi, 2005, Mokaya, 2005, Githinji, 2006). Tafiti nyingine zimeshughulikia uundaji na/au upanuzi wa msamiati wa Sheng' (Echessa, 1990, King'ei, 2001, Ogechi, 2004). Echessa (1990) ameonyesha mikakati mbalimbali ya kimofolojia ya kuunda maneno ya Sheng'. Baadhi yao ni kama vile ufupishaji, usimilishwaji, uongezi wa sauti mwishoni mwa nomino, na kadhalika. Ogechi (2004) amezingatia michakato ya kutoa maana mpya kwa maneno ya Sheng'. Naye King'ei (2001) amesisitiza dai la Echessa (1990) kuhusu mikakati ya kimofolojia ya kuunda maneno ya Sheng'.

Echessa alitafiti kuhusu maumbo na muundo wa maneno ya Sheng'. Alilenga kufafanua mbinu msingi zinazohusika katika uundaji wa maneno ya Sheng'. Alishughulikia mawanda ya kifonolojia. Aligundua kwamba kuna utohozi mahsusi unaohusika katika uundaji wa maneno ya Sheng'. Mbinu mbalimbali za uundaji wa maneno kama vile uhulutishaji, ufupishaji, na unyambuaji zilihusika katika utohozi wa maneno ya Sheng'. Mbinu hizi zilifaulu kutoa maumbo ya maneno ya Sheng' ambayo yalikuwa tofauti na yale ya lugha changizi. Tofauti na utafiti wa Echessa (1990), utafiti huu ulihakiki mbinu zinazotumika kuunda msamiati wa Sheng' kwa kuzingatia vigezo vya pegitosca, kama lengo mojawapo la utafiti huu wa sasa.

Mbaabu na Nzuga (2003) waliibuka na *Engsh* mbali na Sheng'. Wao wamejaribu kutofautisha Sheng' na *Engsh.* Wanasema kuwa *Engsh* inaegemea katika sarufi ya Kiingereza na inazungumzwa na watu wa tabaka teule nchini. Hata hivyo Mazrui (1995) anadai kuwa vijana wa tabaka hili wanayozungumzia Mbaabu na Nzuga hutumia Sheng' ili kujenga ukuruba na wale wa mitaa ya kifahari.

Utafiti mwingine ulifanywa na Fink (2005). Utafiti huu ulilenga kuchunguza mielekeo kuhusu matumizi ya lugha katika jiji la Nairobi. Fink alitumia Sheng' kama mojawapo ya lugha zinazotumika sasa jijini Nairobi. Aliegemea sana kwa mtazamo wa kiisimu jamii ambao hufasili matumizi na mitindo ya lugha kulingana na kategoria za kijamii. Mitazamo hii kwa kawaida huegemea vigezo vya elimu, umri, tabaka na uana. Utafiti wake ulithibitisha kuwa vigezo hivi huathiri matumizi ya Sheng' miongoni mwa wakazi wa jiji la Nairobi. Vijana walionekana kutumia Sheng' zaidi ya makundi mengine. Utafiti ulitoa mwangaza katika kutilia maanani vigezo vya kijamii na tamaduni zake katika matumizi ya lugha. Hata hivyo, utafiti huu unatofautiana na utafiti wa Fink (2005) kwa kuwa hoja kuu inayoshughulikiwa ni athari za Sheng' katika matumizi ya Kiswahili.

Mokaya (2005) alifanya uchunguzi kuhusu Sheng' kama mseto wa kiisimu. Nguzo kuu katika utafiti huu wa Mokaya ilikuwa maoni ya Abdulaziz na Osinde (1997) ambao wanadahili kuwa Sheng' huchanganya leksia kutoka lugha mbalimbali na kutumia mofolojia na sintaksia ya Kiswahili. Mseto huu wa lugha huambatana na ule wa tamaduni za jamii mbalimbali unaodhihirisha uwili wa lugha, yaani lugha kama tukio la isimujamii na lugha kama isimu tekelezi. Mokaya aligundua kuwa vijana ambao ni wasemaji wa Sheng' huathiriwa na mabadiliko ya tamaduni na historia ambayo pia huathiri matumizi yao ya Sheng'. Hulka ya wasemaji hudhihirika katika matumizi yao

ya lugha. Utafiti huu ni tofauti na wa Mokaya kwani ulilenga kuchambua matini za Sheng' kwa misingi ya nadharia ya 4M na Pegitosca.

Ogechi (2005) alifanya utafiti kuhusu mbinu za uleksifikaji wa leksia za Sheng'. Alilenga kuchanganua mbinu za kisemantiki zinazohusika katika maneno ya Sheng'. Aligundua kuwa kuna utohozi wa juu unaohusika katika uundaji wa nomino za Sheng'. Utohozi wa nomino ulifuatiwa na ule wa vitenzi na vivumishi. Kwa hivyo kwa kiwango kikubwa, nomino na vitenzi vilihusika zaidi katika uundaji wa maneno ya Sheng'. Aligundua pia kuwa Sheng' hutumika kama lugha ya kikundi maalum kinachowatenga wengine wasioifahamu. Aligundua ya kwamba kuna mantiki inayohusika katika utohozi wa maneno na kuwa hayatokei tu kiholela. Usimbaji wa maana ulisababisha kutokea kwa sinonimu nyingi. Matumizi mengi ya sinonimu yalidhihirisha tamaduni bayana za wanaSheng'. Utafiti huu ulimpa mtafiti msingi mzuri wa kuendeleza utafiti wa sasa hasa katika kuhakiki mbinu zinazotumika kuunda msamiati wa Sheng', hata ingawa utafiti wa sasa ulikuwa unazingatia vigezo vya pegitosca.

Githinji (2006) alichunguza Sheng' kama lugha ya utambuzi. Aligundua kuwa makundi mbalimbali ya wasemaji hutumia leksia tofauti kama njia ya kujitambulisha na pia kama nyenzo za kuficha maana. Wasemaji walioelewana walionekana kukaribiana zaidi na kujiona kama kundi muhimu. Wasemaji lugha walibadilisha msimbo wao ili ufanane na ule wa walio ndani mwake. Utafiti huu ulitazama Sheng' kama kiwakilishi cha hali halisi ya mahusiano. Matumizi yake yaliongozwa na kaida za kijamii. Utafiti wake ulionyesha kuwa wasemaji pia walitumia msimbo huu kutokana na shughuli zao maalum. Msimbo wa waoshaji magari ulikuwa tofauti na ule wa wanafunzi wa chuo kikuu au shule za sekondari. Kwa mujibu wa Githinji (2006), sinonimu nyingi ziliibuka kutokana na makundi tofauti yaliyokuwa na kaida zao za matumizi ya Sheng'. Utafiti

wa Githinji ulifafanua baadhi ya maneno ambayo yalikuwa na utata. Ulithibitisha kuwa maneno ya zamani ya Sheng' hayatupiliwi mbali, lakini huendelea kutumiwa tu miongoni mwa makundi maalum ya vijana. Makundi haya huyatumia kujitambulisha.

Ogechi (2008) alifanya uchunguzi uliotafuta kujua ikiwa Sheng' ni lugha inayotambulisha vijana. Utafiti huo ulifichua kuwa utambulisho huo wa vijana kupitia Sheng' hubadilikabadilika na kwamba sio vijana wote wanaoelewa na kuzungumza Sheng'. Ogechi aligundua kuwa baadhi ya watu wazima huweza kujitambulisha na vijana na wakati kama huo, vijana wasiotumia Sheng' huachwa nje. Kwa hivyo utafiti huo wa Ogechi ulidhihirisha kuwa Sheng' siyo launi ya vijana pekee.

Utafiti mwingine uliofanywa na Ogechi (2005) ulichunguza mchango wa Sheng' katika upitishaji wa ujumbe kuhusu uzuiaji wa uenezaji wa UKIMWI baina ya vijana nchini Kenya, katika kipindi cha 'Elimika'. 'Elimika' ni kipindi cha vijana kinachowatahadharisha kuhusu UKIMWI. Uchunguzi huo ambao ulifanywa kule Eastleigh, Nairobi mnamo mwezi wa Novemba 2008, ulijishughulisha na matumizi ya Sheng' na kuonyesha jinsi maana ya msamiati huu wa Sheng' ulivyotumiwa katika muktadha wa ngono na UKIMWI. Uchunguzi huo uligundua kuwa Sheng' ina umuhimu na mchango mkubwa wa kimawasiliano katika kuwasilisha ujumbe kwa vijana.

Githinji (2006) katika utafiti wake alichunguza maneno ya Sheng' yenyewe pamoja na yale yaliyokuwa yametoholewa kutoka lugha changizi (Gikuyu, Kiswahili, Kiingereza). Uteuzi huu ulidhamiria kulinganisha maana za maneno katika lugha changizi na maana iliyotoholewa katika Sheng'. Maneno haya yalikusanywa kunakiliwa na kuchambuliwa barabara.

## 2.2 Msingi wa Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili. Vigezo vya nadharia husika vinafafanuliwa kama sehemu 2.2.1 na 2.2.2 kwenye sura hii.

### 2.2.1 Nguzo za Nadharia ya 4M Zinazohusu Miundo

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili ambazo ni **Nadharia ya 4M** iliyoendelezwa na Myers-Scotton na Jake (2000; 2001) na **Nadharia ya Pegitosca** vile ilivyoendelezwa na Kiingi (1989, 1998). Modeli ya 4M ni mwendelezo wa nadharia ya lugha solo ambao umeendelezwa kwa lengo la kufafanua diskosi za kiwingi-lugha. Nguzo za nadharia hii ambazo zilikuwa muhimu kwa utafiti huu zinaangaziwa katika sehemu ifuatayo.

Nadharia hii imekitwa katika nguzo au vigezo viwili vikuu. Kwanza, inadai kuwa katika uzalishaji wa sentensi za kiujozi-lugha (zenye ubadilishaji msimbo), mkuku hujengwa. Pili, inadai kwamba uteuzi wa mofimu za kileksika na za kiuamilifu za lugha zinazoweza kuungana katika matamko yenye UM na huzingatia kanuni.

Matumizi ya dhana ‘mkuku’ katika nadharia hii yanarejelea mfuatano wa vijenzi kabla ya kubainisha wakati na viwakilishi vingine kama vya ngeli. Mkuku huo huamua; (a) namna mofimu zitafuatana na (b) hubainisha jinsi mofimu amilifu zitaunganishwa kwa mofimu za kileksika.

Kipengee kimoja kikuu cha nadharia hii ni kile cha ujenzi wa mkuku au muundo wenye vipashio vya zaidi ya lugha moja. Nadharia hii inadai kuwa katika sentensi yenye UM, mkuku wenye viambajengo vya lugha solo (LS) na Lugha changizi (LC) hujengwa. Lugha solo ni lugha inayodhibiti mpangilio wa mofimu na ni lugha inayozalisha

mofimu amilifu katika sentensi. Ingawa mofimu za kileksika za lugha changizi zinaweza kuchopekwa ndani ya mkuku wa lugha solo, mofimu za kileksika za lugha changizi zinazowiana na mahitaji ya lemma hukubaliwa.

Nadharia hii inaweka wazi kwamba sentensi zenye UM huweza kujengwa kwa mseto wa viambajengo vya LS na LC na vizingwa vya lugha solo vile inavyofafanuliwa hapa. Kwanza, miundo yenye ubadilishaji msimbo inaweza kujengwa kwa mseto wa viambajengo vya LS na LC. Miundo ya aina hii ina vijenzi vinavyotokana na LS na LC. Mfano wa miundo yenye mseto wa LS na LC ni ule wenye neno moja moja la lugha changizi linalotumiwa katika muundo wenye idadi yoyote ya mofimu za LS.

Pili, miundo yenye UM, mintarafu ya nadharia hii inaweza kujengwa kwa kutumia vizingwa vya lugha solo. Hii ni miundo inayojitokeza katika mazungumzo yenye UM inayoundwa kwa viambajengo vya lugha solo pekee. Miundo hiyo ni lazima iweze kukubalika kimuundo kwa mujibu wa sarufi ya lugha solo. Mfano wa kizingwa cha LS ufuatao ulitumiwa na Myers-Scotton (1993b: 78). Mfano:

**5.** Nimemaliza kutengeneza kitanda. Nitatengeneza wardrobes kesho.

Sehemu ya kwanza ya sentensi hii “Nimemaliza kutengeneza kitanda” ni mfano wa kizingwa cha LS. Kwa kuzingatia ufafanuzi wa nadharia ya 4M, lugha solo katika muktadha huu ni Kiswahili.

Tatu, vizingwa vya lugha changizi (LC) ambavyo ni aina ya miundo ambayo ni kinyume cha vizingwa vya LS hubainishwa katika nadharia hii. Vizingwa vya LC ni viambajengo vinavyoshiriki katika kujenga sentensi zenye U.M ambavyo vinajitosheleza na vinaundwa kwa lugha changizi pekee yake. Vizingwa hivyo vya LC

hujitokeza kama miundo (sentensi) inayojengwa kwa vijenzi vya LC pekee. Kizingwa chochote cha LC ni lazima kiwe sahihi kwa mujibu wa sarufi ya LC.

Nne, kigezo kingine muhimu kinachoangaziwa na nadharia hii ni kile cha mkuku wa kimofosintaksia kinachoeleza kwamba katika ujenzi wa miundo yenye vipashio vya LS + LC, mkuku wa kimofosintaksia wa LS hufuatwa. Mtazamo huu unadokeza kwamba ujenzi wa mkuku utakaokaliwa na viambajengo huundwa kabla ya kuingizwa kwa mofimu. Zifuatazo ni kanuni zinazohusu matumizi ya mofimu za aina mbili ambazo ni kanuni ya mfuatano wa mofimu na kanuni ya mofimu amilifu.

Madai ya kanuni ya mfuatano wa mofimu kwa mujibu wa nadharia hii ni kwamba katika miundo yenye leksimu moja moja za lugha changizi zilizochopekwa, mpangilio wa mofimu utakaozingatiwa ni ule wa LS. Kanuni ya Mofimu Amilifu ni kanuni ya pili inayofafanua kwamba katika muundo mseto wenye viambajengo vya LS na LC, mofimu zote amilifu zinazoshirikiana kisarufi na kiambajengo kikuu ni lazima ziwe na LS. Mofimu amilifu ni faridi za kimofolojia zinazobainisha njeo, ngeli na idadi.

Modeli ya 4M ni mkabala wa kinadharia ambao unafafanua kwa uwazi zaidi aina za mofimu zinazohusika katika ubadilishaji msimbo. Inabainisha vilevile mwainisho wa mofimu zinazoweza kutofautisha Pijini au Krioli kutoka kwa msimbo. Uanishaji huo wa mofimu unafanywa kwa mujibu wa dhima zao za kisintaksia na namna zinavyochochewa wakati wa kuzalisha maumbo au miundo ya lugha akilini mwa wazungumzaji (Myers-Scotton na Jake, 2000). Nadharia ya 4M hutumia dhana ‘mofimu’ kurejelea vitomeo dhahania vya kileksika vinavyopatikana akilini na vinavyoamua maumbo na miundo inayotamkwa (Myers-Scotton na Jake, 2000). Kutokana na changamoto zilizobainika katika nadharia ya lugha solo, mkabala wa 4M

ulipendekezwa ili kustawisha namna za kutofautisha mofimu za kileksika dhidi ya mofimu amilifu (Myers-Scotton na Jake, 2000)

Vipengee vingi vinavyoangaziwa zaidi na nadharia ya 4M vimeathiriwa na nadharia za kisaikolojia. Kwa mfano, ubainishaji wa lugha solo (LS) dhidi ya lugha changizi (LC) unahusiana na ubainishaji wa kisaikolojia uliofanywa na Grosjean (1988) kuhusu lugha msingi na lugha ngeni katika ubadilishaji msimbo. Pili, mkabala unaochukuliwa na nadharia hii (ya 4M) umechangiwa na ufafanuzi wa Garret (1975) kuhusu makundi ya faridi wazi na faridi funge. Nadharia ya 4M imefaidika kutokana na ufafanuzi unaohusu uhifadhi wa msamiati na faridi nyingine za kiisimu unaofanyika akilini unaorejelewa kama ‘lemma’ uliofanywa na Levelt (1999). Ufafanuzi huo ulihusu uamilifu wa kisarufi wa taarifa zinazofikiriwa.

Modeli ya 4M inaainisha mofimu kwa kutegemea iwapo zinazanzuliwa akilini au hazizanzuliwi akilini. Mofimu zinaainishwa vilevile kwa kuzingatia namna ambavyo maumbo yanashiriki katika ujenzi wa vipashio vikubwa. Kwa misingi hiyo, kuna mofimu za kileksika na mofimu amilifu.

Mintarafu ya modeli hii ya 4M, mofimu za kileksika ni faridi za kiisimu kama vile ‘paka’, ‘mti’ na ‘mtu’ ni mifano ya mofimu zinazozanzuliwa akilini kulingana na makusudi ya kiisimu ya mzungumzaji. Kwa upande mwingine, mofimu amilifu ni viambata tu vinavyotegemea mkuku wa kisarufi wa sentensi. Kwa mfano, Myers-Scotton na Jake (2000) walifafanua kuwa maumbo ya mofimu amilifu tangulizi kama vile viambishi vya umoja na wingi hutegemea sifa za mofimu za kileksika zitakazoambatishwa. Kwa vile maana za mofimu za kileksika zinahusiana na mofimu amilifu tangulizi zitakazoambatishwa, nadharia ya 4M inaeleza kuwa mofimu zote (za kileksika na amilifu tangulizi) ni faridi zinazozanzuliwa akilini. Kwa misingi ya

nadharia hii, shina au mzizi wa mofimu ya kileksika huchagua kwa njia isiyokuwa wazi mofimu amilifu zitakazotumiwa katika sentensi.

Ili kuondoa utata wa kubainisha mofimu, modeli ya 4M iliibua aina mbili kuu za mofimu amilifu ambazo ni (i) Mofimu amilifu tangulizi na (ii) Mofimu amilifu tamatishi. Aina hizi za mofimu zinaelezewa ifuatavyo:

Mintarafu ya nadharia ya 4M, mofimu amilifu tangulizi kwa pamoja na mofimu za kileksika hushirikiana katika ujenzi wa miundo kama kirai nomino (KN), kirai vumishi (KV) na kirai kitenzi (KT). Myers-Scotton na Jake (2000) wanatumia vibainishi vya Kiingereza ‘a’ na ‘an’ kama mifano ya mofimu amilifu tangulizi zinazoambatana na nomino. Hata hivyo, vibainishi vya aina hiyo havipo katika lugha kama Kiswahili na Sheng’.

Myers-Scotton na Jake (2001) wanaashiria kuwa mofimu amilifu tamatishi ni faridi za kiisimu au aina nyingine za mofimu zinazoshiriki katika ujenzi wa muundo ambazo hazijazanzuliwa wakati wote akilini. Wanaonyesha kuwa mofimu za aina hii huzanzuliwa baadaye katika hatua za kuzalisha vipashio vya lugha kama kishazi.

Dhana ‘tamatishi’ inayojitokeza katika ‘mofimu amilifu tamatishi’ inadokeza kwamba mofimu za aina hii huzanzuliwa baadaye au katika hatua ya mwisho za kuzalisha usemi au sentensi. Mofimu amilifu hujenga mahusiano baina ya vipashio vinavyojenga kishazi. Kama inavyoelezewa na Myers-Scotton (2005: 269), mofimu amilifu tamatishi “ni ‘saruji’ inayounganisha vipande vya kishazi.” Mofimu amilifu tamatishi hazina dhima za thita na hazizanzuliwi katika kiwango cha lemma akilini.


Nadharia ya 4M inaainisha mofimu amilifu tamatishi katika kategoria mbili ambazo ni (a) Mofimu amilifu shirikishi na (b) mofimu amilifu za upatanisho. Jinsi inavyoashiriwa

na anwani ‘shirikishi’, Mofimu Amilifu Shirikishi ni mofimu amilifu tamatishi zenye uamilifu wa kuunganisha au kushirikisha elementi zinazojenga vipashio vikubwa. Mofimu za aina hii hutumiwa kwa kutegemea sifa za viambajengo vingine vinavyoujenga muundo (Myers-Scotton na Jake, 2001). Mofimu hizi huunganisha mofimu za kileksika ili kujenga viambajengo vikubwa. Neno la Kiingereza ‘of’ ni mfano wa mofimu tamatishi yenye uamilifu huo.

Mofimu amilifu za upatanisho wa kisarufi ni aina ya pili ya mofimu tamatishi kwa mujibu wa modeli ya 4M. Aina hii ya mofimu hutumiwa tu kwa kutegemea taarifa au sifa zinazopatikana katika kipashio kingine. Mofimu amilifu za upatanisho wa kisarufi hubainisha mahusiano yanayokiuka kiwango cha neno moja au mpangilio wa maneno. Hizi ni mofimu zinazounganisha elementi katika kiwango kingine kama vile baina ya virai (Myers-Scotton, 2005). Mofimu hizi ni viambishi vinavyounganishwa kwa tungo katika kiwango cha muundo wa nje. Kiambishi cha Kiingereza cha nafsi ya tatu umoja ‘-s’ ni mfano wa mofimu ya aina hii. Kielelezo 2.1 kinaonyesha kwa muhtasari mwainisho wa mofimu zinazoshiriki katika ujenzi wa tungo za kiwingi lugha:

**Kielelezo 2.1: Uanishaji wa Mofimu**

**Aina za Mofimu**




Ukopaji umeelezwa katika nadharia ya Myers-Scotton (1993a) kama mfanyiko unaofungamana na mtagusano wa lugha. Ubainishaji wa kinadharia wa ukopaji ni muhimu kwa vile UM hautaweza kuchunguzwa na kuchanganuliwa kama ukopaji. Myers-Scotton alibainisha aina za ukopaji huku akibainisha kuwa visababishi vya ukopaji hutofautiana. Aliweza kushughulikia suala la kukopa mofimu amilifu na mofimu za kileksika. Mwanaisimu huyu ameonyesha kuwa ubadilishaji msimbo ni kichocheo muhimu cha ukopaji. Anaashiria kwamba kugeuzwa kwa muundo wa neno kimofolojia kunaweza kuashiria ukopaji. Kipengee hiki cha ukopaji kwa mujibu wa UM unashirikisha Sheng' na Kiswahili.

### 2.2.2 Nguzo za Nadharia ya 4M Zinazohusu Upijini/Ukriolishaji

Kazi ya Myers-Scotton (2002: 277-287) imefafanua vigezo ambavyo vinaweza kudhihirisha kwamba launi ya lugha inaimarika kimuundo kuwa Krioli. Myers-Scotton aliweza kufafanua vigezo hivyo vitano kwa muhtasari kwa jinsi ifuatavyo:

(i) Launi-takaro huchangia uzalishaji wa Krioli kwa kuchangia mkuku wa kimofosintaksia usodhahiri wa Krioli hiyo.

(ii) Mofimu za kileksika za lugha-tuhinga ni nyingi kuliko zile za lugha takaro.

(iii) Mofimu za kileksika zinazotoka lugha-tuhinga huweza kugeuzwa na kutumiwa kama mofimu amilifu katika Krioli.

(iv) Mofimu amilifu tangulizi zinazotoka kwa lugha-tuhinga pekee huweza kutimiza mahitaji ya Krioli pekee pale zinapounganishwa na maneno yao makuu.

(v) Mofimu amilifu tamatishi za lugha-tuhinga haziwezi kutimiza mahitaji yanayohusiana na mkuku wa kimofosintaksia wa Krioli kwa sababu ya ugumu wa kuufikia mkuku huo wa kimofosintaksia wa Krioli.

### 2.2.3 Nadharia ya Pegitosca

Pegitosca ni nadharia ya kimofolojia iliyoasisiwa na Kiingi (1989) kwa lengo la kutathmini ufaafu wa msamiati na istilahi zinazoundwa katika lugha. Kimsingi, nadharia hii ilikuwa ikilengwa kutumiwa kukadiria ufaafu wa istilahi za Kisayansi. Matumizi ya nadharia hii yataweza kubainisha iwapo mbinu zinazotumiwa kuunda msamiati wa Sheng’ katika maeneo niliyofanyia uchunguzi ni za kipekee. Kila herufi katika neno ‘Pegitosca’ linawakilisha kigezo kinachoweza kutumiwa kutathmini ufaafu wa msamiati.

#### 2.2.3.1 Nguzo za Nadharia ya Pegitosca

Kwa mujibu wa Kiingi (1989) nadharia ya Pegitosca ina vigezo au mihimili tisa (9) inayoweza kutumiwa kutathmini ufaafu wa msamiati. Kila mhimili huwakilishwa kwa herufi moja inayowakilisha neno la Kiingereza. Kila kigezo huwakilishwa kwa herufi moja kama inavyoonyeshwa katika Jedwali 2.2 lifuatalo:

**Jedwali 2. 2: Vigezo vya Pegitosca**

| | AKRONIMU | KIGEZO | TAFSIRI |
|---|---|---|---|
| (i) | P | Precision | Udhahiri |
| (ii) | E | Economy | Ikitisadi |
| (iii) | G | Generativity | Uzalishaji |
| (iv) | I | Internationality | Umataifa |
| (v) | T | Transparency | Uangavu |
| (vi) | O | Anti-Obscenity | Utusani |
| (vii) | S | Systemicity | Utaratibu maalum |
| (viii) | C | Consistency | Utaratibu ulio sawa |
| (ix) | A | Appropriateness | Ukubalifu na ufaafu |

Nadharia ya Pegitosca ina mihimili tisa iliyoorodheshwa katika Jedwali 2.2.1 hapo juu. Mhimili wa kwanza unahusu **udhahiri** wa neno linaloundwa. Kigezo hiki kinasisitiza kuwa ni lazima neno linaloundwa liwasilishe maana kwa udhahiri au bila utata (Mwaro, 2001). Hii inamaanisha kuwa wazungumzaji wanaweza kupendelea au kuliepuka neno moja kuliko lingine. Kigezo hiki kilitufaa katika kukadiria msamiati wa Sheng' kwa mujibu wa watumiaji wake.

Kigezo cha pili kinahusu **ikitisadi**. Kigezo hiki kinamaanisha ufupi wa neno linaloundwa kama msamiati. Pegitosca inaashiria kwamba ufaafu wa msamiati hufungamana na ufupi wake. Hii inaashiria kwamba neno halipaswi kuundwa kwa

fonimu au silabi nyingi mno. Ikitisadi ni sifabia inayolengwa na kila mfumo lugha. Hii inamaanisha kuwa neno refu sana likiundwa, halitafaa kwa mujibu wa kigezo hiki. Mtafiti aliweza kubainisha katika Sheng' maneno yaliyozingatia kigezo hiki kama yale yaliyozalishwa kupitia ufupishaji au akronimia.

Kigezo cha tatu ni kile cha **uzalishaji**. Kwa mujibu wa kigezo hiki msamiati faafu ni lazima uweze kutumiwa kuzalisha maneno mengine kwa vile linaweza kunyambulikanyambulika. Kigezo hiki kinaweza kufaa zaidi iwapo kuna maneno kadhaa ambayo yameundwa. Hii ni kwa kuwa neno moja linalonyambuli-kanyambulika litaweza kuteuliwa. Baadhi ya maneno huweza kunyambuliwa ili kuzalisha aina nyingine za maneno lakini mengine huweza kunyambuliwa ili kubainisha maana mahususi tu.

**Umataifa** ni kigezo cha nne kwa mujibu wa orodha ya herufi za neno Pegitosca. Dai la kigezo hiki ni kwamba ni lazima msamiati uchukue ishara zilizo kubalika kimataifa kama ilivyo katika mfano huu,

Oksijeni ($O_2$) – “Oxygen”

Neno lililo sawa na maneno mengine yanayotumika kimtaifa kama “Oksijeni” (oxygen) linaweza kuundwa katika lugha. Neno hilo litakuwa sawa na maneno mengine ya aina hiyo yanayotumiwa katika lugha nyinginezo hivi kwamba ishara moja kama vile $O_2$ itaweza kutumika ili kuwakilisha msamiati huo katika lugha husika kama ilivyo katika lugha nyinginezo.

Kigezo cha tano kinachohusu utendakazi wa Pegitosca ni **uangavu.** Mhimili huu hufaa kwa uchunguzi wa uhusiano uliopo baina ya msamiati wa asili na maana. Mathalani, kama anavyofafanua Mwansonko (1990), watumiaji wa lugha wataweza kuchukulia

maneno yanayojitokeza katika upande wa kulia kuwa angavu ilhali yale yanayopatikana katika upande wa kushoto kuwa angavu zaidi. Tazama jedwali hili na mifano ya msamiati aliyotumia Mwansoko (1990:124) inayofafanua kipengele cha uangavu wa msamiati.

| | | |
|---|---|---|
| Nazali | = | King'ong'o |
| Impresti | = | Masurufu |
| Analojia | = | Ulinganishi |

**Utusani** kama mhimili wa sita wa nadharia hii huashiria kwamba msamiati unaofaa ni lazima uepuke maana au maumbo yanayohusu lugha pujufu kwa mujibu wa desturi za jamii lengwa. Kwa sababu ya madai ya baadhi ya wafafanuzi kwamba Sheng' ni msimbo wa siri, mtafiti alichunguza msamiati wa Sheng' ili kubainisha iwapo kigezo hiki cha utusani kinapuuzwa katika uundaji wa msamiati wake. Aidha, haja ya kuzingatiwa kwa **utaratibu maalum** katika uundaji wenyewe wa msamiati husika ni kigezo cha saba cha nadharia hii. Mintarafu ya kigezo hiki, msamiati unaoundwa ni lazima uundwe kwa kufuata utaratibu mahususi. Ili kubainisha iwapo Sheng' imefikia kiwango cha upijinishaji, uchunguzi wa kuzingatiwa kwa kigezo hiki ulikuwa muhimu. Hii ni kwa sababu lugha ambayo ni thabiti (Krioli) inatarajiwa kuunda maneno yake kwa kufuata utaratibu maalum pasipo kuunganisha mofimu kiholelaholela.

Kigezo cha **utaratibu ulio sawa** ni mhimili wa nane unaofafanua namna ya kukadiria ufaafu wa msamiati unaoundwa katika lugha kwa mujibu wa nadharia hii. Kigezo hiki husisitiza kule kuzingatiwa kwa utaratibu thabiti au usiobadilikabadilika katika upanuzi wa msamiati. Hii inamaanisha kuwa neno linaloundwa linafaa lilingane kiumbo na maneno mengine yaliyoundwa katika lugha husika. Kwa mfano:

(i) Tabakanje (epiderm) - tabaka = “derm”, nje = “epi”
(ii) Tabakandami (endoderm”) = ndani = “endo”
(iii)Tabakakati (mesoderm”) - kati = “meso”

Mifano iliyotolewa hapo juu inaashiria kule kutumiwa kwa mzizi mmoja ‘tabaka’ (*derm)* kwa utaratibu sawa ili kuzalisha maumbo mengine kwa kuongeza viambishi. Kigezo cha tisa, na cha mwisho katika nadharia hii kinahusu **ukubalifu**. Kigezo cha ukubalifu kinamaanisha kuwa msamiati ulioundwa unafaa kutumiwa kutaja kirejelewa. Kigezo hiki ni muhimu kwa kila mwanaleksikografia au mwanalugha anayeshiriki katika uundaji wa msamiati kwani kila neno linaloundwa ni sharti liweze kukubalika kwanza katika jumuiya lugha ili liendelee kutumika. Hiki ni kigezo muhimu kinachoshirikisha jamii itakayotumia msamiati unaoundwa katika ukadiriaji wa ufaafu wake. Kigezo hiki kilikuwa muhimu katika kubainisha iwapo kuna baadhi ya maneno ya Sheng’ ambayo yangedhihirishwa na watafitiwa kama yasiyofaa au yasiyokubalika.

## 2.3 Hitimisho

Sura hii imepitia maandishi yaliyopo kuhusu mada ya utafiti. Aidha maandishi kuhusu Chimbuko la Sheng’, uamilifu wa Sheng’, muundo wa Sheng’, athari za Sheng’ katika matumizi ya lugha zingine, tipolojia ya Sheng na yale yanayohusu tafiti za Sheng’ yamehakikiwa. Sura hii vilevile imeangazia nadharia mbili ambazo ni 4M ya Myres-Scotton na Nadharia ya Pegitosca ya Kiingi (1989) zilizoongoza utafiti huu. Mihimili au vigezo vya nadharia hizi mbili vilivyoongoza utafiti huu kulingana na malengo yake vimeshughulikiwa katika sehemu za sura hii. Sura ya tatu inachanganua data inayohusiana na lengo la kwanza na la pili la utafiti huu. Lengo la kwanza ni kubainisha na kufafanua mbinu za uleksikalishaji zinazotumika katika Sheng’. Lengo la pili ni kufafanua sifa zinazopinga upijini na ukriolishaji wa Sheng’. Malengo haya mawili yameshughulikiwa kikamilifu katika sura inayofuata.

# SURA YA TATU

# ULEKSIKALISHAJI, UPIJINI NA UKRIOLISHAJI WA SHENG’

## 3.0 Utangulizi

Sehemu ya kwanza ya sura hii inachanganua data ili kujibu maswali yanayohusiana na lengo la kwanza ambalo ni kubainisha na kufafanua mbinu za uleksikalishaji zinazotumika katika Sheng’ kwa kutumia vigezo vya pegitosca. Data inachanganuliwa pia katika sehemu 3.2 ya sura hii ili kujibu maswali yanayohusiana na lengo la pili ambalo ni kufafanua sifa zinazopinga upijini na ukriolishaji wa Sheng’. Sehemu ya kwanza imejikita katika kuchanganua na kupambanua mbinu za uleksikalishaji katika Sheng’, mathalani, mnyambuliko, uradidi, udondoshaji, uhamishaji wa maana, ufinyaji wa maana, uundaji kinasibu na ufupishaji-tohozi. Sehemu hii pia imeshughulikia usarufishaji na ukopaji kama viambajengo vya uleksikalishaji. Sehemu ya pili imechanganua na kujadili data inayohusiana na upijini na ukriolishaji wa Sheng’. Katika sehemu hii, tumedhihirisha kidata kwamba Sheng’ haijawahi kuwa pijini.

## 3.1 Mbinu za Uleksikalishaji katika Sheng’

Mintarafu ya lengo la kwanza la utafiti huu, sehemu zifuatazo (3.1.1 mpaka 3.1.16) zinabainisha na kufafanua mbinu mbalimbali za uleksikalishaji zilizotumiwa ili kuunda msamiati wa Sheng’. Mbinu zenyewe zimehakikiwa kwa kuzingatia vigezo vya Pegitosca.

### 3.1.1 Mnyambuliko

Utafiti huu umegundua kuwa upanuzi wa msamiati katika Sheng’ hufanywa kwa kutumia mbinu ya kunyambua mizizi kwa kuongeza viambishi awali au vya tamati. Ili

mbinu hii itumike ni lazima msamiati msingi utakaonyambuliwa uwepo. Matokeo ya utafiti huu yamebainisha kuwa mnyambuliko hutegemea dhana inayolengwa kupewa jina. Namna ambavyo mnyambuliko utafanywa katika Sheng' huamuliwa na dhana ya kuwasilishwa. Hii inamaanisha kwamba mnyambuliko haufanywi kinasibu ila unadhibitiwa na maana inayolengwa kuwasilishwa katika neno.

Uchunguzi huu uligundua kuwa mnyambuliko katika Sheng' hufanywa kwa kutanua mzizi kwa kuongezea viambishi ama awali au tamati. Hii inamaanisha kwamba mizizi na viambishi ni viambajengo muhimu katika mchakato wa kuyanyambua maneno ya Sheng' ili kuupanua msamiati wake. Kule kuongezwa kwa mofu kunabadilisha maana ya umbo linalozalishwa hivi kwamba litaweza kuwa neno tofauti linalorejelea dhana tofauti. Msamiati wa Sheng' ulibainika kama unaozingatia maelezo ya Mdee (1986) kwamba kila kiambishi kina maana maalum, na kila kinapoambishwa kwenye mzizi wa neno wakati wa kuunyambua, maana ya kimsingi ya neno hilo hubadilika.

Ubainishaji wa mchango wa mnyambuliko kwa upanuzi wa msamiati wa Sheng' umefanywa kwa kukatakata maneno ili kutenganisha mizizi na viambishi vyao. Mizizi ya Sheng' ilibainishwa katika utafiti huu kwa kuondoa viambishi vyote na kubakisha sehemu ambayo haigawiki zaidi pasipo kubadilisha maana yake ya kimsingi. Hii inamaanisha kuwa mzizi ni sehemu inayosheheni maana ya kimsingi katika maneno ya Sheng'. Kwa mfano:

1. Mapere = ma – pere
   wazazi

Kwa kuondoa kiambishi 'ma' kutoka '*mapere'* katika mfano (1), sehemu ambayo bado inabeba maana ya kimsingi (yaani mzizi) *pere* inabakia. Mofu '*ma'* ni kiambishi kinachowakilisha hali ya wingi katika baadhi ya maneno ya Sheng'. Tofauti na ilivyo

katika Kiswahili, kiambishi hiki kinatumiwa katika Sheng' kama kiambishi cha nomino hisivu zinazopatikana katika ngeli ya A-WA na hata nomino zisizokuwa hisivu. Mofu ya Sheng' *pere* imeundwa kwa kudondosha baadhi ya fonimu zilizounda neno la Kiingereza 'parents*'* na kubadilisha sauti '*a'* na nafasi yake ikachukuliwa na '*e'*. Mchakato huu wa uleksikalishaji kwa jinsi hiyo unaonyesha usimilishwaji unaofanyika katika harakati za kuunda msamiati. Baada ya umbo hilo kusimilishwa, mnyambuliko unaohusu kule kutanuliwa kwa mzizi kwa kuongeza kiambishi awali cha wingi hufanyika.

Mifano (2) na (3) ilinukuliwa kutoka kwa mazungumzo ya watafitiwa. Mifano yenyewe ilifuata utaratibu wa kunyambua mizizi kwa kuongeza kiambishi cha wingi 'ma':

| | ***Umoja*** | | ***Wingi*** |
|---|---|---|---|
| 2. | Nduthi (pikipiki) | = | Manduthi (pikipiki) |
| 3. | Digolo (miwani) | = | Madigolo (miwani) |

Neno la Sheng '*madigolo'* katika mfano (2) uliotolewa hapo juu limeundwa kwa kunyambua mzizi '*digolo'* ili kupata umbo lingine linaloashiria hali ya wingi. Kitendo chenyewe kimefanyika kwa kuongeza kiambishi awali 'ma-' cha mnyambuliko wa nomino katika Sheng'. Kitendo hicho hicho kimefanyika katika uzalishaji wa umbo '*manduthi'* ambalo limeundwa kwa kunyambua mzizi '*nduthi*' kwa kutumia kiambishi kile cha kubainisha hali ya wingi 'ma-'. Matokeo haya yanabainisha kuwa wazungumzaji wa Sheng' hutumia mofu ya mnyambuliko {ma} ili kubainisha hali ya wingi katika Sheng'.  Zifuatazo ni aina za uambishaji unaofanyika wakati wa mnyambuliko:

**(a) Uambishaji wa Viambishi Mseto**

Data iliyozalishwa na watafitiwa inaonyesha kuwa msamiati wa Sheng' unaweza kuundwa pia kwa kutumia viambishi awali na viambishi tamati kwa pamoja. Ijapokuwa kila kiambishi kina maana yake, uambishaji wa viambishi awali na tamati kabla na baada ya mzizi huzua msamiati ambao maana yake huwakilisha maana zilizokusudiwa. Mfano (4) ufuatao, ulionukuliwa kutoka muktadha wa shule, unaonyesha kuwa neno jipya la Sheng' linaweza kuundwa kwa kuunganisha viambishi mseto kwa kuzingatia kanuni 'O + Mzizi + O' ifuatavyo:

4. Hao maodijoz maboi-boi wanachapa wera vinoma joo!
   Hao walimu vijana vijana wanafanya kazi kwa bidii.

Neno '*maodijoz'* katika mfano (4) linadhihirisha leksimu inayoundwa kutokana na uambishaji wa viambishi mseto kama mbinu ya uleksikalishaji katika Sheng'. Hii ni kwa vile kiambishi awali 'o' kimetumiwa kabla ya mzizi kwa pamoja na kiambishi tamati 'o' ili kuunda neno '*odijo'* ambalo linanyambuliwa zaidi kwa kutumia viambishi viwili vya wingi '*ma'* na 'z' ili kuzalisha neno '*maodijoz'*. Neno hili linaafiki vigezo vya nadharia ya Pegitosca kama vile utusani na umataifa kwa vile halina sifa za upujufu na linahusiana na 'teacher' linalotumika katika Kiingereza kama lugha ya kimataifa. Mfano (5) ufuatao ulinukuliwa kutoka muktadha wa Nyalenda.

5. Yule ong'ong'o alituseti tukanaswa na wamama.
   Yule mtu mwenye sura mbaya alitupangia njama tukashikwa na akina mama.

Mofu '*ong'ong'o'* iliyotumiwa katika mfano (5) ni neno lenye asili ya Dholuo linalotumiwa kumrejelea mtu aliye na sura isiyovutia. Neno hili limetoholewa na kutumiwa katika Sheng' katika hali yake asilia, na kwa maana yake ya Dholuo vilevile. Neno hili kwa sasa limekubaliwa kama msamiati wa Sheng'. Neno hili '*ong'ong'o'* limeundwa kwa kuzingatia kanuni 'O + Mzizi + O'. Hii inamaanisha kuwa neno hili

limeundwa kupitia mnyambuliko ambapo, kwanza, mofimu amilifu ‘o’ ilitumiwa kama kiambishi awali cha unominishaji. Pili, mofimu ya kileksika ‘*-ng’ong’-’* ndiyo mzizi na hatimaye mofimu amilifu ‘o’ ilitumiwa kama kiambishi tamati. Ingawa neno hili liliundwa kupitia mnyambuliko, utafiti huu uligundua kuwa haliwezi kunyambuliwa ili kupata maneno mengine mapya kinyume na tarajio la Pegitosca.

**(b) Uambishaji wa Kiambishi -nga/-ngi cha Mazoea**

Kiambishi tamati ‘*-nga’* au ‘*-ngi’* hutumika katika Sheng’ ili kudokeza hali ya mazoea katika kitendo. Kiambishi hiki aghalabu hujitokeza mwishoni mwa mzizi wa kitenzi. Iligunduliwa kuwa matumizi ya mofu ‘*ngi’* au ‘*nga’* hutegemea tangamano la irabu. Hii ni kwa vile usaili wa watafitiwa wetu ulionyesha kuwa hatuwezi kunyambua vitenzi ‘*filingi’* kama ‘*filanga’* au ‘*kiringi’* kama ‘*kiranga’*. Maumbo yote ya Sheng’ yaliyotumia kiambishi hiki ‘*-ngi’* au ‘*-nga’* cha mazoea yalikuwa vitenzi kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo.

6. Anachezanga futa kwa chuo.
   Huwa anacheza kandanda akiwa shule.

7. Tunasafiringi manights.
   Huwa tunasafiri usiku.

8. Sigongangi sops.
   Huwa sinywi pombe.

9. Wanafilingi jij.
   Huwa wanahisi vibaya.

Utafiti huu umegundua kutokana na mifano (6), (7), (8) na (9) kuwa kiambishi cha mazoea ‘-ngi’ hutumiwa katika uleksikalishaji iwapo kitenzi cha Sheng’ ambacho kiko katika hali ya mazoea kinakanushwa kama ilivyo katika ‘*sigongangi’*. Aidha, kiambishi hiki kinatumiwa iwapo mzizi wa kitenzi unaisha kwa irabu ‘-i’ kama ‘*kiri’* ambapo

tunapata '*kiringi'*. Mifano hii inaashiria kuwa tangamano la irabu huhusika katika uamuzi wa kutumia ama '*-ngi'* au 'nga'.

Utafiti huu uligundua kuwa kiambishi hiki '*-nga'* au '*-ngi'* huambikwa katika maumbo ya Sheng' kama kibadala cha mofu 'huwa' ya Kiswahili. Inajitokeza kwa fahiwa hiyo kwamba mofu hii '*-nga'*/'*-ngi'* haiwezi kutumiwa iwapo kitendo kinachorejelewa ni cha kufanyika mara moja. Mifano ifuatao ina vitenzi vilivyonyambuliwa kwa matumizi ya mofu '*-nga'* au '*-ngi'*:

10. Nikirudingi mtaa najikuta niko na maboiz.
    Nikirudi nyumbani huwa najikuta na vijana wenzangu kila mara.

Kiambishi tamati '*-ngi'* kilichotumiwa katika neno '*nikirudingi'* linalojitokeza katika mfano (10) kinabainisha dhana ya mazoea. Neno lenyewe linakubalika kwa wazungumzaji wa Sheng' kama umbo lenye maana. Hivyo basi, mnyambuliko wa aina hii usipofanyika katika maumbo ya Sheng' dhana ya mazoea haitaweza kubainishwa. Haimaanishi kwamba neno 'huwa' limedondoshwa kwa vile neno lenyewe si sehemu ya msamiati wa Sheng'. Kimsingi Sheng' huwakilisha hali ya mazoea kwa kutumia kiambishi tamati chenye sura mbili '*-nga'* au '*-ngi'*.

### (c) Uambishaji wa Kubainisha Hali

Data iliyokusanywa kutoka kwa watafitiwa ilionyesha mwelekeo ambao baadhi ya maneno mapya yanaundwa kwa kunyambua vitenzi ili kubainisha kauli mbalimbali kama vile hali ya kutendea, kutendewa na kutendatenda. Jedwali 3.1 lifuatalo, kwa kutegemea data iliyokusanywa katika utafiti huu linaonyesha muhtasari wa namna mnyambuliko unavyoweza kufanyiwa vitenzi vya Sheng' kama mbinu moja ya uleksikalishaji.

**Jedwali 3.1: Mnyambuliko wa Vitenzi vya Sheng'**

| Mzizi | Hali ya kutenda | Hali ya kutendwa | Hali ya kutendatenda | Maana katika Sheng |
|---|---|---|---|---|
| *Lim* | *Lima* | *Limwa* | *Limwalimwa* | 1. Funga bao<br>2. Chapwa |
| *Mang* | *Manga* | *Mangwa* | *Mangamanga* | Kula |

Jedwali hili (3.1) ni dhihirisho la uambishaji katika Sheng'. Vitenzi viwili, *'lima'* na *'manga'* vimetumiwa kudhihirisha kauli anuai. Usemi ulionukuliwa kama mfano (11) una neno ambalo limeundwa kwa kunyambua neno la Sheng' '*manga'* lenye maana ya 'kula'.

11. Maze tulimangamanga food whole dei. Yaani tulimanga kumanga.
    Jameni siku hiyo tulizururazurura na tukala kweli kweli.

Neno jipya '*tulimangamanga'* limeundwa kwa kutanua mzizi wa kitenzi cha Sheng' *'mang-*' katika mfano (11). Neno '*manga'* pekee yake katika muktadha huu linamaanisha 'kula' lakini '*mangamanga'* ni neno lingine lenye maana ya 'kulakula mara nyingi'. Matumizi ya kirai [*tulimanga kumanga*] katika sehemu ya pili ya diskosi (11) inabeba fahiwa maalum inayohusu matumizi ya kipekee ya msamiati katika Sheng'. Hii ni kwa vile, neno la pili '*kumanga'* katika kifungu chenyewe '*tulimanga kumanga*' limetumiwa kama kielezi cha kuonyesha kiasi cha mlo ulioliwa na wahusika (kula kupita kiasi cha kawaida). Kisemantiki, matumizi ya neno hili '*mangamanga'* katika Sheng' ni tofauti na yale ya Kiswahili sanifu ambapo neno 'mangamanga' linatumika kuashiria 'kuzurura'. Ingawa mfano huu unaonyesha kuwa mbinu hii iliyotumiwa kuzalisha maumbo kama '*manga'* na '*manga kumanga'* inazingatia kigezo cha uzalishaji katika Pegitosca, mnyambuliko wa kutendatenda katika Sheng' una

upekee wake kwa kuwa kiambishi ‘*ku-*’ kinaweza kuongezwa kabla ya shina linalorudiwa katika hali ya kutendatenda kama ‘*manga* *ku*manga’. Utafiti huu ulioonyesha vilevile kuwa kitenzi hiki na vingine vya Sheng’ huweza kunyambuliwa zaidi ili kuibua maana nyinginezo kama ‘*mangwa’* na ‘*mangika’*.

Ufuatao ni mfano mwingine unaochukua mwelekeo huu wa kupanua msamiati kupitia mnyambuliko.

12. Tulilimwa mabao sita nil tukakaa mafala.
    Tuliingizwa mabao sita kwa nunge tukaonekana wajinga.

Mfano (12) uliotolewa hapo juu ulinukuliwa kutokana na mazungumzo ya watafitiwa waliochunguzwa katika shule moja iliyoteuliwa. Mfano wenyewe una neno la Sheng’ ‘*limwa’* ambalo limetumiwa katika Sheng’ kwa maana ya ‘kufungwa’ mabao. Neno hili kwa fahiwa hiyo halijatumika kwa maana ile inayobebwa na umbo hilo ‘*limwa’* katika Kiswahili.

13. Maodijoz walitulima ju tu ya kubonga Sheng’ daro.
    Walimu walituchapa kwa ajili ya kuongea Sheng’ darasani.

Mfano (13) umenukuliwa kutoka kwa muktadha wa shule tofauti na ile iliyozalisha mfano (12). Neno ‘*lima’* linalojitokeza katika mfano (13) lilitumiwa katika Sheng’ ili kuwakilisha fahiwa ya ‘*kuchapwa’* tofauti kabisa na vile linavyotumika katika Kiswahili kwa dhana ya ‘kuandaa shamba’. Kutumiwa kwa neno hili kwa jinsi tofauti tofauti katika sentensi hizi mbili (12) na (13) kunaonyesha kwamba mzizi wake ‘*lim-*’ unaweza kunyambuliwa kama ‘lima’ na ‘limwa’ ili kuwakilisha maana zinazotofautiana katika Sheng’. Uhalisia huu unaonyesha kuwa matumizi ya mbinu hii huzingatia kigezo cha uzalishaji kinachoangaziwa katika nadharia ya Pegitosca.

### 3.1.2 Uradidi

Uradidi ni mojawapo ya mikakati ya uleksikalishaji wa Sheng' iliyodhihirika katika data iliyokusanywa na mtafiti. Uradidi kama unavyojitokeza katika data ya utafiti huu ni mfanyiko tendani wa kimofolojia ambapo neno au kipande cha neno hurudiwa ili kuwakilisha sifa maalum za kisemantiki (Mgullu, 1999; Bauer, 1983). Mbinu hii ambayo ilitumiwa na watafitiwa kuzalisha karibu asilimia ishirini (20%) ya msamiati wa Sheng' hutumika pia katika upanuzi wa msamiati wa Kiswahili. Mara nyingi uradidi hufanya kazi ya kusisitiza au kukashifu kitu fulani. Uchunguzi huu umeonyesha kuwa kuna sura mbalimbali za uradidi unaofanywa katika Sheng'. Mathalani, kuna uradidi wa silabi za neno au wa neno zima.

#### 3.1.2.1 Uradidi wa Silabi

Uradidi wa silabi ni mbinu ya uleksikalishaji iliyotumiwa kwa njia ya kipekee katika uundaji wa maneno ya Sheng'. Tofauti na ilivyo katika Kiswahili, maneno ya Sheng' yalidhihirisha kurudiwarudiwa kwa silabi moja badala ya neno zima ili kuunda neno. Matumizi ya uradidi wa silabi ili kuunda maneno ya Sheng' kama yale yanayojitokeza katika mifano (14) na (15) hufuata misingi ya Pegitosca kama vile utusani, iktisadi na utaratibu. Hii ni kwa vile maneno hayawakilishi matusi, ni mafupi na yameundwa kwa kuzingatia utaratibu maalum. Hata hivyo, uchunguzi huu umeonyesha kuwa maneno yanayoundwa kupitia mbinu hii hayawezi kunyambuliwanyambuliwa zaidi ili kuunda maneno mapya ya Sheng'. Mfano (14) ufuatao vilevile umeundwa kwa kuzingatia mbinu ya uradidi wa silabi:

14. Nakwambia hi chuo si iko na <u>mabobo</u> hot hot?
    Nakwambia hii shule iko na wavulana wazuri wazuri.

Neno la Sheng' '*mabobo'* lililopigwa mstari katika mfano (14) limeundwa kwa kurudia mara mbili silabi '*bo'*. Neno hili limetoholewa kutoka neno la Kiingereza 'boy'. Hii inamaanisha kwamba silabi '*i*' katika neno 'boy' imedondoshwa wakati wa kulisimilisha umbo hili kwenye Sheng' ndiposa silabi moja ikatumika na kurudiwarudiwa.

15. Nimekiki jo. Niliwatch boli the whole night.
Nimesinzia mwenzangu. Nilitazama mpira usiku mzima.

Neno '*kiki'* lililopigwa mstari katika mfano (15) lina maana ya 'kusinzia' katika Sheng'. Watafitiwa waliolitumia walidai kuwa neno hili lina msingi wake katika neno la Kiingereza 'kill' (kuua). Hii inamaanisha kwamba neno '*kiki'* liliundwa kwa kurudia silabi '*ki'* maradufu. Shadda la fonimu [l] kwa hivyo hudondoshwa katika mchakato wa kuliunda neno '*kiki'* katika msimbo wa Sheng'. Neno hili linazingatia vigezo vya iktisadi na utusani walakini halizingatii vigezo vya mnyambuliko na umataifa. Huenda neno hili ni mfano wa baadhi ya maneno ya Sheng' yanayotumiwa kimaeneo kwa vile lilitumiwa tu katika muktadha wa shule ilihali matumizi yake hayakudhihirika kabisa katika mazungumzo ya watafitiwa waliochunguzwa mitaani.

### 3.1.2.2 Uradidi wa Neno zima

Utafiti huu uligundua kuwa maneno mapya yanaweza kuundwa kwa kurudiarudia neno zima mara mbili. Ilijitokeza kwamba kukaririwa kule kwa neno husababisha kuwakilishwa kwa maana tofauti na ile inayobebwa na umbo la neno ambalo halijakaririwa. Data katika mfano (16), (17) na (18) imeonyesha kuwa matumizi ya uradidi wa neno zima kama njia ya kuunda msamiati huzingatia kigezo cha Pegitosca cha mnyambuliko. Tuligundua kuwa baadhi ya msamiati wa Sheng' unaoundwa kwa

kutumia uradidi wa neno zima huzingatia hitaji la Pegitosca kwa vile unaweza kunyambuliwa ili kuzalisha '*lobaloba'*, na '*lobwalobwa'*.

Ifuatayo ni mifano ya sentensi zilizonukuliwa kutokana na mazungumzo ya watafitiwa inayoonyesha matumizi ya uradidi wa neno zima ili kuunda maumbo ya Sheng'.

16. Hii chuo madem na mabobo hulobaloba ka kawa.
    Wasichana na wavulana katika shule hii huanguka anguka mtihani na imekuwa kama kawaida.
17. Wameadmit wasupaa hot hot this year.
    Wamesajili wasichana warembo warembo mwaka huu.
18. Stevo ni deski wa mine ni mhunk, nimemnoki yote yote tho hanyiti.
    Mimi na Steven hukalia dawati moja darasani, ana sura nzuri, namtamani kabisa kabisa ingawa hajagundua.

Neno *'hulobaloba'* lililotumiwa katika mfano (16) ni umbo la Sheng' lililozalishwa kwa kukariri umbo '*loba'*. Kwa mujibu wa maelezo ya watafitiwa waliosailiwa katika utafiti huu, asili ya neno hili '*loba'* ni neno la Kiingereza 'lost' lililo na maana ya kupotea. Ili kuunda neno hili la Sheng' (*loba)* lile la Kiingereza 'lost' limefupishwa kisha umbo lile lililofupishwa 'lo-' likaongezewa silabi '-ba'. Uradidi wa neno unaozalisha '*lobaloba'* hubeba dhana mpya ya kufanyikafanyika kwa kitendo husika mara nyingi tofauti na '*loba'* linalorejelea kufeli mtihani mara moja pekee.

Neno la Sheng' lililotumiwa katika mfano (17) '*hot-hot'* limeundwa kutokana na neno la Kiingereza 'hot' lenye maana ya 'joto'. Hata hivyo, umbo hilo linachukuliwa katika Sheng' na kukaririwa kama kivumishi ili kuwasilisha maana ya 'mrembo' au 'warembo'. Uchanganuzi huu unabainisha kwamba mfanyiko huo wa kuunda msamiati si ukopaji kwa sababu maana ya neno linalozalishwa ni tofauti na maana ya umbo lililohusiana nalo katika lugha chasili. Umbo '*yote-yote*' lililojitokeza katika mfano (18) ni kivumishi kingine cha Sheng' kilichoundwa kwa kukariri umbo lililokuwa la Kiswahili 'yote' mara mbili lakini kwa maana tofauti, yaani 'kabisa'.

Mtafiti hakuweza kupata neno lolote la Sheng' lililoundwa kwa kukariri neno mara tatu au zaidi katika utafiti huu. Tasnifu hii inadokeza kwamba kutokuwepo kwa maneno kama haya kunafungamana na kigezo cha Pegitosca cha iktisadi. Hii ni kwa vile maumbo kama haya yangekuwa na idadi kubwa sana ya silabi itakayosababisha ugumu wa utamkaji.

### 3.1.3 Udondoshaji

Utafiti huu uligundua kuwa udondoshaji wa ama mofimu au silabi ni mbinu mojawapo inayotumiwa kuunda msamiati wa Sheng'. Tofauti na ufupishaji, mbinu hii huondoa sehemu ya neno kama silabi moja ili kupata neno jipya la Sheng'. Mbinu hii huunda maumbo ambayo huweza kuathiri usanifu wa insha za wanafunzi iwapo wanafunzi watatumia katika insha zao za Kiswahili kama 'ye' na 'ka' yanayojitokeza katika mfano (19).

19. Mash anadinda ju ye' hasaki doo ka' sisi.
    Macharia anakataa kwa sababu hatafuti pesa kama sisi.

Maumbo '*ye'* na '*ka'* yaliyotumika katika muundo (19) ni maneno ya Sheng' yaliyoundwa kupitia udondoshaji. Silabi moja '*ye'* imedondoshwa kutoka neno asili 'yeye' ili kuunda neno '*ye'* la Sheng'. Ili kuunda neno '*ka'* la Sheng', silabi moja '*ma'* imedondoshwa kutoka kwa neno la Kiswahili 'kama'. Hata hivyo, dhana za maneno haya mawili '*ye'* na '*ka'* zinadumishwa vile ilivyokuwa katika Kiswahili.

20. Na sa' niaje ile project nilikuwa naulizia niaje nayo?
    Na sasa ule mradi wetu umefika wapi?

Neno '*sa'* katika muundo (20) ni mfano mwingine wa umbo la Sheng' lililoundwa kupitia udondoshaji. Ili kuunda neno hili, silabi moja '*sa'* imedondoshwa kutoka kwa

neno la Kiswahili ‘sasa’. Ingawa mofu {*sa*} haijakamilika katika Kiswahili kama neno, mofu hii inakubalika kama neno katika Sheng. Utafiti wetu uligundua kuwa wazungumzaji wa Sheng’ hawahitajiki kuongeza silabi zilizodondoshwa ili maana ya mofu ‘*sa’* ieleweke. Inamaanisha basi kwamba umbo hili linaeleweka kama neno kamili katika Sheng’. Neno lenyewe ‘*sa’* linazingatia kigezo cha iktisadi cha nadharia ya Pegitosca kwa sababu limeundwa kwa idadi ndogo ya fonimu. Mfano (21) unaonyesha mfano wa mofu ambayo ni kiwakilishi cha nafsi huru ‘*mi’* inayoundwa katika Sheng’ kwa kudondosha silabi ya pili ya neno chanzi ‘mimi’.

21. Si unajua mi si chop ka wewe.
    Si unajua mimi huwa sipendi kusoma kama wewe.

Maneno mawili ya Sheng’ ambayo ni ‘*mi’* na ‘*ka’* ambayo yameundwa kwa kuzidondosha silabi za maneno chanzi yametumiwa katika mfano (21). Neno la Sheng’ ‘*mi’* limeundwa kutokana na kiwakilishi cha Kiswahili ‘mimi’. Kwa fahiwa hiyo, silabi ya pili ‘*mi’* imedondoshwa katika mchakato wa kuunda msamiati mpya. Uchunguzi wa sentensi zilizosheheni maneno ya Sheng’ kama ‘*mi’*, ‘*ka’* na ‘*sa’* ulidhihirisha kutumika kwa Kiswahili kama lugha solo. Jedwali hili (3.2) linaashiria uundaji wa msamiati unaotokana na udondoshaji silabi zilizokuwepo katika neno asilia.

**Jedwali 3.2: Udondoshaji kama Mbinu ya Uleksikalishaji**

| Neno asili | Msamiati wa Sheng' Unaoundwa | Ufafanuzi |
|---|---|---|
| Kama | 'Ka' | Silabi ya pili **'ma'** imedondoshwa katika Sheng' |
| Sasa | 'Sa' | Silabi ya pili **'sa'** imedondoshwa katika Sheng' |

Inadhihirika katika jedwali hili kwamba neno 'kama' limedondoshwa silabi 'ma'. Neno 'sasa' nalo limedondoshwa silabi 'sa'. Ifahamike kwamba silabi ya pili ndiyo inayodondoshwa katika mchakato huu wa uleksikalishaji.

### 3.1.4 Uhamishaji wa Maana

Uhamishaji wa maana ni mchakato ambapo maana ya neno tofauti linahamishwa kwa neno lingine ambalo litapoteza maana yake asili na kupata maana mpya (Brinton, 2005; Geeraerts, 1994). Matokeo ya utafiti huu yameonyesha vilevile kuwa uhamishaji wa maana ni mbinu nyingine inayotumiwa na wasemaji wa Sheng' ili kupanua msamiati. Uhamishaji wa maana unajitokeza katika matumizi ya neno 'mob' lililotumiwa katika usemi (22) ulionukuliwa kutoka mtafitiwa mmoja katika muktadha wa mtaa:

22. Makanjo watakuwa <u>mob</u> tao so hatuwezi drive ile ndai ya buda.
    Askari watakuwa wengi mjini kwa hivyo hatuwezi kuendesha gari la baba.

Mfano (22) unaonyesha kuwa neno '*mob'* lina maana ya 'wingi' katika Sheng'. Neno hili la Sheng' '*mob'* limetokana na neno la Kiingereza '*mob'* lakini halikukopwa na maana yake asili ambayo ni 'kundi la watu wenye fujo' au 'umma'. Kutumiwa kwa neno hili '*mob'* kumaanisha 'wingi' katika Sheng' kunaashiria kwamba mbinu ya ukopaji haikuzingatiwa. Badala yake, mfano huu unaonyesha kuwa uhamishaji wa

maana hutumiwa kama mbinu ya kupanua msamiati wa Sheng'. Neno hili hata hivyo halizingatii vigezo vya uangavu na mnyambuliko vya Pegitosca kwa kuwa linasababisha utata wa kutojua ni maana ipi inayolengwa wakati mwingine. Ufuatao ni mfano mwingine unaoonyesha kule kutumika kwa mbinu ya uhamishaji wa maana katika uleksikalishaji wa Sheng':

23. Msupu wako alini<u>shoo</u> nikushtue. Uliniambia juzi <u>nikuchoree</u> letaa umtumie.
    Mpenzi wako aliniambia nikukumbushe. Uliniambia juzi nikuandikie barua ili umtumie.

Usemi (23) una neno la Sheng' '*shoo'* unaonyesha pia namna msamiati hupanuliwa katika Sheng' kwa kuhamisha maana. Hii ni kwa vile maana asili ya neno lenyewe 'show' katika Kiingereza ilikuwa 'kuonyesha' lakini maana nyingine mpya 'kumwambia' imehamishiwa neno hili katika Sheng'. Hii inaashiria kwamba maana za maneno yenye asili ya lugha nyingine haziwezi kuhusishwa wakati wote na maana zao katika lugha chanzi.

Mifano mingine miwili inayohusu matumizi ya uhamishaji wa maana kama mbinu ya kuunda msamiati katika mfano (23) ni maneno ya Sheng' '*nikushtue'* na '*nikuchoree'*. Hii ni kwa kuwa, ingawa maneno haya mawili ni ya asili ya Kiswahili, yote yanatumiwa kwa maana tofauti katika Sheng'. Kwa mfano, umbo '*nikushtue'* limeingizwa katika Sheng' na likahamishiwa maana mpya ya 'kukumbusha' au kuarifu'. Maana asilia ya neno *'nichoree'* nayo inapuuzwa na kuhamishiwa maana mpya 'uniandikie'. Maana hii mpya, yaani uchoraji, haingehusiana moja kwa moja na uandishi wa barua katika Kiswahili sanifu. Matokeo haya yote yanaashiria uhamishaji wa kimaana kama utaratibu wa kuchukua msamiati kutoka lugha nyingine na kupatia maana mpya katika Sheng'. Utaratibu huu haujawa ukitumika katika uundaji wa maneno ya Kiswahili

ndiposa unajitokeza kama baadhi ya njia za kipekee zinazotumiwa katika Sheng'. Tazama mfano ufuatao:

24. Nilipatana na Timo drama fest akanilenga ni ka hajawai niona.
    Nilikutana na Timothy katika tamasha za drama akanipita kana kwamba hajawahi kuniona

Mbinu ya uhamishaji wa maana imetumiwa ili kuingiza neno '*lenga'* lililotumiwa katika mfano (24) katika msamiati wa Sheng'. Hii ni kwa sababu '*lenga'* katika Kiswahili sanifu humaanisha kunuia kufikia shabaha. Walakini, neno hili limeingizwa katika Sheng' ijapokuwa kwa maana tofauti ambayo ni 'kumpuuza au kutomwona mtu'. Tazama pia mfano (25) ufuatao:

25. Op una-chop poa, mi nimeiva kwa fik na ngoso.
    Nataraji unasoma vyema, mimi ninaelewa sana masomo ya Fisikia na Kiingereza.

Neno '*iva'* katika Kiswahili humaanisha kukomaa au kuwa tayari kuliwa kwa matunda na baadhi ya vyakula vinavyopandwa shambani. Wasemaji wa Sheng, kwa upande mwingine, wamezingatia mbinu ya uhamishaji wa maana ili kuliongeza kwa msamiati wa Sheng'. Huu ni mfano wa uhamishaji wa maana kwa vile maana ya 'kujimudu' imehamishwa kwa umbo ambalo katika lugha chasili lilikuwa likimaanisha 'kukomaa'. Mfano ufuatao unaonyesha uhamishaji wa maana unaohusu kutumiwa kwa umbo kama '*toboa'* lakini kwa kulipatia maana husishi. Kwa mfano:

26. This year round sidhani kama tutatoboa.
    Mwaka huu sidhani kama tutafaulu.

Neno la Sheng' lililo na asili ya Kiswahili '*toboa'* katika mfano (26) linamaanisha 'faulu' katika msimbo wenyewe. Neno hili lina fahiwa tofauti katika Kiswahili kwa vile lina maana ya kuweka mashimo kwenye kitu. Inajitokeza basi kwamba maana mpya ya kufaulu ambayo kifahiwati inahusiana na kufanikiwa imehamishwa kwa umbo

lililokopwa. Hii inamaanisha kuwa umbo pekee lilikopwa bila maana yake kisha likapewa maana mpya katika Sheng' kama msimbo pokezi. Neno hili halina sifa ya umataifa lakini linaweza kunyambuliwanyambuliwa ili kupata maneno mengine ya Sheng' na kwa hivyo linatimiza baadhi ya mahitaji ya Pegitosca. Mfano (27) ufuatao unadhihirisha uhamishaji wa kimaana unaohusu kivumishi.

27. Hiyo chuo ni mixed lakini ina madem kibao.
Hiyo shule ni mseto lakini ina wasichana wengi.

Uhamishaji wa kimaana ulitumika katika mfano (27) kama mbinu ya uleksikalishaji ambapo neno lenye asili ya Kiswahili *'kibao'* lililo na maana ya kipande cha mti limekopwa na kupewa maana mpya katika Sheng'. Uhamishaji huo unahusu kugeuzwa pia kwa nomino '*kibao'* kuwa kivumishi kinachomaanisha wengi. Hata hivyo, uchunguzi huu ulibainisha kuwa neno kama hili linaloundwa kupitia uhamishaji wa maana haliwezi kunyambuliwa ingawa linazingatia vigezo vya Pegitosca kama vile ikitisadi na utusani.

### 3.1.5 Ufinyaji wa Maana

Ufinyaji wa maana ni mbinu ya uleksikalishaji ambapo umbo lenye maana inayorejelea dhana pana linapoteza hali hiyo na fahiwa yake inapunguzwa ili litumike kurejelea fahiwa finyu pekee (Yule, 2006; Geeraerts, 1994). Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa mbinu hii ya ufinyaji wa maana hutumiwa katika uleksikalishaji wa Sheng'. Kwa mfano, baadhi ya maneno yaliyokuwa na maana pana katika lugha chanzi kama vile Kiswahili yamepewa maana finyu ili kurejelea kirejelewa kimoja au sehemu ndogo katika Sheng. Ufinyaji wa maana kama mbinu ya uleksikalishaji umehusika katika uundaji wa neno la Sheng' '*mtaa'* ambalo limetumiwa katika usemi ufuatao [ambao umerudiwa kama mfano (28)] :

28. Nikirudingi <u>mtaa</u> najikuta niko na maboiz.
    Nikirudi nyumbani huwa najikuta niko na vijana wenzangu.

Neno la Sheng' '*mtaa'* lililotumiwa katika mfano (28) lina asili ya Kiswahili. Walakini, katika harakati za kupanua msamiati wa Sheng', mbinu ya ufinyaji wa maana imetumiwa ambapo neno hili limepoteza maana yake asili na likapewa maana mpya. Mbinu hii ya uleksikalishaji ni ufinyaji kwa vile maana yake katika Kiswahili ilikuwa ikirejelea 'eneo pana' lakini imeweza kupunguzwa katika Sheng' ili kurejelea 'nyumba pekee'. Utafiti huu umegundua kuwa mbinu hii inazingatia vigezo vya nadharia ya Pegitosca kama mnyambuliko, utusani na ikitisadi.

### 3.1.6 Uundaji Kinasibu

Uundaji wa kinasibu ni ubunifu na unahusu hali ambapo neno jipya kabisa linaundwa ili kurejelea kitu, dhana au hali (Kingei, 2000; Okombo, 2000). Uchunguzi huu umegundua kuwa uundaji wa kinasibu ni mbinu nyingine ya uleksikalishaji inayotumiwa kupanua msamiati wa Sheng'. Maneno ya Sheng' yaliyoundwa kwa kuzingatia mbinu hii hayana uhusiano wa moja kwa moja na dhana au kiashiriwa. Msamiati unaoundwa huzingatia mpangilio wa fonimu na silabi uliozoeleka katika Sheng'. Data inaashiria kwamba uundaji wa kinasibu haiigizi milio au tabia za virejelewa katika mchakato wa uleksikalishaji. Mfano (29) ufuatao, ambao ulikusanywa kutoka kwa muktadha wa Nyalenda, una maneno ya Sheng' yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii.

29. Mafruits ziko wapi, wamama <u>wanatusenya</u> .
    Matunda yako wapi, akina mama wanatudanganya.

Neno '*senya'* lililotumiwa na watafitiwa katika mfano (29) linamaanisha 'kudanganya'. Watafitiwa waliosailiwa na mtafiti katika mtaa wa Nyalenda, ambapo usemi wenyewe

(29) ulizalishwa, walidai kwamba wao wenyewe waliunda neno lenyewe pasipo kulihusisha na maneno mengine, milio au tabia. Hii inamaanisha kwamba wao waliunda neno husika kinasibu. Tokeo hili linaonyesha kwamba ubunifu wa wazungumzaji unaweza kusaidia katika upanuzi wa msamiati wa launi ya lugha. Usaili huo uliweza kubainishwa kwamba neno hili linaweza kunyambuliwanyambuliwa kama '*senywa*', '*senyika*', '*senywasenywa*'. Hii inaashiria kuwa mbinu hii ya uleksikalishaji inazingatia nguzo ya Pegitosca inayorejelewa kama uzalishaji. Usemi (30) ufuatao ambao ulinukuliwa kutoka mazungumzo ya watafitiwa katika muktadha wa shule una mfano mwingine wa neno lililoundwa kinasibu.

30. Mzae <u>anadoradora</u> na nimesota vibaya maze.<u>.</u>
    Baba (mzazi) anachelewachelewa (hafiki) na nimeishiwa na pesa jameni.

Usaili wa watafitiwa ambao walizalisha mfano (30) ulionyesha pia kwamba neno lililopigwa mstari '*doradora*' limeundwa kwa kunyambua shina la kitenzi cha Sheng' '*dora*'. Neno hili linamaanisha 'kuchelewa'. Usaili huo ulibainisha vilevile kwamba wazungumzaji haohao waliotumia neno hili waliliunda na kulitumia katika muktadha wao. Hii inadokeza pia kwamba neno la aina hii linaweza kuundwa katika eneo moja lakini baadaye likasambazwa na kutumiwa katika miktadha mingineyo. Kuundwa kwake kinasibu kunamaanisha kuwa liliundwa kiubunifu. Neno la Sheng' lililopigwa mstari katika mfano ufuatao liliundwa kinasibu kwa mujibu wa watafitiwa.

31. Exam zikifika mi <u>huloba</u> sijui ka... nini.
    Mitihani ikija (mimi) huwa ninaanguka sana sijui mithili ya nini.

Neno '*loba*' lililotumika katika sentensi (31) kwa mujibu wa usaili wetu limeundwa kinasibu pasipo kuigiza tabia za kitendo husika, kukopa au kupanua maana. Hili ni neno ambalo kwa mujibu wa usaili uliofanywa katika utafiti huu, liliundwa kiubunifu tu. Hii

inamaanisha kwamba hakuna uhusiano wa moja kwa moja wa kitabia au kisemantiki kati ya neno '*loba'* na maana yake 'kuanguka'.

### 3.1.7 Ufupishaji-tohozi

Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kwamba ufupishaji-tohozi ni mbinu ya uundaji wa msamiati inayotumiwa zaidi katika msimbo wa Sheng' kuliko mbinu nyinginezo. Utafiti huu uligundua kuwa mchakato wa ufupishaji-tohozi huanza kwa ukopaji wa msamiati kutoka lugha chasili kisha linafupishwa. Hatua itakayofuata ni kule kutoholewa kwa umbo jipya. Hatimaye umbo lililofupishwa na kutoholewa litaweza kuunganishwa na viambishi vifaavyo kama vile vya umoja au wingi ama vya nafsi na wakati ili liweze kuwakilisha maana kwa mujibu wa muundo wa Sheng'. Data imeonyesha kwamba aghalabu ni mizizi ambayo hufupishwa ndiposa iweze kubeba maana iliyokuwa ikisheheniwa na neno asilia. Utafiti huu haukupata mifano yoyote ya mofimu amilifu kama vile viambishi, viunganishi na vihusishi zilizofupishwa katika Sheng'.

Uchanganuzi huu unabainisha kuwa maneno ya Sheng' yaliyoundwa kwa kuzingatia mbinu hii yanaafiki vigezo vingi vya Pegitosca. Kwa mfano, maneno yenyewe yanatimiza kigezo cha iktisadi. Baadhi ya maneno yanayoundwa katika Sheng' yanaweza kufupishwa kisha yakatoholewa ili yafanane na maumbo mengine ya Sheng'. Kwa mfano, wazungumzaji wa Sheng' wangetarajiwa kuunda neno jipya la Sheng' kwa kulifupisha neno 'mtoto' labda kama '*mto'* lakini inajitokeza kwamba wanachukua hatua ya pili ya kulitohoa umbo lililofupishwa kwa kuongeza irabu kama silabi ya mwisho. Kwa jinsi hiyo, msamiati wa Sheng' '*mtoi'* unaibuka.

Mfano mwingine wa neno lililoundwa kwa ufupishaji-tohozi ni neno la Sheng' '*tizi'* ambalo limeundwa kwa kulifupisha neno la Kiingereza 'practice' kuwa 'tice' na kulitohoa umbo lililozalishwa kuwa '*tizi'*. Usaili wa watafitiwa wetu uliashiria kwamba neno '*tizi'* linaafiki kigezo cha ukubalifu cha Pegitosca kuliko 'tice' katika Sheng'. Hii inaashiria kuwa utohozi huchan+gia ukubalifu wa msamiati katika lugha. Mfano (32) ufuatao una neno 'tizi' lililoundwa kwa njia ya ufupishaji tohozi.

32. Hivi sasa tumemada teo ya end term. Tunafanya <u>tizi</u> za bake.
    Hivi sasa tumekamilisha mtihani wa mwisho wa muhula. Tunafanya mazoezi ya mpira ya vikapu.

Neno '*tizi'* lililotumiwa katika usemi wa mtafitiwa ulionukuliwa kama mfano (32) hapo juu lina maana ya mazoezi katika Sheng'. Kwa mujibu wa watafitiwa wa utafiti huu, neno hili limetumika kwa muda mrefu bila kutafutwa kwa kibadala chake kwa sababu linaeleweka na linakubalika miongoni mwa vijana wanaozungumza Sheng'.

### 3.1.7.1 Ufupishaji-tohozi wa Nomino za pekee

Nomino za pekee ni nomino zinazotaja virejelewa kwa majina yao maalum. Nomino za aina hii hutaja majina mahususi ya watu, nchi, miji, mikoa, milima, makabila, lugha, mito, maziwa, bahari, sayari na majengo. Majina mengi ya wenzao yaliyotumiwa na wanafunzi waliotumia Sheng' ambao walichunguzwa katika utafiti huu yalidhihirisha kule kutumiwa kwa mbinu hii. Mifano ifuatayo imerudiwa kama (33), (34) na (35) kwa lengo la kudhihirisha maneno ya Sheng' yaliyoundwa kwa kutumia mbinu ya ufupishaji-tohozi wa nomino za pekee.

33. Niaje <u>Vini</u> umekawia ka hujanichorea leta yoyote maze.
    Habari yako Vincent, umekawia kabla ya kuniandikia barua.

34. Stivo ni deski wa mine, ni mhunk, nimemnoki yote yote tho hanyiti.
Mimi na Stephen hukalia dawati moja darasani, ana sura nzuri, namtamani lakini hana habari.

35. Nilipatana na Timo drama fest akanilenga ni ka hajawai niona.
Nilikutana na Timothy katika tamasha za drama akanipita kana kwamba hajawahi kuniona.

Mfano (33) unaonyesha matumizi ya mbinu hii katika upanuzi wa msamiati wa Sheng'. Jina 'Vincent', katika mfano huo, ambalo ni la asili ya Kiingereza limefupishwa na kuwa '*Vini'* katika Sheng'. Mifano mingine miwili inajitokeza katika mazungumzo ya watafitiwa (34) na (35) ambapo jina 'Timothy' lenye asili ya Kiingereza limefupishwa kuwa '*Timo'* katika Sheng'. Ufupishaji wa jina 'Stephen' ili kupata '*Stivo'* limehusisha badiliko la kifonolojia ambapo sauti inayotamkwa kwenye midomo [p] iliachwa na nafasi yake ikachukuliwa na sauti inayotamkwa kwa kutumia ufizi wa chini na meno ya juu [v] na nafasi ya irabu ya nusu-chini [e] ikachukuliwa na irabu ya juu [i]. Hata hivyo, kama inavyojitokeza katika majina haya matatu '*Vini'*, '*Timo'* na '*Stivo'*, Sheng' ina mwelekeo wa kutumia irabu ili kukamilisha majina ya watu yaliyokopwa. Ifuatayo ni mifano mingine ya usemi wa watafitiwa uliosheheni maneno ya Sheng' yaliyofupishwa. Mifano yote miwili ni ya nomino za pekee zinazotaja majina ya pekee yanayotaja mahali.

36.Walahi nikishamada fourth naishia Nai na sirudi ata.
Walahi nikimaliza kidato cha nne nitaenda Nairobi na sitarudi kamwe.

Jina lenye silabi nne 'Nairobi' katika mfano (36) limefupishwa na kuwa umbo lenye silabi mbili '*Nai'* katika Sheng'. Ufupishaji kama huo kwa mujibu wa watafitiwa tuliowasaili hulenga kurahisisha mazungumzo. Hii ni kwa vile silabi nyingi zinaondolewa katika neno. Tazama mifano mingine ya nomino zilizofupishwa katika mfano ufuatao:

37. After fest tulienda steto kuimbia prezzo maze ni kunoma.
    Baada ya tamasha tulienda ikulu kumwimbia rais, nakwambia ni kuzuri.

Ufupishaji wa nomino umetokea mara mbili katika mfano (37). Mathalani, neno la Kiingereza 'festival' lilifupishwa kuwa '*fest'* katika Sheng'. Hata hivyo, neno hili, '*fest'*, limekopwa na likafupishwa pasipo kutoholewa kwani sehemu yake ya mwisho '-ival' pekee imeondolewa katika umbo lililozalishwa katika Sheng'. Mifano mingine katika sentensi hii ni maneno *'steto'* lililokopwa kutoka Kiingereza, 'statehouse' na kufupishwa, na *'prezzo'* ambalo vilevile limekopwa kutoka Kiingereza 'president' na kufupishwa pasipo kutoholewa. Baadhi ya watafitiwa walidai kuwa uzungumzaji wenye ufupishaji wa aina hii huvutia. Dai hilo linaashiria kwamba haja ya kufanya mazungumzo yavutie linaweza kuwa motisha moja inayowasababisha vijana wafanye ufupishaji mwingi katika Sheng'. Tazama pia mfano (38) ufuatao:

38. After that tulimwomba masa aturuhusu kwenda Gikosh, na akakubali.
    Baada ya hiyo tulimuomba mama aturuhusu kwenda Gikomba, na akakubali.

Neno 'Gikomba' limeundwa kwa kutumia mbinu ya ufupishaji-tohozi katika mfano (38). Hili ni jina la soko moja kuu kule Nairobi. Jina hili lenye silabi tatu limefupishwa na kuwa neno lenye silabi mbili '*Giko**sh**'*. Utohozi uliofanywa baada ya kufupishwa kwa umbo lenyewe 'Gikomba' uliongeza sauti '*-sh'* na hatimaye neno lililozalishwa limeweza kutamkwa kama maneno mengine ya Sheng' kama '*mre**sh**'* (mrembo) na '*mtu**sh**'* (mtumba). Kwa mujibu wa matokeo haya yanayohusu ufupishaji-tohozi wa majina ya pekee, inajitokeza kuwa ufupishaji huu huenda usitoe mchango kwa ukuaji wa Sheng' kwa jinsi sawa na ufupishaji wa majina yanayotaja virejelewa vipya ambavyo havijakuwa na majina katika msimbo wenyewe kama sehemu za tarakilishi au majina ya kiteknolojia.

### 3.1.7.2 Ufupishaji-tohozi wa Nomino za kawaida

Nomino za kawaida hutaja virejelewa kwa jumla bila kubainisha majina yao mahususi. Mifano ifuatayo ni mazungumzo ya wanafunzi yaliyonukuliwa na mtafiti yenye nomino za jumla za Sheng' zilizoundwa kwa kufupisha.

39. Mapero na siz wako wako poa. Mi naye sioni laif kwa hiyo saamo.
    Wazazi na dada zako ni wazima. Lakini mmi sioni kama hayo mambo yataendelea.
40. Acha kulenga nipe risto za mresh… kwani we' ni mtoi?
    Acha kuhepa, nipe habari za mrembo…kwani wewe ni mtoto?

Kuna maneno matatu ya Sheng' ambayo yamefupishwa katika mfano (39). Neno la kwanza ni '*mapero'* ambalo limekopwa na kufupishwa kutokana na neno la Kiingereza 'parents'. Ufupishaji wenyewe umefanyiwa mzizi wa neno 'parent' kuwa '*par'* kisha sauti 'a' ikageuzwa kuwa 'e', halafu fonimu 'o' ya unominishaji katika Sheng ikaongezwa baada ya mzizi huo na hatimaye mofu 'ma' ya wingi ikaambikwa. Fonimu hiyo 'o' ya unominishaji ilijitokeza katika maumbo mengine ya Sheng' kama '*pero'* (parents), '*odijo'* (teacher), '*storo'* (story) na '*samo'* (something). Watafitiwa wetu hawangeweza kueleza ni kwa nini hawangetumia 'a' ili watamke '*maparo'* badala ya '*mapero'*. Hii inaashiria kwamba uteuzi wa fonimu zinazotumiwa kuunda msamiati hufanywa kinasibu pia.

Neno la pili ambalo limefupishwa katika mfano (39) ni '*siz'*. Huu ni msamiati wa Sheng' unaotokana na neno la Kiingereza 'sister', lenye maana ya 'dada'. Neno la tatu lililofupishwa katika mfano (39) ni '*saamo'*. Neno hili limefupishwa kutoka neno la Kiingereza 'something' ambalo lina maana ya kitu. Mifano hii '*siz'* na *'saamo'* inazingatia kigezo cha iktisadi cha Pegitosca ingawa maneno yenyewe hayawezi kunyambuliwa.

Ufupishaji-tohozi wa nomino za kawaida umejitokeza mara mbili katika mfano (40) uliozalishwa na watafitiwa waliochunguzwa mtaani. Neno ‘*mresh’* ni kifupi cha kiwakilishi ‘mrembo’. Umbo hili ‘*mresh’* ni fupi kwa sababu lina silabi mbili $*m*$ na $*resh*$ ilihali neno ‘mrembo’ lina silabi tatu $m$re$mbo$. Neno hili ‘*mresh’* linazingatia kigezo cha ikitisadi cha Pegitosca kwa sababu limeundwa kwa sauti ambazo hazipiti tano na silabi zake hazipiti tatu.

Mifano (39) na (40) iliyonukuliwa kutoka kwa watafitiwa ina viwakilishi viwili huru vya nafsi ya kwanza umoja na nafsi ya pili umoja vya Sheng’ ambavyo ni ‘*mi’* na ‘*we’*. Viwakilishi hivi viwili ‘*mi’* na ‘*we’* vimeundwa kwa kufupisha maneno ya Kiswahili ‘mimi’ na ‘wewe’. Maumbo haya mawili ‘*mi’* na ‘*we’* yanakubalika katika Sheng’ lakini hayawezi kukubalika katika Kiswahili sanifu. Uchunguzi huu uligundua kuwa viwakilishi vya nafsi vya Sheng’ vilivyoundwa kwa kutumia mbinu hii ni ‘*mi’* (nafsi ya kwanza umoja), ‘*si’* (nafsi ya kwanza wingi) na ‘*we’* (nafsi ya pili umoja) pekee.

Matokeo ya utafiti huu hayakudhihirisha viwakilishi vya nafsi vya Sheng’ vinavyoundwa kutokana na viwakilishi vya nafsi vya Kiswahili kama vile nyinyi, yeye na wao. Isitoshe, neno ‘*mtoi’* lililotumiwa katika mfano (40) limeundwa kwa matumizi ya mbinu ya ufupishaji. Ufupishaji unaojitokeza katika umbo hili unahusu idadi ya fonimu zilizotumika. Hii ni kwa kuwa, umbo la neno chasili la Kiswahili – ‘mtoto’ na umbo la neno zalishwa la Sheng’ ‘*mtoi’* hufanana kwa mujibu wa idadi ya silabi. Matokeo ya usaili wa watafitiwa kuhusu sababu za ufupishaji wa aina hii usiopunguza idadi ya silabi uliashiria kuwa Sheng’ hutumiwa na vijana wanaopenda ubunifu na usemaji unaokiuka kaida za kutumia lugha. Idadi ya fonimu zilizounganishwa ili kuunda neno ‘*mtoi’* inaashiria kwamba neno lenyewe linazingatia kigezo cha ikitisadi cha Pegitosca. Tazama pia mfano ufuatao:

41. Yule odijo hupendanga kuvaa mitush ndo alikuwa duty.
    Yule mwalimu ambaye hupenda kuvalia nguo kuukuu ndiye aliyekuwa zamu.

Sentensi hii ina maneno mawili ambayo yamefupishwa. Kwanza neno '*odijo'* ni kifupisho cha neno la Kiingereza 'teacher' lenye maana ya mwalimu. Neno la pili ni '*mitush'*, na ni kifupi cha neno mitumba, yaani aina ya nguo kuukuu. Mfano ufuatao pia unashuhudia ufupishaji-tohozi.

42. Ninaburn hapa chuo maze nimesota, si uniokolee tu hata finje?
    Ninachomwa na chai bila mkate asubuhi hapa shuleni sina pesa, si unitumie hata shilingi hamsini?

Katika sentensi hii neno lililofupishwa ni '*finje'*. Neno la Sheng' '*finje'* limetokana na neno la Kiingereza 'fifty' ambalo lina maana ya hamsini. Mfano '*finje'* na mifano mingine iliyojitokeza katika data iliyochanganuliwa katika utafiti huu ni dhihirisho tosha kuwa ufupishaji-tohozi ni mbinu ya kuunda msamiati inayopendwa mno na wazungumzaji wa Sheng'.

### 3.1.8 Uundaji Kiakronimia

Hii ni mbinu ya uleksikalishaji ambayo inahusu ufupishaji wa maneno kwa ajili ya kuunda leksimu mpya (Bauer, 1983; Temu, 1990). Aghalabu herufi au silabi za mwanzo wa maneno yanayofupishwa, huunganishwa ili kujenga umbo jipya linalobeba maana. Mbinu hii haitumiwi mara nyingi katika uundaji wa msamiati (Obuchi na Mukhwana, 2010). Maneno mengi ya Kiswahili yaliyoundwa kwa kuzingatia mbinu hii ya uleksikalishaji ni majina ya vyama na mashirika.

Akronimia ni mbinu ya uleksikalishaji iliyotumiwa katika Sheng' ambapo maneno yaliundwa kwa kutumia baadhi ya herufi husus an za maneno makuu kutoka sentensi. Mara nyingi mofimu amilifu huwa hazishirikishwi katika kuunda maneno kiakronimia.

Uteuzi wa silabi za kushirikishwa katika akronimia hutegemea miundo ya silabi za lugha inayohusika. Neno la Sheng' lililoundwa kwa matumizi ya mbinu hii limepigwa mstari katika mfano (43) ufuatao:

43. Alikuwa friend wa madidis ndo amenunua ndinga ka prezo.
    Alikuwa rafiki wa walanguzi wa dawa za kulevya ndiposa amenunua magari kama rais.

Neno '*madidis'* ni umbo la Sheng' lililoundwa kiakronimia kutokana na maneno mawili 'drug dealers'. Hii inamaanisha kwamba sauti za kwanza katika neno 'drug' (d) na neno 'dealers' (d) zilitumiwa kiakronimia kuunda neno '*madidis'*. Umbo kama hili hususan linaweza kueleweka ikiwa litatumiwa na wazungumzaji wa Sheng' wanaomiliki umilisi sawa wa kisemantiki, yaani, wanaolijua na wanajua maana yake. Hii ni kwa vile umbo hilo '*madidis'* litaweza kukosa maana au hata likaweza kuwa na maana tofauti katika eneo lingine ambapo Sheng' huzungumzwa. Ufuatao ni mfano mwingine tena unaoonyesha namna akronimia inavyotumiwa kama mbinu ya uleksikalishaji katika Sheng'.

44. Nitakam kesho mangware sa unigei 1k chali yangu.
    Naja kesho asubuhi na mapema, kwa hivyo uniazime shilingi elfu moja rafiki yangu.

Mfano (44) umeonyesha kuwa wazungumzaji wa Sheng' hutumia umbo '*k*' kiakronomia ili kurejelea '*kapaa'*. Neno hili '*kapaa'* ni leksimu ya Sheng' na linamaanisha elfu moja. Tokeo hilo linaashiria kwamba akronimia huweza kutumiwa kama mbinu ya uleksikalishaji katika Sheng' kwa njia ya kipekee. Hii ni kwa kuwa hata sauti moja, mfano wa '*k*' inaweza kutumiwa. Wasikilizaji wanaweza kumwelewa mzungumzaji wa Sheng' anayeomba asaidiwe shilingi elfu moja anaposema '*k*'. Hii ni kwa maana umbo husika linakuwa sehemu ya umilisi wa kimofolojia wa wazungumzaji

wa Sheng' baada ya kukamilika kwa mchakato wa uleksikalishaji. Mfano huu unaonyesha kuwa, kinyume na mahitaji ya nadharia ya Pegitosca, ni vigumu kufanyia mnyambuliko umbo linaloundwa kwa kutumia mbinu hii ili kuzalisha maneno mapya ya Sheng'.

### 3.1.9 Urefushaji wa Umbo

Utafiti huu uligundua kuwa baadhi ya msamiati wa Sheng' huundwa kuzingatia mbinu ya urefushaji. Mifano ya maneno ya Sheng' yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii ni pamoja na '*beshte'* (kutokana na 'best'), '*tokelezea'* kutokana na 'tokea' na '*maze'* kutokana na 'man'.

Watafitiwa saba tuliowahoji walidai kwamba neno la Sheng' 'maze' linalojitokeza katika mfano (45) lilizalishwa kutokana na neno '*man'* la Kiingereza. Kimsingi neno la asili 'man' limeundwa kwa fonimu tatu lakini neno zalishwa '*maze'* lina fonimu nne. Ni kwa fahiwa hii ambapo tasnifu hii imechanganua mfano huu kama mbinu ya kuunda msamiati kwa kulirefusha umbo asilia. Neno hili haliambatani na jinsia ya kiume katika Sheng' ndiposa linatumiwa kurejelea jinsia ya kike na kiume tofauti na ilivyo kwa Kiingereza ambapo 'man' linamrejelea 'mwanamume'. Hata hivyo, uchunguzi huu ulibainisha kuwa mbinu yenyewe hutumiwa kuunda maneno machache. Licha ya urefushwaji uliofanywa, neno '*maze'* linazingatia sharti la iktisadi la Pegitosca. Tazama mfano huu:

45. <u>Maze</u>, buda amechizi.
    Bwana, mzee ameshikwa na kichaa.

Neno la Sheng' '*tokelezea'* lililotumiwa katika mfano (46) limeundwa kulirefusha shina la kitenzi cha Kiswahili 'tokea'. Mfanyiko huu wa uleksikalishaji si mnyambuliko kwa

sababu neno ‘tokea’ la Kiswahili na ‘*tokelezea’* la Sheng’ hayana maana tofauti vile inavyojitokeza katika ufafanuzi wa Masabo (1995). Neno hili lilitumiwa mara nyingi na watafitiwa katika miktadha ya shule na mitaa katika uchunguzi huu. Asilimia tisini (90%) ya watafitiwa waliohojiwa katika utafiti huu walitaja kwamba neno ‘*tokelezea’* ni la Sheng’ isipokuwa baadhi ya walimu na wanafunzi hivi sasa wanalitumia kama la Kiswahili sanifu katika mazungumzo yao. Matumizi ya mbinu hii yanaashiria uhuru alionao binadamu wa kuunda msamiati kwa kurefusha au kufupisha msamiati kama alivyo na uhuru wa kishairi wa kutumia inkisari (kufupisha) na mazida (urefushaji). Shuhudia mfano ufuatao:

46. Mamanzi wametokelezea vipoa.
    Wasichana wameonekana warembo.

Mifano mingi ya maneno ya Sheng’ yaliyoundwa kwa kutumia urefushaji kama mbinu ya uleksikalishaji, kama vile ‘*maze’* na ‘*tokelezea’* katika mifano (45) na (46), yanazingatia vigezo vya Pegitosca kama vile utusani, uangavu na utaratibu ulio sawa. Walakini maneno yenyewe hayadhihirishi sifa za ikitisadi na uzalishaji.

### 3.1.10 Uundaji wa Kiantonimia

Antonimia ni uhusiano wa kisemantiki ambapo maumbo au miundo huhusiana kwa njia ya unyume (Cruse, 1986; Dahlgren, 1988). Istilahi hii ‘antonimia’ imetumiwa katika tasnifu hii ili kurejelea mbinu ya kipekee inayotumiwa kuunda msamiati wa Sheng’ ambapo neno linachukuliwa kutoka lugha chasili na kupewa maana nyingine ambayo ni kinyume cha maana yake asili. Maana ya neno ‘*lenga’* lililotumiwa katika mfano (47) ufuatao katika Sheng’ (msimbo pokezi) ni kinyume cha maana yake katika Kiswahili (lugha chasili). Hii inamaanisha kwamba mbinu ya unyume au antonimia imetumiwa ili kushirikisha neno na kulipatia maana katika Sheng’. Kwa mfano:

47. Wameni<u>lenga</u> sana, hata hawanitumii doo tena.
    Wamenisahau sana, hivyo hawanitumii pesa.

Muundo (48) nao ni usemi ulionukuliwa kutoka kwa vijana waliochunguzwa katika mtaa mmoja. Umbo '*mnoma'* ni neno la Sheng' lililoundwa kwa kuzingatia mbinu ya antonimia. Hii ni kwa vile neno hili '*mnoma'* lenye maana ya 'hodari' limezalishwa kwa kuipatia maana mpya neno la Sheng' '*noma'* linalomaanisha 'matata' au 'matatizo'. Neno lenyewe '*noma'* liliundwa kutokana na neno la Kiingereza 'normal' lenye maana ya 'kawaida'. Isitoshe, msimbo huu umetumia mbinu hiyo ya unyume ili kulipatia neno '*vinoma'* maana ya 'kwa bidii' ambayo inakinzana na maana ya 'matatizo'. Huu ni utaratibu wa kipekee unaotumiwa katika Sheng' ambao kwa mtazamo wa tasnifu hii, huenda unafungamana na uamilifu wa kuficha siri na kuhusiana na launi za Sheng' zinazozungumzwa katika maeneo tofautitofauti. Uundaji wa maneno haya '*mnoma'* na '*vinoma'* umeonyesha kuwa uleksikalishaji unaofanywa unazingatia kigezo cha Pegitosca cha uzalishaji. Tazama mifano (48) na (49) ifuatayo:

48. Huyo mbaba ni <u>mnoma</u> sana.
    Huyo mwanaume ni hodari sana.

49. Manu ni architect <u>mkali</u>, alichora hiyo dimba.
    Immanuel ni msanifu hodari, alipanga hiyo purukushani.

Mfano (49) mwingine hapo juu ni mfano wa sentensi iliyo na neno la Sheng' lililoundwa kwa kuzingatia mbinu ya antonimia. Umbo '*mkali'* kama lilivyotumiwa katika mfano (49) ni neno la Sheng' lenye asili ya Kiswahili. Maana ya neno hili katika Kiswahili ni hasi kwa kuwa inahusu 'ubaya' au 'hali ya kutokuwa tamu' lakini limepewa maana chanya katika Sheng' kwa kuwa linahusu 'uhodari' au 'uzuri'. Katika msimbo wa Sheng', neno hili basi linazingatia kigezo cha utusani cha nadharia ya Pegitosca.

### 3.1.11 Uundaji wa Kionomatopia

Hii ni mbinu ya uleksikalishaji inayotegemea uigaji wa tabia, uamilifu au mlio wa dhana, kirejelewa au mrejelewa (Crystal, 1987; Mathews, 1974). Mbinu ya onomatopia ilitumika katika uundaji wa maneno ya Kiswahili kama kuku, pikipiki na tingatinga.

Data iliyokusanywa kutoka kwa watafitiwa imedhihirisha kutumiwa kwa onomatopia kama mbinu ya uleksikalishaji katika upanuzi wa msamiati wa Sheng'. Matokeo hayo yameonyesha kuwa maneno machache mno ya Sheng' yameundwa kwa matumizi ya mbinu hii ya uleksikalishaji yakilinganishwa na yale yaliyoundwa kwa kuzingatia mbinu kama ufupishaji na ukopaji. Baadhi ya maneno yaliyoundwa kionomatopia yamepigwa mistari katika mifano (50) na (51) ifuatayo.

50. Sa.. kama beshte nisave tu na hio blingbling yako.
    Wewe kama rafiki unisaidie kwa kunipa hilo pambo lako.

Baadhi ya watafitiwa waliochunguzwa katika utafiti huu walitaja kwamba neno la Sheng' '*blingbling'* limeundwa kwa kuiga tabia za mapambo yanayovaliwa na wasanii wengi. Matokeo ya usaili wao yaliashiria kwamba neno lenyewe linaiga au linahusiana moja kwa moja na tabia ya kumetameta ya virejelewa vinavyorejelewa. Ufuatao ni mfano mwingine ulioundwa kwa kuzingatia mbinu hii ya uleksikalishaji.

51. Ule manzi mwenye alinibamba tukiwa kwa fest. Saa hii ashaingia box na hataniletea nyenyenye tena.
    Yule msichana aliyenivutia wakati wa tamasha sasa amekubali wito wangu na hatanitatiza tena.

Usaili wa watafitiwa wetu uliashiria kwamba neno '*nyenyenye'* lililopigwa mstari katika mfano (51) lilizalishwa kionomatopia. Watafitiwa kadhaa walieleza kuwa neno hili liliundwa kwa kuiga tabia zinazohusiana na kutatiza kama vile kelele. Walieleza kuwa msururu wa silabi '*nyenyenye'* inahusishwa na kelele zinazotatiza utulivu. Utafiti huu uligundua kuwa maneno yanayoundwa kwa kuzingatia mbinu hii ya

uleksikalishaji, kinyume na hitaji la Pegitosca, hayawezi kunyambuliwanyambuliwa ili kuyazalisha maneno mengine ya Sheng'.

### 3.1.12 Usarufishaji

Istilahi usarufishaji imetumiwa katika uchanganuzi huu kurejelea mbinu ya uleksikalishaji inayohusisha kuteuliwa na kuunganishwa kwa maumbo mawili au zaidi ya Sheng' ili kuwakilisha dhana moja. Usarufishaji ulidhihirika, kutokana na data ya utafiti huu, kama mojawapo ya mbinu za uleksikalishaji ya aina yake katika msimbo wa Sheng'. Hii ni mbinu inayotumiwa katika Sheng' ili kujenga misemo kama ile iliyopigwa mistari katika mifano (52) na (53).

52. Konda mwingine wa mathree alikuwa anataka nisilipe soo mbili eti niwache tu on condition that niingie box yake.
    Utingo mmoja wa gari la usafiri alitaka nisilipe nauli ya shilingi mia mbili na badala yake nikubali kuwa mpenzi wake.

Tasnifu hii imechanganua vifungu vya Sheng' kama '*ingia box*' na '*pata ball*' vilivyotumiwa katika mifano (52) na (53) kama maumbo yanayowakilisha leksimu mojamoja. Hii ni kwa vile, jaribio la mtafiti la kutenganisha maneno yenyewe 'ingia' na 'box' au 'pata' na ball' lilionyesha kwamba pasipo kuunganishwa kwao, maumbo haya hayawezi kubeba dhana iliyolengwa katika Sheng'.

Uchanganuzi wa mifano (52) na (53) unaonyesha vilevile kuwa, tofauti na mbinu ya mwambatano, usarufishaji ni mbinu ya kipekee ya uleksikalishaji ambayo ikitumiwa, maana inayozalishwa haihusiani moja kwa moja na maana za maneno yaliyounganishwa. Hii ni kwa kuwa, kipashio '*ingia box'* kingemaanisha 'kuingia sandukuni' lakini matumizi yake katika Sheng' kama inavyojitokeza katika mfano (52) yanamaanisha 'kukubali kuwa mpenzi wa mtu mwingine'. Mfano (53) pia unadhihirisha kutumika kwa mbinu ya usarufishaji.

53. M5: Unakumbuka Lina yule neiba yetu?
Unamkumbuka yule jirani yetu Lina?

M6: Yeah.
Naam.

M5: Alipata ball na sasa ameacha chuo.
Alishika mimba na sasa ameacha shule.

Vilevile, kipashio '*pata ball'* katika mfano (53) kingemaanisha 'kupata mpira' lakini matumizi yake katika Sheng' ni ya kimtindo na kwa hivyo kinamaanisha *'kushika mimba'.* Uchunguzi huu uligundua kuwa mbinu hii hutumiwa mara nyingi katika Sheng' kwa sababu wazungumzaji hulenga kukiuka ukawaida na hata kuficha siri. Mfano ufuatao ulionukuliwa kutokana na mazungumzo ya watafitiwa una kipashio cha Sheng' kilichoundwa kwa kuzingatia mbinu ya usarufishaji.

54. Nakushow nilichapa steam hadi nikamada chupa tatu.
Nakwambia nilikunywa pombe hadi nikamaliza pesa zangu.

Kipashio '*chapa steam*' kilichotumiwa katika mfano (54) kimeundwa kwa kuunganisha mofu mbili 'chapa' na 'steam' ili kuibua mofu moja inayomaanisha 'kunywa pombe'. Uunganishwaji huo wa mofu mbili utakaozalisha kifungu kinachowakisha maana maalum umerejelewa katika tasnifu hii kama mbinu ya usarufishaji. Hii inamaanisha kwamba mbinu hii haijikiti katika uzalishaji wa umbo moja moja la kuwakilisha maana ila inatumia maumbo mawili yanayojumuisha kitenzi na nomino. Ufuatao ni mfano mwingine ulionukuliwa kutoka kwa watafitiwa na unadhihirisha usarufishaji kama mbinu ya uleksikalishaji katika Sheng.

55. Alimwingiza njeve.
Alimtia katika hali ya wasiwasi.

Kipashio '*ingiza njeve*' katika mfano (55) kimeundwa kwa kuunganisha mofu mbili 'ingiza' na '*njeve'* ili kuzalisha leksimu moja inayomaanisha 'kuingizwa woga au wasiwasi'. Neno la kwanza 'ingiza' (tia) ni la Kiswahili na la pili '*njeve'* ni umbo la Sheng' linalomaanisha 'baridi'. Maana mpya inawakilishwa kupitia uunganishwaji huo wa mofu mbili na mchakato wenyewe unarejelewa kama usarufishaji. Hii inamaanisha kwamba mbinu hii haijikiti katika uzalishaji wa umbo mojamoja la kuwakilisha maana ila inaunganisha maumbo mawili yanayojumuisha kitenzi na nomino ili kuunda leksimu moja. Sehemu ifuatayo inachanganua namna ukopaji unajitokeza kama mbinu nyingine ya uleksikalishaji katika Sheng.

### 3.1.13 Ukopaji

Matokeo ya utafiti huu yameonyesha, sawa na ilivyobainishwa na Mazrui (1995) na Githiora (2002), kwamba ukopaji ni mbinu inayotumiwa katika uleksikalishaji wa Sheng'. Hata hivyo, data iliyokusanywa katika utafiti huu imedhihirisha ukopaji unaoambatana na utohozi, ukopaji usioambatana na utohozi na hatimaye ukopaji unaoambatana na usilabifishaji-upya vile inavyochanganuliwa katika sehemu (a), (b) na (c) zinazofuata. Matumizi ya ukopaji unaoambatana na usilabifishaji haukuwa umedhihirishwa katika tafiti za Mazrui na Githiora.

#### (a) Ukopaji Unaoambatana na Utohozi

Mifano miwili ya Sheng' inayowakilishwa katika mfano (56) inadhihirisha kuwa ukopaji unaoambatana na utohozi ni mbinu nyingine ya uleksikalishaji inayotumiwa ili kuyaunda maneno mapya ya Sheng'. Mfano huu hasa unaonyesha ukopaji-tohozi wa maneno kutoka Kiingereza.

56. Deskii wangu ni mchepe jo. Yeye huniokolea masaa zake.
Mwanafunzi tunayekaa pamoja kwa dawati moja hupenda kusoma. Yeye hunisaidia mambo yanapokuwa magumu.

Katika sentensi hii maneno ya Sheng' ambayo ni '*deskii'* na '*mchepe'* yamekopwa kutoka Kiingereza. Neno hili '*deskii'* linabeba dhana ya kuketi pamoja kwenye dawati moja kutokana na 'desk-mate'. Neno '*mchepe'* limetokana na neno la Kiingereza 'chop' lenye maana ya kukatakata kwa vipande vidogovidogo. Neno hili linaashiria namna ubunifu unavyoambatana na ukopaji katika uzalishaji wa maumbo ya Sheng'. Neno '*mchepe'* limetoholewa kwa kukopa sauti za Kiingereza '*mch-p-*' kisha irabu ya nusu chini 'i' ikachopekwa katika uwasilishwaji wa umbo hili kutoka lugha chasili hadi Sheng' ambapo limewakilishwa kama '*mchepe'*.

**(b) Ukopaji Usioambatana Utohozi**

Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa ukopaji wa moja kwa moja usioshirikisha utohozi ni mbinu nyingine ya uleksikalishaji inayotumiwa ili kuyaunda maneno mapya ya Sheng'. Uchanganuzi wa maumbo mbalimbali ya Sheng' umeonyesha kuwa maneno yaliyoundwa kwa kutumia mbinu hii ni yale yaliyodumisha maana zao kama ilivyokuwa katika lugha chasili. Data imeashiria kuwa ingawa lugha solo inayofuatwa na sentensi zenye Sheng' ni Kiswahili, msimbo wa Sheng' umekuwa ukichopeka maneno yaliyokopwa kutoka lugha za kiasili kama vile Dholuo, Kikamba, Kikikuyu na Kimaasai ndani ya mkuku huo. Ifuatayo ni mifano ya mazungumzo ya watafitiwa yenye maneno ya Sheng' yaliyokopwa kutoka lugha nyinginezo.

57. Hachapi wera lakini ana doo mob za kukonja.
Hafanyi kazi lakini ana pesa nyingi kuponda raha.

Mfano (57) una neno moja la Sheng' '*wera'* lililokopwa kutoka Kikikuyu. Neno hili limekopwa pasipo kutoholewa kwa kuongeza au kupunguza baadhi ya sauti au silabi nyingine za Sheng'. Watafitiwa waliosailiwa katika utafiti huu walidai kuwa umbo hili limekuwa likitumika katika Sheng' hivi kwamba limekuwa neno la kawaida lililozoeleka katika Sheng'.

Matumizi ya mbinu hii ya ukopaji usioambatana na utohozi katika uleksikalishaji wa Sheng' yamezalisha maneno ambayo hayawezi kunyambuliwa zaidi ili kupata maneno mengine ya Sheng' kama inavyodokezwa na nadharia ya Pegitosca. Hata hivyo, maneno yenyewe yaliyozalishwa na watafitiwa kwa kutumia mbinu hii yalidhihirika kama yanayozingatia kigezo cha iktisadi kwa vile hayakuundwa kwa kutumia fonimu nyingi. Mfano ufuatao ni usemi mwingine ulionukuliwa kutoka kwa watafitiwa kutoka kwa muktadha wa shule ambao una neno lililokopwa kutoka kwa lugha nyingine.

58. Stevo ni deskii wa mine ni mhunk, nimemnoki yote yote tho <u>hanyiti</u>.
    Mimi na steven hukalia dawati moja darasani, ana sura nzuri, mimi humtamani lakini hana habari.

Mfano (58) una neno lingine la Sheng' lililokopwa kutoka Kikikuyu '*hanyiti'*. Neno hili lina maana ya kuelewa au kugundua. Mfano huu unaashiria kuwa mbinu hii ya uleksikalishaji unaweza kutumiwa tu na watu wenye umilisi wa lugha chasili wanaojua neno na maana yake. Mtu asiyejua maneno ya lugha nyingine hawezi kuyakopa kwa njia yoyote hadi Sheng'. Vivyo hivyo, neno hili halizingatii kigezo cha umataifa kinachohitaji kutimizwa kwa mujibu wa nadharia ya Pegitosca. Usemi wa mtafitiwa ulionukuliwa kama mfano (59) una neno lingine la Sheng' lililokopwa kutoka Kikikuyu.

59. Madem wengi wa chuo yetu hawaelewi risto za tao, hao hutokanga <u>gishagi</u>.
    Wasichana wengi wa shule yetu hawaelewi stori za mjini kwani wao hutoka mashambani.

Usaili wa watafitiwa ulionyesha kuwa neno '*gishagi'* kama lile lililopigwa mstari katika mfano (59) limekopwa kutoka Kikikuyu hadi Sheng'. Neno hili lilikuwa na maana ya mashambani katika lugha chasili na maana hiyo imedumishwa katika Sheng' kama msimbo pokezi. Maneno kadha wa kadha yaliyokopwa kutoka Dholuo hadi Sheng' yalitumiwa katika diskosi za watafitiwa wa utafiti huu kama inavyojitokeza katika mfano ufuataao.

60. We ni mserious na masomo usiwe na was, tuchukulie tu kila kitu mosmos tutamurder 4th.
    Wewe huwa na bidii katika masomo usiwe na wasiwasi, tujikaze hatua kwa hatua na mwishowe tutamaliza kidato cha nne.

Neno la Sheng' '*mosmos'* lililotumiwa katika mfano (60) limekopwa pasipo kutoholewa kutoka Dholuo. Neno hili lilikopwa bila vipande vyake kupunguzwa au vipande vingine kuongezwa kiutohozi katika Sheng'. Neno hili '*mosmos'* katika Dholuo lina maana ya polepole au hatua kwa hatua na maana hiyo hiyo ilidumishwa baada ya kujumuishwa kwa neno lenyewe kwenye msamiati wa Sheng'. Neno hili linazingatia kigezo cha iktisadi katika Pegitosca. Muundo wa neno hili kabla na baada ya kukopwa kwake unadhihirisha kuwa limekopwa na kutumiwa katika msimbo wa Sheng' jinsi lilivyokuwa katika Dholuo pasipo kutoholewa. Sentensi ifuatayo ina mfano mwingine uliopigwa mstari ambao inadhihirisha ukopaji usioambatana na utohozi kutoka lugha za kiasili.

61. Yule beshte wake ong'ong'o… maze anakaa mbaya.
    Yule rafiki yake aliye na sura mbaya… anaonekana vibaya.

Neno la Sheng' '*ongo'ngo'* lililotumiwa katika sentensi hii (61) limekopwa kutoka Dholuo na lina maana ya sura mbaya. Katika sentensi hii, msemaji anatumia neno hili

ambalo limekopwa kutoka lugha za kiasili, kama umbo ambalo ni sehemu ya msamiati wa Sheng'.

62. Princi wetu ni kemoda katika game…yeye huplay futa na sisi chuo.
    Mwalimu mkuu wetu ni mchezaji hodari, yeye hucheza nasi kandanda shuleni.

Neno la Sheng' '*kemoda'* lililopigwa mstari katika mfano (62) lilikopwa kutoka Kimaasai. Maana ya neno hili katika lugha chasili ni hodari au wazimu katika muktadha mwingine. Dhana hiyo ya 'uhodari' imedumishwa katika msimbo wa Sheng' baada ya neno hili kukopwa kutoka Kimaasai. Isitoshe, umbo lenyewe halijabadilishwa kimuundo katika Sheng'. Mfano huu, kwa pamoja na ile ya Dholuo na Kikikuyu iliyochanganuliwa hapo juu inaashiria kwamba mbinu hii ya uleksikalishaji ya kupanua msamiati kwa kukopa bila kutohoa imechangia maneno kadhaa ya Sheng'.

### (c) Ukopaji Unaoambatana na Usilabifishaji-Upya

Dhana hii imetumiwa katika tasnifu hii kurejelea hali ambapo neno linakopwa kutoka lugha chasili na kupewa muundo tofauti wa silabi. Kwa mfano, kupitia usilabifishaji-upya, msamiati wa Sheng' unadhihirisha (i) kuongezeka kwa idadi ya silabi katika neno jipya (ii) kupunguka kwa idadi ya silabi (iii) kudondoshwa kwa baadhi ya silabi au (iv) kugeuzwa kwa mpangilio wa silabi kama inavyoashiriwa na mifano ifuatayo:

| | **Lugha Chasili: Kiingereza** | **Lugha Pokezi: Sheng'** |
|---|---|---|
| i. | Tests /KIKKK/ = silabi moja | Teo /KI/ na /I/ = silabi mbili |
| ii. | House /KI/ /IKI/ = silabi mbili | Hao /KI/ na /I/ = silabi mbili |
| iii. | State house /KKI/ /KI/ # /KI/ /I/ /KI/ = silabi tano | Steto /KKI/ /KI/ = silabi mbili |
| iv. | Kill /KIK/ | Kiki /KI/ /KI/ = silabi mbili |

| | **Lugha Chasili: Kiswahili** | **Lugha Pokezi: Sheng'** |
|---|---|---|
| i. | Matajiri /KI/ /KI/ /KI/ /KI/ = Silabi nne | Masos /KI/ /KIK/ Silabi mbili |
| ii. | Hii /KI/ /I/ = silabi mbili | Hi /KI/ = silabi moja |
| iii. | Sasa /KI/ /KI/ = silabi mbili | Sa /KI/ = silabi moja |

Kama inavyoonyeshwa katika majedwali haya, baada ya mchakato wa usilabishaji-upya, kinachodhihirika ni kuwa neno lililokopwa kutoka lugha chasili hupewa muundo mpya wa silabi katika Sheng'. Kwa mfano neno 'tests' (siabi moja) la Kiingereza linabadilika na kuwa *'teo'* (silabi mbili) katika Sheng'. Hivyo, idadi ya silabi za neno katika lugha chasili huwa tofauti, huongezeka au kupunguka katika lugha pokezi.

### 3.1.14 Mwambatano

Mintarafu ya Kamusi ya TUKI (2004), neno 'mwambatano' limetokana na kitenzi 'ambata' chenye maana ya kunata au kuunganisha. Mbinu ya mwambatano, kwa hivyo, inahusu kule kuambatanisha au kuunganisha maneno mawili au zaidi ili kuunda neno moja jipya. Matokeo ya uchunguzi huu yameonyesha kuwa neno linaloundwa kwa kutumia mbinu hii aghalabu huwa refu.

Data iliyokusanywa katika utafiti huu ilikuwa na maneno ambatani yenye mizizi miwilimiwili na viambishi pekee. Hatukupata neno la Sheng' lililoundwa kwa kuunganisha mizizi mitatu. Uchunguzi wa maneno yaliyoundwa kwa kuzingatia utaratibu huu ulibainisha kwamba hakuna neno ambatano la Sheng' lenye zaidi ya silabi kumi. Kwa mtazamo wa tasnifu hii, huenda kutotukia kwa maneno ambatani yenye zaidi ya silabi kumi ama mizizi mitatu au zaidi kunahusiana na ugumu wa kuchakata neno kama hilo wakati wa kuunda, kutamka na hata kung'amua. Hiki ni kiashiria kwamba maneno yanayoundwa huzingatia kigezo cha iktisadi kama inavyopendekezwa na nadharia ya Pegitosca hata kama yamezalishwa kwa kuyaunganisha maumbo.

Neno ambatani la Sheng' '*Sagodi'* linalojitokeza katika mfano (63) uliozalishwa na mtafitiwa mmoja katika muktadha wa shule limeundwa kwa kuambatanisha silabi

zilizotoholewa kutoka Kiingereza za maneno ‘sir’ (*sa*) na God (*godi*) ili kuunda neno jipya ‘*Sagodi*.’

63. Naomba Sagodi atokelezee kwa hii hali.
    Naomba Mungu Bwana aingilie kati katika hali hii.

Ufuatao ni usemi mwingine wa mtafitiwa ulionukuliwa pia katika muktadha wa shule unaoonyesha mwambatano wa maneno mawili ili kuunda kielezi kimoja.

64. Nimechopia hizo teo mbaya-mbovu.
    Nimesomea hiyo mitihani sana.

Uchunguzi huu ulibainisha kuwa wazungumzaji wa Sheng’ wanatumia mbinu ya kipekee ya kuunganisha vivumishi viwili vile ‘mbaya’ na ‘mbovu’ vilivyotumiwa katika mfano (64) ili kuunda kielezi kimoja ‘*mbaya-mbovu*’ chenye maana ya ‘sana’. Uunganishaji huu wa maneno mawili ambayo ni vivumishi ili kuunda neno moja jipya la aina tofauti hujitokeza kwa nadra katika lugha. Huenda sifa hii ni kibainishi kingine cha upekee wa misimbo ambayo ni misimu kama Sheng’.

### 3.1.15 Upanuzi wa Kisemantiki

Upanuzi wa kisemantiki kama mbinu ya uleksikalishaji huhusu hali ambapo neno linapita mipaka ya yake kimaana na kupewa maana nyingine kando na ile ya kwanza (Traugott na Dasher, 2002). Upanuzi wa kisemantiki hufanyika kwa namna ambavyo maumbo ya lugha nyingine kama Kiswahili yanakopwa, kisha yakafanywa kuwa leksimu ya Sheng’ na kupewa maana nyingine mpya. Mathalan, Ogechi (2005) anasema kuwa nomino kopwa katika Sheng’ hupata upanuzi wa maana kisemantiki. Mfano (65) uliozalishwa na mwanafunzi katika muktadha wa shule unahusu matumizi ya upanuzi wa kisemantiki kama mbinu ya uleksikalishaji katika Sheng’.

65. Niaje <u>mzito</u>?
    Vipi mtu wa maana?

Sentensi hii (65) ina neno '*mzito'* ambalo kimsingi linarejelea kipimo cha nomino inayorejelewa. Upanuzi wa kimaana kama mbinu ya uleksikalishaji umeweza kutumiwa ili kuunda kwa neno hili kwa kulipa maana nyingine ya pili ya kumrejelea mtu muhimu. Inamaanisha kwamba wazungumzaji wa Sheng' hawakuunda neno jipya la kurejelea dhana hiyo ya pili ila walilipa neno lilelile moja maana zaidi ya moja. Sentensi ifuatayo vilevile inaonyesha namna upanuzi wa maana unavyochangia upanuzi wa msamiati katika Sheng'. Kwa mfano, neno '*chuo'* limepewa maana mpya katika Sheng ndiposa likawa na maana zaidi ya moja.

66. <u>Chuo</u> imemboo Giddy, anatuna na wasee wako daro.
    Shule imemsinya Giddy, analala na wenzake wako darasani.

Neno '*chuo'* lililotumiwa katika mfano (66) katika Kiswahili sanifu lina maana ya taasisi ya juu ya elimu inayofuata kiwango cha sekondari. Tokeo hili linaashiria kuwa uleksikalishaji wa neno hili katika Sheng' umehusu kupanuliwa kisemantiki hivi kwamba linatumiwa kurejelea vyuo vikuu, vyuo vya kati, shule za sekondari na hata za msingi. Hii inamaanisha kuwa maana ya neno '*chuo'* katika Sheng' ni pana kuliko maana yake katika Kiswahili sanifu.

### 3.1.16 Ujenzi Ghairi

Ujenzi ghairi ni mbinu ya uleksikalishaji inayohusu upanguaji wa silabi ambapo silabi mbili au zaidi zinabadilishana nafasi katika mchakato wa kuunda neno jipya (Crystal, 2003; Hume, 1998). Upanguaji huo kwa maelezo ya Hume (2004), husababisha paradimu ambapo silabi X inakaliwa na silabi Y huku paradimu ya silabi Y ikikaliwa

na silabi X. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kutumiwa kwa mbinu ya ujenzi ghairi katika uleksikalishaji wa Sheng'. Mbinu hii ni ya kipekee katika Sheng' kwa vile haijakuwa ikitumika kuzalisha maneno ya lugha nyinginezo kama vile Kiswahili.

Ujenzi ghairi umetumiwa kuunda msamiati wa Sheng' kama inavyojitokeza katika neno lililopigwa mstari katika mfano ufuatao.

67. Ile risto yetu iligonga wall.
    Lile suala letu lilikwama

Neno la Sheng' lililotumiwa katika mfano (67) '*risto'* limeundwa kwa kutumia mbinu ya ujenzi ghairi. Hii ni mbinu ya uleksikalishaji inayotumiwa kuunda msamiati wa Sheng' ambayo inahusu upanguzi wa silabi za neno chasili na kuzipanga upya kwa namna ambavyo zitabadilishana nafasi. Kwa mfano, asili ya neno la Sheng' '*risto'* ni neno la Kiingereza 'story' lililotoholewa kama 'stori*'* kabla ya silabi zake kupanguliwa. Silabi ya kwanza inachukua sehemu ya silabi ya pili na huku ya pili ikichukua nafasi ya ile silabi ya kwanza ndiposa neno jipya '*ri-sto'* linaundwa. Tazama pia mfano (68) ufuatao:

68. Baada ya ile concert tulichekiana na msupa wako, alinishoo nikushtue hana mbana zako.
    Baada ya ile tafrija tulionana na mrembo wako, aliniambia nikwambie kuwa hana nambari zako (za simu).

Neno lililopigwa mstari katika mfano (68) '*mbana'* limeundwa kwa kufanyia ujenzi ghairi silabi mbili za neno la Kiswahili 'na' na 'mba' (namba) ili litamkwe kama '*mbana'*. Uhakiki wa matumizi ya mbinu hii kwa kuzingatia vigezo vya nadharia ya Pegitosca unaonyesha kwamba maneno yanayoundwa kwa kuzingatia mbinu hii ya uleksikalishaji hayawezi kunyambuliwanyambuliwa ili kuzalisha maneno mengine mapya. Baadhi ya watafitiwa walidokeza kwamba neno '*mbana'* lina sifa hasi, kuashiria kwamba linaelekea kuwa na sifa ya utusani inayotajwa na wanapegitosca.

Hata hivyo, watafitiwa wenyewe walibainisha kuwa neno lenyewe linafaa au linakubalika katika miktadha ya Sheng'; kuashiria kwamba linatimiza kigezo cha ukubalifu pia.

Utafiti huu umegundua, kwa mujibu wa uchanganuzi uliofanywa hapo juu kuhusu uleksikalishaji kwamba mbinu zaidi ya kumi hutumika katika uleksikalishaji wa Sheng'. Inahitimishika kutokana na uchanganuzi wenyewe kwamba mbinu hizo zote zinazingatia vigezo mbalimbali ya Pegitosca. Hata hivyo, vigezo vingine vya Pegitosca kama vile umataifa na uzalishaji havitimizwi kwa sababu leksimu nyingi zinazoundwa katika Sheng' hazinyambulikinyambuliki kwa ajili ya kupata leksimu mpya na hazihusiani na msamiati wa lugha za kimataifa.

### 3.2 Upijini na Ukriolishaji wa Sheng'

Lengo la pili (1.2.2) la utafiti huu lilikuwa kufafanua sifa ambazo zingepinga au kuthibitisha upijini au ukriolishaji wa Sheng'. Uchanganuzi unaofanywa katika sehemu zifuatazo unalenga kubainisha iwapo Sheng' ni msimu tu ambao haujawahi kuwa Pijini wala Krioli au ni lugha ambayo imeibuka kutokana na ukriolishaji wa Pijini. Hivyo basi, data inachanganuliwa ili kufafanua sifa za Sheng' ambazo zinaweza kuthibitisha au kupinga ukriolishaji wake kuanzia sehemu 3.2.1.

#### 3.2.1 Sifa Zinazoashiria kuwa Sheng' Haijawahi kuwa Pijini

Usaili wa watafitiwa uliweza kubainisha hali ambazo zimeweza kuorodheshwa katika Jedwali 3.3 kama sifa zinazopinga nadharia tete ambayo imekuwa ikitolewa na baadhi ya wataalamu kwamba Sheng iliibuka kama Pijini.

**Jedwali 3.3: Muhtasari wa Sifa Zinazopinga Upijini wa Sheng'**

| | Vibainishi | Sifa Inayopambanua Pijini | Hali Iliyobainika kuhusu Sheng' |
|---|---|---|---|
| 1. | Miktadha ya kuibuliwa | Pijini huibuka katika miktadha ya kibiashara na ya watumwa | Hutumiwa shuleni na mitaani |
| 2. | Urahisishaji wa sarufi za lugha changizi | Fonolojia na mofolojia za Pijini huchangiwa na lugha mbili na hushirikisha urahisishaji mwingi | Aghalabu Sheng' imechangiwa na Kiswahili lakini imechangiwa na lugha nyinginezo [wala sio lugha mbili pekee] |
| 3. | Hushirikisha matumizi mengi ya viziada lugha | Wazungumzaji wa Pijini hutumia ishara nyingi kwa sababu Pijini huwa hazitoshelizi mahitaji yote ya kimawasiliano. | Wazungumzaji wa Sheng' wanaelewa lugha nyinginezo na wanaweza kutumia maneno ya lugha hizo badala ya kutegemea ishara. |
| 4. | Maeneo ya matumizi | Pijini hutumiwa mipakani na katika maeneo ya kibiashara | Hutumiwa katika miktadha ya aina nyingi |
| 5. | Miundo ya kisarufi isiyokuwa thabiti | Pijini huwa na miundo sahili. | Muundo wa Sheng' umekitwa katika mkuku wa Kiswahili |
| 6. | Dhima ya Lingua franka | Pijini hutumiwa na wazungumzaji wasiokuwa na lingua franka. | Sheng' hutumiwa na hata wanafunzi ambao wana lingua franka kama Kiswahili |

Data hii, Jedwali 3.3, inadhihirisha mambo kadhaa ambayo sasa tunayajadili katika sehemu zifuatazo:

### 3.2.1.1 Sheng' Haikuibuka katika Muktadha wa Dharura

Uchanganuzi huu kwa kuzingatia muktadha [Kibainishi 1] ambao msimbo wa Sheng' uliibuka, kama inavyoashiriwa katika matokeo yaliyowasilishwa katika Jedwali 3.3, unapinga wazo kwamba Sheng' iliwahi kuwa Pijini. Hii ni kwa sababu Sheng', kutokana na ufafanuzi wa watafitiwa, haikuwa ikiibuka katika muktadha wa dharura sana kati ya jamii za watu waliokuwa wakiongea lugha tofauti tofauti. Badala yake, waliweza kudokeza kwamba Sheng' inayozungumzwa hapa nchini Kenya iliibuka katika miktadha ya mtaani, kazini, shuleni na hata nyumbani. Vidokezo vya watafitiwa viliashiria kuwa msimbo huu haukuwahi kuwa Pijini kwa maana uliibuliwa na watu

ambao walikuwa na lingua franka kama Kiswahili au Kiingereza lakini waliokuwa wakitaka msimbo wa kuficha siri kwa serikali kama wezi au kwa wakuu shuleni.

#### 3.2.1.2 Fonolojia na Mofolojia za Sheng’ Hazikutokana na Usahilishaji wa Zile za Lugha Changizi

Uchunguzi huu, kwa kuzingatia Kibainishi cha 2 kinachojitokeza katika Jedwali 3.3 hapo juu, uligundua kuwa Sheng’ haikuwahi kuwa Pijini pia. Hii ni kwa vile muundo wake wa kimofolojia (msamiati) na fonolojia yake haikuzalishwa kwa kupunguza au kusahilisha miundo ya lugha mbili changizi. Kama inavyojitokeza katika uchanganuzi wa ukopaji kama mbinu ya kuunda msamiati wa Sheng’, msimbo wenyewe (Sheng’) haukuwa Pijini kwa misingi kwamba umechangiwa kimofolojia na kifonolojia na lugha zaidi ya mbili kama vile Kiswahili, Kiingereza, Dholuo, Kimaasai, Kikikuyu na lugha nyinginezo. Sheng’ kwa misingi hii haikuwa Pijini kwa maana si lugha mahuluti iliyoundwa kwa kuchanganya lugha mbili.

Utafiti huu uligundua kwamba baadhi ya maumbo ya Sheng’ hayalengwi kurahisisha mawasiliano kama sifa muhimu ya Pijini. Hii ni kwa vile kuna baadhi ya maneno ya Sheng’ yanayoundwa kwa kuhamisha maana, kiantonimia kwa kuyapatia maana ambayo ni kinyume cha maana yake katika lugha chasili kama ‘lenga’ kumaanisha ‘nuia’ katika Kiswahili na kumaanisha ‘kupinga au kupuuza’ katika Sheng’, na kwa kutumia tabdila ambapo mpangilio wa silabi unageuzwa kama ‘*risto’* kutokana na ‘story’ au ‘*romo’* kutokana na ‘tommorow’. Mbinu hizi zinazotumiwa katika Sheng’ ni changamani na haziwezi kuwa sehemu ya sifa za Pijini.

Isitoshe, ilijitokeza katika utafiti huu kwamba, kwa vile wale wanaotumia Sheng’ wanaelewa lugha nyinginezo kama Kiswahili, wao wanaweza kuunda sentensi

ambatani, sentensi changamani, sentensi sahili na hata sentensi ambatani changamani zenye maneno ya Sheng' na Kiswahili kama lugha solo. Kule kuundwa kwa sentensi za aina hizi zote si sifa inayohusishwa na Pijini. Utafiti huu unachukulia kwamba wazungumzaji wa Sheng' wamekuwa wakifanya hivi tangu Sheng' ilipoibuliwa. Hakikupatikana kiashiria chochote katika matokeo ya utafiti huu kilichoonyesha kuwa wazungumzaji walioibua Sheng' walianza kwa kutumiatumia sentensi sahili kabla ya kuanza kutumia sentensi changamani na ambatani. Vilevile, diskosi zote zilizonukuliwa na mtafiti zilizokuwa na Sheng' zilionyesha kuwa Sheng' hujitokeza katika vipandevipande tu vya mazungumzo. Hakuna wazungumzaji walioweza kuongea Sheng' pekee katika diskosi yoyote nzima.

#### 3.2.1.3 Sheng' Haijakuwa Ikitegemea Viziada-lugha ili Kujaliza Ukosefu wa Msamiati

Matokeo ya usaili wa watafitiwa katika uchunguzi huu yameashiria vilevile kuwa Sheng' haikuwa Pijini. Hii ni kwa vile, kama inavyobainishwa kuhusiana na Kibainishi cha 3 cha upijini, wazungumzaji wa Sheng', kwa maelezo ya watafitiwa, hawajawa wakitumia viziadalugha kama vile ishara za mikono, sura za nyuso, miondoko ya mwili na kichwa ili kujaliza mazungumzo yao pale walipokosa kujua neno ambalo lingeeleweka kwa wasikilizaji wao. Watafitiwa walidai kuwa wazungumzaji wa Sheng' hapa nchini Kenya zikiwemo jamii za mitaani, wanafunzi na makundi mengine, wanaelewa lugha za kiasili au Kiswahili. Kwa hivyo, hata kama watakosa neno la Sheng' watatumia maneno ya Kiswahili au lugha hizo zingine wanazoelewa.

#### 3.2.1.4 Maeneo ya Matumizi ya Sheng' Yanakiuka Yale ya Pijini

Kwa mujibu wa Todd (1990), Pijini huhusishwa na maeneo mahususi kama yale ya kibiashara, ya kijeshi, ya watalii au watumwa ambao wameunganishwa na watu wengine wasioelewa lugha yao. Kwa upande mwingine, asili ya matumizi ya Sheng' [kama inavyojitokeza katika Kibainishi 4 kwenye Jedwali 3.3] ni tofauti kabisa kwa mujibu wa watafitiwa waliosailiwa katika utafiti huu. Wao waliashiria kwamba asili ya matumizi ya Sheng' hayakuwa muktadha wa kibiashara wala wa kijeshi. Walidokeza kwamba asili ya msimbo huu inahusishwa zaidi na wezi, walanguzi wa dawa za kulevya, utingo na wanafunzi. Kutokana na matokeo haya ya usaili wa watafitiwa, inaakizika kuwa maeneo ambayo msimbo huu ulitumiwa tangu mwanzo yanapinga nadharia tete kwamba Sheng' iliibuka kama Pijini.

#### 3.2.1.5 Sheng' Imekuwa na Miundo Mituamo Kinyume na Ilivyo kwa Pijini

Kibainishi cha 5 kinachojitokeza katika Jedwali 3.3 linalotumiwa katika uchanganuzi huu kinaonyesha kwamba muundo wa Pijini huwa unageukageuka kutoka lugha moja changizi hadi lugha nyingine changizi. Kwa upande mwingine, kama inavyojitokeza katika mifano ya sentensi zenye Sheng' iliyonukuliwa katika tasnifu hii, aghalabu Sheng' hufuata mkuku wa kimofosintaksia wa Kiswahili. Hii inamaanisha kuwa muundo wa msimbo wa Sheng' ni wa msimu wala si wa Pijini kwa kuwa haubadilikibadiliki vile inavyofanyika kwa Pijini.

#### 3.2.1.6 Sheng' Haikuibuliwa kwa Vikundi Viwili vya Kijamii kama Lingua Franka

Mintarafu ya Kibainishi cha 6 kinachoonekana katika Jedwali 3.3, Pijini ni launi iliyoibuka wakati makundi mawili ya watu wenye lugha mbalimbali yalipokutana, wakataka kuwasiliana na hawakuwa na lugha ambayo ingewaunganisha katika

mazungumzo. Hivyo basi wanalazimika kuunda lugha ya kijuujuu itakayowawezesha wawasiliane. Wanaunda Pijini kama launi sahili katika muktadha huo kwa kutumia maneno na sheria za lugha zote mbili. Hivyo basi, kwa mujibu wa uchanganuzi huu, Sheng' si Pijini kwa sababu si matokeo ya mchanganyiko wa lugha mbili ambao muundo wake wa kimofolojia na kisintaksia umerahisishwa ili utumiwe kama lingua franka kwa wazungumzaji wa lugha mbili tofauti. Utafiti huu uligundua kuwa Sheng' si lingua franka ila ni msimbo wa ndani wa kujitambulisha na vikundi kama vya vijana, msimbo wa siri au msimbo wa kubagua wengine katika mawasiliano.

### 3.2.2 Sifa Zinazopinga Ukriolishaji wa Sheng'

Hali za kisarufi na za kijamii zimeainishwa katika sehemu zifuatazo kama vipengee vinavyohusu sarufi ambavyo ni sehemu ya ithibati inayotumiwa katika uchunguzi huu kupinga dai kwamba msimbo wa Sheng' unaweza kuainishwa kama Krioli.

#### 3.2.2.1 Hali Zinazoathiri Usarufishaji wa Sheng'

**[a] Kutobainika kwa Vipashio vya Kimofolojia**

Uchunguzi huu uligundua kwamba kuhusiana na elementi ya kimofolojia, Sheng' haijafikia kiwango cha upijinishaji. Hii ni kwa sababu, iligunduliwa kwamba watafitiwa ambao walikuwa wanafunzi kutoka maeneo tofauti tofauti ya taifa la Kenya walikuwa wakitumia maneno tofauti kurejelea baadhi ya virejelewa. Hali hii, kwa mtazamo wa uchanganuzi huu imekuwa ikiathiri usarufishaji wa Sheng' katika kiwango cha mofolojia.

Kuhusiana na muundo wa kimofolojia, kimsingi Sheng' haijaibuka na muundo wake wa vijenzi kama vile paradimu za viambishi awali, vya kati, mizizi na viambishi vya tamati. Kama ilivyokwisha kubainishwa katika uchanganuzi unaohusu miundo ya

Sheng' mintarafu ya lengo la pili, Sheng' haina viambishi vyake vya nafsi, vya njeo, vya hali ya masharti, vya hali timilifu, vya kukanusha, virejeshi na vinginevyo. Kwa fahiwa hii, paradimu za kifungu tenzi za Sheng' si bayana ila hutegemea paradimu za Kiswahili tu.

Uchanganuzi wa data vilevile unaonyesha kuwa Sheng' haijawahi kubainisha viwakilishi vya nafsi huru (kama vile mimi, sisi, wewe, nyinyi, yeye na wao) wala viambishi vya nafsi tegemezi (kama vile 'ni', 'tu', 'u', 'm', 'a' na 'wa'). Wakati mwingine tu vifupisho vya viwakilishi hivi kama vile '*we*' badala ya 'wewe', '*si*' badala ya 'sisi' na '*mi*' badala ya 'mimi' vimekuwa vikitumiwa katika Sheng.' Hivyo basi, miundo yoyote yenye msimbo huu (Sheng') imekuwa ikitegemea viambishi vya nafsi vya Kiswahili. Ifuatayo ni mifano ya data iliyozalishwa na watafitiwa inayotumia viwakilishi hivi vya Kiswahili ambavyo silabi zimedondoshwa:

69. Mi nimekumbuka ju mi na wewe tulikuwa marafiki.
    Mimi nimekumbuka kwa sababu (mimi na wewe) tulikuwa marafiki.

70. Nakuhimiza we pia ujikakamue uwe mmoja wa wachezaji.
    Nakuhimiza wewe pia ujikakamue ili uwe mmoja wa wachezaji.

Sehemu zilizopigwa mistari katika mifano (69) na (70) inaonyesha vifupisho hivyo vya viwakilishi vya Kiswahili. Uchanganuzi huu unahoji kwamba hali hii imeathiri usarufishaji wa Sheng'. Hii ni kwa sababu, kama ilivyobainika katika baadhi ya mazungumzo yenye Sheng', wazungumzaji wakati mwingine hawavitumii vifupisho hivyo vya viwakilishi vya nafsi vya Kiswahili.

Idadi kubwa ya maneno huhitajika ndiposa Pijini ifuzu kuwa Krioli. Matokeo ya utafiti huu yameonyesha hali kadhaa zinazopinga ukuaji halisi wa idadi ya msamiati wa Sheng'. Kwanza, ilibainika kwamba maneno mengi ya Sheng' huundwaundwa ili

kurejelea dhana moja. Pili, maneno mengi ya Sheng' yaliyodhihirika katika mazungumzo ya watafitiwa yalihusu sajili ya mazungumzo na sokoni zaidi. Mawanda ya matumizi ya Krioli huwa yamepanuliwa ili kukidhi mahitaji yote ya lugha kama ilivyo katika lugha nyinginezo za kawaida. Ingekuwa kwamba msimbo huu wa Sheng' unakua kimsamiati, basi maneno yanayohusiana na sajili za hospitalini, mahakamani, kilimo, dini na nyingine nyingi yangekuwa yameanza kutukia katika diskosi za watumiaji. Hali hii inaashiria kutokua kwake hivi kwamba hauwezi kuhusishwa na upijinishaji.

Isitoshe, matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa ukriolishaji hauwezi kuhusishwa na msimbo wa Sheng' kwa sababu msamiati wake haujawa thabiti. Watafitiwa waliosailiwa waliweza kutaja kwamba msamiati unaolengwa kuwabagua wengine katika mawasiliano kama vile walimu, wazazi au polisi, hubadilishwabadilishwa ili kuhifadhi siri. Hii inamaanisha kwamba msamiati wa Sheng' unaobadilishwabadilishwa hulengwa kufanikisha mawasiliano baina ya wanachama wa vikundi maalum wanaoitumia. Hii inaashiria pia kwamba kikundi kimoja cha Sheng' kinaweza kuwa kinatumia neno fulani ambalo halitumiwi na kikundi kingine kinachotumia Sheng hata katika mji, mtaa au shule moja. Ifuatayo ni mifano ya msamiati unaotumiwa kurejelea polisi kama ilivyodhihirika katika utafiti huu:

71. Mifano ya Maneno Mengi ya Sheng' Yanayorejelea Dhana Moja

a) Ponyi
b) Sonyi
c) Karao
d) Flik
e) Kahio
f) Hina
g) Wahia
h) Gava

Maneno yaliyotolewa katika mfano 71 (a) hadi (h) ni majina yanayorejelea nomino moja tu 'polisi' ambayo yamebadilishwabadilishwa kutoka wakati mmoja hadi mwingine. Kwa mujibu wa watafitiwa wetu, ubadilishwaji huo wa msamiati umekuwa ukifanywa kwa lengo la kuficha siri katika Sheng'.

**[b] Kutobainika kwa Muundo wa Kisintaksia**

Matokeo ya utafiti huu yameashiria kuwa kule kubadilikabadilika kwa mpangilio wa maneno katika Sheng' huathiri usarufishaji wake. Data ilionyesha kwamba wazungumzaji wa Sheng' hawafungwi na utamaduni wowote unaowalazimisha watangulize nomino kabla ya kivumishi au kivumishi kabla ya nomino. Kwa mfano:

72. Hii dinga ni ya mbuyu.
    Hili gari ni la baba.

73. Dinga hii ni ya mbuyu.
    Gari hili ni la baba.

Namna ambavyo kivumishi kinafuata au kinatangulia nomino katika miundo ya Sheng' (72) na (73) inaashiria kwamba kanuni inayohusu mfuatano wa mofimu haijabainika. Hii ni kwa maana kivumishi kimetangulia nomino katika mfano (72) huku nomino ikitangulia kivumishi katika mfano (73).

**3.2.2.2 Hali za Kijamii Zinazoathiri Ukriolishaji wa Sheng'**

**[a] Kutobadilika kwa Hadhi ya Sheng'**

Kwa mujibu wa ufafanuzi wa Fishman (1967) kuhusu diglosia, utafiti huu uliweza kubainisha kwa kuwasaili watafitiwa kwamba mielekeo hasi ya watu wengi imekuwa ikiathiri hadhi ya Sheng' nchini Kenya. Msimbo huu umehusishwa na wakora, wezi, walanguzi wa dawa za kulevya na watu wanaokwepa sheria. Watafitiwa walidai kuwa wakiulinganisha na launi sanifu za lugha, msimbo wa Sheng' umekuwa ukitazamwa

kama launi ya chini (LC). Launi za juu (LJ) mara nyingi hupendelewa na hutumika katika miktadha rasmi kama vile darasani, kanisani, misikitini, afisini na katika uandishi wa stakabadhi za serikali dhidi ya Sheng' kama LC. Hata hivyo, ingawa mtazamo huu ulibainika, wepo wataalamu, wanasiasa, madaktari, waalimu, maafisa wa serikali na hata wahubiri wanawasiliana kwa kutumia Sheng'. Ingawa wahusika hawa wamekuwa wakitumia Sheng', ilijitokeza kuwa hadhi yake haijaweza kubadilika kutoka LC hadi LJ kwa sababu ya mielekeo hasi inayoilenga. Kadiri msimbo unapoendelea kuimarika na kutumiwa kama LJ, ukriolishaji wake utakuwa unafanyika. Walakini, hali hii haifanyiki katika muktadha wa Sheng'.

**[b] Kutotumiwa kama 'Lugha' ya Kwanza**

Watafitiwa wote ambao walikuwa wasemaji wa Sheng' walikiri kwamba, hakuna hata mmoja wao aliyedai kuwa lugha yake ya kwanza ilikuwa Sheng'. Ilibainika kuwa wasemaji wote wa msimbo huu walikuwa wasemaji wazawa wa lugha nyinginezo kando na kwamba walikuwa na ujuzi wa Kiswahili na hata Kiingereza. Asilimia mia moja ya watafitiwa waliosailiwa pia walidai kuwa hawajawahi kumwona yeyote ambaye Sheng' ilikuwa lugha yake ya kwanza. Matokeo haya yanaashiria zaidi kwamba msimbo huu haujatimiza mahitaji ya kuwa Krioli.

Kutokana na sampuli wakilishi ya familia tatutatu za mitaa katika mitaa ya Kondele na Nyalenda iliyoteuliwa na kusailiwa katika utafiti huu, mtafiti aliweza kugundua kuwa, hivi sasa, familia za mitaani (yaani watoto na hata wazazi) wana lugha nyingine za kwanza ambazo si msimbo wa Sheng'. Walibainisha kuwa wengi wa wazazi wa mitaani walikuwa watoto waliotoroka kutoka makwao wakijua lugha fulani za kwanza. Walidhihirisha vilevile kwamba watoto wanaoishi mitaani katika miktadha mingi hujifunza Kiswahili kama lugha ya kwanza kwa pamoja na lugha nyingine

zinazopatikana katika mazingira yale. Kwa mfano, wale wanaopatikana katika mtaa wa Kondele walibainisha kuwa walijifunza Kiswahili na Dholuo kama lugha ambayo inazungumzwa na wengi katika mazingira hayo. Hata hivyo, kuna wale walitorokea mitaani kutoka kwao wakiwa wamejifunza lugha za kwanza za jamii nyinginezo.

Hali hii ilidhihirisha kuwa watoto wanaozaliwa mitaani hawajifunzi Sheng' kama 'lugha' ya kwanza ila wanajifunza kama msimbo wa mtaani. Tukio kama hili lilionekana katika mtaa wa Nyalenda ambapo watafitiwa wengi walisema kuwa watoto wa mitaani hujifunza Kiswahili kama lugha kuu ya mawasiliano jijini kwa pamoja na lugha inayotumiwa na wengi katika mazingira yale kama Dholuo. Usaili wa wazazi na hata watoto hawa wa mitaani ulionyesha kuwa watoto hawa hujifunza Sheng' kadiri wanapotagusana na wengine wanaotumia msimbo huo katika jiji. Ugunduzi huu unapinga tasnifu ya Spyropoulos (1987) kwamba Sheng' ni Pijini ambayo alitabiri kwamba baadaye itakuwa Krioli kwa vile watoto wa familia za mitaani wangeanza kujifunza kama lugha ya kwanza. Hii inamaanisha pia kuwa ugunduzi huu unapinga hitimisho la Githiora (2002) kwamba Sheng' itageuka kuwa lahaja ya Kiswahili inayozungumzwa mijini. Hii ni kwa vile, kwa kudai hivyo, Githiora anadokeza kwamba Sheng' itabadilika kuwa Krioli kwani msimbo hauwezi kamwe kuwa lahaja bila kuchukua sifa za Krioli.

Baadhi ya watafitiwa ambao walikuwa wanafunzi katika shule za upili walieleza kwamba walijifunza Kiswahili kama lugha ya kwanza kwa sababu walizaliwa mijini. Wao walidai kwamba walijifunza msimbo wa Sheng' walipotangamana na watoto wenzao wa majirani na miktadha isiyokuwa rasmi shuleni. Kutokana na hali hii, utafiti huu, kinyume na ilivyodaiwa na Spyropoulos (1987), uliakisi kwamba wahusika

wanaozungumza Sheng’ katika maeneo tofauti nchini Kenya hawaitumii kama ‘lugha’ ya kwanza ila ni wasemaji wazawa wa lugha nyinginezo.

**[c] Kutoimarishwa kwa Mielekeo Chanya na Hadhi Yake**

Mielekeo ya watu kuhusu Krioli huimarika kadiri inapoendelea kustawi kutoka upijini. Hadhi zao huimarika kadiri mielekeo hiyo inapostawi na kwa kutegemea maendeleo yake. Hii inamaanisha kuwa kuendelezwa kwa Krioli kimofolojia na kisintaksia huifanya iweze kutumika kama lugha zingine za kawaida zilizoimarishwa.

Utafiti huu uligundua kuwa hakujawa na juhudi za kuistawisha Sheng’ zaidi kwa kuendeleza mielekeo ya watu kuihusu au kuiendeleza hadhi yake ili iweze kutumika kama lugha msimbo pana. Sheng’ kwa mujibu wa uchunzaji uliofanywa na mtafiti imekuwa ikitumiwa kama msimbo finyu unaofaa kwa vikundi vidogovidogo kama wanafunzi au familia za mitaani. Uchunzaji huo ulionyesha kuwa hakujakuwa na harakati za kuona namna ya kutumia Sheng’ kama lugha ya kufundishia, ya kuunganisha watu katika jamii na hata kuandika vitabu kama vya fasihi. Juhudi za aina hizo kama zile zilizoangaziwa na Jwan (1997) kwenye muktadha wa makao ya watoto wa mitaani au mayatima zikiendelezwa zaidi, mielekeo na hadhi ya Sheng’ huweza kuboreshwa. Hata hivyo, utafiti huu unadokeza kwamba kuimarishwa kwa mielekeo na hadhi pekee hakutaigeuza Sheng’ kuwa Pijini. Hii ni kwa vile, kama ilivyojitokeza katika uchanganuzi kuhusu upijini wa Sheng’, msimbo wenyewe haujawahi kuwa Pijini.

## 3.3 Tofauti baina ya Msimu, Pijini na Krioli

Uchanganuzi uliofanywa hapo juu katika sura hii unaonyesha kuwa Sheng’ si Pijini wala Krioli ila ni msimu. Uchanganuzi wenyewe umeonyesha kuwa Sheng’ haikuwahi

kuwa Pijini wala si Krioli kwa sasa. Uchanganuzi huo umeashiria kwa upande mwingine kwamba baadhi ya sifa za Sheng' zinafanana kisadfa tu na zile za Pijini na hata za Krioli. Jedwali 3.4 lifuatalo linaonyesha baadhi ya sifa zao zinazoweza kutumiwa ili kutofautisha.

**Jedwali 3. 4: Tofauti Kati ya Msimu, Pijini na Krioli**

| | Sifa za Pijini | Sifa za Krioli | Sifa za Msimu (Sheng') |
|---|---|---|---|
| 1. | Haiwezi kusanifishwa | Huweza kusanifishwa | Watafitiwa wetu waliashiria kuwa msimu (Sheng) hauwezi kusanifishwa |
| 2. | Haiwezi kufanywa kuwa launi rasmi wala hazitumiki katika miktadha rasmi. | Inaweza kukubalika katika miktadha rasmi na huweza kufanywa kuwa launi rasmi. | Matokeo ya usaili wa watafitiwa yalionyesha kuwa msimu (Sheng') haukubainika katika miktadha rasmi na hauwezi kufanywa kuwa launi rasmi [Hata hivyo, msimu kama Sheng' huweza kujitokeza katika dayolojia zinazotumiwa kimtindo katika maandishi ya fasihi kama vile riwaya na tamthilia]. Uchunguzi huu ulionyesha kuwa Sheng' huweza kutumiwa katika baadhi tu miktadha rasmi kama launi isiyotarajiwa. |
| 3. | Ni msimbo finyu | Ni msimbo pana | Uchanganuzi wa matumizi ya Sheng' umeonyesha kuwa msimu huu ni msimbo finyu. |
| 4. | Hutokana na haja ya kuwasiliana mahali ambapo hakuna lingua franka. Kulingana na nadharia ya 4M, Kuibuka kwake kunafungamana na mseto wa lugha-tuhinga na lugha-takaro zinazoungana. | Hutokana na Pijini inayoimarika | Hutokana na ubunifu wa wazungumzaji wa lugha moja. Hakuna lugha-tuhinga na lugha-takaro zinazohusika katika uzalishaji wa msimu. |
| 5. | Muundo wake wa kimofosintaksia si thabiti | Msamiati na muundo wa kimofosintaksia umekuwa thabiti | Msamiati wake hugeukageuka |
| 6. | Hutumiwa miongoni mwa wale walioianzisha kama vile wafanyibiashara na watumwa pekee yao. Haitumiwi nje ya miktadha hiyo. | Hutumiwa katika jumuiya lugha nzima. | Hutumika katika makundi madogo madogo kama vile miongoni mwa wanafunzi, baina ya walanguzi na watumiaji wa dawa za kulevya. |
| 7. | Hazichangii msamiati kwa lugha nyinginezo. | Kwa vile msamiati wake unapanuliwa kadiri wakati unapoendelea, inaweza kuchangia msamiati kwa lugha nyinginezo. | Huweza kuchangia msamiati lugha changizi vile ambavyo maneno machache ya Sheng' yanaweza kuingizwa katika Kiswahili na kusanifishwa. |
| 8. | Kuibuka kwake hakuhusiani na umri wala aina za tamaduni zinazopatikana katika jamii. | Kugeuka kwa Pijini kuwa Krioli hakuhusiani na umri maalum au kutofautiana kwa vijana na wazee kwa misingi ya utamaduni. | Mara nyingi msimu unaibukamiongoni mwa vijana ambao wanahusishwa na tamaduni zisizolingana na zile za wazee. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9. | Haitegemei muziki au vyombo vya habari ili kupata msamiati wa kutumiwa ila huteuateua tu kutoka lugha mbili ambazo wazungumzaji hawana lugha shirikishi (lingua franka) | Msamiati wake huweza kuundwa au kupanuliwa kwa njia mbalimbali. Msamiati huo unaweza kusanifishwa iwapo upangaji lugha unahusu Krioli husika utafanywa. | Msamiati wa msimu kama Sheng' unaweza kupanuliwa kupitia tovuso (Facebook), rununu, vyombo vya habari na muziki. |
| 10. | Maneno yanayokopwa hayafupishwifupishwi wala kugeuzwagezwa ila yanatumiwa kama yalivyokuwa katika lugha chasili isipokuwa tu miundo sahili ya sentensi inatumiwa. | Ufupishaji unaweza kutumiwa kama mbinu ya kuunda msamiati mpya wakati kanuni za kimofolojia zinazotawala miundo ya maneno katika Krioli husika zitakuwa zimebainika. | Maneno aghalabu yanafupishwa na urari wa silabi huweza kutokea. |
| 11. | Aghalabu kila neno hubeba maana moja ambayo ni sahili na halipewi fahiwa inayorejelea kinyume cha maana yake. | Maneno hayatumiwi kupitisha kinyume cha maana zao isipokuwa tu pale ambapo mabadiliko ya kisemantiki yanatokea katika lugha. Aghalabu maana za maneno yanayoingizwa kutoka lugha zingine hudumishwa. | Maneno yanayokopwa huweza kupewa maana ambayo ni kinyume kama vile 'baya' kuwa 'zuri' au 'zuri' kuwa 'baya' vile inavyojitokeza katika mfano: Tulicheza ball mbaya. Maneno mengine yanayokopwa hupewa maana tofauti kabisa na maana zao asili katika msimu. |
| 12. | Motisha ya kutumia Pijini ni lengo la kufanya mawasiliano. | Kuibuka kwa Krioli hakutokani na haja ya kukiuka ukawaida au kwa sababu za kimtindo. | Motisha ya kutumiwa kwa misimu huweza kuwa wa kuendeleza ubunifu kama inavyojitokeza katika muziki |
| 13. | Matumizi yake hayahusishwi na ufichaji wa siri. Pijini haianzishwi kwa lengo la kuwatenga wengine ila kuunganisha. | Hutumiwa kama kitambulisho cha jamii nzima na hata huweza kutumiwa kama lingua franka au lugha inayounganisha kikundi kizima. | Hutumiwa kwa maarubu ya kuwabagua wengine kimawasiliano na kuficha siri. |
| 14. | Neno huweza kutumiwa wakati wote bila kuachwa ili neno jipya litumike kama kibadala chake. | Maneno mapya hayaundwiundwi ili kuchukua nafasi ya yale yaliyozoeleka. | Maneno mapya huundwaundwa ili kuchukua nafasi ya maneno ambayo yamezoelewa ili kuendelea kuficha siri. |
| 15. | Huhusishwa zaidi na watumwa, wafanyabiashara na mabaharia wanaofikia nchi mbalimbali ambapo hawana lingua franka ya kutumia ili kuwasiliana na wenyeji. | Haihusishwi na majangili au vijana ila inahusishwa na jamii nzima inayoitumia. | Huhusishwa zaidi na walanguzi wa dawa za kulevya, vijana, wezi, wachopozi na wanamuziki ambao aghalabu ni vijana. |
| 16. | Aghalabu inahusishwa na sajili ya biashara. | Inaweza kutumiwa kwa takribani sajili zote kwa kutegemea kiwango cha kuimarika kwake. | Haitumiki katika sajili kama za sheria, bunge, sayansi na hata katika sajili ya hospitalini. |
| 17. | Matumizi yake hayaambatani na miktadha rasmi na matumizi yake yanaweza kupunguza urasmi kwa jinsi ambavyo msimu (Sheng') unaweza kufanya. | Isipokuwa pale ambapo kuna lugha nyingine inayotumika kama launi ya juu huku Krioli yenyewe ikitumika kama launi ya chini; matumizi ya Krioli hayawezi kupunguza urasmi katika muktadha wa mawasiliano. | Matumizi ya Sheng' yanaweza kuvunja urasmi hasa iwapo watu wazima watatumia Sheng' wakizungumza na vijana au wakizungumza katika miktadha rasmi. Hivi, msimu hufaa kwa ujenzi wa umoja na ushirikiano baina ya vijana na wazee. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 18. | Pijini hutizamwa kama lugha mbovu na kwa hivyo haipendwi na wazungumzaji wa lugha zilizoimarika. | Kadiri launi inapoendelea kuimarika kuwa Krioli na matumizi yake yanapanuka, wengi huanza kuipenda. | Watu wengi na hata taasisi wana mielekeo hasi kuhusu misimu kama vile Sheng' na Slang. |

Sifa zilizobainika katika kitengo kinachobainisha sifa za msimu cha jedwali 3.4 hapo juu zilitokana na usaili wa watafitiwa katika utafiti huu na zinaonyesha hasa kwamba Sheng' haijawahi kuwa Pijini na hivi sasa si Krioli wala lugha ila ni msimu. Uchunguzi uliofanywa na mtafiti ulibainisha kwamba msimbo huu umetumiwa katika maandishi mbalimbali. Kwa mfano, ilibainika kwamba Sheng' imetumiwa katika matini za katuni kwenye gazeti la *Daily Nation* hasa toleo linaloambatishwa kwa magazeti ya Jumamosi yanayolenga vijana. Gazeti la *Nairobian* nalo lina kitengo kilichotengewa msimbo wa Sheng'. Ingawa hii ni hatua muhimu inayohusiana na upijinishaji, haitoshelezi na haiwezi kutegemewa kama kigezo cha kubainisha kuwa Sheng' ni Krioli. Hata hivyo, kule kutumiwa katika maandishi kama magazeti kunaweka msimbo huu katika kiwango kingine cha kukua kwake.

Isitoshe, mtafiti aligundua kuwa kamusi ya Sheng' ilikwisha kuchapishwa. Vilevile, kuna kamusi ya Sheng' inayopatikana kwenye tovuti inayoitwa '*Sheng Nation'* ambayo inatoa maelezo kuhusu maneno ya Sheng'. Kamusi hiyo huwasaidia watafiti kutafsiri maneno ya lugha nyingine hadi Sheng. Hatimaye kuna mitandao kwenye tovuti inayoendeleza msimbo wa Sheng'. Licha ya hayo yote, tasnifu hii inahitimisha kwamba uzito wa sifa za Sheng' kwa sasa bado haujatosheleza ule wa Krioli.

### 3.4 Hitimisho

Matokeo yaliyochanganuliwa hapo juu kuhusu upijini na ukrioli wa Sheng' yanabainisha sifa za msimbo wenyewe. Kutokana na matokeo haya, utafiti huu unahalalisha nadharia tete ya pili ya utafiti huu kwamba 'sifa za Sheng' zinapinga

upijini au ukriolishaji wake'. Matokeo hayo basi yanapinga nadharia tete zilizoshikiliwa na watafiti wanaorejelea Sheng' kama lahaja ya Kiswahili (Tazama utafiti wa Bosire, 2006), Sheng' kama lugha mahuluti (Tazama utafiti wa Abdulaziz na Osinde, 1997), Sheng' kama Pijini au Krioli (Tazama Spyropoulos, 1987) au Sheng' kama ubadilishaji msimbo (Tazama utafiti wa Myers-Scotton, 1993a) kwa kuithibitisha kama msimu.

Sura inayofuata inajadili data mintarafu ya lengo la tatu na la nne, katika sura hiyo, tumepambanua mikakati ya kiwingi-lugha katika Sheng' na uchanganuzi wa tungo zake kwa vigezo vya Nadharia ya 4M.

# SURA YA NNE

# MIKAKATI YA KIWINGI-LUGHA KATIKA SHENG' NA UCHANGANUZI WA TUNGO ZAKE KWA VIGEZO VYA 4M

## 4.0 Utangulizi

Sehemu 4.1 na 4.2 za sura hii zinachanganua data ya utafiti huu kwa mujibu wa lengo la tatu ambalo ni kupambanua mikakati ya kiwingi lugha inayojitokeza katika miundo yenye Sheng', na lengo la nne, ambalo ni kuchanganua tungo zenye Sheng' kwa kuzingatia Nadharia ya 4M. Sehemu 4.1 kwa hivyo inafafanua mikakati ya kiwingi-lugha ambayo ni uchanganyaji msimbo, wingishaji-maradufu, ushabihiano, ujozi msimbo na utatu msimbo. Sehemu 4.2 nayo inachanganua miundo ya Sheng'. Katika sehemu hii tumechanganua mchango wa LS na LC kwa miundo yenye UM, mseto wa viambajengo vya LS na LC, vizingwa vya LS katika miundo yenye UM, na vizingwa vya LC katika miundo yenye UM. Sehemu ya 4.3 ya sura hii nayo inaangazia mkuku wa kimofosintaksia unaozingatiwa katika uzalishaji wa miundo yenye vipashio vya LS + LC. Kanuni mbili ambazo ni kanuni ya mfuatano wa mofimu na kanuni ya mofimu amilifu kama zilivyofafanuliwa na Myers-Scotton katika nadharia ya 4M zinafafanuliwa kwa undani huku kanuni hizi zikituongoza katika uchanganuzi wa data ya utafiti huu.

## 4.1 Mikakati ya Kiwingi-Lugha katika Diskosi Zenye Sheng'

Sehemu zifuatazo za sura hii zinachanganua data ya utafiti kwa mujibu wa lengo la tatu la utafiti huu la kufafanua mikakati ya kiwingi-lugha inayohusika katika miundo yenye Sheng'. Mikakati inayobainishwa ni pamoja na uchanganyaji msimbo, wingishaji-maradufu, ushabihiano, ujozi-msimbo na utatu-msimbo.

### 4.1.1 Uchanganyaji Msimbo

Dhana hii kama ilivyofafanuliwa katika sehemu ya istilahi zilizotumiwa katika uchunguzi huu imetumiwa katika tasnifu hii kurejelea aina ya uchanganyaji wa viambajengo vya zaidi ya msimbo mmoja unaofanyika ndani ya kishazi au sentensi moja. Sentensi ifuatayo iliyozalishwa na mwanafunzi katika shule moja ilikuwa na uchanganyaji msimbo ambao ulihusu misimbo miwili, yaani lugha moja ambayo ni Kiswahili na msimu mmoja ambao ni Sheng'.

74. Sisi ni magwiji wa swa ndo niliona nikushoo.
Sisi ni magwiji wa (somo la) Kiswahili kwa hivyo niliona nikujulishe.

Muundo (74) ni mfano wa uchanganyaji msimbo kama baadhi ya mikakati inayotumiwa na wazungumzaji wa Sheng' katika mazungumzo yao ya kiwingi-lugha kwa vile ina maumbo ya Kiswahili na Sheng' ndani ya sentensi moja. Maneno kama vile 'sisi', 'ni', 'magwiji', 'wa' na 'niliona' ni maumbo ya Kiswahili. Maneno mengine ni ya Sheng'. Kwa mfano, neno '*swa'* ni kifupisho cha Sheng' cha neno 'Kiswahili'. '*Niku-shoo'* nalo ni umbo la Sheng' lililoundwa kwa kutumia mbinu ya uhamishaji maana. Hii ni kwa vile *'shoo'* halina maana ya 'kuonyesha' katika Sheng' kama ilivyokuwa katika Kiingereza. Badala yake, umbo hili '*shoo'* lina maana ya nikujulishe katika Sheng' kunaonyesha kwamba lugha hizi mbili zinaweza kushirikiana katika uzalishaji wa miundo yenye maana ukiwa mfanyiko mmoja wa kiwingi-lugha unaotumiwa kuhusiana na Sheng'. Kielelezo 4.1 kifuatacho kinaonyesha uchanganyaji-msimbo kama mgotanisho wa faridi za misimbo miwili kama Sheng' (msimu) na Kiswahili (lugha) unaofanyika ndani ya sentensi moja. Uchanganyaji msimbo ni mkakati mmoja wa kiwingi-lugha unaotokea wakati msimu unahusika katika UM na lugha.

**Kielelezo 4. 1: Uchanganyaji-Msimbo baina ya Msimu na Lugha**

| Sentensi yenye U.M. | = | Msimbo 1<br>[Viambajengo vya **msimu** (Sheng')] | + | Msimbo 2<br>[Viambajengo vya **lugha** (Kiswahili)] |
|---|---|---|---|---|

Mfano (75) unadhihirisha mkakati mwingine wa kiwingi-lugha unaozingatia mkuku wa kisarufi wa Kiswahili. Mkakati wenyewe unaohusu matumizi ya mofimu amilifu ya Kiswahili 'ni-' ambayo ni kiambishi kitegemezi cha nafsi ya kwanza umoja na mofimu mbili za kileksika za Sheng' '*save'* (saidia) na *'blu'* (shilingi ishirini).

75. Nisave hiyo blu.
    Uniauni shilingi ishirini.

Mkakati uliotumiwa katika muundo (75) ni wa uchanganyaji msimbo kwa sababu unahusisha ugotanishaji wa mofu za Kiswahili na msimbo wa Sheng' ndani ya sentensi moja. Mfano (75) unafanana sana na sentensi zinazoundwa kwa maneno ya Kiswahili pekee. Mfano ufuatao ulinukuliwa kutoka kwa muktadha wa shule.

76. Beshte wetu amelenga chuo.
    Rafiki yetu ameacha shule.

Muundo wa mfano (76) una neno la Sheng' '*beshte'* lililotoholewa kutoka kwa neno la Kiingereza 'best' ambalo lina maana ya kitu kizuri kuliko vyote. Kwa hivyo umbo '*beshte'* hutumiwa katika Sheng' kwa maana ya rafiki wa dhati. Aidha, kuna maneno '*lenga'* na '*chuo'* yenye asili ya Kiswahili ambayo kupitia mbinu ya uhamishaji wa maana yamepewa maana tofauti katika Sheng' ili yamaanishe 'kuacha' na 'shule (hata za msingi na za upili)' mtawalia. Neno *'lenga'* katika Kiswahili sanifu lingemaanisha 'dhamiria' na neno *'chuo'* linamaanisha 'taasisi ya juu ya elimu'. Sentensi hii vilevile ina neno la Kiswahili ambalo ni 'wetu'. Kutumiwa kwa maneno ya aina hii ya msimbo

wa Sheng' kwa pamoja na lile la Kiswahili kulitokea kama mkakati wa kiwingi-lugha, baina ya msimu wa Sheng' na lugha ya Kiswahili unaoweza kutumiwa na wazungumzaji wa Sheng' ili kuwasilisha maana. Mfano mwingine ni (77) ufuatao:

77. Mapero na siz yako kimaisha wako poa?
    Wazazi na dada yako ni wazima?

Katika sentensi hii (77) uchanganyaji msimbo umetokea baina ya Kiswahili na Sheng'. Maumbo ya Kiswahili katika sentensi hii ni 'na', 'yako', 'kimaisha' na 'wako'. Maumbo ya Sheng' hapa ni *'mapero', 'siz'* na '*poa'*. Maumbo haya ya Sheng' yana asili yake katika Kiingereza. Yalikopwa na sasa ni maumbo ya Sheng'. Neno '*mapero'* limetokana na neno la Kiingereza 'parents' lenye maana ya wazazi na '*siz'* limetokana na neno 'sister' lenye maana ya dada. Neno *'poa'* katika muktadha huu wa Sheng' lina maana ya 'sawa' lakini katika Kiswahili neno hili lina maana ya kupoteza joto. Tazama pia mfano (78):

78. Msupa wako alinishoo nikushtue.
    Kidosho wako aliniambia nikujulishe.

Sentensi hii (78) ina umbo moja la Kiswahili na maumbo matatu ya Sheng'. 'Wako' ni umbo la Kiswahili ilhali '*msupa', 'alinishoo'* na '*nikushtue'* ni maumbo ya Sheng'. Maumbo ya Sheng' '*msupa'* na '*alinishoo'* yana asili ya Kiingereza, kwani ni msamiati wa Sheng' uliokopwa kutoka Kiingereza. Neno '*msupa'* limetokana na la Kiingereza 'super' lenye maana ya kitu kizuri, na hivyo katika Sheng' likapewa maana ya kidosho. Vilevile, neno '*alinishoo'* limetokana na la Kiingereza 'show' lenye maana ya kuonyesha lakini katika Sheng' neno hili lina maana ya kujulisha. Shuhudia mfano ufuatao:

79. Mboch wetu ni fala… yaani ni mshamba mbaya.
    Kijakazi wetu ni mshamba sana.

Uchanganyaji msimbo unaotokea katika sentensi (79) unafanyika baina ya lugha moja na msimbo mmoja, yaani Kiswahili na Sheng'. Maumbo ya Kiswahili ni 'wetu', 'ni', 'fala', 'yaani', 'mshamba' na 'mbaya'. Hata hivyo jinsi maneno *'mshamba mbaya'* yalivyotumiwa katika sentensi hii inakubalika tu katika Sheng' wala sio katika Kiswahili sanifu, na kwa hivyo yamejitokeza kama maumbo ya Sheng'. Umbo *'mboch'* vilevile ni la Sheng'. Neno '*mboch'* lina maana ya kijakazi. Shuhudia pia mfano ufuatao:

80. Saa hii sina nangos chuo, siwezi vuta waya.
Sasa hivi sina simu shuleni, kwa hivyo siwezi kupiga simu.

Sentensi hii (80) ina uchanganyaji msimbo unaotokea baina ya misimbo miwili pia ambayo ni Kiswahili na Sheng'. Maumbo ya Kiswahili katika sentensi hii ni 'saa', 'hii', 'sina' na 'siwezi'. Maumbo ya Sheng' ni *'nangos'*, *'chuo'* na *'vuta waya'*. Asili ya neno '*nangos'* haijulikani ingawa lina maana ya simu ya mkono. Neno '*chuo'* lina maana ya shule katika Sheng' na '*vuta waya'* ina maana ya kupiga simu. Mfano huu unadhihirisha vilevile kwamba uchanganyaji msimbo ni mkakati mwingine wa kiwingi-lugha ambao unahusika katika uwasilishaji wa maana wakati watu wanapotumia Sheng'. Ufuatao ni mfano mwingine unaodhihirisha kuhusika kwa uchanganyaji msimbo kama mkakati wa kiwingi-lugha unaohusisha Sheng'.

81. Muhula ulipita nilikuwa majuu.
Muhula uliopita nilikua ughaibuni/ng'ambo.

Sentensi hii (81) ina maumbo ya Kiswahili na Sheng'. Maumbo ya Kiswahili ni 'muhula', 'ulipita', na 'nilikuwa'. Ingawa haya ni maumbo ya Kiswahili, sentensi hii ina kosa moja kubwa kisarufi kwani haina kielezi. Ingekuwa bora kwa msemaji kusema 'muhula ambao ulipita' au 'muhula uliopita nilikuwa....' Hapa tunashuhudia hali ambapo neno nzima limedondoshwa katika sentensi. Hali hii inakubalika katika Sheng'

lakini haikubaliki katika Kiswahili sanifu. Kwa hivyo katika muktadha huu, neno *'ulipita'* ni la Sheng'. Sentensi hii ina umbo lingine la Sheng' ambalo ni *'majuu'*. Neno hili lina asili ya Kiswahili lakini maana yake ya Sheng' katika muktadha wa sentensi hii ni ughaibuni/ng'ambo. Mfano huu unaonyesha hali ambapo msimbo wa Sheng' hutegemea muundo na baadhi ya maneno na viambishi vya lugha (Kiswahili) ili kuzalisha sentensi zinazobeba maana. Sentensi zilizoundwa kwa maneno yote na viambishi vyote vya Sheng' hazikudhihirika katika utafiti huu. Mfano mwingine ni (82):

82. Niko poa lakini ni venye maisha iko gwan.
    Niko salama lakini maisha yamekuwa magumu.

Sentensi hii (82) inadhihirisha uchanganyaji msimbo wa misimbo miwili ambayo ni Kiswahili na Sheng'. Hii inamaanisha kuwa ugotanishaji misimbo umefanyika ndani ya sentensi moja. Maumbo ya misimbo hii imeshiriki katika kujenga sentensi na kuwasilisha maana. Maumbo ya Kiswahili yaliyoshiriki ni 'niko', 'lakini', ni na 'maisha'. Maumbo ya Sheng' ni *'poa, iko gwan* na *venye'*. *'Poa'* katika Sheng' lina maana ya sawa. *'Iko gwan'* ina maana kuwa (maisha) ni magumu. Ingawa neno *'venye'* lina asili ya Kiswahili halikubaliki kutumiwa vile katika Kiswahili. Aidha katika Kiswahili linaweza kutumiwa kama kielezi pamoja na majina ya ngeli mbalimbali huku likichukua viambishi awali vinavyoandamana na ngeli hizo. Kwa mfano kisintaksia, ngeli ya a-wa, tunapata mfano wa mtoto mwenye, mwenyewe, na kadhalika. Katika sentensi hii neno hili limetumika badala ya neno 'vile' au 'jinsi'. Hali hii inakubalika katika Sheng' lakini haikubaliki katika Kiswahili.

### 4.1.2 Wingishaji-Maradufu

Katika sentensi (83) ifuatayo, kiambishi awali cha Kiswahili 'ma-' na kiambishi tamati cha Kiingereza '-s' ni mofu za wingi ambazo zimetumiwa katika neno moja. Ingawa mofu moja ya Kiingereza '-s' ingebainisha hali ya wingi, hitaji kwamba mofimu amilifu kama vile viambishi vya umoja na wingi vinapaswa kutokana na lugha solo huwalazimisha wazungumzaji wa Sheng' wanaobadilisha msimbo kufanya wingishaji maradufu.

83. Utengano iko na <u>ma</u>teaching<u>s</u> kibao kwetu.
    (Riwaya ya) 'Utengano' ina mafunzo mengi kwetu.

Mfano (83) unaashiria hali ambapo neno linapokopwa kutoka lugha ya Kiingereza, wingishaji-maradufu hufanyika ili neno husika liweze kusimilishwa katika mofolojia ya Sheng'. Baada ya kusimilishwa kwa neno kama 'teachings' mofimu amilifu ya upatanisho wa kisarufi '-s', ingawa itabaki kwenye umbo, haitatekeleza tena kazi ya kubainisha wingi na badala yake mofimu '*ma-'* ya Sheng' itaambikwa kama kibainishi cha wingi. Ifuatayo ni mifano mingine ya namna wingishaji-maradufu unavyotokea katika maumbo yanayotumiwa kama viambajengo vya sentensi.

84. Alitumia doo kununua mambuzi. Hizo mambuzi zimezaana.
    Alitumia pesa kununua mbuzi. Mbuzi hao wamezaana.

85. Mainzi ni wengi ocha siku hizi.
    Siku hizi nzi ni wengi mashambani.

86. Anafanya biashara ya kununua na kukinda maumbwa tao.
    Anafanya biashara ya kununua na kuuza mbwa (wengi) mjini.

Msamiati wa wanyama uliotumiwa katika mifano (84), (85) na (86) *'mambuzi'*, *'mainzi'* na '*maumbwa* ni mfano mwingine wa namna wingishaji maradufu unavyojitokeza wakati maneno ya Kiswahili yanaposimilishwa katika Sheng'. Maneno

haya 'nzi, mbwa na mbuzi' hujitokeza katika ngeli ya a-wa katika Kiswahili. Usimilishwaji wa maneno hayo hadi Sheng' kutoka Kiswahili umefanywa kwa kutumiwa mofu ya kubainisha wingi 'ma-'.

Mfano (84) unaonyesha namna neno 'mbuzi' ambalo halingebadilishwa katika hali ya wingi katika Kiswahili linabadilishwa kuwa *'mambuzi'*. Isitoshe, mofu ya ngeli 'zi' ambayo ni kipatanishi cha nomino zisizokuwa hai inatumiwa kulirejelea neno 'mbuzi' katika Sheng.' Mofu hii hutumiwa katika Sheng' bila kujali iwapo nomino zinazorejelewa ni hisivu au si hisivu. Kwa mtazamo wa tasnifu hii, hapana budi kwamba hali hii huwaathiri wanafunzi ambao ni wasemaji wa Sheng' katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Uchanganuzi huu unaashiria kwamba Sheng' haizingatii mofosintaksia ya Kiswahili kwa maana haizingatii kanuni za mnyambuliko za umoja na wingi pamoja na upatanisho wa kisarufi baina ya nomino na vivumishi au nomino na vitenzi. Usemi (87) ufuatao vilevile una mfano wa umbo linalodhihirisha sifa za wingishaji maradufu unaojitokeza katika Sheng'.


87. Tunangoja tu hizo <u>ma</u>pepa<u>s</u> halafu tuanze kudunga revision.
    Tunasubiri tu hizo karatasi halafu tuanze kufanya udurusu.

Kiambishi awali cha wingi 'ma-' kilichopigwa mstari katika mfano (87) kimetumiwa katika neno '*mapepas'* ilihali tayari kuna kiambishi tamati '*-s'* ambacho katika Kiingereza kinawakilisha hali ya wingi. Kwa mujibu wa nadharia ya 4M, kutumiwa kwa mofu 'ma' hufanywa kwa sababu Kiswahili ni lugha solo ya sentensi (87). Usaili wa watafitiwa wetu uliashiria kuwa sababu za kisaikolojia kama kufikiri kwamba hawataeleweka huwafanya wazungumzaji wateue na kutumia mofu za wingi za lugha chasili (kama *'-s'*) lakini sababu za kimofolojia zinawafanya wateue mofu za lugha solo (kama 'ma-').

88. Venye <u>maodijoz</u> walienda strike fom ilikuwa ni mabiz tu.
Wakati walimu walikuwa wamegoma shughuli zilikuwa za biashara tu.

Muundo wa neno '*maodijoz'* lililopigwa mstari katika mfano (88) ni mfano mwingine wa wingishaji maradufu unaofungamana na matumizi ya mofu mbili amilifu. Kwanza, mofu *'ma-'* imetumiwa kama kiambishi kibainishi cha wingi kabla ya mzizi '*odijo'*. Pili, mofu *'z'* ambayo, kwa mtazamo wa tasnifu hii, ni kibadala cha mofu ya wingi katika Kiingereza 's' imetumiwa baada ya mzizi. Hivyo basi, maumbo mawili 'ma' na 'z' yenye uamilifu wa kubainisha wingi katika Kiswahili '*ma'* na Kiingereza 's' katika lugha chasili yametumiwa kabla na baada ya mzizi wa nomino. '*Maodijoz'* ni umbo la Sheng' lenye maana ya 'walimu'. Mintarafu ya uchanganuzi huu, wingishaji maradufu kama mkakati wa kiwingi-lugha unaweza kuwakilishwa kwenye Kielelezo 4.2 kwa jinsi ifuatavyo:

**Kielelezo 4. 2: Wingishaji-Maradufu kwenye Nomino za Sheng'**




Katika Kielelezo 4.2 inabainika kwamba katika wingishaji-maradufu kwenye nomino za Sheng', kiambishi awali cha kubainisha wingi cha Kiswahili ma- huunganishwa na mzizi wa nomino na kisha kufuatwa na kiambishi tamati cha kubainisha wingi chenye asili ya Kiingereza -z (s).

### 4.1.3 Ushabihiano

Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa ushabihiano ni mojawapo ya mikakati ya kiwingi-lugha inayotumiwa na wazungumzaji wa Sheng' ili kufanikisha mawasiliano. Ushabihiano ni dhana inayorejelea ubadilishaji fiche wa kimuundo unaohusu mkuku wa kimofolojia au wa kisintaksia unaokaliwa na vijenzi. Schmitt (2000) anafafanua

ushabihiano kama tukio la mtagusano wa lugha linalotokea wakati muundo wa kileksia wa lugha moja huathiriwa na muundo wa lugha nyingine. Ushabihiano ukitokea, muundo utakaozalishwa utakuwa na lugha solo zaidi ya moja (composite ML).

Data iliyonukuliwa kutoka kwa mazungumzo ilidhihirisha dai la nadharia ya 4M. Hii ni kwa kuwa baadhi ya miundo iliyozalishwa ilikuwa na ushabihiano kama mfanyiko tendani uliotokea na kusababisha kuundwa kwa muundo wa kiisimu wenye viambajengo vya lugha tofauti vinavyofuata mkuku wa lugha nyingine. Uchanganuzi wa data kuhusiana na upijini na ukriolishaji wa Sheng' unadokeza dai la Myers-Scotton (2002) kwamba ushabihiano ni mfanyiko ambao hatua kwa hatua husababisha uundaji wa Krioli si sahihi kwani mfanyiko huo pekee yake hauwezi kuwa kibainishi cha upijinishaji. Mifano ya ushabihiano iliyonukuliwa katika utafiti huu kama mkakati wa kiwingi-lugha unaotumiwa na wazungumzaji wa Sheng ni kama ifuatayo:

89. Mabuddy walicome kunicheki, maadvise kibao na malectures from paros.
    Marafiki walikuja kuniona, kulikuwa na ushauri mwingi kutoka kwao na wazazi.

Sentensi hii ni ya msimbo wa Sheng'. Neno '*maadvice'* linaashiria kutumika kwa ushabihiano kama mkakati wa kiwingi-lugha katika mfano (89). Hii ni kwa vile, kwa kuzingatia nadharia ya 4M, mofimu amilifu 'ma' ambayo ni kiambishi cha hali ya wingi katika Kiswahili na msimbo wa Sheng' limetumiwa katika nafasi inayokaliwa na viambishi vya wingi vya Sheng' au Kiswahili ilihali hali ya wingi katika neno 'advice' ingebainishwa kwa kuongeza mofu '-s' mwishoni mwake. Neno *'malectures'* hata hivyo si kiashiria cha ushabiahiano ila ni mfano wa wingishaji maradufu. Hii inamaanisha kuwa zaidi ya mkakati mmoja wa kiwingi-lugha huweza kutumiwa ndani ya sentensi moja. Ufuatao ni mfano mwingine wa usemi wenye ushabiahiano uliozalishwa na mmoja wa wanafunzi waliochunguzwa katika utafiti.

90. Hiyo teo iliarrive maze nikaichangamkia mara <u>that that.</u>
    Huo mtihani uliwasili nikaufanya mara hiyo hiyo.

Msamiati *'that that'* katika mfano (90) ni leksimu moja ambayo imeundwa kwa kurudufisha neno la Kiingereza 'that' lenye maana ya 'hiyo hiyo'. Si sahihi kwa mujibu wa sarufi ya Kiingereza kuunganisha vivumishi viashiria viwili kama 'that that'. Walakini, uhuru wa wazungumzaji wa Sheng' wa kutumia mkakati huu wa kiwingi-lugha (ushabiahiano) huwawezesha wazalishe sentensi kwa kuchopeka vipashio kama hivyo pale ambapo sheria za lugha nyingine kama Kiswahili zinaruhusu. Hii ni kwa sababu ingekuwa sahihi katika Kiswahili kusema 'mara hiyo hiyo' Hii inamaanisha kwamba katika muktadha huu, Kiswahili ilikuwa lugha solo iliyotoa mkuku wa kukaliwa na vipashio husika. Ingawa mfuatano wa maneno haya mawili '*that that'* haungekubalika katika sarufi ya Kiingereza, tasnifu hii ina hoja kwamba mkakati kama huu hutumika katika mazungumzo halisi, huwasilisha maana na hueleweka kwa wazungumzaji wa kisajili. Tazama mfano huu mwingine:


91. Shule <u>nado</u> poa but ni tu ngoso ndo bado sijapull up.
    Shuleni ninaendelea vyema ingawa bado sifanyi vizuri katika (somo la) Kiingereza.

Ushabihiano unajitokeza vilevile katika mfano (91) ulionukuliwa hapo juu ambao una maneno ya Kiingereza, Kiswahili na ya msimbo wa Sheng'. Ushabiahiano huo unahusu kule kuunganishwa kwa mofu 'na' na kitenzi cha Kiingereza 'do' ili kuunda umbo *'nado'*. Kulingana na nadharia ya 4M, 'na' ni mofimu amilifu huku 'do' ikiwa mofimu ya kileksika. Kwa mujibu wa sarufi ya Kiingereza, umbo 'do' halingepaswa kuunganishwa kwa kiambishi chochote cha awali. Hata hivyo, kuwepo kwa mkuku wa Kiswahili unaokubali kuongezwa kwa viambishi kabla ya vitenzi kunaruhusu ushabihiano ambapo kiambishi cha nafsi kinaambatanishwa kwa kitenzi *'nado'* na maana inawakilishwa.

### 4.1.4 Ujozi-Msimbo

Ujozi-msimbo au uwili msimbo ni dhana iliyotumiwa katika utafiti huu kurejelea hali ya kiwingi-lugha inayohusu ujuzi na matumizi wa misimbo miwili ya lugha baina ya sentensi na sentensi katika mawasiliano ambapo mmoja unaweza kuwa msimu wa lugha (kama Sheng') huku nyingine ikiwa lugha bainifu (kama Kiswahili au Kiingereza). Kielelezo 4.3 kifuatacho kinaonyesha ujozi-msimbo, wala sio ujozi-lugha, kama mkakati mmoja wa kiwingi-lugha unaotokea wakati Sheng' (msimu) inahusika katika UM na lugha kama vile Kiswahili au Kiingereza. Jedwali lifuatalo linaonyesha ujozi-msimbo baina ya msimu kama vile Sheng' na lugha kama vile Kiswahili au Kiingereza.

**Kielelezo 4. 3: Ujozi-Msimbo baina ya Msimu na Lugha**





Utafiti huu umeonyesha kuwa wasemaji wa Sheng' hutumia ujozi lugha kama mkakati wa kiwingi-lugha ili kupitisha ujumbe kwa kuteua maumbo ya msimbo wa Sheng' na kuyateua maumbo mengine ya Kiswahili kutoka kwa akili zao na kuyaunganisha ili kuunda sentensi za kiujozi-lugha. Huu ni mkakati unaowafanya wasemaji wa Sheng' wanaoelewa Kiswahili kuwa tofauti na wale wanaoelewa Kiswahili pekee. Hii ni kwa vile wale wanaoelewa Kiswahili bila ujuzi wa msimbo wa Sheng' au lugha nyingine hawawezi kutumia mkakati huu wa kiwingi-lugha (yaani, ujozi lugha) ila wanaweza kuunda sentensi za kiumoja-lugha pekee. Dhukuru usemi ufuatao ambao umerudiwa kama mfano (92).

92. Hao maodijoz maboiboi wanachapa wera vinoma jo!
    Wale walimu vijana vijana wanafanya kazi kwa bidii.

Maneno yaliyotumiwa katika mfano (92) yanaainishwa kama msamiati wa Sheng' na wa Kiswahili katika tasnifu hii. Uchanganuzi huu unafafanua kwamba maneno ya Sheng' yamehifadhiwa ndani ya ubongo mmoja wa mwanaujozi-lugha aliyezalisha muundo huu kwa pamoja na yale ya Kiswahili. Hivyo basi, anateua maneno ya Kiswahili na kuyaunganisha na yale ya Sheng' kama mkakati wa kiwingi-lugha unaoweza kutumiwa na mwanaujozi-lugha kwa mawasiliano kwa jinsi ifuatayo:

**Kielelezo 4.4: Mkakati wa Kiwingi-lugha akilini mwa Mwanaujozi-msimbo**





Kielelezo 4.4 kinaonyesha namna mwanaujozi-lugha anavyotumia mkakati wa kiwingi-lugha wa kuteuateua msamiati kutoka kwa Sheng' na Kiswahili na kuyaunganisha ili kuunda sentensi za kiujozi-lugha zinazoeleweka kwa wasemaji wengine wa Sheng' na Kiswahili. Nadharia ya 4M inabainisha vijenzi hivi vya sentensi za kiujozi-lugha zinazofanana na mfano (92) kama mofimu za kileksika mithili ya *'odijo', 'vinoma', 'hao'* na *'jo'*, na mofimu amilifu mfano wa '-na-', 'wa-', na 'ma-'.

### 4.1.5 Utatu-Msimbo

Hii ni hali ya matumizi lugha iliyodhihirika katika utafiti huu uliohusisha matumizi ya misimbo mitatu katika usemi mmoja. Kwa misingi hiyo, kielelezo 4.5 kifuatacho kinaonyesha utatu-msimbo kama mkakati mwingine wa kiwingi-lugha unaotokea wakati Sheng' (msimu) inahusika katika UM na lugha mbili kama vile Kiswahili na Kiingereza.

**Kielelezo 4. 5: Utatu-Msimbo baina ya Msimu Mmoja na Lugha mbili**




Kielelezo 4.5 kinafafanua mfano wa wa sentensi yenye UM ambayo imeundwa na vijenzi vya msimu kama vile Sheng', vijenzi vya lugha kama vile Kiingereza na vijenzi vya lugha ingine kama vile Kiswahili.

Ubadilishaji msimbo uliojitokeza katika sentensi ifuatayo iliyozalishwa na mwanafunzi katika muktadha wa shule ulikuwa mgotanisho baina ya misimbo mitatu ya lugha katika sentensi moja.

93. Wale mastude wawili wenye walidunga supra za purple walirobiwa na gondi kwa ile road inaendanga odhumo.
    Wale wanafunzi wawili waliokuwa wamevaa viatu vya rangi ya zambarau waliibiwa na mwizi kwenye barabara kuu ya kwenda Kisumu.

Sentensi (93) iliyonukuliwa hapo juu ina maumbo ya misimbo mitatu, Kiswahili, Sheng' na Kiingereza. Maumbo ya Kiswahili katika sentensi hii ni 'wale', 'wawili', 'wenye', 'na', 'kwa' na 'ile'. '*Mastude', 'walidunga', 'za', 'gondi', 'inaendanga'* na '*Odhumo'* ni maumbo ya Sheng'. 'Purple', 'rob' na 'road' ni maumbo ya Kiingereza.

Neno la Sheng' '*mastude'* lina maana ya wanafunzi, *'walidunga'* lina maana ya walivaa, '*walirobiwa'* lina maana ya waliibiwa, *'gondi'* ni mwizi, *'inaendanga'* lina maana ya huenda na '*Odhumo'* ni Kisumu katika Kiswahili cha kawaida. Neno la Kiingereza 'purple' lina maana ya aina ya rangi ya zambarau, na 'road' lina maana ya barabara katika Kiswahili. Matumizi ya maumbo haya yaliyotokana na misimbo mitatu ndani ya usemi wenyewe (93) yanaonyesha kuwa utatu-msimbo ni mkakati mwingine wa kiwingi-lugha unaotumiwa na wazungumzaji wa Sheng' ili kufanikisha mawasiliano. Tazama pia mfano (94):

94. Masa alikuwa ameishia market kununua unga.
    Mama alikuwa ameenda sokoni kununua unga.

Sentensi hii (94) ina maumbo ya misimbo mitatu. Inaonyesha utatu-msimbo unaotokea baina ya Kiswahili, Sheng' na Kiingereza. Maumbo 'alikuwa', 'kununua' na 'unga' ni ya Kiswahili. '*Masa'* na *'ameishia'* ni maumbo ya Sheng'. Neno la Sheng' *'masa'* lina maana ya mama katika Kiswahili, na *'ameishia'* lina maana ya ameenda katika Kiswahili sanifu. Neno 'market' ni la Kiingereza na lina maana ya sokoni katika Kiswahili sanifu. Ufuatao ni mfano mwingine.

95. Immediately umepata mra yoyote we nivutie.
    Mara tu utakapopata mradi wowote unijulishe (kupitia simu).

Sentensi (95) vilevile ina maumbo ya misimbo mitatu: Kiswahili, Sheng' na Kiingereza. Hivyo tunapata ubadilishaji msimbo wa misimbo mitatu katika sentensi moja. Maumbo 'umepata' na 'yoyote' ni ya Kiswahili. Maumbo *'mra', 'we'* na *'nivutie'* ni ya Sheng'. '*Mra'* (mradi) na '*we'* (wewe) ni maumbo yaliyoathirika na udondoshaji wa mofimu. Hata hivyo maumbo haya yanakubalika hivyo katika Sheng'. 'Immediately' ni umbo la Kiingereza ambalo lina maana ya mara tu. Ingawa ubadilishaji msimbo umeshuhudiwa katika mfano huu, tasnifu hii inahoji kwamba aina hii ya UM si ya kiutatu-lugha ila ni

ya kiutatu-msimbo kwa maana Sheng' si lugha. Ingawa UM wa aina hii haukuangaziwa na nadharia ya Myers-Scotton iliyoongoza utafiti huu, uchanganuzi huu unaashiria kwamba katika UM wa aina hii, mofu za misimbo tofautitofauti huungana ili kujenga sentensi zitakazowakilisha maana. Tazama mfano (96).

96. Mi niko poa, ni laif tu ya shule ndo ni hard kiasi.
Mimi niko sawa, maisha ya shule ndiyo yaliyo magumu kidogo.

Kule kutumiwa kwa maumbo ya misimbo mitatu katika sentensi (96) kunadhihirisha ubadilishaji msimbo wa kiutatu-msimbo. Maumbo 'niko', 'ni', 'tu', 'ya', 'shule' na 'kiasi' ni ya Kiswahili. Maumbo '*mi', 'poa' 'laif'* na *'ndo'* ni ya Sheng'. Umbo 'hard' ni la Kiingereza. Maumbo ya Sheng' '*mi', 'laif'* na '*ndo'* yameundwa kwa kuzidondosha mofu kutoka maneno ya Kiswahili 'mimi' na 'ndiyo'. Umbo la Kiingereza 'hard' lina maana ya ugumu ilhali neno 'life' lina maana ya maisha katika Kiswahili sanifu. Mfano ufuatao pia unashuhudia hali ya utatu-msimbo.

97. Laif inakupelekaje? Vipoa au imekuchapia dry?
Maisha yanakwendea vipi? Vyema au yamekuwa magumu?

Katika sentensi hii (97) tunashuhudia vilevile ubadilishaji msimbo baina ya misimbo mitatu: Kiswahili, Sheng' na Kiingereza. Inakupelekaje na au ni maumbo ya Kiswahili. '*Vipoa'* na '*imekuchapia dry*' ni maumbo ya Sheng'. '*Vipoa'* lina maana ya 'vyema' ilhali *'imekuchapia dry'* lina maana ya (maisha) kuwa magumu. Umbo la Kiingereza katika sentensi hii ni 'dry' ambalo lina maana ya 'kavu'. Neno la Sheng' '*laif'* limetoholewa kutoka kwa Kiingereza na lina maana ya 'maisha'. Mfano mwingine ni ufuatao:

98. Yule dame alikunywa mixture dangerous sana akitaka kuflash mtoi yuko hali zii.
    Yule msichana ambaye alikunywa mchanganyiko hatari sana akitaka kuavya mimba yuko hali mbaya.

Sentensi hii (98) imeundwa kwa kuyaunganisha maumbo ya misimbo mitatu. Maumbo ya Kiswahili ni 'yule', 'alikunywa', 'sana', 'akitaka', 'yuko' na 'hali'. Maumbo ya Kiingereza ni 'mixture' na 'dangerous'. Neno 'mixture' lina maana ya mchanganyiko, ilhali 'dangerous' linamaanisha hatari. Maumbo ya Sheng' katika sentensi hii ni *'dame'*, *'kuflash'*, *'mtoi'* na *'zii'*. Neno la Sheng' '*dame'* lina maana ya msichana, '*kuflash'* lina maana ya kuavya mimba na *'mtoi'* lina maana ya mtoto. Ingawa neno 'zii' ni la Kiswahili, matumizi yake katika sentensi hii ni ya Sheng' kwani katika Sheng' neno hili lina maana ya 'la' na katika Kiswahili ni tamko la kuzomea au kubeza kitu, au hali ya kutokuwepo kwa sauti ya aina yoyote. Matumizi ya maumbo haya ya Sheng', Kiswahili na Kiingereza katika sentensi hii yameashiria utatu-msimbo kama mkakati wa kiwingi-lugha unaotumiwa na wazungumzaji wa Sheng' ili kuwakilisha maana. Mfano ufuatao ni ushuhuda zaidi.

99. Huku tao wasee hupenda kuvaa lebo ziko kul Fridays … hapo ndo idea ilitoka.
    Huku mjini watu hupenda kuvaa mitindo mizuri Ijumaa, hapo ndipo wazo hilo lilitokea.

Sentensi hii ni mfano mwingine wa utatu-msimbo unaoshirikisha Kiswahili, Sheng' na Kiingereza kama mkakati wa kiwingi-lugha uliotumiwa na watafitiwa katika uchunguzi huu. 'Huku', 'hupenda', 'kuvaa' na 'ziko' ni maneno ya Kiswahili. Kutokana na neno la Kiingereza 'Cool' tumepata umbo la Sheng' *'kul'* ambalo limetoholewa na kupewa maana mpya katika Sheng'. Neno 'cool' lina maana ya kitu kionekanacho kuwa kizuri machoni mwa watu. Maumbo mengine ya Sheng' katika sentensi hii ni *'tao'*, *'wasee'* na *'lebo'*. Neno *'tao'* lina maana ya mjini, '*wasee'* lina maana ya vijana na *'lebo'* linatokana na neno la Kiingereza 'label' lenye maana ya mtindo wa kisasa. Maumbo

'Friday' na 'idea' ni ya Kiingereza ambayo hayajakopwa katika Sheng'. Ufuatao ni mfano mwingine unaodhihirisha mchakato wa utatu-msimbo.

100. Risto ya bodo at first ilinibamba, lakini saa hii nachora vile naeza nikajikata
Hadithi ya (shule ya) bweni mara ya kwanza ilinifurahisha, lakini sasa hivi ninapanga vile ninaweza nikajiondoa.

Sentensi hii (100) ina maneno yenye maumbo ya misimbo mitatu ambayo ni Sheng', Kiingereza na Kiswahili. Kimsingi msimbo mmoja kama Kiswahili au Kiingereza ungeweza kutumiwa ili kupitisha maana. Walakini, uteuzi wa mzungumzaji wa msamiati wa lugha misimbo mitatu na kuunganisha ili kuwasilisha maana umerejelewa kama utatu-msimbo katika tasnifu hii kwa sababu ingawa Sheng' si lugha, launi hizi zote (Kiswahili, Sheng' na Kiingereza) ni misimbo.

### 4.2 Uchanganuzi wa Tungo Zenye Sheng' kwa Vigezo Vya 4M

Sehemu 4.2.1 hadi 4.3.2 za sura hii zinachanganua data ya utafiti mintarafu ya lengo la nne la utafiti huu. Uambajengo wa elementi za LS na LC unaangaziwa katika sehemu 4.2.1 huku mkuku wa kimofosintaksia unaozingatiwa katika ujenzi wa tungo zenye Sheng' ukichanganuliwa katika sehemu 4.3 na vijisehemu vyake 4.3.1 na 4.3.2.

#### 4.2.1 Mchango wa LS na LC kwa Miundo Yenye UM

Uchanganuzi wa tungo zenye Sheng' unaofanywa katika sehemu zifuatazo za sura hii kwa kuongozwa na nadharia ya 4M unaonyesha kwamba baadhi ya tungo zinaundwa kwa kuviunganisha viambajengo vya LS na LC. Tungo zingine zinadhihirisha kwamba vizingwa vya LS na LC vinaweza kushiriki katika uzalishaji wa sentensi. Mkuku wa kimofosintaksia na kanuni zinazofuatwa zimeweza kuchanganuliwa pia katika sehemu zingine za sura hii.

#### 4.2.1.1 Mseto wa Viambajengo vya LS na LC

Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa baadhi ya miundo yenye UM iliyoshirikisha Sheng' ilidhihirisha miundo iliyoundwa kwa kuunganisha viambajengo vya LS na LC. Utafiti huu umegundua kuwa aina za mofimu zinazohusika katika miundo ya aina hiyo hutofautiana kutoka muundo mmoja hadi mwingine. Data inaashiria kwamba mofimu hizo, kwa sababu ni za aina mbalimbali, zinazansuliwa katika viwango tofauti katika lemma kama inavyofafanuliwa na nadharia ya 4M. Usemi ufuatao ambao umerudiwa hapa kama mfano (101) ulinukuliwa kutoka kwa watafitiwa na unadhihirisha mseto huo wa viambajengo:

101. Depoo wetu ni mnew. Mamode wetu wawili wa fik wamekuwa majatelo wameenda chuo zingine kuwa maprinci.
Naibu wa mwalimu wetu mkuu ni mpya. Walimu wetu wawili wa (somo la) Fisikia wamekuwa watu wa hadhi, wameenda shule zingine kuwa walimu wakuu.

Maumbo '*Depoo, fik* na *maprinci'* ni maneno ambayo yametoholewa kuwa ya Sheng', kutoka Kiingereza. Maneno mengine kama 'wetu, ni, wawili, wameenda, zingine na kuwa' ni ya Kiswahili. Hivyo basi, mfano (101) unadhihirisha vile mseto wa viambajengo vya LS (Kiswahili) na LC (Sheng') vinavyoweza kushirikiana katika ujenzi wa miundo yenye UM. Kwa kutegemea mwongozo wa nadharia ya 4M, inabainika kuwa mofimu za kileksika kama vile '*Depoo, chuo, mamode, fik* na *princi'* huwa zimezanzuliwa awali kuliko viambishi kama 'ma' katika '*maprinci'* au 'wa' na 'me' katika 'wamekuwa'. Hii inamaanisha kwamba maneno hayo huwa hayajaongezwa viambishi vya wingi katiki akili kabla ya kutumiwa katika sentensi. Inajitokeza pia kwamba kiambishi 'm' kinaunganishwa kwa kivumishi kama vile 'new' kama kipatanishi cha kisarufi wakati wa kuunda sentensi kwa kutegemea sifa za nomino patanishi. Kutokana na mfano huu, utafiti huu unagundua kuwa akili za watu zinaweza

kuwa na misamiati ambayo tayari imezansuliwa ikingojea kutumiwa tu kuzalisha usemi.

#### 4.2.1.2 Vizingwa vya Lugha Solo katika Miundo yenye UM

Data iliyokusanywa kutoka kwa watafitiwa wa utafiti huu imeonyesha kuwa baadhi ya miundo yenye UM iliyoshirikisha Sheng' ilidhihirisha sentensi au vishazi vilivyoundwa kwa viambajengo vya lugha solo pekee. Data imebainisha kuwa miundo ya aina hiyo inafuata kanuni za kisarufi za lugha solo.

Ufuatao ni mfano wa usemi wenye UM baina ya Sheng' na Kiswahili ulionukuliwa kutoka kwa watafitiwa ambao unadhihirisha vizingwa vya lugha solo:

102. M11: Niaje jo!
Vipi rafiki.
M12: Down down maze, nililoba odijo akaniwahi vinoma. Sijui nitafanyaje.
Vibaya, vibaya mwenzangu, nilifeli mwalimu akaniadhibu vibaya. Sijui nitafanyaje ili nipite.

Lugha solo katika mfano (102) ni Sheng' kwa maana ni lugha iliyotawala mazungumzo kati ya watafitiwa M11 na M12 na ilichangia mofimu amilifu na za kileksika katika muundo. Sehemu mbili zilizopigwa mistari katika diskosi hii "*Niaje jo*" na "*Down, down maze, nililoba odijo akaniwahi vinoma*" ni mfano wa kizingwa cha LS ambayo ni Sheng' katika muktadha huu. Sehemu ya mwisho wa usemi huu 'Sijui nitafanyaje' iliendelezwa kwa Kiswahili pekee. Tasnifu hii inachanganua sehemu hiyo ya mwisho kama kizingwa cha LC kwa maana Sheng' imetawala mazungumzo hayo.

Mfano ufuatao nao unaonyesha namna Kiswahili kinajitokeza pia kama lugha solo katika mazungumzo yenye Sheng:

103. M4: Mlifikaje shuleni?
M5: Vyema kabisa. Na wewe ulifika poa?
Vyema kabisa. Na wewe ulifika salama?

Kiswahili kinajitokeza kama lugha solo katika mfano (103) ambao ni usemi baina ya watafitiwa M4 na M5. Hii ni kwa sababu sentensi za watafitiwa wote wawili zinazingatia mofosintaksia ya Kiswahili isipokuwa umbo moja tu la kileksika '*poa'*, la Sheng' ambalo limechopekwa. Uchopekaji huo wa msamiati wa Sheng' unathibitisha dai la nadharia ya 4M kwamba mofimu amilifu hutokana na lugha solo na mofimu ya kileksika kama '*poa'* huweza kuchopekwa kwa kuzingatia paradimu za lugha inayotawala mpangilio, ambayo ni Kiswahili katika mfano (103).

### 4.2.1.3 Vizingwa vya LC katika Miundo yenye UM

Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kuwa katika UM unaofanyika baina ya Sheng' na Kiswahili kuna vizingwa vya Sheng' pekee. Hii inamaanisha kuwa kuna miundo inayojitokeza katika mazungumzo yenye ubadilishaji msimbo inayoundwa kwa viambajengo vya Sheng pekee ndani ya diskosi ambayo kimsingi imeendelezwa kwa Kiswahili kama ilivyofafanuliwa na nadharia ya 4M. Miundo hiyo ina msamiati wa Sheng pekee na huzingatia ruwaza za kimofosintaksia zinazohusu Sheng'. Mfano (104) ulinukuliwa kutokana na mazungumzo yaliyofanyika baina ya watafitiwa wawili katika mtaa wa Kondele. Mfano wenyewe unadhihirisha mchango wa kizingwa cha LC katika miundo yenye UM baina ya Sheng' na Kiswahili:

104. Alifika juzi saa tatu usiku akapigiwa kelele na akaulizwa kwa nini alichelewa na hali alikuwa ameondoka mapema. Manzee chali alifreeze. Hivo amekataa kuchukua simu yangu.

Sehemu ya kwanza ya mfano (104) [Alifika juzi saa tatu usiku akapigiwa kelele na akaulizwa kwa nini alichelewa na hali alikuwa ameondoka mapema] imeendelezwa kwa Kiswahili. Sehemu ya kati ambayo imepigwa mstari [*Manzee chali alifreeze*] ni mfano wa kizingwa cha LC kwa vile imeendelezwa kwa Sheng pekee. Sehemu ya mwisho pia imejengwa kwa kutumia msamiati wa Kiswahili na kwa kuzingatia sintaksia ya Kiswahili. Mfano huu unadhihirisha dai la nadharia ya 4M kwamba viambajengo vya lugha solo na vizingwa vya LC huweza kuunganishwa katika ujenzi wa miundo yenye UM.

## 4.3 Mkuku wa Kimofosintaksia Unaozingatiwa

Kwa mujibu wa nadharia iliyoongoza utafiti huu, mkuku wa kimofosintaksia wa LS hufuatwa katika uzalishaji wa miundo yenye vipashio vya LS + LC. Baadhi ya miundo iliyozalishwa na watafitiwa iliyoshirikisha UM baina ya Sheng' na Kiswahili imedhihirisha kwamba mkuku utakaokaliwa na viambajengo vya lugha moja unaweza kuteuliwa na mzungumzaji na kuziingiza mofimu. Utafiti huu uligundua kuwa kanuni huhusika katika uamuzi na ujenzi wa mkuku wa kimofosintaksia uliozingatiwa katika uzalishaji wa miundo iliyohusisha UM baina ya Sheng' na Kiswahili. Kanuni mbili ambazo ni kanuni ya mfuatano wa mofimu na kanuni ya mofimu amilifu zilizofafanuliwa na Myers-Scotton katika nadharia yake huzingatiwa kama inavyoelezewa katika sehemu 4.3.3.1 na 4.3.3.2 zifuatazo:

### 4.3.1 Kanuni ya Mfuatano wa Mofimu

Dai la nadharia ya 4M kuhusu kanuni ya mfuatano wa mofimu ni kwamba katika miundo yenye leksimu mojamoja za lugha changizi zilizochopekwa, mpangilio wa mofimu utakaozingatiwa ni ule wa LS. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa

kuna baadhi ya miundo yenye U.M. inayoshirikisha Kiswahili na Sheng' inayokiuka kanuni hii lakini mingine inazingatia. Kwa mfano:

105. Nimeshamada na naishia Nai moro.
Nimemaliza na ninaenda Nairobi kesho.

Muundo (105) ni mfano wa sentensi iliyozalishwa na watafitiwa yenye viambajengo vya Sheng' ambavyo vimeunganishwa na viambajengo vingine ili kujenga sentensi ambatano inayozingatia mfuatano wa mofimu wa Kiswahili. Hii ni kwa vile, mintarafu ya kanuni za Kiswahili, mofimu za nafsi na za njeo au hali hutangulia mzizi wa kitenzi kama 'ni', 'me' na 'sha' katika 'ni-me-sha-*mada'* pamoja na 'na' katika 'na-*ishia*.'

Aidha, mpangilio wa mofu katika kishazi cha pili cha sentensi hii '*naishia Nai moro*' unafuata utaratibu wa Kiswahili. Hii ni kwa vile mofu ambayo ingekuwa 'ni' na 'na' zimedondoshwa na zikawakilishwa kwa kiambishi kimoja 'na'. Kiwakilishi hiki kinatumiwa badala ya nomino katika sentensi hii. Kwenye kirai kitenzi (*ninaishia Nai moro*), kitenzi kimefuatwa na vielezi viwili.

Kielezi cha pili '*moro'*, ambacho ni cha Sheng', kinatoa maelezo zaidi kuhusu wakati wa kuenda lakini kile cha pili '*Nai'* ambacho pia ni cha Sheng' kinaeleza kuhusu mahali pa kwenda. Mkuku wa kimofosintaksia wa Kiswahili uliotawala uundaji wa sentensi, kama inavyofafanuliwa na nadharia ya 4M, unaruhusu mpangilio huo wa vijenzi kuanzia nomino au kiwakilishi, kitenzi na vielezi mtawalia. Mfano ufuatao unadhihirisha hali ilivyo kuhusiana na matumizi ya kitenzi kishirikishi katika sentensi zenye ubadilishaji msimbo baina ya Sheng' na Kiswahili:

106. Fansii ni msupuu.
Fancy ni mrembo.

Kanuni ya mfuatano wa mofimu inayohusu matumizi ya kitenzi kishirikishi katika sentensi za Kiswahili huhitaji kitenzi cha aina hiyo kifuatwe na nomino au kivumishi pekee. Mfano (106) unaonyesha kwamba kivumishi cha Sheng' '*msupuu'* kinaweza kujaliza kitenzi kishirikishi 'ni'. Vitenzi vya aina nyinginezo haviwezi kufuatwa moja kwa moja na kivumishi. Hiki ni kiashiria kwamba mfuatano wa mofimu unaozingatiwa ni ule unaodokezwa na nadharia ya 4M wa lugha solo katika muktadha huu. Mfano ufuatao unaonyesha kuzingatiwa kwa kanuni inayohusiana na kitenzi kisoelekezi:

107. (a) Mimi niko ocha. Nimesota vinoma.
Mimi niko nyumbani. Nimeishiwa vibaya.

(b) *Mimi niko ocha. Nimesota nyumba.

Uchanganuzi wa (107) unaashiria kwamba, kinyume na inavyodaiwa na nadharia ya 4M kwamba katika miundo yenye leksimu mojamoja za lugha changizi zilizochopekwa, mpangilio wa mofimu utakaozingatiwa ni ule wa LS, mpangilio wa mofimu huamuliwa na aina ya kitenzi kitakachoteuliwa (Sawe, 2015). Mathalani, kule kuteuliwa kwa kitenzi kisoelekezi '*nimesota'* (nimeishiwa) kungemruhusu mzungumzaji akiunganishe na kielezi tu. Jaribio la kushirikisha nomino, ambalo linadhihirisha utoshelevu wa nadharia ya 4M, lingesababisha kuundwa kwa muundo usiokubalika na usiobeba maana kama 107(b). Hali hii ni dhahiri pia katika matumizi ya vitenzi vielekezi mosi kama inavyojitokeza katika mfano (108) ufuatao:

108. (a) Roy amekinda tenje.
Roy ameuza redio.

(b) *Roy amekinda.

Kule kutumiwa kwa kitenzi cha Sheng' '*amekinda'* katika mfano 108 (a) hapo juu kunaonyesha kuwa ni lazima nomino moja ishirikishwe katika nafasi ya yambwa ilmuradi kitenzi kielekezi mosi kitatumiwa katika muundo. Kanuni hii inayomlazimu

mzungumzaji ashirikishe nomino moja baada ya kitenzi hutawala uamuzi wake kuhusu aina ya neno litakalokalia nafasi katika muundo wa sentensi. Mfano 108 (b) unaonyesha kuwa muundo usiokuwa sahihi unaweza kuzalishwa kwa sababu ya kutoshirikishwa kwa nomino kwenye nafasi ya yambwa iwapo kitenzi kilichoteuliwa ni kielekezi mosi. Mfano (109) unahusu kanuni zinazotawala sentensi za kiwingi-lugha zenye kitenzi kielekezi maradufu.

109 (a) Chali amemnunulia kenge ndula.
Kijana amemnunulia kipusa chake viatu.

(b) *Chali amenunulia.
Kijana amenunulia.

Data iliyonukuliwa kutoka kwa watafitiwa wa utafiti huu kama mfano 109 (a) pia imeonyesha kuwa kutumiwa kwa kitenzi kielekezi maradufu kama 'nunulia' huathiri ruwaza za mofimu katika sentensi. Hii inamaanisha kuwa namna ambavyo nomino mbili '*kenge'* na '*ndula'* zinafuata kitenzi katika mfano 109 (a) haujakuwa wa kisadfa au wa kinasibu ila unafungamana na kule kutumiwa kwa kitenzi kielekezi kinachomshurutisha msemaji ashirikishe nomino mbili.

Mfano 109 (b) hasa unaonyesha kuwa kanuni inayohusika haiwezi kukiukwa kwani kukiukwa kwake kutasababisha kuzalishwa kwa muundo usiokuwa na maana. Tokeo hili la utafiti huu vilevile linaashiria kwamba kanuni ya mfuatano wa mofimu inayopendekezwa na nadharia ya 4M inafaa kwa ufafanuzi wa miundo ya Sheng' yenye UM. Hata hivyo, kanuni hiyo ina udhaifu wa kutoipa nafasi kanuni inayohusu uteuzi madhubuti wa vijenzi unaohusiana na matumizi ya vitenzi vielekezi au visoelekezi.

### 4.3.2 Kanuni ya Mofimu Amilifu

Data iliyokusanywa katika utafiti huu imeonyesha kwamba aghalabu Kiswahili huzalisha mofimu amilifu katika sentensi zenye UM baina yake na Sheng'. Mofimu amilifu zinazozalishwa na Kiswahili ni pamoja na viambishi vya nafsi, viambishi vya njeo na hali, viambishi vya masharti, viambishi vya O-rejeshi na vya mnyambuliko wa kitenzi. Uchunguzi huu umebainisha kwamba Sheng' haina mofimu amilifu za aina hizi ila hutumia zile za Kiswahili. Hata hivyo, baadhi ya mofimu amilifu kama '*ma*-' ya kubainisha wingi na '*-nga'* ya kubainisha hali ya mazoea huzalishwa na Sheng'. Utafiti huu umegundua vile vile kwamba mara nyingi Kiswahili inajitokeza kama lugha solo katika miundo yenye UM baina yake na Sheng'. Hii ni kwa vile Sheng' haina mofimu amilifu nyingine mithili ya viunganishi na vihusishi na kwa misingi hiyo hutumia zile za Kiswahili.

Kwa ujumla, mofimu amilifu nyingi zilizotumiwa katika diskosi za watafitiwa ni za Kiswahili. Ufafanuzi wa awali wa nadharia ya lugha solo ungebainisha Sheng' kwa misingi hiyo kama LC (Myers-Scotton, 1993a na b; Nishimura, 1997). Hata hivyo, upanuzi uliofanywa na Myers-Scotton na Jake (2002) kuhusu dhana ya mofimu amilifu unabainisha Sheng' katika baadhi ya miundo kama LS. Hii ni kwa vile Sheng' hutumia kiambishi kipatanishi '*zi*-' ambayo ni mofimu amilifu hata kama nomino ni hisivu kama inavyojitokeza katika sentensi ifuatayo ambayo imerudiwa kama mfano (110):

110. Alitumia doo kununua mambuzi. Hizo mambuzi zimezaana.
Alitumia pesa kununua mbuzi (wengi). Mbuzi hao wamezaana.

Lugha solo katika mfano (110) kwa mujibu wa modeli ya 4M ni Sheng' kwa vile imechangia mofimu amilifu za upatanisho wa kisarufi zilizopigwa mistari. Kiswahili ingekuwa lugha solo, kiambishi cha upatanisho wa kisarufi kinachowakilisha neno

'mbuzi' hakingekuwa '*zi'* kama ilivyo katika maneno '*hizo*' na '*zimezaana'*. Kiambishi ambacho kingetumiwa kwa fahiwa hiyo kingekuwa 'wa'. Ufuatao ni mfano mwingine (111) wa muundo wa Sheng' unaochukua mwelekeo sawa na ule wa mfano (110):

111. Vitabu zangu zililetwa na hasii wa Flo.
Vitabu vyangu vililetwa na mume wa Florence.

Mofimu ya upatanisho wa kisarufi ya Sheng' iliyotumiwa katika mfano (111) ni '*zi*-' kama inavyojitokeza katika sehemu zilizopigwa mstari. Uchanganuzi huu unafafanua kwamba mofimu ya upatanisho wa kisarufi iliyotumiwa ni ya Sheng' kwa maana ingekuwa ya Kiswahili kiambishi cha ngeli ya 7 'ki' kingetumika kwenye kivumishi (kama changu) na kitenzi (kama kililetwa) badala ya kiambishi cha ngeli ya 10 'zi' jinsi ilivyo kwa maneno '*zangu'* na '*zililetwa*.'

**4.4 Hitimisho**

Sura hii imefanya uchanganuzi wa data kulingana na lengo la tatu na la nne. Mikakati mbalimbali ya kiwingi-lugha inayohusika katika ujenzi wa tungo zenye Sheng' imeangaziwa katika sehemu ya kwanza. Baadhi ya mikakati iliyowasilishwa ni pamoja na uchanganyaji msimbo, wingishaji-maradufu, ushabihiano na utatu-msimbo. Imebainika kwamba mikakati hii huhusika ili kufanikisha uwasilishaji wa maana katika diskosi zinazoshirikisha Sheng'. Uchanganuzi wa tungo zenye Sheng' umefanywa katika sehemu ya pili ya sura hii ambao mkuku wa kimofosintaksia unaozingatiwa umefafanuliwa. Kanuni zinazohusika katika uzalishaji wa miundo ya kiwingi-lugha yenye Sheng' pia zimeelezewa kwa kutumia data ya utafiti. Imedhihirika kwamba mkuku unaofuatwa na mofimu katika ujenzi wa miundo ya Sheng' na mofimu zinazoshiriki si bainifu. Katika sura ifuatayo ya tano, tutahitimisha tasnifu yetu.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Sehemu 5.1 ya sura hii inaeleza yale yaliyogunduliwa kulingana na malengo ya utafiti huu. Katika sehemu hii tutaelezea matokeo ya utafiti huu. Sehemu 5.2 inafafanua mahitimisho ya mtafiti kuhusiana na mada ya utafiti. Sehemu ya mwisho (5.3) inatoa mapendekezo ya utafiti na ya kinadharia kuhusiana na malengo na matokeo ya utafiti huu.

## 5.1 Matokeo ya Utafiti

### 5.1.1 Matokeo kulingana na lengo la kwanza la utafiti

Mintarafu ya lengo la kwanza la utafiti huu, ambalo lilikuwa kubainisha na kufafanua mbinu za uleksikalishaji zinazotumiwa katika Sheng' kwa kuzingatia vigezo vya Pegitosca, mbinu kumi na sita za uleksikalishaji zinazotumiwa ili kuunda msamiati wa Sheng' zilibainika. Mbinu zenyewe zilihakikiwa kwa kuzingatia nguzo za nadharia ya Pegitosca ambapo ilibainika kwamba karibu kila neno la Sheng' linazingatia baadhi tu ya nguzo za nadharia hiyo.

Iligunduliwa pia katika utafiti huu kwamba matumizi ya mnyambuliko kama mbinu ya kuunda msamiati wa Sheng' hutegemea dhana inayolengwa kupewa jina. Namna ambavyo mnyambuliko utafanywa katika msimbo wenyewe hudhibitiwa na maana inayolengwa kuwasilishwa. Tokeo hili linadhihirisha kuwa mnyambuliko haufanywi kinasibu. Uchunguzi wa mnyambuliko vilevile umeonyesha kwamba ingawa viambishi vya kukopwa mfano wa 'ma' hutumiwa katika uleksikalishaji, viambishi hivyo hupoteza sifa asilia za kiisimu katika Sheng'. Kutumiwa kwa mofu 'ma' katika Sheng'

kwa ajili ya kubainisha hali ya wingi, hakuhusiani moja kwa moja na 'ma' ya Kiswahili ambayo ilisheheni dhana za wingi, ukubwa usiokuwa wa kawaida, matunda na mengineyo.

Ilibainika kuwa mofu '*-nga'* au alomofu yake '*-ngi'* hutumika kama kiambishi tamati katika Sheng' ili kudokeza hali ya mazoea kuhusiana na kitendo. Iligunduliwa kuwa kiambishi hiki hutumiwa mwishoni mwa kitenzi. Utafiti huu uligundua pia kwamba kutumiwa kwa '*-nga'* au '*-ngi'* hutegemea tangamano la irabu. Kwa sababu ya kanuni zinazohusu tangamano, watafitiwa hawakukubali matumizi ya maumbo '*filinga'* badala ya '*filingi'* au '*kiringa'* badala ya '*kiringi'* kama maneno ya Sheng'.

Matokeo ya uchunguzi huu yameonyesha kuwa kuna sura mbalimbali za uradidi unaotumiwa kama mbinu ya uleksikalishaji katika Sheng'. Data ilidhihirisha uradidi wa neno zima au wa silabi za neno. Uchambuzi wa data ulionyesha kwamba matumizi ya mbinu hii yanazingatia vigezo vya Pegitosca ambavyo ni utusani, iktisadi na utaratibu. Maneno ya Sheng' yanayoundwa kupitia uradidi wa silabi hayaundwi kwa kutumia fonimu nyingi kupita kiasi isipokuwa hayawezi kunyambuliwanyambuliwa zaidi ili kuunda maneno mapya ya Sheng'.

Ilijitokeza vilevile kwamba baadhi ya maneno ya Sheng' hutumiwa zaidi katika baadhi ya miktadha lakini hayatumiki katika miktadha mingine. Mtafiti aligundua kupitia usaili wa watafitiwa kwamba baadhi ya maneno ya Sheng' yalikuwa yakijulikana kwa wanafunzi pekee ilihali mengine yalikuwa yakijulikana kwa watumiaji wa Sheng' walioishi mitaani. Tokeo hili linaashiria kuwepo kwa launi za Sheng' zinazofungamana na maeneo ya matumizi.

Kutokana na uchanganuzi wa data, mtafiti aligundua kuwa udondoshaji wa ama mofimu au silabi hutumiwa kama mbinu ya uleksikalishaji katika Sheng'. Matokeo yenyewe yalionyesha kuwa mbinu ya udondoshaji ni tofauti na mbinu ya ufupishaji kwa vile udondoshaji huondoa sehemu ya neno kama silabi moja ili kupata neno jipya la Sheng' lenye maana ile ile. Namna ambavyo mbinu ya udondoshaji wa silabi inaweza kutumika katika uundaji wa msamiati wa Kiswahili haijaweza kudhihirishwa katika maandishi.

Ufinyaji wa maana ni mbinu ya uleksikalishaji ambayo inahusu kuchukuliwa kwa umbo lililokuwa na maana pana katika lugha chanzi na kulipea maana finyu. Neno jumuishi kwa misingi hiyo linaweza kupewa maana inayohusu kirejelewa kimoja au sehemu ndogo badala ya kitu kamili katika Sheng. Hii inamaanisha kuwa ufinyaji wa maana si ukopaji kwa sababu fahiwa ya umbo hubadilika.

Data imeonyesha kuwa majina yenye silabi nyingi aghalabu yanafupishwa wakati wa uleksikalishaji wa Sheng' ili kuibua maumbo yenye silabi chache. Matokeo ya usaili katika utafiti huu yamebainisha kuwa ufupishaji unaofanywa katika Sheng' hulenga kurahisisha utamkaji (mazungumzo). Hii ni kwa vile silabi nyingi(ne) zinaondolewa katika neno. Pili, matokeo yaliashiria kwamba haja ya kufanya mazungumzo yavutie yanaweza kuwa motisha moja inayowasababisha wazungumzaji wafanye ufupishaji mwingi katika Sheng'.

Matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa mbinu ya uleksikalishaji inayojulikana kama akronimia hutumiwa kwa nadra sana katika Sheng'. Mintarafu ya maneno ya Sheng' yaliyochanganuliwa, imetokea kuwa mbinu hii ilitumiwa ili kuunda maneno machache tu. Matokeo hayo yanadhihirisha kuwa mofimu amilifu huwa hazishirikishwi katika mfanyiko wa kuunda maneno kiakronimia katika Sheng'. Uteuzi wa silabi za

kushirikishwa ili kujenga akronimu hufanywa kutoka mofimu za kileksika na hutegemea miundo ya silabi za Sheng'.

Mtafiti aligundua pia kuwa baadhi ya msamiati wa Sheng' huundwa kuzingatia mbinu ya urefushaji wa umbo ambayo haikuwa imebainishwa na wachunguzi wa uleksikalishaji wa Sheng'. Mifano iliyochanganuliwa katika tasnifu hii inadhihirisha maneno mapya yenye herufi au fonimu nyingi kuliko maneno yaliyotumiwa ili kuyaunda. Kwa fahiwa hiyo, neno lenye silabi moja linaweza kutumiwa ili kuunda neno jipya lenye silabi mbili au zaidi katika Sheng'.

Mbinu nyingine ya uleksikalishaji inayotumiwa katika Sheng' iliyogunduliwa katika utafiti huu ambayo haikuwa imebainishwa katika tafiti zilizotangulia ni ile ya uundaji wa kiantonimia. Ili kuzalisha neno kwa kutumia mbinu hii, umbo huchukuliwa kutoka lugha chasili na kupewa maana nyingine ambayo ni kinyume cha maana yake asili. Hii inamaanisha kwamba neno la lugha nyingine linaingizwa kwenye msamiati wa Sheng' kisha mbinu ya unyume inatumiwa ili kulipa maana.

Uchanganuzi wa data pia umedhihirisha kwamba onomatopia ni mbinu nyingine ya uleksikalishaji inayotumiwa katika upanuzi wa msamiati wa Sheng'. Ilijitokeza kwamba wazungumzaji wa Sheng' hawaitumii sana mbinu hii ikilinganishwa na mbinu nyinginezo za uleksikalishaji. Ilitokea kuwa maneno yanayoundwa kionomatopia katika Sheng' yanaundwa kwa kuiga tabia au sifa za virejelewa au uhusishaji. Utafiti huu uligundua hatimaye kuwa maneno yanayoundwa kwa kuzingatia mbinu hii ya uleksikalishaji hayawezi kunyambuliwanyambuliwa ili kuyazalisha maneno mengine ya Sheng'.

Ilibainika pia kuwa usarufishaji ni mbinu nyingine ya uleksikalishaji inayotumiwa katika Sheng'. Usarufishaji huwezekana kupitia uteuzi na uunganishwaji wa maumbo mawili au zaidi ya Sheng' ili kuwakilisha dhana moja. Mbinu hiyo ya usarufishaji haikubainishwa na watafitiwa wengine waliotangulia katika uchunguzi wa mbinu za uleksikalishaji katika Sheng'. Kutokana na jaribio lake la kuyatenganisha baadhi ya maneno yaliyotokana na usarufishaji, mtafiti aligundua kwamba maneno yaliyounganishwa kupitia usarufishaji yakitenganishwa hayataweza kubeba dhana ile iliyobebwa na maumbo yaliyounganishwa. Ilijitokeza pia kuwa mbinu ya usarufishaji ikitumika katika uleksikalishaji, maana inayozalishwa haihusiani moja kwa moja na maana za maumbo yaliyounganishwa. Hata hivyo, data ilionyesha kuwa leksimu za Sheng' zilizoundwa kupitia usarufishaji haziwezi kunyambuliwanyambuliwa kwa ajili ya kuzalisha maneno mapya.

Kwa mujibu wa data iliyokusanywa katika utafiti huu, ilibainika kuwa ukopaji ni mbinu inayotumiwa katika uleksikalishaji wa Sheng'. Kuna ukopaji unaoambatana na utohozi, ukopaji usioambatana na utohozi na hatimaye ukopaji unaoambatana na usilabifishaji-upya katika uundaji wa maneno ya Sheng'. Tafiti za awali kama vile zile za Mazrui (1995) na Githiora (2002) hazikuwa zimedhihirisha ukopaji unaoambatana na usilabifishaji katika Sheng'.

Ukopaji mwingi huweza kuchangia kile kinachorejelewa na wanaisimu kama uchafuzi wa launi ya lugha. Hata hivyo, matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwa ukopaji wa moja kwa moja usioshirikisha utohozi ni mbinu nyingine ya uleksikalishaji inayotumiwa ili kuyaunda maneno mapya ya Sheng'. Usaili wa watafitiwa ulibainisha baadhi ya maneno ya Dholuo, Kikamba, Kikikuyu na Kimaasai ambayo yameweza kukopwa na kuchukuliwa na wazungumzaji wa Sheng' kama msamiati wa msimbo huo.

Mtafiti aligundua kuwa maumbo hayo yaliyokopwa hadi Sheng' pasipo kutoholewa, hudumisha maana zao jinsi yalivyokuwa katika lugha chasili. Ilibainika kwamba katika upanuzi wa msamiati unaotegemea mbinu hii, neno linadumisha fonimu na hata silabi zilizoshiriki kulijenga katika lugha chasili na huanza kuzoeleka na hatimaye kuchukuliwa kuwa la kawaida katika Sheng'.

Uchunguzi huu ulithibitisha kwamba uundaji wa kinasibu ni mbinu nyingine ya uleksikalishaji inayotumiwa kupanua msamiati wa Sheng'. Hii inamaanisha kwamba baadhi ya maneno ya Sheng' huundwa pasipo kuigiza milio au tabia za virejelewa wala kukopwa kutoka lugha zingine.

Matokeo ya uchunguzi huu kuhusu mwambatano kama mbinu ya uleksikalishaji wa Sheng' yameashiria hali mbili muhimu. Kwanza, imedhihirika kwamba aghalabu maneno mawilimawili huambatanishwa ili kuzalisha maneno mapya katika Sheng'. Hali ambapo maneno matatu au hata zaidi yangeambatanishwa ili kujenga neno moja jipya haikutukia katika utafiti huu. Pili, data ilidhihirisha upekee kuhusiana na matumizi ya mbinu ya mwambatano katika uleksikalishaji wa Sheng'. Hii ni kwa sababu, tofauti na ilivyo katika Kiswahili, vivumishi viwili huweza kuambatanishwa ili kuunda kielezi. Mofu mbili 'mbaya' na 'mbovu' ziliweza kuambatanishwa ili kuunda kielezi kimoja '*mbaya-mbovu'* chenye maana ya 'sana'. Hapana budi kwamba hii ni sifa nyingine inayobainisha upekee wa msimbo wa Sheng'.

Ujenzi ghairi ni mbinu nyingine ya uleksikalishaji iliyogunduliwa katika utafiti huu. Ingawa mbinu hii inatumiwa kupanua msamiati wa Sheng', watafiti waliochunguza uundaji wa msamiati katika Sheng' hawakuwa wamebainisha wala kuifafanua. Maneno kadhaa ya Sheng' yalidhihirisha kuundwa kupitia ujenzi ghairi kwa maana silabi za neno chasili zilipanguliwa kwa namna ambavyo angalau silabi mbili au zaidi

zingebadilishana nafasi katika mchakato wa kuunda neno jipya. Hii ni mbinu nyingine tena iliyogunduliwa katika utafiti huu ambayo ni ya kipekee katika Sheng' kwa vile haijawa ikitumika kuzalisha maneno ya lugha kama vile Kiswahili. Matokeo ya uchunguzi huu yameweka wazi uhalisia kwamba maneno yanayoundwa kupitia ujenzi ghairi hayawezi kunyambuliwanyambuliwa ili kuzalisha maneno mengine mapya. Hata hivyo, imekuwa bayana kwamba neno la Sheng' lililoundwa kwa kutumia ujenzi ghairi linaweza kosa umataifa, kunyambulikanyambulika au likakosa kutimiza sharti la utusani lakini wakati huo huo litimize sharti la ukubalifu miongoni mwa wasemaji wa Sheng'.

Ingawa upanuzi wa maana ni badiliko la kisemantiki linaloweza kutukia katika lugha, utafiti huu umeweza kufafanua kwa kutumia data namna ambavyo unatumika kama mbinu ya uleksikalishaji katika Sheng'. Iligunduliwa kuwa wazungumzaji wa Sheng' hulipa neno maana mpya hivi kwamba neno husika litakuwa na fahiwa zaidi ya zile za awali. Tokeo hili linaashiria hali ambapo neno jipya haliundwi ila lile ambalo tayari linatumika linapanuliwa kisemantiki ili kurejelea dhana nyingi. Hii inamaanisha kwamba hakutakuwa na neno jipya lakini msamiati wa lugha utakuwa umepitia ustawishwaji unaolengwa kugusa urejelezi wa dhana nyingi.

Iligunduliwa pia katika utafiti huu kuwa uhamishaji wa kimaana ni mbinu nyingine inayotumiwa katika uleksikalishaji wa Sheng'. Hii inamaanisha kuwa umbo lililokuwa na maana nyingine katika lugha linapewa maana iliyohusiana na umbo lingine. Uhamishaji wa maana haujitokezi kwa sababu umbo jipya limeundwa isipokuwa kwa sababu umbo lililokuwepo linahamishiwa maana mpya ambayo awali ilikuwa ya umbo tofauti. Mbinu hii ya uleksikalishaji haikuwa imegunduliwa na watafiti waliochunguza uundaji wa msamiati katika Sheng'.

Utafiti huu umegundua, mintarafu ya uchanganuzi uliofanywa hapo juu kuhusu uleksikalishaji, kwamba mbinu zaidi ya kumi hutumika katika uleksikalishaji wa Sheng'. Kutokana na uchanganuzi wenyewe, mbinu hizo zote zinazingatia vigezo mbalimbali vya Pegitosca. Hata hivyo, vigezo vingine vya Pegitosca kama vile umataifa na uzalishaji havitimizwi kwa vile leksimu nyingi zinazoundwa katika Sheng' hazinyambulikinyambuliki kwa ajili ya kupata leksimu mpya na hazihusiani na msamiati wa lugha za kimataifa. Ugunduzi huu unachangia kudhihirisha kuwa Sheng' ni msimu wala sio lugha. Hii ni kwa sababu msamiati wa msimbo wa Sheng' hautimizi usayansi unaolengwa na nadharia ya Pegitosca kikamilifu.

### 5.1.2 Matokeo Kulingana na Lengo la Pili la Utafiti

Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa kufafanua sifa zinazopinga upijini na ukriolishaji wa Sheng'. Kwa mujibu wa lengo hili, ithibati ya data iliyotokana na watafitiwa inapinga dai kwamba msimbo wa Sheng' unaweza kuainishwa kama Krioli. Ithibati hiyo inaweza kutegemewa kwa sababu msimbo huu uliweza kudhihirika kwa sura tatu. Kwanza ilitokea kwamba vipashio vingi vya kimofolojia vya Sheng' havijabainika. Tokeo la pili lilionyesha kuwa muundo wa kisintaksia wa Sheng' si bainifu, na hatimaye iligunduliwa kuwa sifa zake za kijamii zinapinga ukriolishaji wa Sheng' huku zikiikwamiza katika hadhi ya msimu.

Iligunduliwa kwamba wazungumzaji wa Sheng' wanaotoka maeneo tofautitofauti hutumia maneno tofauti kurejelea baadhi ya virejelewa. Ilibainika kuwa hali hiyo huathiri usarufishaji wa Sheng' katika kiwango cha mofolojia. Havipo vizuizi vinavyoweza kupinga uundaji wa maneno mengine hata kama tayari kuna mengine yanayobeba dhana sawa. Matokeo yaliashiria kwamba dhana moja inaweza kurejelewa kwa maneno mengi kisinkronia. Isitoshe, maneno yanayoundwa hutumiwa kwa vipindi

vifupi tu kisha vibadala vingine vinaundwa tena. Hii ni sifa mojawapo inayopinga upijini na ukriolishaji wa Sheng'.

Idadi na hata mawanda ya matumizi ya maneno huhitajika kuimarika ndiposa Pijini ifuzu kuwa Krioli. Iligunduliwa katika utafiti huu kwamba maneno mengi ya Sheng' yanahusu sajili ya mazungumzo ya sokoni zaidi. Hali hii inapinga ukuaji wa launi hii kwa sababu mawanda ya matumizi hayapanuliwi ili kukidhi mahitaji yote ya lugha kama ilivyo katika lugha nyinginezo za kawaida. Watumiaji wa msimbo huu wangeunda maneno yanayohusiana na sajili za hospitalini, mahakamani, kilimo, dini na nyingine nyingi, Sheng' ingeingia kwenye mkondo wa upijinishaji.

Matokeo ya usaili yaliashiria kuwa Sheng' kama msimu hauwezi kusanifishwa, haiwezi kufanywa kuwa launi rasmi ila huweza kutumika katika miktadha rasmi kama launi isiyotarajiwa – launi zingine hutarajiwa kutumika katika miktadha hiyo. Uchanganuzi wa matumizi yake umedhihirisha kwamba Sheng' ni msimbo finyu ambao, tofauti na Pijini, huweza kuibuka kwa ajili ya kutimiza haja za kimawasiliano hata katika miktadha yenye lingua franka kama vile Kiswahili.

Pijini kwa madai ya De Camp (1971) haidhihirishi sifa za uhusika wa kisarufi mithili ya jinsia na idadi. Matokeo ya utafiti huu yameashiria kwamba Sheng' inakiuka sifa hiyo ya upijini kwa sababu imekuwa ikitumia viambishi vya kubainisha idadi (umoja na wingi) ambavyo ni vibainishi vya uhusika wa kisarufi.

Nadharia tete inayofafanuliwa na McMahon (1994) inahusisha asili ya Pijini na hali kadhalika Krioli na usemaji wa mtoto anayejifunza lugha (*baby talk hypothesis*) inalinganisha Pijini na usemaji wa mtu anayejifunza lugha ya kigeni. Inalinganisha tena uzungumzaji wa Pijini na uzungumzaji wenye ufilisi wa watu waliojifunza lugha ya pili. Matokeo ya utafiti huu yanapinga upijini au ukrioli wa Sheng' kwa fahiwa hii pia.

Hii ni kwa maana Sheng’ si zao la utamkaji mbaya, uundaji mbovu wa sentensi uliofanywa na watu waliokuwa wakijifunza Kiswahili. Badala yake, utafiti huu umegundua kuwa wazungumzaji waliolenga kuwabagua wengine kimawasiliano au kujitambulisha na makundi maalum waliunda msimbo wa Sheng’ kama msimu kutokana na launi ya kawaida ambayo ni Kiswahili

Iligunduliwa pia kuwa maneno mengi sana ya Sheng’ yana visawe. Neno moja linaweza kuwa na kisawe kimoja au hata visawe kumi. Utafiti huu umegundua kuwa kuwepo kwa hali hii inaashiria mambo kadha wa kadha kuhusiana na msimbo wa Sheng’. Kwanza, inaashiria kukua kwa msimbo wenyewe kwa maana msamiati wake unaongezeka. Pili, inaashiria kutukia kwa mabadiliko ya kisemantiki yanayohusiana na upolisemia kwa vile maneno mengi yanaanza kutumiwa kuashiria kirejelewa kimoja kimoja. Tatu, inaashiria ubunifu wa wazungumzaji wa Sheng’ ambapo wanaweza kugeuzageuza sura za maumbo ili kuzalisha maumbo mapya yenye maana kama vile *nare* au *nari* (kiberiti) na *doo, nadu* au *niado* (pesa). Nne, inaonyesha kuwa hamna maumbo sanifu katika Sheng’ na kwa hivyo hakuna yule anayeweza kupinga au kuidhinisha kutumiwa au kutotumiwa kwa umbo la asili au umbo jipya kama *manzi, manyake, manyaks* au *chiko.* Tano, kuwepo kwa sinonimu zisizofanana kimuundo kama *sonyi, ponyi, pai, karao,* na *wahia* kunaonyesha uwezekano wa kuwepo kwa launi za kimaeneo za Sheng’. Sita, kubadilikabadilika kwenyewe kwa maneno yanayotumiwa kurejelea dhana moja yanaashiria kwamba Sheng’ haiwezi kufikia kiwango cha uthabiti ambapo wanajumuiya msimbo wote watakuwa wanajua neno fulani linatumika kwa maana maalum wakati wote. Kizuizi hiki cha uthabiti katika uleksikalishaji ni kipingamizi kikuu kinachozuia Sheng’ ili kisiweze kudhihirisha sifa za Krioli.

### 5.1.3 Matokeo Kulingana na Lengo la Tatu la Utafiti

Lengo la tatu la utafiti huu lilikuwa kufafanua mikakati ya kiwingi-lugha inayohusika katika miundo yenye Sheng'. Uchanganyaji misimbo, wingishaji-maradufu, ushabihiano, ujozi-msimbo na utatu-msimbo ni baadhi ya mikakati iliyodhihirika katika uchunguzi huu. Matokeo ya uchanganuzi wa data yalionyesha aina ya uchanganyaji misimbo wa kipekee ambapo kuna uchanganyaji wa viambajengo vya zaidi ya msimbo mmoja unaofanyika ndani ya kishazi au sentensi moja. Uchanganyaji misimbo huo ulihusu *misimbo miwili* yaani, *lugha moja* ambayo ni Kiswahili na *msimu mmoja* ambao ni Sheng'.

Data ya utafiti huu imedhihirisha kutukia kwa ujozi-msimbo kama mkakati mwingine wa kiwingi-lugha unaojitokeza katika miktadha ya matumizi ya Sheng'. Ujozi msimbo ni hali ya uwili msimbo ambapo misimbo miwili ya lugha hutumiwa baina ya sentensi na sentensi katika mawasiliano. Ujozi-msimbo hutofautiana na uchanganyaji-misimbo kwa vile ujozi-msimbo unahusu mgotanisho wa misimbo miwili au zaidi baina ya sentensi na sentensi. Uchanganyaji misimbo kwa upande wake unafanyika ndani ya sentensi moja. Matokeo ya utafiti huu, hivyo basi, yalibainisha ujozi-msimbo ambapo msimu wa lugha kama Sheng' uliweza kushirikiana na lugha nyingine bainifu kama Kiswahili au Kiingereza ili kujenga sentensi zenye mseto wa viambajengo.

Uchunguzi huu umedhihirisha vilevile utatu-msimbo kama mkakati wa kiwingi-lugha unaotumiwa na wazungumzaji wa Sheng' kwa nadra sana. Matokeo yenyewe yalionyesha kuwa wazungumzaji wa Sheng' hutumia mkakati wa ujozi-msimbo mara nyingi kuliko utatu-lugha. Hii ni kwa vile kwa misimbo mitatu inayohusika, miwili ni lugha ambayo ni Kiswahili na Kiingereza lakini mwingine ni msimu ambao ni Sheng'. Sentensi kadha wa kadha zilionyesha matumizi ya misimbo mitatu katika usemi mmoja.

Mkakati kama huu hauwezi kutumiwa na mtu anayeelewa lugha moja au mbili pasipo kujua msimbo wa tatu. Huenda kutotumika mara nyingi kwa mkakati huu wa utatu-misimbo kunahusiana na ugumu wa kisaikolojia wa kuchakata sentensi zenye misimbo mitatumitatu akilini.

Matokeo ya usaili wa watafitiwa yameonyesha vilevile kwamba kuna motisha za kisaikolojia [kama kufikiri kwamba hawataeleweka] na za kiisimu zinazowasababisha wazungumzaji wa Sheng' wazingatie wingishaji-maradufu kama mkakati mwingine wa kiwingi lugha. Motisha hizo huwasababisha wadumishe mofu ya kubainisha wingi ya lugha chasili na kuongeza mofu ya wingi katika msimbo pokezi. Hivyo basi tunapata mofu mbili za wingi katika sentensi moja.

Kutokea kwa data iliyokusanywa kutoka utafiti huu yenye miundo ambayo ina lugha solo zaidi ya moja kumeonyesha kuwa ushabihiano ni mkakati mwingine wa kiwingi-lugha unaotumiwa katika Sheng'. Ingawa mkakati huu wa kiwingi-lugha haukudhihirika mara nyingi katika utafiti huu, wazungumzaji wa Sheng' waliweza kuutumia ili kufanikisha mawasiliano katika miktadha kadhaa. Ushabihiano uliotokea ulihusu kuundwa kwa muundo wa kiisimu wenye viambajengo vya lugha tofauti vinavyofuata mkuku wa lugha nyingine. Ingawa matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha ushabihiano kama mojawapo ya mikakati wa kiwingi-lugha inayotumiwa katika Sheng', yanapinga dai la nadharia ya 4M (Myers-Scotton, 2002) kwamba ushabihiano ni mfanyiko ambao hatua kwa hatua husababisha uundaji wa Krioli. Imebainika kwamba mfanyiko huo pekee yake hauwezi kuashiria ukriolishaji wa Sheng' kwa vile vibainishi vingine vingi vimepinga ukriolishaji wake.

### 5.1.4 Matokeo Kulingana na Lengo la Nne la Utafiti

Lengo la nne la utafiti huu lilikuwa kuchanganua tungo zenye Sheng' kwa kuzingatia nadharia ya 4M. Matokeo ya uchanganuzi wa tungo zenye Sheng' yamethibitisha madai ya nadharia ya 4M. Mosi, yamethibitisha kwamba viambajengo vya LS na LC hushiriki katika ujenzi wa tungo hizo. Yamebainisha tena kuwa vizingwa vya LS na LC huweza kushiriki katika uzalishaji wa sentensi zenye Sheng'.

Matokeo pia yameonyesha kuwa aina za mofimu zinazohusika katika ujenzi wa tungo zenye Sheng' hutofautiana kutoka muundo mmoja hadi mwingine. Matokeo hayo kwa misingi hiyo yanadokeza kuwepo kwa viwango tofauti vya usanzuzi katika lemma vinavyohusika katika uzalishaji wa tungo hizo vile inavyofafanuliwa na nadharia ya 4M.

Utafiti umebainisha kutokana na data pia kuwa mkuku wa kimofosintaksia hufuatwa katika uzalishaji wa miundo ya kiwingi-lugha yenye Sheng'. Imedhihirika kwamba wazungumzaji hufanya uteuzi wa mkuku utakaokaliwa na viambajengo akilini mwao kuingiza mofimu. Matokeo yameashiria kwamba kanuni ya mfuatano wa mofimu na kanuni ya mofimu amilifu huhusika katika uteuzi wa viambajengo vya zaidi ya msimbo mmoja vitakavyounganishwa ili kujenga miundo ya kiwingi-lugha yenye Sheng'.

Baada ya kuchanganua data, mtafiti aligundua kuwa kanuni ya mfuatano wa mofimu inayohusu matumizi ya kitenzi kishirikishi katika sentensi huhitaji kitenzi cha aina hiyo kifuatwe na nomino au kivumishi pekee. Matokeo yamedhihirisha kwamba kitenzi kishirikishi kikitumiwa katika miundo ya kiwingi-lugha yenye Sheng' kinafuatwa na ama nomino au kivumishi. Ilijitokeza kwamba nafasi ya nomino inaweza kukaliwa na kiwakilishi chake.

Isitoshe, matokeo yameashiria uhalisia mwingine kuhusiana na mpangilio wa mofimu katika sentensi za kiwingi-lugha. Mathalani, kinyume na dai la nadharia ya 4M kwamba katika miundo yenye leksimu mojamoja za lugha changizi zilizochopekwa, mpangilio wa mofimu utakaozingatiwa ni ule wa LS, imebainika kuwa mpangilio wa mofimu huamuliwa na aina ya kitenzi kitakachoteuliwa. Kutumiwa kwa kitenzi kisoelekezi katika muundo wa kiwingi-lugha humruhusu mzungumzaji akiunganishe na kielezi tu. Ilibainika pia, vile anavyobainisha Sawe (2015) kwamba muundo wa kiwingi-lugha wenye kitenzi kielekezi mosi hauwezi kukamilika kisarufi pasipo kukaliwa kwa nafasi ya yambwa. Jaribio la kushirikisha nomino lilidhihirisha kwamba nadharia ya 4M kwa sasa haina utoshelevu wa kiufafanuzi. Hii ni kwa vile haiwezi kuelezea ni kwa nini baadhi ya miundo ya kiwingi-lugha haiwezi kuzalishwa.

Utafiti huu umepata matokeo kadha wa kadha kuhusiana na kanuni ya mofimu amilifu katika tungo za kiwingi-lugha zenye Sheng'. Kwanza, matokeo ya utafiti huu yameonyesha kwamba mara nyingi Kiswahili huzalisha mofimu amilifu katika sentensi zenye UM baina yake na Sheng'. Pili, imebainika kuwa mofimu amilifu zinazozalishwa na Kiswahili ni pamoja na viambishi vya nafsi, viambishi vya njeo na hali, viambishi vya masharti, viambishi vya O-rejeshi na vya mnyambuliko wa kitenzi. Hatimaye, uchunguzi huu umebainisha kwamba Sheng' haina mofimu zake bali inatumia zile za Kiswahili. Hata hivyo, baadhi ya mofimu amilifu kama '*ma-*' ya kubainisha wingi na '*-nga'* ya kubainisha hali ya mazoea huzalishwa na Sheng'.

Aidha, kuhusiana na miundo ya tungo za kiwingi-lugha zenye Sheng, utafiti huu umegundua vilevile kwamba mara nyingi Kiswahili inajitokeza kama lugha solo katika miundo yenye UM baina yake na Sheng'. Hii ni kwa vile Sheng' haina mofimu amilifu

kama vile viunganishi, viwakilishi, viambishi na vihusishi na kwa misingi hiyo hutumia zile za Kiswahili.

**5.2 Mahitimisho**

Tasnifu hii inahitimisha kuwa uundaji wa kinasibu wa msamiati wa Sheng' hauashirii tu kuwa lugha ni mfumo nasibu ila unaashiria pia ubunifu wa binadamu katika matumizi ya lugha. Ubunifu huo umewezesha kule kuundwa kwa maneno ya Sheng' yasiyohusiana moja kwa moja na dhana au kiashiriwa. Huenda kutoundwaundwa kwa maneno mengi ya Sheng' kwa kutumia mbinu hii kunachangiwa na ukosefu wa motisha ya kubuni.

Utafiti huu haukupata mifano yoyote ya mofimu amilifu ambayo ni pamoja na viambishi, viunganishi na vihusishi zilizoundwa katika harakati za uleksikalishaji wa Sheng'. Kwa sababu ya tokeo hilo, mtafiti anahitimisha kuwa Sheng' bado ni msimbo usiojitegemea kama lugha ila inategemea mofimu amilifu nyingi za lugha solo kama Kiswahili. Imedhihirika kimsingi kwamba mofimu nyingi zilizoundwa katika uleksikalishaji wa Sheng' ni mofimu za kileksika.

Msimbo au lugha huzaliwa na huweza kukua na hata kufa kwa kutegemea matumizi yake na athari kutoka kwa mazingira. Kuzaliwa kwa Sheng' kunahusiana na kule kubainika kwa fonimu, silabi, mofimu na hata mipangilio inayokubalika ya maneno katika sentensi. Kwa sababu hii, maneno yanayoundwa katika Sheng' yanaweza kufupishwa kisha yakatoholewa ili yafanane na maumbo mengine ya Sheng'. Hivi, baadhi ya maneno yanayoundwa yanaishia 'i' (*tizi, mtoi*) au 'o' (*storo, romo*). Inahitimishika basi kuwa uhalisia huu huchangia kukubalika au kutokubalika kwa msamiati unaoundwa katika msimbo.

Uchanganuzi uliofanywa katika tasnifu hii ulidhihirisha kuwa maneno mapya ya Sheng’ yanaweza kuundwa kwa kutumia mbinu ya urefushaji wa umbo. Inahitimishika kwamba matumizi ya mbinu hii yanaashiria uhuru alionao mzungumzaji wa Sheng’ wa kuunda msamiati kwa kurefusha au kufupisha msamiati vile mwandishi alivyo na uhuru wa kishairi wa kutumia mazida (urefushaji). Ilimradi umbo lililozalishwa lijulikane kwa wazungumzaji wengine wa msimbo huu, Sheng’ haina taasisi au baraza linaloidhinisha msamiati wake.

Baadhi ya maneno ya Dholuo, Kikamba, Kikikuyu na Kimaasai yameweza kukopwa na kutumiwa kama msamiati wa Sheng’ bila kutoholewa. Hitimisho lingine la utafiti huu kwa misingi hiyo ni kwamba, kabla ya kusambazwa kwa maneno yanayokopwa moja kwa moja pasipo kutoholewa, yanaweza kutumika na kueleweka katika maeneo finyu. Usambazwaji wa msamiati wa Sheng’ (uliokopwa kutoka lugha za kigeni au/na za kiafrika) huchangia upanuzi wa mawanda ya matumizi. Usambazaji huo huendeleza umilisi wa wazungumzaji ambao wataweza kueleweka wanapotumia msamiati husika na wataweza kuwaelewa wengine wanaotumia msamiati huo uliozalishwa wa Sheng’.

Usilabifishaji-upya katika Sheng’ hufanyika pale ambapo neno linakopwa kutoka lugha chasili na kupewa muundo tofauti wa silabi. Tasnifu hii inahitimisha kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu kwamba mbinu hii ya usilabifishaji-upya inadhihirisha sura nne katika mchakato wa uleksikalishaji wa Sheng’. Sifa ya kwanza ya usilabishaji-upya ni ile ya kuongezeka kwa idadi ya silabi katika neno jipya; ya pili inahusu kupunguzwa kwa idadi ya silabi; ya tatu huhusu udondoshaji wa baadhi ya silabi na sura ya nne inaweza kutokea kwa njia ya kugeuzwa kwa mpangilio wa silabi ili kuunda neno jipya.

Matokeo ya uchanganuzi wa maneno yaliyoundwa kwa kuzingatia utaratibu huu ulibainisha kwamba hakuna neno ambatano la Sheng' lenye zaidi ya silabi kumi. Hitimisho la tasnifu hii ni kwamba huenda kutotukia kwa maneno ambatani yenye zaidi ya silabi kumi ama mizizi mitatu au zaidi kunahusiana na ugumu wa kuchakata neno kama hilo wakati wa kuunda, kutamka na hata kung'amua. Kutoambatanishwa kule kwa zaidi ya maneno matatu ni sababu mojawapo inayochangia kule kutoundwa kwa maneno yasiyozingatia kigezo cha iktisadi kinachopendekezwa na nadharia ya Pegitosca.

Kuhusiana na lengo la pili la utafiti huu, kinadharia, launi inayokua kutoka Pijini ikielekea kuwa Krioli ingetarajiwa kubainisha muundo wake wa kimofolojia. Walakini, matokeo ya uchunguzi huu yanaonyesha kuwa Sheng' haijaibuka na muundo wake ambao ungebainisha paradimu zinazoweza kukaliwa na vijenzi vya maneno kama viambishi awali, vya kati, mizizi na viambishi vya tamati. Hili, kwa pamoja na tokeo kwamba Sheng' haina viambishi vyake vya nafsi, vya njeo, vya hali ya masharti, vya hali timilifu, vya kukanusha na virejeshi ndiyo sababu ya hitimisho la utafiti huu kwamba launi yenyewe si Krioli ila ni msimu tu ambao unategemea Kiswahili kama lugha solo.

Tasnifu hii inahitimisha kuwa huenda ukuaji wa Sheng' kutoka msimu hadi kuwa lugha bainifu usiwezekane. Hii ni kwa vile, msamiati wake haujakuwa thabiti. Motisha za kuwabagua wengine katika mawasiliano kama walimu, wazazi au polisi husababisha kubadilishwabadilishwa kwa msamiati mara kwa mara ili kuhifadhi siri. Kubadilishwa huko kwa msamiati wa Sheng' hulengwa kufanikisha mawasiliano ya wale wanaofahamiana. Hivi, mintarafu ya matokeo ya uchunguzi huu, kikundi kimoja kinachotumia Sheng' (jumuiya msimbo) kinaweza kutumia neno fulani ambalo

halitumiwi na kikundi kingine kinacholitumia hata katika mji, mtaa au shule moja. Hata hivyo, kuna baadhi tu ya maneno ya Sheng' ambayo yamedumishwa kimatumizi kwa mujibu wa uchunguzi wetu.

Iligunduliwa katika utafiti huu pia kuwa mielekeo hasi ya watu wengi imeathiri hadhi ya Sheng' nchini Kenya. Matokeo hayo yaliashiria kuwa msimbo wenyewe umehusishwa na wakora, wezi, walanguzi wa dawa za kulevya na watu wanaokwepa sheria. Msimbo wenyewe unaainishwa kwa fahiwa hiyo kama launi ya chini (LC). Kwa misingi hiyo, tasnifu hii inahitimisha kwamba kwa ujumla msimbo wa Sheng' ni launi isiyopendelewa na jamii pana inayotumika katika miktadha isiyokuwa rasmi mara nyingi. Hata hivyo, iligunduliwa kuwa msimbo wenyewe hutumika wakati mwingine katika baadhi ya miktadha rasmi kama launi isiyotarajiwa. Kutumiwa kule katika miktadha hiyo rasmi hakutoshelezi kuifanya Sheng' kuwa launi ya juu (LJ).

Miongoni mwa watafitiwa waliochunguzwa katika utafiti huu hakuna hata mmoja wao aliyedai kuwa lugha yake ya kwanza ilikuwa Sheng'. Matokeo ya utafiti uu huu yaliashiria kuwa wasemaji wa msimbo wenyewe (waliochunguzwa) walikuwa wasemaji wazawa wa lugha zingine za kwanza ambazo hazikuwa Sheng'. Usaili wa watafitiwa ulionyesha kwamba watafitiwa wote hawakuwa wamemwona yeyote ambaye Sheng' ilikuwa lugha yake ya kwanza. Mintarafu ya matokeo haya, tasnifu hii inahitimisha kwamba msimbo wa Sheng' hauna watu wanaoizungumza kama lugha ya kwanza kabisa ndiposa haujatimiza hitaji hilo muhimu la upijini. Hitimisho hili lilitiliwa uzito na matokeo kuhusu familia za mitaani (yaani watoto na hata wazazi) kwamba walikuwa wana lugha zingine za kwanza ambazo hazikuwa msimbo wa Sheng'. Tokeo kwamba baadhi ya watoto na wazazi wengi wa mitaani waliotoroka kutoka makwao wakijua lugha fulani za kwanza ambazo hazikuwa Sheng'.

Hitimisho la utafiti huu kwamba wasemaji wa Sheng' waliochunguzwa hawakujifunza msimbo huo kama lugha ya kwanza linapinga dai la Spyropoulos kwamba Sheng' ilikuwa Pijini kwa wakati wa utafiti wake (1987) ambayo alitabiri kwamba ingekuwa Krioli. Hili, alidai lingetukia kwa sababu watoto wa familia za mitaani wangeanza kujifunza Sheng' kama lugha ya kwanza. Matokeo ya utafiti huu, ambao umefanywa zaidi ya miaka ishirini baadaye, bado yanapinga nadharia tete yake. Hitimisho lili hili linapinga lile la Githiora (2002) kwamba Sheng' itageuka kuwa lahaja ya Kiswahili inayozungumzwa mijini. Hii ni kwa kuwa Sheng', kulingana na matokeo ya uchunguzi huu, imebaki kuwa msimu wala haijaweza kubadilika kuwa Krioli au lahaja. Sifa zake za kimofolojia, kimofosintaksia na kiisimu jamii zinaiainisha katika kategoria ya misimu.

Mielekeo ya watu wengi kuhusu Sheng' kwa mujibu wa matokeo ya uchunguzi huu haijaimarika kutoka hasi kuelekea chanya. Hadhi yake vilevile haijaimarika kutoka kwa launi ya chini kuelekea kwenye launi ya juu. Iligunduliwa katika misingi hiyo kuwa hakujawa na juhudi za kuistawisha Sheng' zaidi kwa kuendeleza mielekeo ya watu kuihusu au kuiendeleza hadhi yake ili iweze kutumika kama lugha au msimbo pana. Kimatumizi, Sheng' imeendelea kubaki kama msimbo finyu unaofaa kwa vikundi vidogovidogo kama wanafunzi au familia za mitaani. Hata hivyo, tasnifu hii inahitimisha kwamba kuimarishwa kwa mielekeo na hadhi pekee hakutaigeuza Sheng' kuwa Pijini wala Krioli.

Tasnifu hii inahitimisha kuwa Sheng' haikuwahi kuwa Pijini, kwanza, kwa sababu haikuibuka katika miktadha ambapo lingua franka haikuwepo. Pili, muundo wake wa kimofosintaksia kwa mujibu wa matokeo ya usaili haukuanza kwa ule usiokuwa thabiti ila umekuwa ukikitwa katika mkuku wa Kiswahili kama lugha solo. Tatu, kuhusiana

na dai la nadharia ya 4M, hakuna lugha-tuhinga na lugha-takaro zinazohusishwa na msimu wa Sheng'. Kwa misingi hiyo, kama Sheng' haikuwahi kuwa Pijini hatuwezi kudai kwa namna yoyote ile kwamba imeimarika kuwa Krioli.

Inahitimishika kutokana na sifa za uleksikalishaji wa Sheng' kwamba, tofauti na Pijini, neno moja huweza kubeba maana zaidi ya moja au hata likapewa fahiwa inayorejelea kinyume cha maana yake katika Sheng'. Aidha, tofauti na Pijini, maana za maneno yanayokopwa kutoka lugha zingine si lazima zidumishwe. Hii inamaanisha kuwa maana za maneno yanayokopwa hadi kwa Pijini hudumisha maana zao lakini maneno mengine yanayokopwa hadi kwa msimu huweza kupewa maana tofauti kabisa na maana zao asili.

Baadhi ya motisha zilizoashiriwa na watafitiwa kama vichocheo vya asili ya Sheng' zinaongeza sifa zinazohalalisha hitimisho kwamba haijawahi kuwa Pijini wala kuhitimu kama Krioli. Kwanza, matumizi ya Sheng' huhusishwa na ufichaji wa siri, sifa ambayo ni nadra itokee katika Pijini. Pili, Sheng' huweza kutumiwa kwa ajili ya kuwabagua wengine au kuficha siri katika mawasiliano lakini Pijini huanzishwa kwa lengo la kuwaunganisha watu wasiokuwa na lingua franka. Kwa sababu hiyo, tofauti na ilivyo katika Pijini, maneno mapya huweza kuundwa katika msimu au Sheng' ili kuchukua nafasi ya yale yaliyozoeleka ili kuendelea kuficha siri.

Mtafiti amefikia hitimisho pia kwamba matumizi ya Sheng' hupinga ukriolishaji wake kwa kuwa hayaegemei katika miktadha rasmi na badala yake matumizi hayo yanaweza kupunguza urasmi wa mawasiliano. Isipokuwa pale ambapo kuna lugha nyingine inayotumika kama launi ya juu; matumizi ya Krioli hayawezi kupunguza urasmi katika muktadha wa mawasiliano. Hivyo basi, msimu unaweza kufaa kwa ujenzi wa ukuruba na ushirikiano katika mazungumzo.

Matokeo ya uchanganuzi wa data kuhusu upijini na ukriolishaji yamebainisha sifa zinazothibitisha kuwa msimbo wa Sheng' ni msimu na sio Pijini wala Krioli. Kutokana na matokeo haya, utafiti huu unahalalisha nadharia tete ya pili ya utafiti huu kwamba 'sifa za Sheng' zinapinga upijini au ukriolishaji wake'. Matokeo hayo basi yamepinga nadharia tete za watafiti kama Bosire (2006) wanaodai kuwa Sheng' ni lahaja ya Kiswahili, kama Abdulaziz na Osinde (1997) wanaoashiria kuwa Sheng' ni lugha mahuluti, au Spyropoulos (1987 anayedokeza kwamba Sheng' ni Pijini au Krioli au Myers-Scotton (1993b) anayebainisha Sheng' kama ubadilishaji msimbo. Hivyo basi, tasnifu hii inahitimisha kuwa Sheng' ni msimu.

Ilitukia vilevile kuwa uradidi wa kivumishi kama umbo la Kiswahili au Kiingereza huweza kuzalisha kivumishi kipya cha Sheng' ambacho maana yake ni tofauti kabisa na ya kivumishi cha lugha chasili. Inatokea kwamba mfanyiko huo wa kuunda msamiati si ukopaji kwa sababu fahiwa ya neno linalozalishwa ni tofauti na fahiwa iliyobebwa na umbo la lugha chasili. Matokeo hayo hayakuonyesha maneno ya Sheng' yaliyoundwa kwa kulikariri neno mara tatu au zaidi. Mtafiti amehitimisha kwamba huenda kutotukia kwa uleksikalishaji unaofanyika kwa jinsi hiyo kunasababishwa na uwezekano kwamba leksimu za aina hiyo zingekuwa na idadi kubwa sana ya silabi ambayo ingesababisha ugumu wa utamkaji.

Tasnifu hii inahitimisha vilevile kwamba matumizi ya ufupishaji kama mbinu ya kuunda msamiati unaweza kushirikisha upunguzaji wa idadi ya silabi au fonimu pekee. Idadi ya fonimu na silabi za neno chasilia na neno zalishwa haziwezi kuwa sawa iwapo mbinu ya ufupishaji ilitumika ili kuzalisha neno jipya. Ingawa hatukulenga kuchunguza sababu za kutumiwa kwa ufupishaji kama mbinu ya kuzalisha msamiati, matokeo ya usaili wa watafitiwa yamechangia hitimisho la tasnifu hii kwamba uundaji wa msamiati

mpya na hata matumizi ya Sheng' wakati mwingine unajitokeza kama matumizi ya mtindo kama ukiushi kutokana na kaida. Kwa vile Sheng' ni mtindo wa kutumia lugha, wazungumzaji wana uhuru wa kutumia *'mtoi'* badala ya 'mtoto', *'anaendanga'* badala ya 'huenda' na mengine mengi kama njia za kujieleza. Uhuru huo kwa pamoja na umilisi unaomilikiwa na wahusika ambao ni pamoja na vijana na familia za mitaani huwawezesha wahusika wazungumze na kuelewana.

Kuhusiana na mnyambuliko unaofanyiwa maumbo ya Sheng', mtafiti anahitimisha kuwa mnyambuliko ni mfanyiko unaohusu utanuzi wa mzizi kwa kuongeza viambishi vya awali au vya tamati. Viambishi hivyo katika Sheng' vinaweza kuwa vile vya unominishaji au vya hali mbalimbali. Mnyambuliko mwingi unaofanyiwa kauli mbalimbali za vitenzi vya Sheng' unahusu viambishi vya hali za kutendeka, kutendewa, kutendesha na kutendatenda vya Kiswahili. Hii inamaanisha kuwa Sheng' haina viambishi vyake vya hali mbalimbali isipokuwa kile cha hali ya mazoea '-nga'. Hili tokeo linadhihirisha kwamba si mkuku wa kisarufi wa Kiswahili pekee unaozingatiwa katika Sheng' ila mofu zake nyingi zinatumika katika kuzalisha hata maneno mapya. Imejitokeza kuwa kuongezwa kwa mofu hubadilisha maana ya umbo linalozalishwa kupitia mnyambuliko hivi kwamba umbo hilo linakuwa neno tofauti linalorejelea dhana tofauti. Kwa fahiwa hiyo, kila kiambishi (mofu) kinachoshiriki katika maneno ya Sheng' yaliyoundwa kupitia mnyambuliko kinawakilisha maana maalum (mofimu). Mtafiti alihitimisha vilevile kwamba viambishi awali na vya tamati pekee hutumiwa ili kujenga miundo ya maneno ya Sheng' lakini uambishaji kati haufanyiki kamwe katika msimbo huo.

Pijini na Krioli ni lugha zilizoibuliwa katika miktadha ya kibiashara na ya utumwa kwa ajili ya kuwawezesha watumiaji ambao ni wasemaji wasiokuwa na lingua franka

kuwasiliana na kuyafikia malengo yao. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, tasnifu hii inahitimisha kuwa Sheng' haikuzaliwa kama Pijini ila kama msimbo baguzi uliolengwa kuwabagua wengine katika mawasiliano ya siri kama vile walimu, wazazi na polisi. Hapana budi kwamba wale walioanzisha Sheng' walikuwa na lingua franka ya kuwaunganishwa kwa mawasiliano.

Utafiti huu unahitimisha kuwa Sheng' ni msimu ambao haukutokana na Pijini. Hata hivyo, Sheng' inamiliki sifa chache tu zinazoifanya ilingane na Pijini. Sifa moja ni kwamba msimu wenyewe kwa namna sawa na Pijini hauna wasemaji wazawa. Hii inamaanisha kuwa hakuna upokeaji wa Pijini wala msimu mfano ya Sheng' kama lugha ya kwanza.

Tasnifu hii inahitimisha vilevile kwamba ingawa msimbo wa Sheng' si Pijini, inatumika kama msimbo finyu sawasawa na Pijini. Hii ni kwa kuwa, kama ilivyothibitishwa katika utafiti huu, Sheng' hairuhusiwi kutumika katika baadhi ya miktadha ikiwemo ile ya darasani, ya uandishi rasmi na mengineyo. Wazungumzaji wa Sheng' hulazimika kutumia misimbo pana kama Kiswahili sanifu, Kiingereza au hata lugha za kiasili katika miktadha hiyo. Kwa fahiwa hii, msimu mithili ya Sheng' sawa na Pijini huweza kutumika kama Pijini finyu. Kwa mtazamo wa tasnifu hii pia, hali hii haionyeshi kuwa Sheng' ni au ilikuwa Pijini ila inaashiria kuwa baadhi ya sifa zao zinafanana.

Tasnifu hii imechanganua miundo mbalimbali yenye Sheng' kwa kuzingatia modeli ya 4M ya Myers-Scotton na ikagundua kuwa Sheng' haina muundo wake tofauti. Inajitokeza kuwa miundo ya tungo zinazozalishwa katika msimbo wa Sheng' imekitwa katika mkuku wa Kiswahili ambayo ni lugha solo.

Uchanganuzi uliofanywa katika tasnifu hii umeibuka na maelezo yanayoweza kutumiwa kujeleza au kufafanua dhana za Pijini na Krioli. Inahitimishika kwamba iwapo Sheng' haikuwahi kuwa Pijini, haiwezekani kuirejelea baadaye kama Krioli kwa kuwa Krioli haiwezi kuibuka pasipo kuwepo kwa Pijini. Aidha, ukriolishaji hauwezekani iwapo Pijini haitapata mazingira kama ya uleksikalishaji na usarufishaji yanayoruhusu kuimarika kwake hadi kiwango cha kutumiwa kama lugha ya kwanza. Hata hivyo, kwa mujibu wa uchanganuzi uliofanywa katika sura ya nne ya tasnifu hii, kuimarika kwa msimu kimaandishi pekee kama ilivyokwisha kufanyika kwa Sheng' hakuwezi kuwa kiashiria kinachotosheleza cha upijinishaji.

Uchanganyaji misimbo uliogunduliwa katika utafiti huu ulihusu launi za misimbo miwili zisizofanana kwa vile moja ilikuwa lugha, ilihali launi, nyingine ilikuwa msimu. Kutokana na ithibati hiyo, tasnifu hii inafikia hitimisho kwamba uchanganyaji-misimbo unaohusiana na Sheng' unapaswa kuangaziwa kama mgotanisho wa faridi za misimbo miwili, ambayo inaweza kutofautiana kwa misingi ya hadhi ya kiisimu, unaofanyika ndani ya sentensi moja. Uchanganyaji huo hutumiwa kama mkakati wa kiwingi-lugha wenye uamilifu wa kimawasiliano.

Wingishaji-maradufu ulitumiwa kama mkakati wa kiwingi-lugha katika Sheng'. Viambishi vya wingi vya Kiswahili na vya Kingereza vilitumiwa kwa wakati mmoja ndani ya neno moja lililokopwa. Kutokana na hili, mtafiti anahitimisha kwamba mofu ya pili inayobainisha wingi hutumika hata kama kuna mofu nyingine kwa sababu mofu ya pili ni mofimu amilifu ya lugha solo ambayo ni lazima iwepo ili mpangilio wa vijenzi uwe sawa na maana ibainike.

Uchunguzi huu umeonyesha ukiushi mwingi wa sarufi ya Kiswahili unaofanywa katika Sheng'. Imetokea kwamba nomino ambazo hujitokeza katika ngeli ya kwanza na ya pili

(A/WA) katika Kiswahili huongezewa viambishi vya wingi vya ngeli ya LI/YA. Hivi, mofu ya wingi 'ma' hutumiwa katika Sheng' bila kujali iwapo nomino zinazorejelewa ni hisivu au si hisivu. Tasnifu ya utafiti huu ni kwamba ukiushi huo huwaathiri wanafunzi ambao ni wasemaji wa Sheng' katika ujifunzaji na matumizi yao ya Kiswahili sanifu. Hivyo basi, ni dhahiri kwamba Sheng' haizingatii mofosintaksia ya Kiswahili kwa vile haizingatii kanuni za mnyambuliko za umoja na wingi pamoja na upatanisho wa kisarufi baina ya nomino na vivumishi au nomino na vitenzi.

Tasnifu hii inahitimisha kuwa ushabihiano ni zao la mtagusano wa lugha unaoambatana na uhuru wa mwanawingi-lugha katika matumizi ya lugha. Ujuzi wa maneno na kanuni za zaidi ya lugha moja huwapa wahusika uwezo wa kuzalisha miundo inayozingatia kanuni za lugha moja (lugha zote) au kanuni za zote (kiushabihiano). Matokeo haya yanaashiria kuwa mfuatano wa maneno unaojitokeza wakati wa ushabihiano hutumika katika lugha ya mazungumzo na hueleweka kwa wazungumzaji kwa kutegemea makubaliano yao. Watu wengine ambao si wanajumuiya-msimbo huenda wasielewe maana inayopitishwa kwa vile haya si sehemu ya umilisi wao.

Tasnifu hii inazidi kuhitimisha kwamba maneno ya Sheng' na yale ya Kiswahili huhifadhiwa ndani ya akili za wasemaji ambao wataweza kuzalisha miundo ya Sheng' pekee, ya Kiswahili pekee au iliyochanganya Kiswahili na msimbo wa Sheng'. Msemaji akiteua maneno ya Kiswahili na kuyaunganisha na yale ya msimbo wa Sheng' atakuwa akitumia mkakati wa kiwingi-lugha kufanikisha mawasiliano. Pasipo kuunganisha maumbo ya misimbo miwili au zaidi, msemaji anaweza kuzalisha miundo isiyokuwa ya kiwingi-lugha. Msemaji wa Sheng' ataweza kuelewa sentensi zinazoundwa na wasemaji wengine wa Sheng' kwa sababu wao wamehifadhi maneno ya Sheng' akilini na wanajua maana zake.

Kuhusiana na matumizi ya ushabihiano, ujozi-msimbo, utatu-msimbo na uchanganyaji-msimbo kama mikakati ya kiwingi-lugha katika Sheng', tasnifu hii inahitimisha kwamba kiamuzi kikuu ni uteuzi wa msemaji ni haja ya kupitisha maana. Kimsingi msimbo mmoja kama Kiswahili au Kiingereza ungeweza kutumiwa ili kupitisha maana. Walakini, uteuzi wa mzungumzaji wa kuunganisha viambajengo vya misimbo miwili au mitatu, kufanya ushabihiano au wingishaji-maradufu hulengwa kuwasilisha maana na hutegemea uteuzi wa mzungumzaji ambaye huwa halazimishwi kutumia idadi fulani ya misimbo.

Mintarafu ya lengo la nne, uchanganuzi kuhusu uambajengo wa tungo zenye Sheng' umethibitisha dai la nadharia ya 4M kwamba baadhi ya tungo zenye U.M. zinaweza kuundwa kwa kutumia vizingwa vya LS na LC. Kwa mujibu wa launi za lugha zilizochunguzwa, utafiti huu unahitimisha kuwa uambajengo wa tungo za aina hiyo hushirikisha mgotanisho wa vipashio vya misimbo miwili au zaidi.

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, tasnifu hii inafikia hitimisho kwamba aina za mofimu zinazohusika katika miundo yenye Sheng' iliyoundwa kwa kuunganisha viambajengo vya LS na LC hutofautiana. Hivyo basi, hapana budi kwamba mofimu hizo za aina mbalimbali huzansuliwa katika viwango tofauti katika lemma vile inavyofafanuliwa na nadharia ya 4M. Hii ni kwa vile mofimu zingine ambazo ni pamoja na viambishi huingizwa tu kwenye muundo wakati wa kuunda ili maana inayolengwa ibainike na upatanisho udhihirike. Hitimisho hili linaambatana na dhana kwamba hakuna mkusanyiko wa sentensi katika akili ila zinaundwa wakati zinahitajika ambapo uzansuaji mofimu tamatishi unaanza. Tokeo hili linaashiria kwamba viambishi, vihusishi na viunganishi havizansuliwi katika kiwango cha awali hadi pale haja ya kuunda kishazi au sentensi itakapoibuka.

Kutokana na uchanganuzi wa data, ni dhahiri kwamba miundo ya sentensi zenye U.M. unaoshirikisha Sheng' huweza kuundwa kwa kutumia viambajengo vya msimbo solo pekee kama vizingwa. Uundaji wa vizingwa vya aina hiyo hufuata kanuni za kisarufi za msimbo solo. Hata hivyo, kwa vile wazungumzaji wana uhuru wa kimazungumzo, wanaweza kuzalisha vizingwa vya msimbo solo vinavyoghairi baadhi ya kanuni za msimbo/lugha solo. Kuhusika kwa lugha solo kulidhihirishwa kwa njia nyingi katika utafiti huu. Mosi, lugha solo zimedhihirika zikitawala katika tungo nyingi zenye mseto wa vijenzi vya Sheng' na Kiswahili. Pili, data imethibitisha hali nyingi ambapo lugha solo ilichangia mofimu amilifu na za kileksika katika muundo. Tatu, imekuwa dhahiri kwamba mkuku au mfuatano wa vijenzi wa Kiswahili hufuatwa katika mgotanisho wa vijenzi vya Kiswahili na Sheng'. Isitoshe, imebainika kuwa lugha solo huamua namna mofimu hufuatana na jinsi mofimu amilifu huunganishwa kwa mofimu za kileksika katika sentensi zenye mseto wa vijenzi vya Sheng' na Kiswahili. Kwa misingi hii, mtafiti anahitimisha kwamba madai ya nadharia ya 4M kuhusu sifa za lugha solo katika ujenzi wa sentensi zenye U.M. yanathibitishika.

Baadhi ya sentensi zenye U.M. unaofanyika baina ya Kiswahili na Sheng' zimeundwa kwa kuchopeka msamiati wa Sheng' ndani ya miundo inayozingatia mpangilio wa vijenzi wa Kiswahili. Tokeo hili linadhihirisha kuhusika kwa vizingwa vya Sheng' pekee katika ujenzi wa sentensi zenye U.M. Inamaanisha basi kwamba katika mazungumzo yenye U.M. unaofanyika baina ya Kiswahili na Sheng', neno moja la Sheng' – kama kizingwa – linaweza kushirikiana na maneno mengi ya Kiswahili kama viambajengo vya sentensi. Data imethibitisha na kwa hivyo tasnifu hii inahitimisha kwamba kizingwa chenyewe huchopekwa kwa kuzingatia sintaksia ya lugha solo vile wanavyodai Myers-Scotton na Jake (2000; 2001) katika ufafanuzi wao wa nadharia ya 4M.

Kuhusiana na lengo la nne la utafiti huu, mtafiti anahitimisha kuwa uzalishaji wa miundo yenye U.M. huhusu uteuzi na upangaji wa vijenzi vya zaidi ya lugha moja. Uteuzi huo huwezekana kwa sababu mzungumzaji ana ujuzi wa mofimu aliouhifadhi akilini mwake. Upangaji wa mofimu zinazoteuliwa hufuata mpangilio/mkuku wa lugha solo isipokuwa kwenye vizingwa. Kila kizingwa – kiwe cha LS au LC – huzingatia kanuni au mpangilio wa msimbo au lugha inayohusika. Kanuni mbili ambazo ni kanuni ya mfuatano wa mofimu na kanuni ya mofimu amilifu huhusika katika mfanyiko huo wa kuzalisha sentensi zenye U.M.

Mintarafu ya matokeo ya utafiti huu  tasnifu hii inapinga dai la nadharia ya 4M kuhusu kanuni ya mfuatano wa mofimu. Nguzo hiyo hueleza kuwa katika miundo yenye leksimu moja moja za lugha changizi zilizochopekwa, mpangilio wa mofimu utakaozingatiwa ni ule wa LS. Kwa sababu matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kinyume chake, tunahitimisha kuwa, kanuni hiyo haina usifabia na inaweza kukiukwa katika U.M. baina ya jozi zingine za misimbo vile ilivyodhihirika katika utafiti huu.

Tasnifu hii inahitimisha kinyume na inavyodaiwa na nadharia ya 4M. Inapinga wazo kwamba katika miundo yenye leksimu mojamoja za lugha changizi zilizochopekwa, mpangilio wa mofimu utakaozingatiwa ni ule wa LS. Badala yake, inahitimisha kwamba mpangilio wa mofimu hudhibitiwa na sifa za msamiati unaotumiwa. Iwapo kitenzi kisoelekezi kitateuliwa, mzungumzaji ataweza tu kukiunganisha na kielezi. Uteuzi wa kitenzi kielekezi humshurutisha mzungumzaji kuongeza nomino (ya ama LS au LC) kwenye nafasi ya yambwa. Hii inamaanisha kwamba uteuzi wa kitenzi chenye sifa maalum huathiri sifa za maneno mengine yatakayoteuliwa kama idadi (umoja/wingi) au hisia (hisivu/si hisivu). Elementi hii kanuni ya uteuzi madhubuti haikuangaziwa na Myers-Scotton katika ufafanuzi wa nadharia ya 4M.

Data iliyokusanywa katika utafiti huu imeonyesha mwelekeo bainifu kuhusiana na U.M. baina ya Kiswahili na Sheng'. Imekuwa dhahiri kwamba mofimu nyingi amilifu zinazotumiwa katika U.M. huo ni za Kiswahili. Mofimu hizo amilifu ni pamoja na viambishi vya nafsi, viambishi vya njeo na hali, viambishi vya masharti, viambishi vya O-rejeshi na vya mnyambuliko wa kitenzi. Utafiti huu unahitimisha kwamba, kwa vile Sheng' haina mofimu zake amilifu, msimu wenyewe hutumia zile za Kiswahili. Hata hivyo, Sheng' ina mofimu chache amilifu ndiposa tasnifu hii inahusisha hali kwamba mara nyingi Kiswahili ni lugha solo katika miundo yenye UM baina yake na Sheng'. Msimbo wa Sheng' ungeimarika kiasi cha kuwa na mofimu amilifu nyingi, huenda ingeweza kutumiwa mara nyingi pia kama lugha solo.

Mofimu amilifu nyingi zinazotumiwa katika maumbo ya Sheng' zinatumiwa kwa njia za kipekee. Mofimu amilifu ya wingi 'ma' huwa inatumika katika ngeli ya '6' (YA) ili kubainisha hali ya wingi ya nomino. Walakini, matumizi yake katika Sheng' hujumuisha nomino hisivu kama '*mambuzi*'. Mofimu amilifu ya upatanishi 'zi-' inafaa kutumiwa kuhusiana na ngeli ya 10 (ZI) lakini matumizi yake katika Sheng' yanaghairi kanuni hiyo ya Kiswahili.

### 5.3 Mapendekezo

1. Utafiti huu ulikumbwa na matatizo kadhaa ya kinadharia. Kwanza, nadharia ya 4M iliibuliwa kwa ajili ya kuchunguza, kuchanganua na kufafanua U.M. unaofanyika baina ya lugha na lugha. Nadharia yenyewe haikueleza chochote kuhusu mgotanisho unaoweza kutokea baina misimbo yenye hadhi zinazotofautiana kama msimu (Sheng') na lugha (Kiswahili). Tasnifu hii inapendekeza kwamba upungufu huo wa kinadharia unapaswa kuondolewa kwa

kushirikisha nguzo au elementi zitakazoweza kubainisha vile watafiti watakavyoweza kufanya wanapokumbana na launi tofauti za lugha.

2. Mtafiti anapendekeza kustawishwa kwa nadharia ya 4M ili kuibua modeli mseto yenye mihimili ya kutofautisha Pijini na Krioli. Hii ni kwa vile, jinsi ilivyo kwa sasa, nadharia ya 4M ina mihimili inayojikita zaidi katika ufafanuzi wa Krioli. Ubainishaji huo utakuwa muhimu kwa taaluma ya Isimu kwa kuwa utaweza kuweka mipaka iliyopo kati ya misimu, Pijini, Krioli, lahaja na lugha. Hivi, watafiti hawataweza kuashiria kuwa msimu ni Pijini au krioli au lugha vile ilivyokwisha kufanywa katika tafiti za awali zilizochunguza Sheng'. Mtafiti anapendekeza kushirikishwa kwa elementi zilizobainishwa katika uchanganuzi wa data kwenye jedwali kuhusu lengo la pili kuhusu upijini na ukriolishaji wa Sheng'.
3. Madai ya nadharia ya 4M kuhusu viwango vya kusanzuliwa kwa aina nne za mofimu yameweza kuthibitishwa kutokana na utafiti huu wa U.M. unaoshirikisha Sheng. Kwa fahiwa hivyo, inapendekezwa hapa kwamba nadharia ya 4M iweze kupanuliwa zaidi ili iweze kufafanua miundo ya lugha moja moja pia. Hii ni kwa vile nadharia kama sarufi zalishi hazijaweza kuwa thabiti licha ya uchunguzi wa miaka mingi. Nadharia itahitajika kuangazia namna za kuchambua fonimu na maana. Hivyo, nadharia hii itakuwa inaendelezwa ili iweze kufafanua viwango vyote vya lugha ambavyo ni fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki ndiposa iweze kuwa na utoshelefu wa kiufafanuzi.
4. Tasnifu hii imefafanua mbinu mbalimbali za uleksikalishaji zinazotumiwa katika uzalishaji wa msamiati wa Sheng'. Inapendekezwa kwamba mbinu hizi zinapaswa kushirikishwa kwenye mafunzo yanayohusu mofolojia ya uundaji

wa maneno. Kupitia ufunzaji huo, wahusika watakaonufaika wataweza kuzitumia kiutekelezaji katika uzalishaji wa maneno mapya ya lugha zingine.

5. Uchunguzi utakaochukua mkondo wa kiisimu-saikolojia waweza kufanywa baada ya utafiti huu. Uchunguzi huo utaweza kubainisha motisha za kisaikolojia zinazochochea ubadilishaji msimbo. Utafiti huo utaweza kulenga ubainishaji wa namna maneno ya lugha zinazotofautiana yanavyohifadhiwa akilini. Utafiti huo utaweza kutoa mchango muhimu kuhusu viwango vya kusanzuliwa kwa vijenzi vya sentensi zenye U.M. na hata lugha moja moja. Huenda utafiti huo utatoa mwanga zaidi kuhusu asili ya ushabihiano katika sentensi zenye U.M.
6. Kwa mujibu wa nadharia ya Pegitosca kuna nguzo kuu zinazoweza kutumiwa ili kutathmini ufaafu wa msamiati unaoundwa kwa sayansi, swali linalopaswa kujibiwa linahusu namna ya kuondoa mwegemeo kwenye sayansi zaidi. Ni kwa kiwango kipi ambacho nadharia ya Pegitosca ambayo inasisitiza usayansi itafaa kwa uchunguzi wa msamiati wa sajili ya sayansi kwa kulinganisha na sajili ya mazungumzo ya kawaida au msimu. Wanaisimu nadharia wanapaswa kutathmini iwapo mihimili mingine itapunguzwa au itaongezwa kwa Pegitosca ili kupanua mawanda yake ya kimatumizi.
7. Utafiti mwingine wa kisinkronia na wa kiadiakronia utaweza kuweka wazi hali halisi na mabadiliko ambayo yametokea katika msimbo wa Sheng’ kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na hata kisemantiki. Matokeo ya uchunguzi huo yataweza kuonyesha ruwaza za uleksikalishaji na za ukuaji wa msimu wa Sheng’. Utafiti huo utaweza kuchunguza kitakwimu mbinu mbalimbali zinazotumiwa kwa ajili ya kuunda msamiati katika msimu huo. Kupitia utafiti huo, itabainika kama Sheng’ imeanza kudhihirisha uthabiti katika matumizi ya sauti, msamiati na hata miundo ili kuwasilisha maana katika vipindi mbalimbali.

8. Kuna haja ya kutenganisha katika uchunguzi wa U.M., watafitiwa ambao wameanza kujifunza lugha ya pili na wale ambao wamepata ukwasi wa kiwango cha juu kwa lugha zote anazotumia. Watafiti wanaochunguza ubadilishaji msimbo miongoni mwa watu wanaojifunza lugha ya pili huenda wasipate matokeo sawa na yale yatakayotokana na wazungumzaji wenye umilisi. MacSwan (1997) amerejelea wazungumzaji ambao hawana ujuzi wa kutosha wa lugha mbili au zaidi kama wanaunusu-lugha. Inadaiwa kwamba wao huweza kubadilisha msimbo kwa sababu ya kukosa msamiati mwingine. Inamaanisha kwamba wao hawawezi kudhibiti mawasiliano kwa msimbo mmoja. Tasnifu hii hivyo basi inadokeza kwamba tafiti za U.M. unaofanyika baina ya lugha na lugha zinapaswa kubainisha barabara umilisi wa watafitiwa. Uchunguzi huu kwa upande wake haungeathiriwa na hali hiyo kwa sababu ulihusu U.M. baina ya msimu na lugha.
9. U.M. baina ya msimbo wa Sheng' na Kiswahili umebainishwa katika tasnifu hii kama matumizi lugha yanayoongozwa na kanuni. Hivyo basi, mtafiti anapendekeza kwamba maoni ya wataalamu wanaofafanua U.M. kama utendaji wa watu ambao hawana umilisi wa kutosha wa lugha, yanafaa kupuuzwa na wale wanaolenga kuutumia kama mkakati wa kufundisha. Motisha ya pendekezo hili ni uchanganuzi uliofanywa katika tasnifu hii ambao umeonyesha kuwa U.M. huongozwa na kanuni za 4M wala sio utendaji wa kiholelaholela. Kutokana na hayo, mtafiti anapendekeza kwamba mitalaa ya taasisi za watoto wa mitaani inayotumia U.M. baina ya Sheng' na Kiswahili kama chombo cha kufundisha kama ile inayorejelewa na Jwan na Ogechi (2004) inafaa kuidhinishwa na kukubaliwa.

10. Tasnifu ya mtafiti ni kwamba huenda U.M. baina ya misimbo miwili au zaidi utafanikisha mawasiliano kwa njia mwafaka au kwa wepesi zaidi katika baadhi ya miktadha kushinda matumizi ya lugha moja tu. Hivyo basi, anapendekeza kwamba wahusika ambao ni pamoja na wafanyibiashara, wahubiri na wengineo, hawapaswi kuogopa au kukwepa matumizi ya U.M. iwapo yatawafaa kama rasilmali ya kufanikisha mawasiliano. Hii inamaanisha kwamba ujumbe hautapotoshwa kwa kisingizio cha kuhifadhi usanifu au usafi wa lugha.
11. Uchunguzi wa tofauti za kimitindo za ubadilishaji msimbo kwa kutegemea umri, jinsia na mada unaweza kuwa mada muhimu ya utafiti wa baadaye. Uchunguzi wa aina hiyo unaweza kupambanua sifa za mitindo ya ubadilishaji msimbo kwa kulinganisha usemi wenye U.M. wa watafitiwa wa kike na wa kiume. Umri utaweza kuwa kiwakala muhimu kinachoamua mitindo ya U.M. inayoshirikisha Sheng' na Kiswahili. Utafiti wa aina hiyo utaweza kubainisha namna U.M. baina ya Sheng' na Kiswahili unaweza kutumiwa kimtindo kama njia ya kukwepa lugha mwiko.
12. Kwa kuongozwa na nadharia mbili zilizozingatiwa katika uchunguzi huu, tafiti zingine zinazochunguza madhumuni kama yale yaliyolengwa na mtafiti zinazojikita katika misimu tofauti zinafaa kufanywa. Utafiti linganishi kisha utaweza kufanywa kwa ajili ya kuweka wazi vipengele vinavyotofautiana na vile vyenye usifabia kuhusiana na misimu. Hii ni kwa vile utafiti huu haujachunguza misimu mingineyo na kwa fahiwa hiyo mahitimisho yake hayatoshelezi kutumika katika kuyafanyia maamuzi ya kijumla kuhusu U.M. unaohusisha misimu yoyote au misimu yote. Kutekelezwa kwa tafiti za aina hiyo huenda kutajenga msingi wa kuibuliwa kwa nadharia fafanuzi zaidi inayohusu misimu kama Sheng', 'Slang' na 'Luyaye'.

13. Ijapokuwa mtafiti hakuwa akinuia kuchunguza U.M. kama kiashiria cha badiliko la mada katika mazungumzo, ruwaza za data zimeashiria uwezekano huo. Kuna miktadha kadhaa iliyojitokeza katika uchunguzi huu iliyoashiria uhusiano baina ya U.M. na mada ya mazungumzo iliyokuwa ikiendelezwa na watafitiwa. Mathalani, baadhi ya mada zilizozungumziwa na wanafunzi zilizoonyesha U.M. zilikuwa za sayansi. Ilionekana kwamba msamiati huweza kuteuliwateuliwa kutoka msimbo mmoja kwa kutegemea mada ya mazungumzo au sentensi. Uchunguzi wa aina hiyo huenda ukafaa kwa ubainishaji wa tofauti na mahusiano baina ya mada ya usemi na mada ya sentensi mojamoja.
14. Kwa ujumla, ilitambuliwa katika mazungumzo ya watafitiwa yenye U.M., mada zilikuwa zikibadilikabadilika. Ilibainika pia kwamba mofimu amilifu kama vile viambishi vya ngeli katika vitenzi havikuwa vinawiana na nonimo ya kiima. Baadhi ya sentensi vilevile zilizalishwa bila viunganishi. Elementi hizi zilizokosekana ni viungo muhimu vya mshikamano. Kukosekana huko kumeichochea tasnifu hii ipendekeze kwamba utafiti wa baadaye unafaa uchunguze namna mshikamano na muwala unavyoibuliwa katika U.M. baina ya misimbo ya Sheng’ na Kiswahili.

**MAREJELEO**

Abdulaziz, M., & Osinde, K. (1987). Sheng' and Engsh in Nairobi. Katika *International Journal of the Sociology of Language.* 125: 1-21.

____________(1997). Sheng' and Engsh in Nairobi. Katika *International Journal of Sociology of Language.* 125: 43-63.

Amisi, O. (1997). Sheng' Vernacular Effect Performance in English. Katika *Daily Nation.* Tarehe 25/1/97. Uk. 13.

Bakhtin, M. (1981). *The Dialogic Imagination.* Austin: Texas University Press.

Barasa, L. (1997). *English Language Teaching in Kenyan Secondary Schools Policy, Planning and Practice*. Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Hull.

Bauer, L. (1983). *English Word Formation.* Cambridge: Cambridge University Press.

Bhattacherjee (2012). *Social Science Research Research: Principles, Methods and Practices.* London: Global Text Project.

Bentahila, A., & Davies, E. (1983). *Code-Switching and Language Dominance.* London: Academic Press.

Bosire, M. (2006). Hybrid Languages: The Case of Sheng'. Katika Olaoba F. Arasanyin na A., Michael (Wahar.) *Selected Proceedings of the 36th Annual Conference on African Linguistics,* Pemberton, *185-193.* Somerville, MA: Cascadilla Proceedings Project. Imepakuliwa Tarehe 20 Mei, 2016 kutoka www.lingref.com.

Brinton, L. (2005). *Lexicalization and Language Change*. Imepakuliwa Tarehe Mei 20, 2016 kutoka http://www.cambridge.org/uk/catalogue/catalogue/brintonlaurel.htm.

Childs, G. (1997). The Status of Isicamntho, an Nguni-based Urban Variety of Soweto. Katika Spears A. na D. Winford (Wahar.), *The Structure and Status of Pidgins and Creoles.* Amsterdam: John Benjamins.

Chimera, R. (1988). *Kiswahili: Past Present and Future Horizons.* Nairobi: Nairobi University Press.

____________(2003). *Vipengele Vilivyosahauliwa katika sarufi ya Kiswahili.* Makala yaliyotolewa katika Kongamano la Kiswahili lililofanyika Bayreuth, Ujerumani mwezi wa Mei, 2003.

Chiragdin, S., & Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.

Comrie, B. (1989). *The World's Major Language*. London: New Fetter Lane.

Cruse, D. (1986). *Lexical Semantics.* New York: Cambridge University Press.

Crystal, D. (1987). *The Cambridge Encyclopedia of Language*. Cambridge: Cambridge University Press.

_________ (2003). *A Dictionary of Linguistics and Phonetics*. London: Black Wells Publications.

Dahlgren, K. (1988). *Naive Semantics for Natural Language Understanding.* Boston: Kluwer Academic Publishers.

De Camp (1971). Implication of Sheng' and Sociolinguistic Linearity. Katika *Linguistics*. Vol. 130: 30-43.

Echessa, P. (1990). *A Study of Word Structure and Processes involved in Word Formation in Sheng': A Case Study of Eastlands Area in Nairobi.* Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Enon J. (1998). *Educational Research Statistics and Measurement*. Kampala: Makerere University Press.

Fardon, R., & Furniss, G. (1994). *African Languages, Development and the State*. London: Routledge.

Fink, T. (2002). *Attitudes Towards Languages in Nairobi*. Imepekuliwa Tarehe Desemba 17, 2016 kutoka http://etd.library.pitt.edu/ETD/available/etd-04212005-12.427/7.

__________ (2005). *The Major Participants in Language Change*. London: Academic Press.

Fishman J. (1967). Who Speaks What Language to Whom and When? Katika *La Linguistique*, 2: 67-88.

Gall, M. (1996). *Educational Research: An Introduction*. New York: Longman.

Garret, M. (1975). The Analysis of Sentense Production. Katika Bower, G. (Mhar.) *Psychology of Learning and Motivation*, 9: 133-137. New York: Academic.

Geeraerts, D. (1994). Lexical Meaning Types. Katika Asher na Simpson (Wahar.) *Encyclopedia of Language and Linguistics.* New York: Pergamon Press. Uk. 182-198.

Gibbe, A. (1983). Maendeleo ya Istilahi za Kiswahili. Katika *Lugha ya Kiswahili:* Makala ya semina ya kimataifa ya Kiswahili. TUKI: Chuo Kikuu cha Dares-salaam.

Githinji, P. (2003). *Language Attitudes: Nairobi People and Sheng'*. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Michigan State.

__________ (2006). Bazes and their Shibboleths: Lexical Variations and Sheng' Speakers' Identity in Nairobi. Katika *Nordic Journal of African Studies* 15(4): 443-473.

Githinji, P. (2007). Risky Discourse and Sociocultural Commentary. Katika *Cultural Production and Social Change in Kenya: Building Bridges* Uk. 81-110.

__________ (2009). *Sheng' Style Shifting and Construction of Multifaced Identities: Discursive Practices in the Social Negotiation of Meaning.* Port Louis: VDM Publishing House Ltd..

____________ (2013). Kwa Miaka Hamsini, Sheng' Imekitunza Kiswahili au Imekiua? Katika Simala, I na Chacha, L. (Wahar.) *Miaka Hamsini ya Kiswahili Nchini Kenya*. Cape Town: Centre for Advanced Studies of Frican Society.

Githiora, C. (2002). Sheng': Peer Language, Swahili Dialect or Emerging Creole? *Journal of African Cultural Studies*. 15(2): 159-181. Imepakuliwa Tarehe Novemba 17, 2017 kutoka http://www.jstor.org/stable/3181415.

Grosjean, F. (1988). Exploring the Recognition of Guest Words in Bilingual Speech. *Language and Cognitive Progress.* 3: 233-74.

Hayes C., Ornstein, J., & W. Gage (1987). *The ABCs of Languages and Linguistics.* Chicago: Voluntad Publishers Inc.

Hume, E. (1998). Metathesis Data, Motivation and Phonological Theory: The Case of Ieti. *Lingua* 104: 147-86.

__________ (2004). Indeterminacy/Attestation Model of Syllabic Inversion. *Language* 80(2): 203-237.

Iribe, M., & A. Mukhwana (2011). *Isimujamii.* Nairobi: Focus Publishers Limited.

Jwan, J. (1997). *Code Switching as a Strategy for Teaching in the Street Children Rehabilitation Centres: A Case study of Eldoret Children's Rescue Centre*. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa: Chuo cha Moi.

Jwan, J., & Ogechi, N. (2004). Bilingual Education for Street Children in Kenya: Evidence from Language Mixing. *Journal of Language and Learning.* 2(2): 65-98.

Kashoki (1972). The Language of the City: Town Bemba as Urban Hybridity. Katika *Journal of Linguistic Anthropology* 8(1): 30-59.

Katamba, F. (1993). *Morphology.* London: Mac Millan Press Ltd.

Kembo-Sure, E. (1992). The Coming of Sheng'. katika *English Today*. Uk.26-28.

___________(1994). *Language Altitudes, Use and Profieciency. A Socio-Linguistic Study of English in Kenya.* Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Moi.

Kiessling, R., & M., Mous (2004). Urban Youth Languages in Africa. *Anthropological Linguistics* 46(3): 303-341.

Kiingi, K.B. (1989). *A Systematic Approach to the Problem of Expressionism Modernization in the Formal and Natural Science: The Case of Luganda:* Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Bielefeld: Chuo Kikuu cha Bielefeld.

___________(1998). *A Theory of Scientific Terminology*. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa: chuo Kikuu cha Kenyatta.

___________ (2001). The "Kamusi Sanifu ya Biolojia, Fizikia na Kemia" and the Pegitosca Criterion. Katika Shitemi, N. Na wenzie (Wahar.) *Kiswahili A Tool for Development: The Disciplinary Approach.* Eldoret: Moi University Press. Uk. 206-214.

Kimei, P. (1997). Sheng' a Major Threat to English and Kiswahili. *Kenya Times* Tarehe 16/7/97. Uk. 12.

Kingei, K. (1987). Putting the Sheng' 'ghosts' to rest. *Kenyatta University Bulletin*. 2:22-23.

___________ (2000). Kiswahili Technical Terminology: Problems of Development and Usage In Kenya. Katika Kingei, K. (Mhar.) *Kiswahili* Juzuu la 63: 55-70.

__________ (2001). *Language and Identity: The challenge of Sheng' in Kenya.* Makala ya Kongamano la Association of Third World Studies Conference. Septemba 17-19, 2001. Njoro: Chuo Kikuu cha Egerton.

Kioni, K. (2002). Sheng' Takes its Toll on Performance of Languages. Katika *Kenya Times*, Tarehe 26/3/2002. Uk. 12.

Kothari, K. (1992). *Research Methodology. Methods and Techniques*. New Delhi: Willey Eastern.

Krashen, S., & Terell, T. (1983). *The Natural Approach*. Oxford: Pergamon Press.

Leedy, P. D. (2000). *Practical Research: Planning and Design*. New York: Pearson Publishers.

Lefebre, C. (1988). *Creole Genesis and the Aquisition of Grammar*. Cambridge: Cambridge University Press.

Levelt, W.J. M. (1999) *Speaking: From Intention to Articulation*. Cambridge Mass: MIT Press.

Luke, A. (1997). Theory and Practice in Critical Science Discourse. Katika L. Saha (Mhar.) *International Encyclopedia of Sociology of Education.* Imepakuliwa Tarehe Novemba 13, 2010 kutoka http://www.gseis.ucla.edu/courses/ed253a/Luke/SAHA6.html.

Mac Swan, J. (1997). *A Minimalist Approach to Intrasentential Code Switching: Spanish-Nahauati Bilingualism in Central Mexico.* Tasnifu ya Uzamifu: Chuo Kikuu cha California. Imepakuliwa tarehe Februari 18, 2016 kutoka https://liduaeka.Weebly.com.

Mac Swan, J. (2000). The Architecture of the Bilingual Language Faculty: Evidence from Intrasentential Code Switching. *Bilingualism, Language and Cognition*, 3, 37-74. Google Scholar, Crossref.

Mac William, A. (1986). *Mbinu za Kupata Istilahi Kutokana na Lugha za Kibantu*. Makala yaliyowakilishwa katika Kongamano la BAKITA. Workshop on Language Standardization Strategies, DMS, 5-7 1986.

Maingi, M. (2014). Kenya Should Celebrate its Backstreet Language. Imepakuliwa Tarehe Septemba 9, 2015 kutoka http://www.press reader.com/south-africa/business-day.

Masabo, T. (1995). Uingizaji wa Istilahi Kwenye Kamusi ya Msamiati wa Jumla. Katika J. G. Kiango na J.S. Mdee (Wahar.) *Utafiti na Utungaji wa Kamusi*. Uk 95-99. Dar es salaam: TUKI.

Masinde, E. (2007). *Mawanda ya Isimu jamii*. Eldoret: Taaluma Publishers.

Massamba, D.P.B. (1989). An Assesment of the Development and Modernization of Kiswahili Language in Tanzania. Katika F. Coulmas (mhar.) *Language Adaptation.* Uk. 60-78. Nairobi: JKF.

Mathews, P. (1974). *Morphology: An Introduction to Word Structure*. Cambridge: Cambridge University Press.

Mbaabu, I. (1996). *Language policy in East Africa: A dependency Theory Perspective*. Nairobi: ERAP.

__________ (2002). A Case for the Use of Kiswahili as a Language of Instruction in Lower Primary Schools in Kenya. Katika K. Njogu na wengine (Wahar.) *Kiswahili katika Karne ya Ishirini na Moja.* Cape Town: Centre for Advanced Studies of African Society.

Mbaabu, I., & Nzuga, K. (2003). *Sheng' English Dictionary, Deciphering East Africa's Underworld Language.* Dar es salaam: TUKI.

Mazrui, A. (1995). Slang and Code-Switching: The Case of Sheng' in Kenya. *Africaistisch Arbeitspapier* 42: 168-179.

Mazrui, A., & Mphande, L. (1990). How is a Code-mixer's Grammar Organised: Evidence from Sheng'. Paper presented at the 21st Annual Conference on African Linguistics. April 12-14, 1990. Athens:University of Georgia.

McGregor, S. (2003). Critical Science Approach: a Primer. Imepakuliwa Tarehe Novemba 29, 2010 kutoka http://www.kon.org/cpf/critical science primer.pdf.

McMohan (1994). Understanding Language Change. Imepakuliwa Tarehe Machi 29, 2016 kutoka https:www,jstor.org.

Mdee, J. (1986). *Kiswahili: Muundo na Matumizi Yake*. Nairobi: Intercontinental Publishers.

Mdee, J. (2010). *Nadharia na Historia ya Leksikografia*. Dar es Salaam: TUKI.

Mgullu, R. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia.* Nairobi: Longhorn Puplishers Ltd.

Mlacha, A. (1995). Lugha Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili. Imepakuliwa Tarehe January 6, 2018 kutoka www.worldcat.org.oclc.

Moga, Jacko na Fee, Dan. (1983). *Sheng' Dictionary*. Nairobi: Ginseng Publisher.

Mohochi, E.S. (2000). Language Choice for Development: The Case for Swahili in Kenya. *Journal of African Cultural Studies.* 16(1): 85-94.

___________(2002). Language and Regional Intergration: Foreign or African Languages for the African Union? Katika F.A. Yieke (Mhar.) *East Africa: In Search of National and Regional Codeisria, Dakar.* Uk. 41-54.

___________ (2005). *Students Attitudes Towards Kiswahili and their Effects on Performance in the National Form Four Examination in Coast and Nyanza Provinces, Kenya.* Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Egerton, Njoro.

Mokaya, B. (2005). Hybrid Languages: The Case of Sheng. Imepakuliwa . Tarehe Juni 20, 2010 kutoka http://www.lingref.com/cpp/acal/36/paper 1423.pdf.

Momanyi, C. (2001). Matumizi ya Kiswahili katika Njia Panda: Mtazamo wa Kiisimu-jamii. Katika N. Shitemi na wenzie (Wahar.) *Kiswahili: A Tool for Development: The Multidisciplinary Approach*. Uk. 83-89. Eldoret: Moi University Press.

__________ (2000). Nafasi ya Kiswahili katika karne ya 21. Katika Hassan, A. (Mhar.) *JUA* 3/3 Jan/Feb. Cologne: OMIME Intercultural Publishers.

___________ (2009). The Effects of Sheng' in the Teaching of Kiswahili in schools. *Journal of Pan African Studies 2*, (8): 127-138.

Mugenda, A., & Mugenda, O. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: ACTS Press.

Mukama, (1989). Hali ya Kiswahili Nchini Uganda. Katika *Usanifishaji wa* I*stilahi za Kiswahili.* Dar es Salaam: TUKI.

Muysken, P. (1996). Media Lengua. Katika S. Thomasoon (Mhar.), *Contact Languages: A Wider Perspective (*Uk. 365-426). Amsterdam: Benjamins.

Mwansoko, M.J. (1990). *The Modernization of Swahili Technical Terminologies: An Investigation of Linguistics and Literature Terminilogies*. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa. Chuo Kikuu cha New York.

Mwaro, G. (2001). Uendelezaji wa Leksikoni ya Kiswahili kwa Kufufua Msamiati wa Zamani na Vigezo vya Pegitosca. Katika N. Shitemi na wenzake (Wahar.) *Kiswahili: A Tool for Development. The Multidisciplinary Approach.* Eldoret: Moi University Press.

Mwihaki, A. (2006) *Sheng' and Kiswahili Studies: A Linguistic Approach*: Makala ya Kongamano: Hayajachapishwa.

Mwiria, K., & Wamahiu, S. (1995). *Issues in Educational Research in Africa.* Nairobi: E.A.E.P.

Myers-Scotton, C. (1993a). *Duelling Languages: Grammatical Structure on Code-switching*. New York: Oxford University Press.

____________(1993*b*). *Social Motivations for Code Switching: Evidence from Africa*. New York: Oxford University Press.

Myers-Scotton, C., & Jake, J. (2000). Testing a Model of Morpheme Classification Language Contact Data. Special Issue: *International Journal of Bilingualism* 4(1): 1-8.

___________ (2001). Explaining Aspects of Code-Switching and their Implications. Katika Nicol, J. (Mhar.) *One Mind Two Languages: Bilingual Language Processing.* Uk. 84-116. Malden, MA.

Myers-Scotton, C. (2002a). *Contact Linguistics, Bilingual Encounters and Grammatical Outcomes.* Oxford: Oxford University Press.

____________(2002b). *Frequency and Intentionality in (un)Marked Choices in Code Switching. 'This is a 24-hour Country.* Oxford: Oxford University Press.

____________(2005). *Uniform Structure: Looking beyond the Surface Structure in Code-Switching and Bilingual Language Processing and Production*. Cambridge: CUP.

Namba, K. (2004). An overview of Myers-Scotton's Matrix Language Frame model. Imepakuliwa Tarehe Oktoba 23, 2016 kutoka http://www.(nja.fi//vol.10nom3/namba.pdf.

Ngesa, M. (2002). And Sheng' lives on.... Katika Life Magazine. Februari 11, 2002. *East African Standard.* Uk.13.

Nishimura, M. (1997). *Code Switching: Syntax and Pragmatics.* New York: Peter Lang Publishers.

Njogu, K. (2008). *Culture, Performance and Identity: Paths of Communication in Kenya*. Nairobi: Twaweza Communications Ltd.

Nyagaka, G. (1995). Sheng' May be Here to Stay but.... Katika *Sunday Nation*. Tarehe 19/03/95. Uk. 11.

Nyawade, A. (1985). *An Investigation into the Influence of Kilugha on the Learning of English*. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Obuchi, S., & Mukhwana, A. (2010). *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na Vipengele.* Nairobi: A-Frame Publishers.

Obuchi, S., & Sangili, N. (2016). *Taaluma ya Maana: Semantiki na Pragmatiki*. Nairobi: JKF.

Ogechi,N., Shitemi, N., & Simala, K. (2008). *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.* Eldoret: Moi University Press.

Ogechi N. (2002). *Trilingual Code-Switching in Kenya: Evidence from Ekegusii, Kiswahili, English and Sheng'.* Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Hamburg.

__________ (2005). On Lexicalisation in Sheng'. *Nordic Journal of African Studies.* 14(3):334-355(205).

___________ (2008). Sheng' as a Youth Identity Marker: Reality or Misconception? Katika Njogu, K. (Mhar.) *Culture, Performance and Identity.* Nairobi: Paths of Communication in Kenya. Nairobo: Twaweza Communications Ltd. Uk. 117-129.

Okombo, O. (2000). Building Techniques in African Languages. Katika *African Voices: An Introduction To Languages and Linguistics of Africa.* Nairobi: Oxford University Press.

Omulando, C. (2001). *The Effect of Kiswahili on the use of English as a medium of Instruction and Language in Kenyan Secondary Schools: A case study of selected Secondary Schools in Bungoma District*. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Moi.

Onwong'a, Y. (2010). Kiswahili Language has Grown Beyond the Borders. Katika *The Standard*, Wednesday 27/1/2010. Uk. 16.

Obbo, O. (2006). Sheng' Spreads as a Complete System..... Katika *Daily Nation.* Tarehe 23/4/2006. Uk. 10.

Orengo P., & Opiyo, P. (2011). Sheng' Affecting English, Kiswahili Performance. Katika *The Standard*. Tarehe 29/12/2011. Uk. 8.

Osinde, K. (1986). *Sheng': An Investigation into the Social and Structural Aspects of an Evolving Language*. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Republic of Kenya (2010). *Kenya National Bureau of Satistics*. Nairobi: Government Printer.

Samper, D. (2002). *Talking Sheng': The Role of a Hybrid Language in the Construction of Identity and Youth Culture in Nairobi.* Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Pennsylvania.

Sawe, S. (2015). *Mshikamano na Muwala katika Diskosi za Kiwingi-lugha: Hali katika Vyuo Vikuu Nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu ambayo haijachapishwa: Chuo Kikuu cha Laikipia.

Schmitt, N. (2000). *Vocabulary in Language Teaching*. Cambridge: Cambridge University Press.

Shitemi, N. (2007). Pidginization, Sheng', The Melting Pot of the Kenyan Language and Anti-Babel Development. *Kiswahili* 64:1-15.

Spyropolous, M. (1987). Sheng': Some Preliminary Investigation into a Recently Emerged Nairobi Street Language. *Journal of the Anthropological Society at Oxford.* 18 (18) 125-136.

Temu, A. (1990). Swahili Vocabulary Expansion: A Preliminary Observation. Katika *Kiswahili Jarida La TUKI*, Juzuu la 42/1: 87-102. Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Todd, L. (1990). *Pidgins and Creoles*. London: Routledge.

Traugott, E., & Dasher, R. (2002). *Regularity in Semantic Change*. Cambridge: Cambridge University Press.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Toleo la pili*. Nairobi: Oxford University Press.

Waihenya, W. (1996). Evolution of Sheng' in our School system. *East Africa Standard* 12/10/96. Uk. 11.

Wamahiu, S., & Karugu, A. (2002). *Education and Development in Kenya*. Nairobi: Oxford University Press.

Wodak, R., & M. Meyer (2001). *Methods of Critical Discourse Analysis*. London: Sage Publications.

Yule, G. (2006). *The Study of Language*. (Toleo la 3). Cambridge: Cambridge University Press.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho I: Mwongozo wa Usaili

Maswali yafuatayo yaliongoza usaili wa watafitiwa katika utafiti huu:

1. Kuna watoto ambao wamezaliwa na wamejifunza Sheng’ kama lugha ya kwanza?
2. Iwapo kunao, je wamejifunza lugha nyingine kando na Sheng’?
3. Je, kuna msamiati unaotumika kutoka kizazi kimoja hadi kingine?
4. Je, kuna miktadha mingine ambamo Sheng’ inatumika?
5. Je, kuna vitabu vyovyote vya Sheng’?
6. Je, Sheng, inayozungumzwa hapa iliibukaje?
7. Ilitokana na mchanganyiko wa Kiswahili na lugha za hapa?
8. Kulikuwa na ukosefu wa lugha nyingine ndio watu wakaanza kutumia Sheng’?
9. Je, kuna kamusi zozote zilizoandikwa za Sheng’?
10. Umewahi kuzisoma?
11. Je, kuna vitabu vyovyote vya sarufi vya Sheng’?
12. Kuna maandishi yoyote ya fasihi kama vile hadithi fupi, tamthilia, riwaya ambazo zimeandikwa kwa Sheng’?
13. Je, iwapo zipo umewahi kuzisoma?
14. Unafikiri neno hili linafaa zaidi au halifai?
15. Je unaweza kunyambuanyambua neno hilo ili kupata maneno mapya?
16. Neno hili la Sheng’ linatumika kwingine ama ni hapa Kisumu pekee yake?
17. Je, unafikiri msamiati huu unafaa zaidi au kuna mwingine unaofaa zaidi?
18. Kwa mtazamo wako, msamiati/maneno yanayotumiwa katika Sheng’ yamedumishwa ama yamekuwa yakibadilikabadilika kila wakati?
19. Je, mmeishi mtaani kwa muda upi?
20. Kama mke na mume mna lugha zenu za kwanza?
21. Je, mna lugha inayowaunganisha katika mawasiliano? (lingua franka)
22. Mmefundisha watoto wenu lugha yenu ya kwanza au mliwafundisha Sheng’?
23. Je, katika familia nyingine za mtaani, watoto hujifunza Sheng’ kama lugha ya kwanza kutoka kwa wazazi wao au wanajifunza kutoka kwa watu/watoto wengine mtaani?
24. Je, unatoka eneo la Kisumu au maeneo mengine ya nchi ya Kenya?
25. Kwa mtazamo wako, msamiati/maneno ya Sheng’ yanayotumiwa na wanafunzi kutoka maeneo mengine yanalingana ama yanatofautiana?
26. Kwa mtazamo wako, maneno yanayotumiwa katika Sheng’ yamedumishwa ama yamekuwa yakibadilikabadilika kila wakati?

**Kiambatanisho II: Idhini ya Utafiti Kutoka NACOSTI**

NACOSTI

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION**

Telephone: 020 400 7000,
0713 788787,0735404245
Fax: +254-20-318245,318249
Email: dg@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke
When replying please quote

NACOSTI, Upper Kabete
Off Waiyaki Way
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI-KENYA

Ref. No. **NACOSTI/P/18/75309/20957**

Date: **31st January,2018**

Harriet Khatenje Ibala
Moi University
P.O. Box 3900 - 30100
**ELDORET.**

**RE: RESEARCH AUTHORIZATION**

Following your application for authority to carry out research on ***"Uleksikalishaji, ukriolishaji na mikakati ya kiwingi - lugha katika diskosi za sheng"*** I am pleased to inform you that you have been authorized to undertake research in **Kisumu County** for the period ending **31st January, 2019.**

You are advised to report to **the County Commissioner, the County Director of Education, Kisumu County** before embarking on the research project.

Kindly note that, as an applicant who has been licensed under the Science, Technology and Innovation Act, 2013 to conduct research in Kenya, you shall deposit **a copy** of the final research report to the Commission within **one year** of completion. The soft copy of the same should be submitted through the Online Research Information System

GP Kalerwa
**GODFREY P. KALERWA MSc., MBA, MKIM**
**FOR: DIRECTOR-GENERAL/CEO**

Copy to:
The County Commissioner
Kisumu County.

The County Director of Education
Kisumu County.

National Commission for Science, Technology and Innovation is ISO9001:2008 Certified

## Kiambatisho III: Kibali Cha Utafiti

**CONDITIONS**

1. The License is valid for the proposed research, research site specified period.
2. Both the Licence and any rights thereunder are non-transferable.
3. Upon request of the Commission, the Licensee shall submit a progress report.
4. The Licensee shall report to the County Director of Education and County Governor in the area of research before commencement of the research.
5. Excavation, filming and collection of specimens are subject to further permissions from relevant Government agencies.
6. This Licence does not give authority to transfer research materials.
7. The Licensee shall submit two (2) hard copies and upload a soft copy of their final report.
8. The Commission reserves the right to modify the conditions of this Licence including its cancellation without prior notice.

**REPUBLIC OF KENYA**

NACOSTI

**National Commission for Science, Technology and Innovation**

**RESEARCH CLEARANCE PERMIT**

**Serial No.A 17336**

**CONDITIONS: see back page**

**THIS IS TO CERTIFY THAT:**
***MS. HARRIET KHATENJE IBALA***
**of MOI UNIVERSITY, 0-30100 ELDORET,has been permitted to conduct research in *Kisumu County***

**on the topic: *ULEKSIKALISHAJI, UKRIOLISHAJI NA MIKAKATI YA KIWINGI - LUGHA KATIKA DISKOSI ZA SHENG'***

**for the period ending:**
***31st January,2019***

**Permit No : NACOSTI/P/18/75309/20957**
**Date Of Issue : 31st January,2018**
**Fee Recieved :Ksh 2000**



..............................
***Applicant's Signature***

..............................
***Director General***
***National Commission for Science, Technology & Innovation***